Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Hamsini na Mbili - Tarehe 22 Agosti, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa natoa taarifa kwamba Mheshimiwa Mussa Hamisi Silima, Mbunge kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, jana Jumapili, tarehe 21 Agosti, 2011 majira ya jioni kama saa mbili kasorobo hivi walipokuwa wakirejea kutoka Dar es Salaam, yeye na familia yake walipata ajali mbaya sana katika eneo la Nzuguni, Mjini Dodoma.

Katika ajali hiyo, mke wa Mbunge huyo aitwaye Mwanaheri Twalib amefariki dunia na mwili wa Marehemu upo hospitali ya Mkoa hapa Dodoma ukiandaliwa kupelekwa Zanzibar leo hii Jumatatu, tarehe 22 August, 2011 kwa mazishi yatanayotarajiwa kufanyanyika alasili ya leo. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tusimame dakika chache tumkumbuke. *(Heshima ya Marehemu, dakika moja)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama kwa dakika moja)*

Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, amina. Ahsanteni sana, tukae. Kwa hiyo sasa hivi tunavyoongea Mheshimiwa Mbunge ambae nae pia ameumia vibaya na dereva wake wanaondoka na ndege sasa hivi kusudi waweze kupata yanayohusika kule Dar es Salaam na pia kule watakuwa na watu wa kuwaangalia zaidi. Lakini walikwenda Zanzibar kumzika kaka yake na Marehemu huyu mama. Kwa hiyo, wamemzika marehemu basi wakawa wanawahi Bunge la leo ndiyo jana usiku wamepata ajali.

Kwa hiyo, watakaokwenda kusindikiza msiba, ndege itaondoka kama saa tano watakwenda wafuatao, watakwenda Wabunge nane pamoja na mfawidhi zanzibar yeye anaongozana na mgonjwa sasa hivi lakini ataungana na wale kwenye mazishi. Kwa hiyo, atakwenda yupo Mbunge Mstaafu Juma Suleiman N'hunga, kwa sababu ni ndugu yake lakini pia anafahamu mazingira ya kule, lakini pia atakwenda Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Waridi Bakari Jabu, Mheshimiwa Mnadhi Juma Maalim, Mheshimiwa Juma Habib Mnyaa, Mheshimiwa Heri Khamis Ali, atakwenda na Mheshimiwa Zaynab Vulu na atakwenda na Mheshimiwa Rosweeter Kasikila. Hawa inabidi wajiandae ndege itakayochukua mwili wa Marehemu itaondoka kama saa tano. Kwa hiyo, wataondoka na ndege mpaka Zanzibar, maandalizi yote yanayotakiwa ya kiisalam yatafanyika hapa halafu yatamalizikia huko Zanzibar. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wale niliowataja basi wajiandae vizuri. Katibu.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatayo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Taarifa ya Mwaka na Hesabu Zilizokaguliwa za Halmashauri ya Biashara ya Nje kwa Mwaka wa Fedha 2007/2008 *[The Annual Report and Audited Accounts of the Board of External Trade (BET) for the Financial Year 2007/2008].*

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Wakala wa Usajilio wa Biashara na Leseni kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 *[The Annual Report and Audited Accounts of Business Registration and Licensing Agency (BRELA) for the Financial Year 2008/2009].*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya maji kwa Mwaka wa Fedha, 2011/2012.

**MHE. NEEMA M. HAMID (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka 2010/2011 Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA MAJI:** Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Maji Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

## MWASWALI NA MAJIBU

Na. 460

### Ujenzi wa Barabara ya Bukoba Mjini hadi Rubafu

**MHE. PETER J. SERUKAMBA (K.n.y. MHE. JASSON S. RWEIKIZA)** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Bukoba Mjini hadi Rubafu (Bukoba Kabanga Bay km 42) kwa kiwango cha lami haujaanza licha ya mipango iliyopo na licha ya vituo vya ujenzi na makambi ya mkandarasi kukamilishwa.

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utaanza na kukamilishwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Bukoba Mjini, hadi Rubafu yenye urefu wa kilomita 42 ulianza mwezi Oktoba 2007 baada ya kupatikana kwa Mhandisi Mshauri *(M/S ITECO Consults (T) Ltd).* Ujenzi wa barabara hii utagharimu shilingi bilioni 45.6 na utafanyika kwa awamu tano hadi kukamilika kwake. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 19 Juni, 2008 kati ya Mkandarasi wa Kampuni ya *Jessie and Company Ltd.* Fedha zilizokwisha tolewa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi ni shilingi bilioni 1.4.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 mradi huu ulitengewa shilingi bilioni 1. Aidha katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi milioni 250 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu. Kukamilika kwa ujenzi wa barabara hii kutategemea upatikanaji wa fedha zinazotengwa katika Bajeti ya kila mwaka.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majawabu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, Waziri anasema barabara hii kukamilika inahitaji bilioni 45 na tayari wameshasaini mkataba, huoni kwamba sasa kwa kutotenga fedha maana yake mwisho wa siku tutalipa pesa nyingi sana kama interest na *idle time* na mkandarasi kufanya kazi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Peter Serukamba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, anachosema Mheshimiwa Peter Serukamaba ni sahihi, najua yeye ni Mwenyekiti wa Kamati ile Miundombinu analielewa hilli, hela hizi ambazo ziliombwa na mradi huu tunaouzungumzia hapa uko chini ya *RAS* Mkoa wa Kagera ni mradi wa huko nyuma nimeeleza hapa na shilingi bilioni 45.6 ndizo zinazohitajika ambacho tumezungumza nao, tumekubaliana, ukiacha mpango huu chini ya *RAS,* haitawezekana, mishahara pamoja na maendeleo na kila kitu wanapata bilioni 3.8 na hapa tunapozungumza bilino 1 waliyoomba hawakupata.

Mheshimiwa Spika, wamepata milioni 250, tunachofanya sasa hivi na walichoshauri ni kwamba tunawasiliana na wale wadau wengine wote, Waziri wa Ujenzi ananisikia hapa, wa Uchukuzi ananisikia hapa na wale Mawaziri wengine wanahusika wa *East African Community,* wote hawa wametamkwa katika hili. Mpango tulionao ni kuzungumza na wadau hao ili kila mmoja achukue kipande chake tuweze kusaidia katika jambo hili ambalo ni muhimu sana kwa uchumi wan chi yetu. *(Makofi)*

Na. 461

**Ajira ya Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. REGIA E. MTEMA** aliuliza**:-**

Kwa muda mrefu sana jamii ya watu wenye ulemavu imekuwa nyuma katika kupata ajira na kuna walemavu wengi sana wenye fani mbalimbali lakini hawako kwenye soko la ajira yeyote.

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi ya kukabiliana na changamoto hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira,napenda kujibu swali la Mheshimiwa Regia Estelatus Mtema, Mbunge Viti Maalum kama ifuatavyo:

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2008 na Shirika la Takwimu la Taifa *NBS* ni asilimia 3.1 ya watu wenye ulemavu nchini walio kwenye ajira za kipato na silimia 14.5 wapo kwenye ajira za kujiajiri wenyewe.

Mheshimiwa Spika, lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata fursa sawa katika ajira ya kulipwa na kujiajiri kulingana na ujuzi na uwezo walio nao. Mikakati ya Serikali katika kukabiliana na changamoto za ajira kwa watu wenye ulemavu ni pamoja na ifuatayo:-

(a) Bunge lako Tukufu imetunga Sheria ya watu wenye ulemavu namba 9 ya mwaka 2010. Ndani ya Sheria hii kifungu namba 31(2) kinamtaka kila mwajiri mwenye wafanyakazi kuanzia 20 na zaidi kuajiri watu wenye ulemavu wasiopungua asilimia tatu.

(b) Serikali imeendelea kutoa mafunzo ya ufundi stadi kupitia vyuo vya ufundi stadi mbalimbali. Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita takribani watu wenye ulemavu 2,500(wanawake 980 na wanaume 1520) wamepata mafunzo ya kuwawezesha kuajiriwa na kuajiri.

(c) Programu ya mafunzo ya kuwezesha wananchi kujiajiri kwa Wilaya za vijijini (*Demand Driven Skills Development Programme*) iliyotekelezwa katika Halmashauri za Wilaya nchini mwaka 2001/1002- 2009/2010 ilizingatia kuwapa pia fursa watu wenye ulemavu.

(d) Kuwapa fursa wajasiriamali wadogo wenye ulemavu kushiriki kwenye maonyesho ya nguvu kazi/jua kali za nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki.

(e) Kushirikisha watu wenye ulemavu kupitia shirikisho la vyama vyao kwenye Kamati za Kukuza ajira za Mikoa na Wilaya wakiwa ni wajumbe watakao wakilisha kundi hili katika kamati husika.

(f) Kuendelea kuhamasisha watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi na *SACCOS* ili kuweza kufaidika na huduma mbalimbali za kibiashara ikiwa ni pamoja na mafunzo na mikopo ya kuwawezesha kuanzisha na kuboresha miradi yao ya kiuchumi ya kujiajiri na kuajiri wengine.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo marefu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini kuna kipengele hayuko sahihi. Amesema kwamba sheria Na. 9 ya mwaka 2010 ya watu wenye ulemavu imeanza kutekelezwa si kweli, sheria hii bado haijaanza kutekelezwa kwa kuwa Kanuni ndogo za utekelezaji wa sheria hii bado haijatungwa mpaka sasa, ningependa alithibitishie Bunge hili je ni kweli sheria hii imeanza kutekelezwa? Bahati nzuri Mwanasheria yuko hapa.

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma wao wana mwongozo wa huduma za watumishi wa Umma kwa watu wenye ulemavu ambayo inaelekeza namna ya kuwasaidia wa hapo kazini, ningependa kujua. Je Wizara ya Kazi inayo mwongozo kwa waajiriwa wa sekta binafsi wenye ulemavu?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Regia Mtema, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema sheria hiyo imetungwa mwaka 2010, sheria Namba 9, sasa anavyosema kwamba haijaanza kutekelezwa, hilo ni jambo la kuangalia kama kweli kanuni unazosema hazijataharishwa, mimi kwa mujibu wa taarifa nilizonazo ni kwamba sheria hiyo imeanza kutumika, lakini tunaweza tukaangalia, tukafuatilia tuone hali ikoje kuhusu hizo kanuni.

Kuhusu huo mwongozo, siwezi kuamini kwamba kuna mwongozo huo unaosema katika maeneo mengine, lakini niseme tu kwamba katika suala la walemavu, hata sheria ya ajira ya mahusiano kazini inasisitiza suala hilo la kuajiri watu walemavu na pale ambapo kuna nyanyasaji katika ajira, hili suala la kutoajiri watu wenye ulemavu inachukuliwa kama ni suala la ubaguzi kwa mujibu wa kifungu na 7(4).

Kwa hiyo, mimi naweza kusema tu kwamba kwa kweli tumeweka, ukichukua sheria ile ulemavu, ukichukua sheria ya ajira na mahusiano kazini zote hizo zinaelekeza namna ya Kuwa na adhabu kama watu wamevunja hii sheria kwa makusudi bila kufuata vigezo vya kutoajiri walemavu.

Kwa hiyo, mimi nilitaka nimhakikishie tu Mheshimiwa Mtema kwamba tunazingatia hili, suala sasa ni kuendelea tu kufuatilia hizi sheria na kanuni zilizopo na hizo taratibu ili walemavu waendelee kuajiriwa kama watu wengine wasiokuwa walemavu. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukukuru kwa kuniona. Nina swali dogo tu la nyongeza.

Katika maelezo ya Mheshimiwa mjibu swali amesema kwamba watu wenye ulemavu hasa wale ambao hawana ajira wana ajira yao binafsi, wanasaidiwa na hiki na kile.

Je, Serikali inafahamu kwamba watu wenye ulemavu wanapata shida sana ya kukuza mitaji yao kwa sababu hawapati mikopo?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Margareth Mkanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli watu wenye ulemavu kama walivyo watu wengine vijana wanapata matatizo ya kupata mikopo, lakini juhudi ambazo zimekuwa zikifanywa na Serikali hasa kwenye upande huu walemavu, nimetaja hapa kwamba tumekuwa tunaendelea kuwahamasisha watu wenye ulemavu kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi na *SACCOS* na pale ambapo misaada inawezekana wamekuwa wakipatiwa.

Sisemi kwamba sasa tatizo hili limekwisha, lakini juhudi hizi zipo na wamekuwa wakisaidiwa sio tu na Serikali, lakini taasisi mbalimbali wamekuwa wakisaidia vikundi vya aina hii vya watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, tuendelee kushirikiana kama jamii kuwasaidia wenzetu hawa.

Na. 462

**Shida ya Makazi na Usafiri kwa Maafisa Uhamiaji Wilaya ya Micheweni**

**MHE. RASHID ALI OMAR (K.n.y. HAJI KHATIB KAI)** aliuliza:-

Maofisa Uhamiaji walioko Wilaya ya Micheweni wanakabiliwa na shida ya makazi na usafiri kwani nyumba wanazoishi ni mbovu sana na mitaro ya maji taka imejaa na haihudumiwi hivyo kuwafanya washindwe kufanya kazi zao sawasawa kwa kuzingatia usafiri mbovu wa pikipiki walio nao:-

Je, Serikali inao mpango gani wa kuwaondolea kero hizo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nyumba wanazoishi Maafisa Uhamiaji katika Wilaya ya Micheweni ni za kukodi kutoka Wizara ya Majenzi na Makazi Zanzibar. Kutokana na hali ya ubovu wa nyumba hizo, tayari Wizara kupitia Idara ya Uhamiaji inafanya jitihada za makubaliano na mmiliki wa nyumba hizo ili ziweze kufanyiwa ukarabati.

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza tatizo la nyumba za makaazi kwa wafanyakazi katika Wilaya ya Micheweni, Idara ya Uhamiaji tayari imepata viwanja viwili (2) kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la usafiri ni kweli kuwa pikipiki iliyopo ni chakavu. Ili kutatua tatizo hilo, Idara ya Uhamiaji kupitia Bajeti ya mwaka 2010/2011 imenunua jumla ya pikipiki 42 ambazo zimepokelewa mwisho mwa mwezi Julai, 2011. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Ofisi ya Uhamiaji Wilaya ya Micheweni itapatiwa pikipiki moja (1) STK 8530.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri yenye matumaini. Ninataka kuuliza swali moja la nyongeza.

**SPIKA:** Hapo pana matatizo na hiyo mashine, hamia pengine. Inapiga kelele.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri yenye matumaini yenye kutia matumaini. Mimi nitakuwa na swali moja tu la nyongeza. Kwa sababu Wizara tayari imepata viwanja viwili, kwa nini isifanye mipango ya kujenga jengo moja na hatimaye kuweza ku-*avoid* masuala kwenye ukarabati baadhi ya nyumba hizi za askari hawa? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimeusikia ushauri wake. Nitatazama katika *plan* zetu na hususani fedha zitaturuhusu kiasi gani. Lakini ni ushauri ambao nimeupokea.

Na. 463

**Uvunjivu wa Haki za Binadamu – Tarime**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Pamoja na nchi kusimamia haki na Utawala Bora kwa raia wake, lakini kumekuwa na uvunjivu wa haki za binadamu katika jimbo la Tarime na Serikali haionekani kuchukua hatua yo yoyote:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya hatma ya wakazi wa Nyamongo ambao wamekuwa wakiuawa kwa kupigwa risasi na walinzi wa mgodi wa *North Mara?*

(b) Je, Serikali inatamka nini juu ya kina mama wa kijiji cha Kwebeye ambao polisi wa Kanda Maalum ya Tarime na Rorya waliamuru mama na mwanaye kufanya tendo la ngono na hakuna hatua zozote zilizochukuliwa dhidi ya polisi hao licha ya kwamba aliyekuwa Mbunge wa Tarime Mheshimiwa Mwera kuhoji juu ya unyama huo bila mafanikio?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Ndani, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakiri kwamba hali ya Nyamongo imekuwa na matukio ambayo si mazuri hata kidogo. Ni hali ambayo baadhi ya wananchi na walinzi wa mgodi unaomilikiwa na Kampuni ya *African Barrick Gold* wamepoteza maisha.

Hatima ya wakazi wa Nyamongo imo mikononi mwa Wizara ya Nishati na Madini na Wawekezaji wa *African Barrick Gold Mines.* Mazungumzo yaliyopo kati ya Wizara na wananchi kuhusu wachimbaji wadogo wadogo kupata maeneo mbadala na mwekezaji kuhusu maendeleo ya eneo la Nyamongo ndiyo njia pekee ya kuleta amani na utulivu katika eneo la Nyamongo.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu akijibu swali la papo kwa papo katika Mkutano wa 20 wa Bunge lako Tukufu aliahidi kufanyia uchunguzi na kuchukua hatua stahiki juu ya suala hili. Wizara yangu iliunda Tume ya Maofisa kutoka Jeshi la Polisi, Idara ya Usalama wa Taifa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya uchunguzi juu ya tuhuma hizo. Timu imetoa taarifa kuhusu tukio hilo.

Ni kweli tarehe 6 Mei, 2010 usiku askari polisi walikwenda nyumbani kwa Hellen Mugaya kwa ajili ya kuwafikisha katika vyombo vya Sheria, Mugaya Chandi Mwita na Shemeji yake Nyaheti Chandi Mwita kwa tuhuma za mauaji, wizi wa mifugo na kuharibu mali. Polisi waliongozana na Mwenyekiti wa Kijiji cha Kabweye Ndugu Ambrose Basil Mora, ambaye katika ushahidi wake, anakataa kuona kitendo chochote cha udhalilishaji kilifanywa na polisi dhidi ya mtu yeyote.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Ninashukuru Mheshimiwa Spika. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Naibu Waziri anakiri kwamba hatima ya wananchi wa Nyamongo kuendelea kuuawa na kupigwa risasi na kuwa walemavu iko chini ya Wizara ya Nishati na Madini na Mwekezaji wa *African Barrick.*

Ningependa kuuliza sasa kwamba Serikali inachukulia vipi hili kwa sababu kabla ya uwekezaji wananchi wa Nyamongo na wengine wote waliokuwa wakifanya shughuli za uchimbaji katika mgodi ule chanzo chao kikuuu cha kujipatia mapato ilikuwa ni uchimbaji wa madini haya.

Sasa kwa sababu Serikali iliamua kuwekeza haioni kwamba sasa inawajibika kupunguza huu uuwaji wa wananchi na ulemavu wa wananchi na utesaji wa wananchi kwa sababu kabla

hata ya mauaji ya tarehe 15 Mei bado kumeendelea kuwepo kutokea mauaji na ulemavu wa wananchi.

Je, Serikali haioni kwamba inatakiwa kuchukua hatua mbadala sasa kwa kuwagawia hawa wananchi ambao walikuwa wakitegemea uchimbaji kama kipato chao maalum kwenye uchimbaji mdogo mdogo?

Pili kwenye swali langu la pili

**SPIKA:** Ila uliulize kifupi siyo hotuba.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Swali la pili Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwamba Tume iliundwa na imeonyesha kwamba hawa watu hawakutendewa madhila yale. Lakini ukweli ni kwamba Tume hii imejumuisha jeshi la polisi, usalama wa taifa na Afisa mmoja kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Inasemekana kwamba kwa taarifa iliyopo jeshi la polisi liliienda likamtisha mwana mama yule Hellen Mugaya na akawajibika kuandika ripoti nyingine ya pili ambayo inakinzana na ile ya kwanza.

Je, Serikali haioni kwamba ni dhahiri kwamba inatakiwa iunde Tume huru ambayo haitahusisha maafisa wa polisi, maafisa wa Usalama wa Taifa na Maafisa kutoka kwa Mwansheria Mkuu wa Serikali kwa maana ya wanajeshi na wananchi ili waweze kuchunguza tuhuma hii maana yake ni kweli hawa watu walitendewa dhima hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Maswali yako marefu mno.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza kama nilivyosema ni kwamba kweli yaliyotokea yanasikitisha na kama alivyowahi kusema *Attorny General* hapa ndani ya Ukumbi huu wako Tukufu ni kwamba vifo au kifo cha mtu mmoja ni kitu ambacho kinachukuliwa kwa uzito sana. *(Makofi)*

Lakini kama nilivyosema na ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Mbunge amenielewa ni kwamba hili jambo tunalipa uzito na ndiyo maana kuna mazungumzo ambayo yanaendelea kati ya Wizara husika ya Nishati na Madini, wamiliki wa mgodi wa *Nyamongo African Barrick Gold Mines* kwa shabaha ya kuona hawa wachimbaji wadogo wadogo wanaweza wakapata maeneo mbadala na ahadi nyingine ambazo zilikuwa zimekwama au ambazo zimekuwa zinazungumzika zinakamilika kwa shabaha ya kumaliza mzozoro huu ama tatizo ambalo tumekuwa nalo.

Kuhusu suala la pili Mheshimiwa Spika, niseme kwamba ni maoni ya Mheshimiwa Mbunge kwamba Tume haikuwa huru na ni maoni yake.

Lakini niseme kwamba Tume yoyote ambayo itakuwepo lazima Serikali itahusika na Tume hiyo na niseme kwamba maoni yake kwamba Tume imefanya kazi yake lakini bado kama wanaona kwamba hakuna kuridhishwa kokote, basi kama nilivyokuwa nimesema awali mimi mwenyewe nitafanya safari ya kwenda Nyamongo tutakutana na watu husika na tutatazama tunatafuta muafaka gani kuhusu suala hili na ukweli uko wapi katika suala hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Pole maswali hauwezi kuuliza. Limechukua dakika 10 lenyewe peke yake. Mheshimiwa Martha Umbulla, atauliza swali linalofuata.

Na. 464

**Uhitaji wa Benki ya Tarafa za Mkoa wa Manyara**

**MHE. MARTHA J. UMBULLA** aliuliza:-

Katika mpango wa uwezeshaji wananchi kupitia uanzishwaji wa *SACCOs* na VICOBA umefanikiwa kuwawezesha wananchi kiuchumi hasa katika Mkoa wa Manyara, lakini hakuna Benki mahali pa wananchi kutunzia pesa zao wanazopata kupitia mafanikio yao ya kiuchumi:-

Je, ni nini mkakati wa haraka wa Serikali kupeleka huduma za kibenki angalau kwa kila Tarafa za Mkoa wa Manyara ili kuhakikisha usalama wa fedha za wanachama wa *SACCOs* na *VICOBA?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kupeleka huduma za kibenki karibu na wananchi. Hata hivyo, kufuatia mageuzi ya sekta ya fedha nchini kuanzia mwaka 1991, Serikali haijihusishi moja kwa moja na uendeshaji wa biashara za kibenki. Biashara za kibenki hufanywa na sekta binafsi kwa kuzingatia maslahi ya kibiashara na sheria za nchi, chini ya usimamizi wa Benki Kuu. Kwa hiyo, ufunguzi wa benki au matawi ya benki za kibiashara Mikoani na Wilayani unategemea mbali na ushawishi wa Serikali, maamuzi ya kibiashara ya kibenki.

Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha kuwa huduma za kibenki zinapatikana karibu na wananchji wenye uwezo mdogo, Serikali kupitia Benki Kuu imetoa vigezo nafuu vya uanzishwaji wa Benki za Wananchi (*Community Banks).* Katika kanuni za leseni za benki na taasisi za fedha za mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la viongozi wa kisiasa na taasisi mbalimbali kuhakikisha na kuwawezesha wananchi katika maeneo yao kuanzisha benki za wananchi kama ni mkakati wa kupeleka huduma za kibenki karibu na wananchi ikiwa ni pamoja na usalama wa fedha za wanachama wa *SACCOs* na *VICOBA.*

Mheshimiwa Spika, Serikali na mamlaka husika zinaendelea kutengeneza mazingira mazuri ya ukuaji wa shughuli za kiuchumi katika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuvutia wawekezaji ikiwemo ufunguzi wa matawi ya benki kwenye Wilaya na Tarafa mbalimbali.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi. Siajapata vizuri majibu ya swali kuonyesha dhahiri ni namna gani Serikali inahusika katika kuanzisha benki kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali haihusiki lakini vile vile amesema uanzishwaji wa Benki ni suala la kisheria chini ya Benki Kuu. Lakini vile vile amesema Serikali inahusika kushawishi kulingana na biashara. Sasa nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa *Community Banking* ama benki ya jamii inahitaji mtaji mkubwa ambayo hajataja ni kama milioni 250 hadi 500 jambo ambalo wananchi wa vijijini hawawezi kupata. Je, Serikali iko tayari sasa kuondoa ama ku-*subsidize* kigezo hiki ambacho ni kigumu sana kwa vijijini kutekeleza?

Swali la pili mwaka 2005 hadi 2010 Serikali ilihamasisha uanzishwaji wa *SACCOs* na *VICOBA* hapa nchini jambo ambalo limefanikiwa sana ikiwepo katika Wilaya zetu za Hanang, Mbulu na Babati Mkoani Manyara ambako urejeshwaji sasa ni mkubwa sana kwa wananchi wanaobeba hizo fedha kupeleka kama kilometa 50 hadi 60 kufuata benki. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba kwa utafiti aliofanya bado Serikali inawajibika kushawishi uanzishwaji wa tawi la benki katika Tarafa ya Dongobeshi ama Haidom kule Manyara?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana kwa Mheshimiwa Mbunge kwa shughuli anazofanya kuhakikisha kwamba masuala ya *SACCOs* katika Tarafa za Dongobeshi na kwingine zinazaa matunda mazuri.

Mheshimiwa Spika, kuna masharti ya kuanzisha benki za wananchi na kigezo cha chini ni shilingi 250 milioni na kuna mahitaji mengine ambayo ni madogo kuliko uwezo huo wa kifedha. Hata hivyo Serikali kupitia Benki Kuu tunaweza tukaendelea kutazama hiki kigezo isipokuwa kigezo

hiki kimewekwa kwa upande mmoja pia kuhakikisha usalama wa fedha nyingine kuliko mtu yoyote kuamua kwenda kuanzisha benki halafu mwishoni ikawa *DECI* nyingine.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, ni kwamba Serikali ina lengo la kuhakikiksha wananchi wanapata huduma na ni dhahiri inajua kwamba wananchi wengine wanaishi mbali na maeneo ambako kuna benki kama Dongobeshi, ni kilomita kama 50 lakini Serikali kwa sheria zilizopo ni mraghibishi na mshawishi kuwasukuma benki waweze kuzisogeza hizo huduma vijijini na hilo Serikali itaendelea kulifanya. Lakini pia kuna maendeleo ya TEHAMA na kuweka mazingira mazuri bado itakuwa ni kazi ya Serikali katika kuhakikisha kwamba wananchi na fedha zao ziko salama.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipatia nafasi kuuliza swali la nyongeza. Ukiangalia Wilaya Mheshimiwa aliyetoka wao wamehamasisha VICOBA pamoja na *SACCOs* kama sisi tulivyofanya katika Wilaya yetu ya Misenyi. Je, Serikali inaonekane kuweka nguvu pia katika kusaidia VICOBA kama inavyofanya kwenye *SACCOs* maana benki nyingi hazikubali kukopesha VICOBA wakati tumefanikiwa sana kuhamisha *VICOBA?*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie kwamba Serikali iko tayari kulifuatilia suala hili na matatizo ya VICOBA na kutoa msaada unaowezekana kibajeti na kiutendaji.

Na. 465

**Ujenzi wa Maabara na Maktaba Shuleni**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MOHAMMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Wananchi wa Jimbo la Singida Mjini wametelekeza kwa kiwango kikubwa Sera ya *CCM* ya kujenga shule za Sekondari kwa kila Kata.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunga mkono juhudi za wananchi kwa kujenga maabara na maktaba kwa kila shule iliyojengwa:-

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohammed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifiatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, wananchi wa Tanzania wameitikia kwa moyo wote Sera ya Ujenzi wa shule za sekondari katika kila Kata hapa nchini. Hatua hii imewezesha vijana wengi kupata nafasi ya kusoma elimu ya sekondari. Hata hivyo, kumejitokeza changamoto kadhaa katika utekelezaji wa Sera hiyo, hususan kukosekana au kutokamilika kwa baadhi ya majengo muhimu yakiwemo maabara na maktaba.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua na kuthamini mchango wa wananchi, Serikali imechangia kwa kutoa ruzuku ya ujenzi ili kukamilisha na kujenga majengo hayo. Katika kipindi cha 2005 – 2009, wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya kwanza, Serikali ilitoa ruzuku ya ujenzi wa vyumba vya maabara 311 na vyumba 57 vya maktaba kama nilivyobainisha wakati nikijibu Swali Na. 332 la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, tarehe 29 Julai, 2011 lililohusu ujenzi wa maabara nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Awamu hii ya Pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (2010 – 2015) Serikali imekusudia kuendelea na utaratibu wa kukamilisha majengo ya maabara na maktaba katika shule za sekondari kwa awamu.

Kwa mwaka 2011/2014 jumla ya shule 264 kwa maana ya shule 2 kila Halmashauri, zitakamilishiwa na kujengewa majengo mbalimbali ikiwemo Maabara na nyumba za walimu. Utaratibu huu utaendelea kwa awamu kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge Mohamed Gulam Dewji amefanya kazi kubwa sana ya kujenga shule hizi karibu shule zote nusu ya gharama ni pesa zake mwenyewe. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amekubali kwamba atapeleka pesa kwa ajili ya ujenzi wa maabara pamoja na Maktaba.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ataona ni vema sasa kujenga maabara hizo pamoja na kupeleka walimu wa sayansi pamoja na vifaa? Ili sualal hili liende sambamba?

Swali la pili, kwa kuwa katika shule hizi Mheshimiwa Mbunge wa jimbo ameshajenga hosteli shule zote na kufikia ngazi ya upauaji.

Je, Serikali haioni sasa kuna kila sababu ya kumtua mzigo Mheshimiwa Mbunge kumalizia shule hizi ili Mbunge huyo aendelee kupata moyo wa kuwasaidia wananchi wa jimbo lake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa taarifa hii ambayo mimi binafsi nimeridhika nayo napenda tu kumpongeza Mheshimiwa Dewji Gulam, Mbunge wa Singida Mjini, kwa jitihada anazozifanya katika kusaidia wananchi wake wa jimbo hilo kukamilisha ujenzi wa hizi shule za sekondari za Kata na napenda kutoa mwito kwa Wabunge wote kuiga mfano huo. Namshukuru sana.

Hata Serikali sasa inatamka kwamba Jimbo la Singida Mjini tutalipatia walimu wa Sayansi kwa ajili ya kumpa moyo Mheshimiwa Mbunge huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile katika Jimbo la Singida Mjini, Serikali imepanga kujenga shule za mfano mbili, na nimesema ni katika kila Halmashauri. Lakini kwa upande wa Singida Mjini, Mheshimiwa Gulam, atajengewa katika shule waliyochagua Halmashauri, *Dokta Salmini Secondary School* na Shule ya Sekondari Mwenge. Kwa hiyo, nampongeza sana na Serikali iko nyuma yake katikakuunga mkono juhudi anazozifanya Jimboni kwake.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa, tatizo la maabara liko katika shule nyingi sana hapa nchini. Na kwa kuwa, wanafunzi wanapofika kidato cha IV (Nne) hutahiniwa kwa kufanana *whether* wana maabara au hawana maabara. Matokeo yake wanafunzi wasiokuwa na maabara wamekuwa wakifeli sana masomo ya Sayansi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni imefika wakati sasa kuwa na mitihani tofauti ili wale wasiokuwa na maabara wapewe mtihani mwingine na wale wenye maabara wapate mitihani mingine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Susan Lyimo, Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Baraza la Mitihani lina aina mbili za mitihani kwa masomo ya Sayansi. Kwa zile shule ambazo zinakuwa hazina maabara na hawasomi masomo hayo kwa mfumo wa vitendo, huwa wanatunga mitihani inaitwa *Alternative to Practical* na kwa masomo ya Sayansi, kunakuwa na mitihani inayoitwa *Real Practical.* Kwa hiyo, wanafunzi ambao wanakosa maabara hawanyimwi haki ya mitihani ya Sayansi, bali wanafanya ile *theory* ambayo inakuwa ni *alternative to practical.* Kwa hiyo, wote wanapata masomo sawa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, shule za sekondari tumejenga kila Kata. Na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri, hapa amesema kwamba kutoka mwaka 2011 mpaka 2014 ni maabara 214 tu zitakazojengwa. Na kwa maana hiyo ni kwamba, ni shule mbili mbili tu ndizo ambazo zitaweza kupata maabara.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni kwamba jitihada hizi za polepole zitakwamisha sana kuwawezesha wanafunzi kupata maabara haraka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, Mpina, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema ni kwamba, hizi shule zetu za wananchi, Ngazi ya Kata, ni shule ambazo sasa zinamilikiwa na wananchi wenyewe kupitia Mkurugenzi. Kwa hiyo, hapa sijasema kwamba Serikali kwa sababu itatoa shule mbili kwa shule za mfano kujengewa maabara kwamba, basi wananchi kule wasiendelee kujenga vyumba vya maabara, la hasha!

Mheshimiwa Spika, nimesema Serikali katika maandiko yake imepata fedha kwa ajili ya kusaidia kuweka nguvu, angalao shule mbili kila Halmashauri. Tutajenga maabara pamoja na nyumba zile 1,200 za walimu; tunataka tuweke kila Halmashauri kuwe kuna shule mbili za mfano. Sasa katika mfano ni lazima tuweke na maabara iliyo *well equipped.* Kwa hiyo, sijasema kwamba labda wananchi wasiendelee kujenga vyumba vya maabara, waendelee na tunawapongeza sana kwa juhudi hizo.

Na. 466

**Serikali Kusaidia Wanaoshindwa Kufaulu Mitihani**

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA** aliuliza:-

Watoto wengi wanaomaliza shule za msingi na sekondari hufeli mitihani yao.

Je, Serikali ina mpango gani wa kwasaidia watoto hawa wanaoshindwa kufaulu mitihani yao?

Je, Serikali haioni kuwa huu ni wakati muafaka wa kujenga Vyuo vya Ufundi kwa kila Tarafa ili kuwasaidia vijana hao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu Swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jukumu kubwa la Wizara yangu ni kutoa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa rika lengwa la Watanzania. Katika kutekeleza jukumu hili Wizara yangu imekuwa ikichukua hatua kwa wanafunzi wanaoshindwa mitihani yao kama ifutavyo:-

(i) Kukubali warudie mitihani hiyo kama watahiniwa binafsi kwa upande wa elimu ya sekondari.

(ii)Kutoa nafasi za kujiendeleza ki-elimu kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kufanya Mtihani wa Maarifa *(Qualifying Test)*.

(iii)Kutoa nafasi za kujiendeleza katika mafunzo ya ufundi kupitia Vyuo vya Ufundi Stadi vya *VETA* na vyuo binafsi.

(iv) Kusajili shule na vituo vya mafunzo vingi zaidi nchini, vinavyomilikiwa na Mashirika na watu binafsi ili kuwawezesha vijana walioshindwa kufaulu mitihani yao kuendelea kupata fursa ya kujiendeleza kiuchumi, kielimi na kiutamaduni.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuongeza Vyuo vya Ufundi ili kuwapatia Watanzania wengi zaidi stadi za kazi katika Nyanja mbalimbali. Kwa sasa, katika kila mkoa kuna chuo cha *VETA.* Aidha, vyuo vya *VETA* vitaendelea kujengwa katika kila wilaya. Serikali itakapokamilisha ujenzi wa Vyuo vya Ufundi vya Wilaya itaangalia uwezekano wa kujenga vyuo vya Tarafa kulingana na mahitaji.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Jimbo la Mufindi Kusini, ni Jimbo Kubwa, vijana wengi waliomaliza elimu ya sekondari wako mitaani na Serikali bado haijaanza kuchukua hatua. Je, wananchi wakichukua hatua ya kuanza kujenga Chuo cha Ufundi, katika Jimbo la Mufindi Kusini, Serikali ipo tayari kuwasaidia?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu Swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa leo niungane na Mbunge wa Singida Mjini, kukupongeza kama unaweza ukahamasisha wananchi wa Jimbo lako, waweze kutujengea majengo.

Serikali tuko tayari kuanzisha Chuo cha *VETA* na kukuletea vifaa, kwa sababu, nia ya Serikali ni kusaidiana. Na hata juzi tu nimetoka Wilaya ya Bahi, nimekwenda kuangalia majengo ambayo tayari yalikuwa Chuo cha *VETA* zamani lakini kutokana na matatizo ya kiutawala yakachukuliwa na shirika moja hivi *(KISEDET).* Lakini juzi Mheshimiwa Mbunge, alinipeleka pale nikayathibitisha yale majengo na nitatuma timu ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, upande wa Ufundi, wakaangalie pale ili ndio kiwe Chuo cha *VETA* cha Wilaya. Kwa hiyo, wananchi wakijenga, sisi tuko tayari kuwahudumia. *(Makofi)*

**MHE. ROSE K. SUKUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Na mimi naomba nimwulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vijana wamehangaika kutafuta vyuo mbalimbali na wamekosa kwa ajili ya uwingi wao.

Je, sasa Serikali haioni kuna umuhimu wa kuchukua shamba la *BASOTU Plantation* ambalo limekaa halikupata Muwekezaji, ifungue chuo cha muda ili wanafunzi waliomaliza Kidato cha IV, Wilaya ya Hanang au Mkoa wa Manyara, wakapata nafasi ya kuweza kujiendeleza kwenye chuo hicho? Naomba sana hili kwa sababu, tuwaokoe kwa kuwa muda wa kujiandikisha ni sasa.

**SPIKA:** Ahsante! Mheshimiwa Kamili, swali limeeleweka. Naomba ujibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Mkiuliza kwa kifupi, wanakuwa Wabunge wengi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rose Kamili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wingi wa vijana katika Mkoa wa Manyara, hususan Jimbo la Hanang, kwamba wamekosa pa kwenda na vyuo vya ufundi kule hakuna! Nataka tu nikutaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari mwezi wa kwanza mwaka 2012, Serikali itafungua Chuo cha *VETA,* Mkoa wa Manyara ambacho ni Chuo cha Mkoa. Kwa hiyo, nataka ukirudi tu kule Jimboni, ukawahamasishe vijana hao wajiunge mwezi wa kwanza kwenye Chuo cha VETA Manyara.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu shamba la *BASUTO…*

**SPIKA:** Si swali moja tu! Mheshimiwa Anne Kilango, swali lingine.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa hiyo, haya ndio majibu kwamba, Chuo cha VETA Manyara, kitafunguliwa Januari, 2012. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza naomba niipongeze Serikali sana kwa kuanzisha huu mtindo wa Sekondari za Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika Sekondari yangu ya Kata ya Mpinji, kuna mtoto mmoja ambaye Serikali imemsomesha kuanzia *Form I* mpaka *Form IV* na akafaulu kwenda *Form V, Division One (I),* akaenda *Ilboru Secondary School.*

Mheshimiwa Spika, Je, Serikali kwa unyenyekevu mkubwa inaweza ikanisaidia kumsaidia huyu mtoto kusomeshwa Chuo Kikuu; kwa sababu, nina uhakika atafaulu tena kwenda Chuo Kikuu?

**SPIKA:** Eeh, hilo swali si ni *private,* jamani! Mheshimiwa Naibu Waziri, hebu jibu. Maana kila mtu akileta majina hapa, yatakuwa mengi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni juzi tu hapa Mheshimiwa Waziri wangu, ametoa vigezo vya vijana kujiunga na Chuo Kikuu, wakiwemo vijana waliopata *Division One.*

Kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa tuonane tuweze kuangalia *criteria* na vigezo vya kijana huyo ili tuweze kuona namna ya kumsaidia. *(Makofi)*

Na. 467

**Ujenzi wa Barabara ya Makutano – Butiama – Mto wa Mbu**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI K.n.y. MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE** aliuliza:-

Ujenzi wa barabara ya Makutano – Butiama – Mto wa Mbu, kwa kiwango cha lami, uliahidiwa na Mheshimiwa Rais na pia kwenye Ilani ya CCM:-

(a) Je, Ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa kilometa 420 utaanza lini?

(b)Je, ni kazi gani inaendelea katika barabara hiyo hivi sasa?

(c)Je, fidia kwa wananchi walioko eneo itakapopita barabara hiyo itaanza kulipwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Makutano – Butiama – Mto wa Mbu, yenye urefu wa Kilometa 420 kwa sehemu za Makutano – Mugumu (Km 117) na Mto wa Mbu – Loliondo (Km 214) Utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu, uandaaji wa nyaraka za zabuni na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi.

(b) Mheshimiwa Spika, kazi zinazoendelea hivi sasa ni kukamilisha usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Aidha, matengenezo ya barabara hiyo yanaendelea kufanyika ili iendelee kupitika wakati wote.

(c) Mheshimiwa Spika, ulipaji wa fidia utafanyika baada ya usanifu kukamilika na fedha za zoezi hilo kupatikana. Hata hivyo, fidia itahusisha tu wananchi wanaostahili kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007. Wale ambao watakuwa wamejenga ndani ya hifadhi ya barabara hawatalipwa fidia.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri. Hata hivyo ningependa kufahamu kwamba, kazi za usanifu na uandaaji wa nyaraka, zinahitaji fedha. Je, fedha zimepatikana kwa kipande hicho cha barabara ya kutoka Butiama – Mto wa Mbu?

Mheshimiwa Spika, la pili ni kwamba, ahadi za Mheshimiwa Rais ya utengenezaji wa barabara kwa kiwango cha lami ni nyingi ikiwepo barabara ile ya kutoka Muheza – Amani. Je, ni

mkakati gani umeandaliwa na Wizara sasa, wa kukamilisha usanifu na uandaaji wa zabuni kwa ajili ya barabara hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Herbert Mntangi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumeshasema kazi ya usanifu inaendelea, kwa hiyo ina maana kwamba, tayari kuna fedha kwa ajili ya usanifu. Tunachosubiri ni ukamilishaji wa usanifu na baada ya pale tunaanza utengenezaji wa nyaraka za zabuni. Na kama tulivyosema, tunajenga barabara hii ya lami, sehemu tu ya ile ambayo haiingii ndani ya Mbuga ya Serengeti.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Muheza – Amani, ili kuwapa wananchi wa Muheza haki yao ya kupata jibu kamilifu; Mheshimiwa Mbunge, tunaomba atuletee hilo swali, tuweze kulijibu kikamilifu. *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona. Naipongeza pia Serikali kwa kuamua kujenga barabara hiyo ya Nata – Mugumu – Loliondo. Na ninaipongeza pia Serikali, kwa kuamua tena kujenga barabara ya Nata – *Fort Ikoma.* Na kwa kuwa, sisi Wabunge wa Mkoa wa Mara, tulishafanya mazungumzo na Waziri Mkuu, kuhusiana na barabara hii ya Nata – *Fort Ikoma Gate,* yenye urefu wa kilometa 47 kuwa *replaced* na barabara ya Mugumu Mjini inayopita Morotonga, inayopita Bwitengi, inayopita Ikoma Lobanda, hadi kufika *Ikoma Gate,* ambako inapita kwenye maeneo ya wananchi na ni kilometa 41 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Je, Wizara sasa iko tayari kutubadilishia barabara hii ya Nata – *Fort Ikoma Gate,* yenye kilometa 47 na kujenga barabara ya Mugumu – *Fort Ikoma Gate,* ambayo inapita maeneo ya watu yenye kilometa 41? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kirigini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ningependa tu nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge, aende kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tuliyoitoa wakati wa hotuba yetu ya Bajeti, ukurasa wa 117. Tumetenga pesa pale tayari kwa ajili ya hiyo barabara ya kuishia *Fort Ikoma.*

Lakini kama tunavyosema mara kwa mara, kupanga ni kuchagua. Mheshimiwa Mbunge, basi pia tujadiliane tuangalie hizo *merits* za hayo mabadiliko badala ya kuyatolea ufafanuzi hapa wakatti wa kujibu maswali. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, amejibu swali vizuri sana. Lakini nataka tu nimjulishe Mheshimiwa Kirigini kwamba, ujenzi wa barabara ya kutoka Makutano – *Fort Ikoma,* katika Bajeti yetu kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, tunaanza na kilometa 50 ambazo zitajengwa katika Bajeti ya mwaka huu 2011/2012.

Lakini utekelezaji wa barabara hizi kuzibadilisha, hatuwezi kubadilisha. Kwa sababu, ni utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi na barabara hizi ambazo zimezungumzwa ziko ukurasa wa 75, ikiwa ni pamoja na barabara ya Makutano – Nata – *Fort Ikoma,* barabara ya Makutano – Nata – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu. Kwa hiyo, hatuwezi kwenda pembeni na hayo.

Tutatekeleza Ilani ya Uchaguzi na bahati nzuri Mheshimiwa Kirigini ni mtekelezaji mzuri wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM). *(Makofi)*

Na. 468

**Kupeleka Umeme Tarafa ya Mlola – Lushoto**

**MHE. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa ahadi nyingi zimetolewa na Serikali pamoja na Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa 2010 kuwa umeme utapelekewa Tarafa ya Mlola Jimbo la Lushoto katika Kata za Mlola, Kwekanga, Malibwi Kilole, Ngwelo na Makanya:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani katika kutekeleza ahadi hiyo?

(b) Je, Serikali inasemaje juu ya ahadi yake ya kutoa umeme kutoka Mlalo kwenda Ngwelo, Kwekanga, Kilole Makole hadi Mlola kwani wananchi wa maeneo hayo wana matumaini makubwa?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, umeme katika Tarafa ya Mlola Jimbo la Lushoto utatoka katika kijiji cha Nyasa inapopita njia ya umeme wa *KV 33* kuelekea Mlalo. Kwa mujibu wa tathmini ya awali iliyofanyika mwezi Oktoba, 2010, mradi huo utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *KV 33* yenye urefu wa kilomita 25.

Uwekaji wa *transfoma* mbili za *KVA 50* kila moja maeneo ya Hemtoe na Masale, uwekaji wa *transfoma 2* za *KVA 100* kila moja maeneo ya Makole na Mlola na uwekaji wa *transfoma* moja ya *KVA 100* kwenye njia panda kwenda Ngwelo.

Gharama za mradi huo zinakadiriwa kufikia shilingi bilioni 1.6. Serikali kupitia wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inafanya jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya ufadhili wa mradi huo.

(b) Mheshimiwa Spika, kutoa umeme Kwemakame ambako kuna umeme kwenda maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge ya Ngwelo, Kwekanga, Kilole, Makole hadi Mlola, kutahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *KV 11* yenye urefu wa kilomita 11, na uwekaji wa *transfoma* mbili zenye ukubwa wa *KVA 100* kila moja kwenye vijiji vya Malibwi na Kwekanga. Gharama za mradi huo zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 694.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu punde fedha zitakapopatikana utekelezaji wa miradi hii itatekelezwa mara moja.

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nafurahi sana kwa majibu mazuri ya Waziri, majibu ya kutia moyo. Kwa kuwa, Waziri wakati anakabidhi Taarifa yake ya Bajeti, walipunguza fedha hata katika matumizi yao kuweka ili ziende *REA.*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa matumaini kwamba, fedha angalao kiasi zimepatikana. Waziri anatamka nini kuwapa moyo wananchi wa Mlola, kupata umeme?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Shekifu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza tunamshukuru kwa kutambua juhudi zinazofanywa na Serikali, lakini pia tunampongeza kwa ufuatiliaji wake wa karibu. Mheshimiwa Shekifu, ni kati ya Waheshimiwa Wabunge, ambao wamekuwa wakiwasiliana na Ofisi yetu mara kwa mara kufuatilia utekelezaji wa miradi yao.

Mheshimiwa Spika, matumaini ninayowapa wananchi wa Jimbo lake Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, na hili ni katika utekelezaji na juhudi za Serikali, pamoja na Majimbo mengine.

Hapa karibuni, Bunge hili Tukufu limeishauri Serikali liongeze vyanzo vya kutunisha mfuko wa Nishati vijijini. Na sasa hivi sisi kiserikali chochote tunachofanya kutoa kwenye vyanzo vingine, na kwa kadri ambavyo mfuko utaongezeka, nina imani uwezekano huo wa kuwa na fedha zaidi

za utekelezaji wa miradi ambayo Mheshimiwa Shekifu anaulizia, utaanza ndani ya kipindi hiki cha mwaka wa fedha, ahsante sana.

**MHE. BRG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuwa matatizo ya umeme katika jimbo la Lushoto yanafanana kabisa na matatizo ya umeme tarafa ya Mtae katika jimbo la Mlalo.

Je, Mheshimiwa Waziri ataeleza nini kwa sababu tatizo la Mtae ni kwamba mradi ulikwishafanyiwa upembuzi yakinifu na bei yake ikajulikana na wananchi wakaambiwa waweke waya kwenye nyumba zao? Nashukuru.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwilizi, kama ifuatavyo. Ni kweli mradi alioutaja Mheshimiwa Mbunge katika maeneo ya Mtae tumeutolea taarifa mara kadhaa kwa kipindi kilichopita na kwa kweli juhudi za Serikali ilikuwa hivyo kwamba uwe umekwishatekelezwa hadi sasa. Changamoto tuliyokuwa nayo ni kutopatikana fedha kwa wakati lakini napenda nimpe matumaini Mheshimiwa Brg. Gen. Hassan Ngwili, kwamba kwa niaba ya Wananchi wake Serikali kama nilivyosema kwa vyanzo ambavyo sasa hivi tunavitanua tuna hakika kwamba ukamilishaji wa mradi huu utafanyika kama ambavyo tumekuwa tukimpa taarifa ahsante sana. *(Makofi)*

Na. 469

**Wananchi wa Mufindi Kufaidika na Mavuno ya Misitu**

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA** aliuliza:-

Serikali ilipoomba ardhi kwa wananchi wa Wilaya ya Mufindi kwa ajili ya kupanda miti iliwaahidi wananchi kuwa watapata ajira ya uhakika na kuokota kuni kwenye msitu huo wa Serikali lakini badala yake wakazi wa vijiji vinavyouzunguka msitu huo wanathaminiwa tu pale wanapojitokeza kuzima moto pindi yatokeapo majanga ya moto ambapo wakati mwingine huchukua hata muda wa mwezi mzima na wanavijiji hao hawalipwi chochote.

Je, ni lini Serikali itatoa umuhimu wa kutoa mgao unaotokana na mavuno ya msitu huo kwa ajili ya watu wa Mufindi hasa wale wanaoishi karibu na msitu huo wa Serikali?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa ni kweli kwamba Shamba la Miti, *Sao Hill* lilianzishwa baada ya Serikali kuwaomba wananchi wa Mufindi kuachia maeneo yao na kwa ridhaa yao waliipa Serikali hekta 135,905 zilizohifadhiwa kwa ajili ya kupanda miti.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijiji vinavyozunguka shamba pamoja na wakazi wa wilaya ya Mufindi wamekuwa wanapata manufaa mengi kwa kuwepo kwa Shamba la Miti la *Sao Hill.* Kwa mfano, kati ya watumishi wa kudumu 356 walioajiriwa, watumishi 207 (58%) ni wenyeji wa Mufindi. Shamba linaajiri vibarua wa kutwa zaidi ya 1000 kwa mwaka kwa ajili ya kufanya kazi mbalimbali mashambani ambao wote hawa ni wenyeji wa Mufindi kutoka katika vijiji vinavyozunguka shamba.

Kwa mwaka wastani wa wanajamii wapatao 30,000 wanapata ajira mbalimbali katika viwanda vya kupasua mbao na kiwanda cha karatasi cha Mgololo na zaidi ya 1000 hufanya shughuli mbalimbali za kuwaptia kipato . Mfano ni kama mama lishe, *viosk* mbalimbali, usafirishaji wa bidhaa ikiwemo mazao ya misitu.

Katika biashara ya mazao ya mbao, wastani wa 62% ya watu wenye vibali vya kuvuna miti na kupasua mbao katika shamba la miti *Sao Hill* ni wenyeji wa wilaya ya Mufindi na kutoka vijiji vinavyozunguka shamba.

Mheshimiwa Spika, katika nyanja ya elimu, wavunaji wa miti wanachangia 0.5% ya mrahaba wanaolipa wanaponunua miti kwa ajili ya kuendeleza elimu katika wilaya ya Mufindi. Fedha hizi zimefunguliwa akaunti ambayo inasimamiwa na Mkuu wa Wilaya ya Mufindi na hadi sasa kiasi cha Sh. 267,803,202.60 zimekusanywa.

Katika miradi wa maendeleo kuanzia mwaka 2010/2011 shamba la miti, *Sao Hill* limetenga sh. 25,000,000/= katika Bajeti yake kwa ajili ya kuchangia uendelezaji wa miradi ya Maendeleo kwa vijiji vinavyozunguka shamba. Mwaka huu 2010/2011, vijiji vya Kitasengwa, Ilhalimba, Itimbo, Nyololo na Mninga vimenufaika na utaratibu huu. Kuhusu mchango wa shamba katika mapato ya wilaya, jumla ya Sh. 1,467,333,703 zimekusanywa kama ushuru ya magongo *(LOG CESS)* kwa kipindi cha miaka mitatu kwa ajili ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mifano hiyo michache niliyoisainisha, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekuwa ikitoa umuhimu wa kutoa mgao unaotokana na mavuno ya shamba hilo kwa ajili ya watu wa Mufindi hasa wale wanaoishi kando kando ya m situ huo wa Serikali.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA**: Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo marefu ya Mheshimiwa Waziri naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza, la kwanza kwa kuwa Serikali ilipewa eneo kubwa katika wilaya Mufindi na kuna baadhi ya maeneo wameshindwa kuyatekeleza. Kwa nini Serikali isirudishe baadhi ya maeneo kwa wananchi wa Mufindi wanapata shida kwa ajili ya kulima na maeneo ya kupanda miti?

(b) Mheshimiwa Spika, mwaka 1979 Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Sweden, walianzisha Chuo cha Misitu pale *Sao Hill,* lakini kitu cha kusikitisha mwaka 2001 Chuo kile kilifungwa na kilikuwa kinawasaidia sana wananchi wa Mufindi. Kwanini Serikali isiamue kukianzisha kile chuo ili wananchi wa wilaya ya Mufindi wapate nafasi ya kusoma na kujiendeleza katika chuo kile?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mgimwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kwanza kwamba eneo lote la shamba kwa sasa halina miti kwa maana ya kwamba hatulitumii lote. Nipende kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba tatizo kubwa ambalo limekuwepo kwa kweli ni fedha kwa ajili ya kuendeleza shamba hilo.

Lakini mahitaji ya mazao ya misitu yanazidi kuongezeka kila mwaka na mpango wa Serikali kupitia Wizara yangu, ni kuendelea kupanua kilimo au upandaji wa miti ili miti iweze kupatikana kwa wingi kwenye nchi yetu na hivyo kwa wananchi wengi kuweza kumudu gharama za mbao. Kuhusu suala la pili la kufufua chuo, sababu kubwa ya kufunga chuo kwa wakati huo ilikuwa ni ukosefu wa fedha baada ya ule ufadhili kuwa umeisha. Kupitia *TFS* ambayo tumeanzisha mwaka huu kama nilivyoliarifu Bunge lako Tukufu, tunakusudia kuanza kuanzisha vyuo vidogo vidogo ambavyo vitasaidia wananchi elimu ya uhitaji. Vilevile kuweza kuwachangia kwenye miradi yao ikiwemo kufufua chuo kama hiki.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kwa kuwa Serikali inatoa asilimia 1 tu ya pato litokanalo na mazao ya misitu kurudi kwenye Halmashauri husika. Kiasi hiki ni kidogo sana hakikidhi mahitaji ndiyo maana wananchi hawanufaiki vizuri na rasilimali hii inayowazunguka.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupandisha asilimia hii kutoka 1 kwenda 20 ili Halmashauri zetu ziweze kunufaika na hivyo ziweze kuwa na uhifadhi endelevu kwenye misitu hiyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Magdalena Sakaya, kama ifuatavyo. Serikali imekuwa ikitoa asilimia 5 siyo asilimia moja. Hata hivyo, asilimia hii 5 haitoshi na wananchi walio wengi wameonyesha *concern* kuhusu swali hili. Tayari tumekwishakuanza kuzungumza na Halmashauri kupitia TAMISEMI ili kuweza kurekebisha kiasi hiki. Kwa hiyo, tutarekebisha kiasi siwezi nikasema tutafikia asilimia ngapi. Lakini kwenye asilimia hizo nilizosema tunaweza tukafika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha na maswali yenyewe yameisha. Tunao wageni katika ukumbi wetu ambao inabidi tuwatambulishe. Kwanza kabisa tunao wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Eng. Gerson Hosea Lwenge, ambao ni familia yake, katika familia yake kuna watu wengi sana pamoja watoto wake wawili, huyu sijui kwanini mke hajaonyeshwa hapa sijui. Naomba familia ya Mheshimiwa Lwenge wasimame walipo. Wako wengi sasa hapa, hajasema habari ya mke wake kuna watoto na majina mengine. Ahsante sana, karibuni sana msindikizeni baba atakavyochangia hapa mambo. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wa Wizara ya Maji, ambao kwanza ni Eng. Christopher Sai, Katibu Mkuu wa Wizara, Eng. Bashiri Mrindoko, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, wajumbe wa Bodi za Mamlaka ya Maji, hakuzitaja wapo hapo, wajumbe wa Bodi zote sijui ni wangapi hao, wasimame hawakutajwa kwa majina. Kuna wafanyakazi wa *TANROAD* wa Wizara kutoka Dodoma hawa wasimame walipo, tukiona barabara mbovu Dodoma tunajua wenyewe wapo. Kuna Wakurugenzi Wasaidizi, watendaji wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara na maafisa kutoka Wizara ya Maji na mara nyingi watakaa katika sehemu yao ya kazi pale.

Tunao wageni wengine waliofika kwa ajili ya mafunzo, Wanafunzo 55 wa shule ya msingi ya Chalula na Mvumi Makulu Dodoma, hawa wasimame mahali walipo pamoja na walimu, ahsanteni sana tunashukuru sana kwa kuja na mjifunze ahsante sana.

Tuna wanafunzi wengine 50 kutoka shule ya msingi Makole Dodoma, hili ni kundi lingine wako wapi wasimame walipo, ahsante sana tunashukuru sana. Pia wananchi wote waliokuja katika ukumbi tunawakaribisha leo ni Wizara ya Maji.

Matangazo ya kazi, kuna Mwenyekiti wa Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya *PAC*, kwamba kutakuwa na Semina inayohusu masuala ya *Public Private Partnership (PPP),* leo tarehe 22 Agosti, 2011 kuanzia saa saba kamili mchana. Semina hii inatolewa na *Parlimentary Centre* ya Canada, na itafanyika katika Ukumbi wa *St. Gaspar.* Hivyo usafiri wa kwenda huko utakuwepo mbele ya lango kuu. Hawa ni saa saba mchana. Wanasema saa saba kamili lakini na robo maana yake hapa ndiyo tunaahirisha kazi. Kwa hiyo, Kamati ya Uchumi na Fedha na Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)*.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi H. Chana, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo tena tarehe 22 Agosti, 2011 Saa saba na robo, kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo katika Ukumbi Na. 219 gorofa ya pili. Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba leo saa saba na robo, watakuwa na kikao chao katika ukumbi wa Msekwa B.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa James Lembeli, anaomba niwatangazie Wabunge wa Kamati yake kwamba watakuwa na kikao saa saba na robo katika Ukumbi wa Msekwa C, kwa hiyo wajumbe wote wahudhurie.

Lakini nina matangazo mengine, Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club,* Mheshimiwa Idd Azzan, anaomba kuwasilisha matokeo ya mchezo wa mpira wa miguu kati ya *Bunge Sports Club* na *Makambako Veteran,* uliochezwa tarehe 20, Jumamosi, kwamba *Bunge Sports Club* wamepata magoli mawili, *Makambako Veteran,* goli moja. Aidha, mchezo huu ulikuwa mzuri na wa kuvutia. Nyota wa mchezo huu alikuwa Mheshimiwa Amos Makalla, kama kawaida yake.

Lakini nachotaka kusema ile Kamati ya ufundi nafikiri inayoongozwa na Waziri Mkuu na Maji Marefu nayo inafanya kazi mmewashinda hata *Makambako Veteran?* Sikutegemea hiyo. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini pia Mheshimiwa Mwenyekiti wa Simba anasema kesho kutwa Alhamisi hao jamaa Simba watakuja hapa Dodoma Bungeni, kwa hiyo mjiandaye. Katibu wa Cocus ya Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Uongozi ya Chama, siyo ile ninayoongoza mimi kuwepo kwa kikao cha Kamati hiyo leo tarehe 22 Agosti, 2011 saa saba na robo mchana katika ukumbi wa Spika. Ni ile Kamati ya Chama siyo ile ya Uongozi ya Wenyeviti wangu. Kwa hiyo, saa saba na robo katika ukumbi wa Spika.

Halafu Katibu wa Wanawake wa Bunge wa CCM, humu Bungeni, huyu ni Mheshimiwa Mary Chatanda, naona alichaguliwa juzi juzi, anaomba niwatangazie Wabunge wanawake wa CCM kuwa watakuwa na kikao leo tarehe 22 Agosti, 2011 ukumbi wa Pius Msekwa saa saba na robo baada ya Kuahirisha Bunge, sijui wale wanaokutana Msekwa B na C ni wapi lakini huyu Katibu anawaambia wanawake wa CCM wote wakakutane kule Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu, Waziri wa Maji bado yuko kwenye matibabu India, kwa hiyo Waziri atakayesoma kwa niaba yake kwa utaratibu wa Serikali kunakuwa na Waziri anayemkaimu Waziri mwenzake atakuwa Mheshimiwa Stephen Wasira, atasaidiwa na Naibu Waziri, naomba ushirikiano wenu kwao.

Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowatangazia leo asubuhi, ule mwili wa Marehemu wetu unatakiwa kuondoka sasa hivi na ningependa kuwa *Dodoma Airport.* Sasa namwomba Mheshimiwa Mwenyekiti Simbachawene aje anisaidie. Ahsanteni sana.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. George B. Simbachawene) Alikali Kiti*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2011/2012 Wizara ya Maji

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge leo tunaendelea na shughuli ya Bajeti na tuna Wizara ya Maji. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa niaba yake naomwona Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU (K.n.y. WAZIRI WA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya, naomba niwasilishe katika Bunge lako Tukufu mpango na makadiri ya mapato na matumizi ya fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2011/2012. Mheshimiwa Waziri wa Maji, Prof. Mark James Mwandosya, yuko nchini India kwa ajili ya matatibabu na leo hii nimeongea naye, kwa hiyo habari za uhakika ni kwamba anaendelea vizuri. *(Makofi)*

Naomba nitumie fursa hii kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumtakia kila la kheri ili apone haraka na hatimaye arejee katika majukumu yake ya ujenzi wa taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Maji kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kwa ushirikiano wa dhati unaoendelea kutoa kwa Wizara yangu.

Naishukuru Kamati kwa maoni na maelekezo iliyoyatoa wakati nilipowasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa mwaka 2010/2011 na mpango wa maendeleo wa Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012.

Ushauri maoni na mapendekezo ya Kamati yamezingatiwa kikamilifu katika kuandaa mpango na bajeti ya Wizara yangu, kwa mwaka 2011/2012. Tutazingatia kikamilifu, ushauri maoni na mapendekezo ya Kamati hiyo katika kutekeleza mpango wa bajeti wa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, kwa kupata ushindi usio na shaka katika uchaguzi mkuu uliofanyika mwezi Oktoba, 2010.

Ushindi huo ni ishara ya imani ya wananchi waliyoanyo kwa Rais, na Makamu wa Rais na kwa Chama cha Mapinduzi CCM. Nakipongeza Chama cha Mapinduzi kwa ushindi huo mkubwa, siyo tu katika uchaguzi wa Rais, bali pia kwa uchaguzi wa Wabunge na Madiwani. Natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Maji.

Wizara inayomgusa kila Mtanzania. Hakuna njia ya kurudisha imani hiyo kubwa isipokuwa kutoa utumishi uliotukuka kwa wananchi wa Tanzania. Naahidi kufanya hivyo kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi, kwa kuteuliwa kwake na Mheshimiwa Rais, na baadaye kuthibitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu.

Kuteuliwa na baadaye kuthibitishwa kwake kuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mara ya pili, ni ishara tosha ya imani aliyo nayo Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wa Tanzania kwa utumishi wake uliotukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha ninampongeza Mheshimiwa Spika Anne Makinda (Mb) kwa kuchaguliwa kwake kuwa Spika wa kwanza Mwanamke na Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Kwanza mwanamke wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hivyo, kuandika historia mpya ya Bunge hili, na Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb) kwa kuchaguliwa na Waheshimiwa Wabunge kuwa Naibu Spika.

Nawapongeza Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama (Mb), Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb) ambaye umekalia kiti sasa, na Mheshimiwa Silvester Massele Mabumba (Mb) kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge hili tukufu. Nawapongeza pia, Makamishna wa Bunge na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa kuchaguliwa kwao na hivyo, kukamilisha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Mhandisi Gerson Hosea Lwenge (Mb) kwa kuteuliwa kwake kuwa Naibu Waziri wa Maji na Mhandisi Bashiri Juma Mrindoko kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara yangu. Kuteuliwa kwao ni ushahidi tosha kwamba walifanya kazi nzuri katika nafasi walizokuwa nazo kabla ya uteuzi huu kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii na hivyo, Mheshimiwa Rais kuwateua kwa imani iliyotokana na uchapaji kazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwa dhati kabisa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, kwa ushirikiano inayoendelea kutoa kwa Wizara yangu. Naishukuru Kamati pia kwa ushauri, maoni na maelekezo iliyoyatoa wakati nilipowasilisha taarifa ya kazi zilizotekelezwa mwaka 2010/2011 na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012. Ushauri, maoni na mapendekezo ya Kamati yamewezesha kuboresha kwa kiwango kikubwa Mpango na Bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012. Tunaiahidi Kamati hiyo kwamba tutazingatia ushauri, maoni na mapendekezo yake katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, nawashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu; Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, Waziri wa Fedha kwa hotuba zao ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa bajeti, uchumi na utekelezaji wa kazi za serikali kwa mwaka 2011/2012. Nawapongeza pia, Mawaziri wenzangu wote walionitangulia kuwasilisha hoja zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelekezo ya ilani ya uchaguzi ya chama cha mapinduzi. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005. Katika Hotuba yangu niliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu mwaka jana, nilielezea kwa kina mafanikio ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kwa Sekta ya Maji kwa kipindi cha kuanzia Desemba 2005 hadi Juni 2010. Wizara yangu iliendelea kusimamia utekelezaji wa malengo ya Sekta na hadi kufikia Desemba 2010 mafanikio yalikuwa kama ifuatavyo:-

Upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika maeneo yavijijini kuongezeka kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005 hadi asilimia 57.8;

Upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama katika miji mikuu ya mikoa 19 imeongezeka kutoka asilimia 78 mwaka 2005 hadi asilimia 86;

Vyombo vya watumiaji maji vilivyoanzishwa na kusajiliwa kisheria viliongezeka kutoka 121 mwaka 2005 hadi 700;

Ujenzi na ukarabati wa mabwawa 16 ya ukubwa wa kati kwa matumizi mbalimbali;Ujenzi na ukamilishaji wa Mradi mkubwa wa kutoa maji Ziwa Victoria kuhudumia miji ya Kahama na Shinyanga, na vijiji 41 vya mikoa ya Mwanza na Shinyanga;

Kuanza utekelezaji wa upanuzi wa Mradi wa Chalinze awamu ya pili unaohusisha usambazaji wa majisafi katika vijiji 48 katika Wilaya za Bagamoyo na Morogoro ambapo hadi kufikia Desemba 2010, utekelezaji ulifikia asilimia 60;

Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya kuboresha huduma ya maji katika Jiji la Dar es Salaam kwa kukarabati na kupanua miundombinu ya majisafi na majitaka;

Kuhamasisha utumiaji wa teknolojia ya kuvuna maji ya mvua kwa kujenga matanki ya mfano 313 na kuzishauri Halmashauri kutunga sheria ndogo kuzitaka taasisi na kaya kuvuna maji ya mvua kutoka kwenye mapaa ya nyumba zao; na

Kupitishwa na kuanza kutumika kwa Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, na Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010. Katika kuhakikisha Sekta ya Maji inachangia lengo la Serikali la kuwapunguzia wananchi umaskini na inachangia zaidi katika Pato la Taifa, Wizara yangu inaongozwa na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 87 ya Ilani hiyo kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kufikia asilimia 75 vijijini na mijini asilimia 95 ifikapo mwaka 2015;

(ii)Kuandaa na kutekeleza mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde yote tisa ya maji kwa kuimarisha uwezo wa Ofisi za Mabonde hayo na Maabara za Maji. Mabonde hayo ni ya Mto Pangani, Rufiji, Wami/Ruvu, Ruvuma, Maziwa ya Victoria, Rukwa, Nyasa na Tanganyika na Bonde la Kati (Mto Bubu, Ziwa Eyasi na Ziwa Manyara);

(iii)Kuendelea kushirikisha kwa ukamilifu nguvu za wananchi katika hatua zote za kutoa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na kupanga, kujenga, kuendesha na kumiliki miradi yenyewe kwa njia ya kueneza Kamati za Maji za Vijiji, sambamba na kuimarisha mifuko ya maji;

(iv)Kuimarisha ushiriki wa Tanzania katika matumizi na usimamizi wa maji shirikishi;

(v)Kuimarisha utunzaji wa vyanzo vya maji na kudhibiti uchafuzi wa mazingira;

(vi)Kuendeleza utekelezaji wa ujenzi wa malambo na mabwawa mapya, kukarabati na kufufua malambo ya zamani ili maji mengi zaidi yaweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo;

(vii)Kutunga sheria itakayoiwezesha Serikali kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji unaongezeka nchini kwa njia ya kila shule, chuo, taasisi, wizara, hoteli, kiwanda, kata, vijiji na mtu binafsi atakayejenga nyumba ya kisasa mjini au kijijini anajenga miundombinu ya kuvuna na kutumia maji ya mvua;

(viii)Kutekeleza mradi mkubwa wa kufikisha maji katika miji ya Igunga, Nzega hadi Tabora kutoka mkoa wa Shinyanga;

(ix)Kuboresha huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa na wilaya kwa kukarabati na kujenga miundombinu ya majisafi na majitaka;

(x)Kuimarisha na, au kukarabati miradi ya kitaifa ya Wanging'ombe, Maswa, Mugango–Kiabakari, Handeni Trunk Main (*HTM*), Chalinze, Makonde na Kahama – Shinyanga ili iwe endelevu;

(xi)Kuhakikisha kwamba kila mamlaka ya maji mjini inadhibiti upotevu wa maji katika eneo lake lote kwa kukagua na kukarabati mara kwa mara miundombinu ya maji ili huduma itolewe kwa gharama nafuu; na

(xii)Kujenga uwezo wa kuhudumia miradi ya maji vijijini kwa kutoa mafunzo ya wataalam na mafundi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira, dhamira na majukumu ya wizara ya maji. Wizara ya Maji kwa mwaka 2011/2012 itaendelea kutekeleza majukumu yake kulingana na Sera ya Maji; Mkakati wa Maendeleo ya Sekta ya Maji; na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (*WSDP*). Kwa kuzingatia sera na mikakati hiyo dira na dhamira ya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Dira: Kuwa na mfumo endelevu wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji utakaoleta manufaa ya kijamii na kiuchumi kwa lengo la kuongeza Pato la Taifa ili kupunguza umaskini.

Dhamira: Kuhakikisha rasilimali za maji zinasimamiwa, zinaendelezwa na zinatumika kwa njia endelevu na shirikishi ili kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali kwa kuweka mfumo madhubuti wa kitaasisi wa kusimamia rasilimali za maji, kuboresha miundombinu ya usambazaji majisafi na uondoaji wa majitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara inazingatia ahadi zilizotolewa na Serikali, malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Malengo ya Milenia, na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Majukumu hayo ni pamoja na:-

(i) Kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera, Mikakati na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;

(ii) Kutayarisha na kusimamia sheria, kanuni na taratibu za kusimamia Sekta ya Maji;

(iii) Kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji;

(iv) Kukusanya, kuchambua, kutafsiri na kuhifadhi takwimu muhimu za Sekta ya Maji;

(v) Kutoa miongozo ya kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji;

(vi) Kutoa miongozo ya utoaji wa huduma za maji na usafi wa mazingira mijini na vijijini;

(vii) Kutoa mafunzo kwa wataalam wa Sekta ya Maji katika ngazi na kada mbalimbali za utekelezaji;

(viii) Kuendeleza tafiti kuhusu teknolojia zinazotumika katika kutoa huduma ya maji; na

(ix) Kuratibu majukumu ya, na kutekeleza ushauri wa Bodi ya Taifa ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya taifa ya maji. Wizara yangu inatekeleza majukumu iliyokasimiwa kulingana na Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 ambayo madhumuni yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuweka mfumo endelevu na shirikishi wa kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji;

(ii) Kuweka misingi madhubuti ya kusimamia rasilimali za maji kwa njia endelevu;

(iii) Kuhakikisha kuwa gharama zote za utoaji huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka mijini zinalipwa na wakazi wa miji husika; na

(iv) Kushirikisha wananchi wa vijijini katika kupanga, kutekeleza, kugharamia na kuendesha miradi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio katika utekelezaji wa Sera hiyo ni pamoja na uanzishaji kisheria na uimarishaji wa taasisi za usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika ngazi za Bodi ya Taifa ya Maji, Bodi za Mabonde ya Maji, Kamati za mabonde madogo ya maji na Vyama vya Watumiaji Maji. Bodi ya Taifa ya Maji ilifanya kikao chake cha kwanza tarehe 26 Mei, 2011.

Kwa upande wa utoaji wa huduma za maji, taasisi za kutoa huduma hiyo zimeendelea kuimarishwa ikiwa ni pamoja na Halmashauri, Mamlaka za maji katika miji mikuu ya mikoa, wilaya na miji midogo na Vyombo vya watumiaji maji. Katika kuzipa nguvu ya kisheria taasisi zinazosimamia na kutoa huduma, Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, na Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira zimepitishwa na zinatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikutano na maadhimisho muhimu. Mkutano wa Kutathmini Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kwa mujibu wa makubaliano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji, Wizara yangu hufanya mkutano wa kutathmini utekelezaji wa Programu hiyo kila mwaka. Kwa kipindi cha mwaka 2010/2011, mkutano wa kujadili matokeo ya tathmini hiyo ulifanyika mwishoni mwa mwezi Septemba 2010. Katika mkutano huo, Serikali iliwakilishwa na Wizara yangu, Wizara ya Fedha na Uchumi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na wadau wengine. Tathmini hiyo ilibaini maeneo muhimu ya utekelezaji:-

(i) Kukamilisha usanifu wa Mfumo wa Kieletroniki wa Menejimenti ya Taarifa na Takwimu za Sekta ya Maji, na kuwapatia mafunzo wataalam waendeshaji ili mfumo huo uwe unajazwa takwimu za kila wiki na kila mwezi kwa ajili ya kuuwezesha ufanye kazi ya kutoa taarifa sahihi za utekelezaji kila robo mwaka, nusu mwaka na taarifa za mwaka;

(ii) Kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa mpango wa kujenga uwezo wa wataalam na uwezo wa kitaasisi wa kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika maeneo yote ya mijini na vijijini;

(iii) Kuanza maandalizi ya awamu ya pili ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itakayotekelezwa kuanzia mwezi Julai 2012 hadi mwezi Juni 2017; kwa kubaini maeneo muhimu yatakayozingatiwa wakati wa awamu hiyo;

(iv) Kuandaa mpango kazi na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi maalum wa programu ya maji uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwezi Agosti 2010, na kusimamia utekelezaji wake;

(v) Kukamilisha mapitio ya mpango kazi wa muda wa kati wa programu na kufanya marekebisho ya vipaumbele na malengo kwa kipindi cha miaka miwili ya 2010/2011 na 2011/2012 kulingana na uwezo wa kifedha wa programu;

(vi) Kuweka utaratibu utakaohakikisha kuwa utoaji wa fedha unazingatia kupatikana kwa taarifa za utekelezaji. Inasisitizwa kuwa taasisi yoyote inayotekeleza programu ya maji itakayoshindwa kuwasilisha taarifa ya utekelezaji haitapatiwa fedha zaidi za utekelezaji;

(vii) Kuboresha uhusiano wa kiutekelezaji kati ya *DAWASA* na *DAWASCO* ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa programu katika Jiji la Dar es Salaam;

(viii) Kuwezesha usajili wa haraka wa vyombo vya jamii vya usimamizi na uendeshaji wa miradi ya maji vijijini na kuvijengea uwezo wa kusimamia kikamilifu miradi hiyo ili kuhakikisha utoaji wa huduma endelevu; na

(ix) Kuziwezesha ofisi za mabonde ya maji kuwa na mikakati ya mawasiliano na wadau ili kuhakikisha wadau katika maeneo yote yaliyo chini ya mabonde wanazielewa Sheria za maji, ambazo ni Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 12 ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikutano ya Kimataifa Kuhusu Majishirikishi. Masuala ya matumizi na usimamizi wa rasilimali za Majishirikishi yanahitaji maelewano baina ya nchi husika. Ili kufikia azma hii, mikutano ya pamoja ni muhimu katika kuendeleza rasilimali hizo. Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2010/2011 ilishiriki mikutano ifuatayo:-

(i) Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Maji kutoka nchi za Tanzania na Malawi kuhusu programu ya maendeleo ya bonde la Mto Songwe uliofanyika katika jiji la Mzuzu, Malawi mwezi Machi 2011. Wakati wa mkutano huo nchi zetu zilisaini hati ya makubaliano ya ushirikiano ambayo ilihusu utekelezaji wa awamu ya pili ya miradi itakayohusisha usanifu wa kina na maandalizi ya awamu ya tatu;

(ii) Mkutano wa nane wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Bonde la Ziwa Victoria ulifanyika Mjini Kisumu, Kenya mwezi Januari 2011. Lengo lilikuwa kupokea taarifa za utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotekelezwa chini ya uratibu wa Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, kujadili na kutoa maelekezo. Pamoja na miradi mbalimbali iliyojadiliwa na kufanyiwa maamuzi, Sekretarieti ya Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria iliagizwa na Baraza kushirikiana na nchi za Kenya na Tanzania kutoa msaada wa kitaalam pamoja na ushauri wa namna ya kutunza na kuendeleza Ikolojia ya Ziwa Chala, Jipe na Mto Umba;

(iii) Ujumbe wa Serikali ulifanya ziara nchini DRC mwezi Agosti 2010 kuwasilisha ujumbe wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Rais wa DRC kuhusu mapendekezo ya namna ya kushughulikia suala la kushuka kwa kina cha maji cha Ziwa Tanganyika. Mawasiliano yanaendelea; na

(iv) Mkutano wa 14 wa Baraza la Mawaziri wa Nchi za Maziwa Makuu katika Bonde la Mto Nile (*NELCOM*) ulifanyika Entebbe, Uganda mwezi Desemba, 2010 ili kujadili utekelezaji wa kazi za Sekretarieti (*NELSAP*) na miradi ya ushirikiano katika Bonde hilo.

Pamoja na kuridhishwa na hatua zilizofikiwa, Baraza liliiagiza Sekretarieti kuharakisha utekelezaji wa mradi wa umeme wa maporomoko ya Rusumo na kushughulikia tatizo la magugu *"feverfew"* lililojitokeza katika Bonde la Mto Mara. Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria imeanza kutafiti chanzo cha magugu hayo kwa lengo la kukabiliana nayo na kuzuia uharibifu wa uoto mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maadhimisho ya Wiki ya Maji kila mwaka nchi yetu huadhimisha Wiki ya Maji kuanzia tarehe 16 hadi 22 Machi, ambayo ndiyo kilele na Siku ya Maji Duniani. Maadhimisho hufanyika katika ngazi za kijiji, wilaya, mkoa na kitaifa.

Madhumuni ya maadhimisho ya Wiki ya Maji ni kutoa fursa kwa wadau wa sekta ya maji kushiriki kwa pamoja katika kuelimisha na kuhamasisha utekelezaji wa Sera ya Maji, mikakati na mipango ya maendeleo ya sekta, ikiwa ni pamoja na kupima mafanikio na changamoto zilizopo. Maadhimisho hayo huhusisha uendeshaji wa warsha, mafunzo, semina na maonesho ya vifaa, teknolojia na huduma za maji. Maadhimisho hutumika kuhamasisha wananchi kushiriki katika kupanga, kujenga, kusimamia na kuendeleza miradi ya maji na kutunza vyanzo vya maji na mazingira ikiwa ni pamoja na kuweka mawe ya msingi na kuzindua miradi ya maji. Kila mwaka, Maadhimisho huambatana na kaulimbiu inayoweka msisitizo kwenye suala maalum lililochaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu, 2011, Maadhimisho ya 23 ya Wiki ya Maji yalifanyika kitaifa mkoani Mwanza. Kaulimbiu ya Maadhimisho hayo ilikuwa: Maji kwa Ajili ya Miji: Kukabiliana na Changamoto za Maji Mijini. Changamoto hizo ni pamoja na ongezeko kubwa la watu mijini kupita uwezo wa miundombinu ya huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka, ukuaji wa miji usiozingatia mipangomiji na gharama kubwa za uwekezaji na uendeshaji wa huduma za majisafi na majitaka mijini. Athari zake ni kuzidiwa uwezo wa vyanzo vya maji kutokana na mahitaji makubwa kupita kiasi na uchafuzi wa vyanzo vya maji na mazingira unaosababisha magonjwa mbalimbali. Mheshimiwa Dk. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mgeni Rasmi kwenye kilele cha Maadhimisho hayo.

Miradi iliyozinduliwa wakati wa kilele cha Maadhimisho ya kitaifa ni Mradi wa Majitaka wa Jiji la Mwanza na Mradi wa Maji Vijijini kwa mikoa ya Mwanza na Mara sawia. Mheshimiwa Makamu wa Rais alitumia fursa hiyo kuelekeza kwamba tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Serikali wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji ifanyike mwaka huu, ukiwa ni mwaka wa tano tangu Mkakati huo ulipotangazwa rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako tukufu, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dk. Mohamed Gharib Bilal kwa kukubali kuwa mgeni rasmi. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wote walioshiriki katika maadhimisho hayo. Nawashukuru viongozi wote kuanzia ngazi ya kijiji, wilaya hadi mkoa kwa kuratibu na kusimamia vizuri maadhimisho hayo. Nawashukuru kipekee viongozi wa mkoa wa Mwanza, wananchi na washiriki wote wa maonesho yaliyofanyika kwa wiki nzima katika uwanja wa Nyamagana, Mwanza. Mwisho, napenda kuwapongeza sana washindi wote waliotunukiwa zawadi katika maonesho ya mwaka huu na kuwaomba wananchi wengi zaidi washiriki mwaka ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya sekta ya maji. Rasilimali za Maji. Nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali nyingi za maji ingawa rasilimali hizo hazipatikani kwa uwiano ulio sawa katika maeneo yote. Rasilimali za maji zilizopo ni pamoja na maziwa makuu ya Victoria, Nyasa, Rukwa na Tanganyika na mito ya Rufiji, Kilombero, Ruvuma, Ruhuhu, Malagarasi, Pangani, Ruvu, Wami, Mara na Kagera. Rasilimali hizo zinakadiriwa kuwa kilomita za ujazo 89. Nchi yetu inakadiriwa kuwa na hifadhi ya rasilimali za maji chini ya ardhi zipatazo kilomita za ujazo 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa na rasilimali nyingi za maji, maeneo mengi ya nchi yetu yameendelea kuwa na uhaba wa maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali. Uhaba

huo unasababishwa na mabadiliko ya tabianchi ambayo kwa kiwango kikubwa yameathiri mwenendo na upatikanaji wa mvua za kutosha na vipindi virefu vya ukame.

Kutokana na tathmini iliyofanywa sehemu mbalimbali duniani, katika miaka 200 iliyopita, kumekuwepo na ongezeko la joto la wastani wa nyuzi joto 0.7 sentigredi ikiambatana na uhaba wa mvua na kupungua kwa kina cha maji katika maziwa na mabwawa.

Tathmini hiyo pia, inaonyesha kwamba kati ya miaka 50 hadi 100 ijayo kutakuwa na ongezeko la joto la wastani wa nyuzi joto moja hadi tatu katika nchi yetu. Sababu nyingine ni pamoja na gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu ya kuhifadhi rasilimali za maji; matumizi ya maji yasiyozingatia ufanisi; uchafuzi wa vyanzo vya maji unaosababishwa na shughuli za kibinadamu kwenye vyanzo; na kasi kubwa ya ongezeko la watu linalochangia kuwa na mahitaji makubwa ya matumizi ya maji kwa shughuli za kiuchumi na kijamii, na makazi na shughuli mbalimbali zinazohitaji maji kuanzishwa mbali na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa pamoja na nchi yetu kuwa na maji mengi kwa sasa, mahitaji ya maji nchini yanaongezeka na hivyo kiwango cha maji yaliyopo kwa mtu kwa mwaka kimeendelea kupungua kutoka wastani wa mita za ujazo 2,700 mwaka 1999 hadi kufikia mita za ujazo 2,080 mwaka 2011. Inakadiriwa kuwa kiwango cha maji kwa mtu kwa mwaka kitaendelea kushuka hadi kufikia mita za ujazo 1,950 ifikapo mwaka 2015 na mita za ujazo 1,500 ifikapo mwaka 2025. Kiwango hicho kikifikiwa nchi inatambulika kama yenye uhaba wa maji *(water stress).* Serikali itaendelea kuhakikisha rasilimali hizo zinatunzwa na kuendelezwa kwa njia endelevu kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo kwa kuzingatia mfumo wa mabonde ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Maji Vijijini. Serikali imeendelea kuboresha huduma za maji vijijini. Uboreshaji huo ulihusu ujenzi wa miradi mipya, upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya maji vijijini ikiwa ni pamoja na kujenga visima virefu na vifupi na kujenga mabwawa katika maeneo kame. Wizara imetekeleza hayo kwa kushirikisha wananchi katika hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kupanga, kusanifu, kujenga, kusimamia na kuendesha miradi ya maji. Upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama umepanda kutoka asilimia 53.7 mwaka 2005 hadi asilimia 57.8 ilipofika Desemba 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Maji Mijini. ili kuboresha huduma za majisafi na uondoaji majitaka mijini, Serikali kupitia Mamlaka za maji mijini imeendelea na ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miundombinu ya majisafi katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya maji ya kitaifa. Kama ilivyoelezwa awali, kutokana na juhudi hizo, upatikanaji wa huduma ya maji katika miji mikuu ya mikoa 19 umeongezeka kutoka wastani wa asilimia 78 mwaka 2005 hadi kufikia asilimia 86 mwezi Desemba 2010. Utoaji wa huduma ya maji kwa sasa katika miji mikuu ya wilaya, miji midogo na maeneo yanayohudumiwa na miradi ya kitaifa ni wastani wa asilimia 53.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo inayohudumiwa na *DAWASCO*, kiwango cha utoaji wa huduma ya majisafi ni asilimia 55 kwa wastani wa saa 9 kwa siku. Kiwango hicho ni kidogo ikilinganishwa na miji mingine kutokana na kukua kwa kasi kwa Jiji la Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la watu ambalo linakadiriwa kuwa asilimia 6 kwa mwaka, tofauti na wastani wa asilimia 4.5 mijini kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2010/2011 na mpango wa mwaka 2011/2012. Sehemu hii inahusu utekelezaji wa mpango wa mwaka 2010/2011 na malengo ya mwaka 2011/2012 katika maeneo ya rasilimali za maji, huduma ya maji na usafi wa mazingira vijijini, huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka mijini, na masuala mengine mtambuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rasilimali za Maji. Wizara yangu iliendelea kuimarisha usimamizi wa rasilimali za maji kwa madhumuni ya kuhakikisha rasilimali hizo, katika kila bonde la maji, zinatumika kwa uwiano kwa sekta zote na kwa njia endelevu. Miongoni mwa hatua zilizochukuliwa ni: kuchunguza na kutathmini rasilimali za maji nchini; kuimarisha ufuatiliaji wa rasilimali za maji; kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji ili zisimamie kikamilifu rasilimali hizo; kuandaa mipango

shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Mabonde ya Maji; na kuweka misingi ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya kipaumbele ya kuhifadhi rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa Programu ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji kwa kutekeleza kazi katika maeneo yafuatayo: ufuatiliaji wa mwenendo wa rasilimali za maji, utafutaji wa vyanzo vipya vya maji na uchimbaji wa visima, matumizi bora ya rasilimali za maji, utayarishaji wa mipango shirikishi ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji, kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji, kukusanya maduhuli, kudhibiti migogoro baina ya watumia maji, uhifadhi wa vyanzo vya maji na mazingira, na usimamizi wa rasilimali za majishirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ufuatiliaji wa mwenendo wa rasilimali za maji. Wizara yangu huchunguza wingi na ubora wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa kutumia mtandao wa vituo vya kufuatilia mwenendo wa rasilimali hizo. Takwimu na taarifa zinazopatikana kutoka vituo hivyo huchambuliwa, na matokeo yake huiwezesha Serikali kuchukua hatua za tahadhari dhidi ya majanga ya ukame na mafuriko na pia hutumika katika kubuni, kusanifu na kujenga miradi mbalimbali ikiwemo ya maji. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kununua vifaa vya kukusanya takwimu na taarifa hizo. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu imenunua jumla ya vifaa 517 vya kupimia maji *(Acoustic doppler profile instruments for discharge measurement, Land surveying and mapping equipment, Current meters and suspension equipment, Water quality analysis kit, and Groundwater surveying equipment)* kwa ajili ya Ofisi za Mabonde ya Maji. Wizara imekamilisha mafunzo kwa watumishi 78 watakaotumika katika ujenzi na ukarabati wa vituo vipya 292 pamoja na ukusanyaji wa takwimu za rasilimali za maji katika Mabonde. Pia, Wizara yangu imeendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo 70 vya kupima wingi wa maji katika mito na mabwawa katika Mabonde ya Pangani (13), Ruvuma (7), Ziwa Rukwa (18), Ziwa Tanganyika (20), Ziwa Victoria (9) na Bonde la Kati (3). Wizara ilikagua vituo 11 vilivyojengwa chini ya mradi wa *Southern African Development Community – Hydrological Cycle Observing System (SADC - HYCOS)* ili kuhakikisha vinaendelea kutoa takwimu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuimarisha mtandao wa kufuatilia mwenendo wa rasilimali za maji juu na chini ya ardhi kwa kujenga na kukarabati vituo, ikiwa ni pamoja na kufunga vifaa vya kupimia wingi na ubora wa maji na kukusanya takwimu za rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utafutaji wa vyanzo vipya vya maji na usimamizi wa uchimbaji wa visima. Maji chini ya ardhi ni chanzo cha uhakika cha kuwapatia wananchi maji, hasa katika maeneo kame. Ili kuboresha huduma za maji nchini, Wizara yangu kupitia Ofisi za Mabonde ya Maji, katika mwaka 2010/2011, iliendelea na utafiti wa kubaini maeneo yanayofaa kuchimba visima vya maji. Maeneo yaliyobainishwa ni 733 kama ifuatavyo:- Bonde la Pangani (120), Bonde la Wami/Ruvu (70), Bonde la Rufiji (42), Bonde la Ruvuma (33), Bonde la Kati (142), Bonde la Ziwa Rukwa (120), Bonde la Ziwa Nyasa (50), Bonde la Ziwa Tanganyika (52) na Bonde la Ziwa Victoria (104). Katika mwaka 2011/2012 Wizara itachunguza maeneo 820 ili kubaini maeneo zaidi yanayofaa kuchimba visima virefu vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uchimbaji wa visima vya maji unaotekelezwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na kampuni binafsi. Lengo la uratibu huo ni kuhakikisha kwamba taratibu za kitaalam zilizowekwa zinafuatwa ili kudhibiti uchimbaji holela wa visima unaoweza kusababisha athari za kiafya na uharibifu wa mazingira. Kwa mwaka 2010/2011 Wizara ilihakiki uchimbaji na kusajili visima 962. Kati ya visima hivyo, 236 vilichimbwa na Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa na 726 vilichimbwa na kampuni binafsi kama inavyooneshwa katika Jedwali Na. 1 na 2. Kampuni binafsi 7 za uchimbaji wa visima zilisajiliwa.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuratibu uchimbaji wa visima vya maji kwa kuimarisha usimamizi na udhibiti kupitia Ofisi za Mabonde ya Maji. Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu taratibu za kufuatwa katika uchimbaji wa visima, ikiwa ni pamoja na kuwa na hati za haki ya kutumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha huduma ya maji safi na salama kwenye maeneo kame, katika mwaka 2009/2010, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Misri ilikamilisha uchimbaji wa visima 39 ambapo visima 30 vilikuwa na maji. Katika hotuba yangu ya Bajeti ya mwaka jana, nilieleza kuwa Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Misri ingechimba jumla ya visima 70 katika maeneo kame ya Shishiyu, Mwabulimbu, Mwang'honoli, Kadoto, Mwamanege, Mwabomba na Sangamwalugesha (Maswa); Sunzula, Kabale, Lagangabilili, Gambasingu, Mwanunui, Nanga, Bumela, Nkoma, Laini, Kilulu, Nkololo, Kidinda (Bariadi); Lutale, Kitumba, Shighala, Ng'hanya, Mwamigongwa, Lwangwe, Mwakiloba, Mwamgoba, Badugu na Kinango (Magu); Nyasincha na Kibaso (Tarime); Minigo, Omoche, Nyamasanda na Nyambori (Rorya); Karukekere, Buzimbwe, Buguma, Nyangere, Kitaramanka, Nyang'aranga, na Marambeka (Bunda); Namelock, Ilera, Chapakazi, Kijungu, Loitepasi, Dongo, Engongangare na Katikati (Kiteto); Mwembe, Makanya, Mgwasi, Same mjini, Mvure, Kongei na Mheza (Same); na Mwanga mjini (Mwanga). Kazi hiyo haikufanyika mwaka 2010/2011 kutokana na kutokamilika kwa taratibu za ununuzi kwa upande wa Serikali ya Misri. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itafuatilia kwa karibu ili kuhakikisha mpango huo unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi bora ya rasilimali za maji. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kusimamia matumizi bora ya rasilimali za maji kwa kutoa vibali vya kutumia maji 205. Lengo ni kuimarisha matumizi endelevu na kuhakikisha kuwa rasilimali za maji zinagawanywa kwa uwiano kulingana na mahitaji ya sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Jumla ya matoleo 121 yalikaguliwa kulingana na masharti ya vibali vya kutumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia Ofisi na Bodi za Mabonde ya Maji itaendelea kutoa elimu kwa wadau juu ya umuhimu wa kuwa na vibali vya kutumia maji na kuendelea kubaini matoleo mengine zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ina jukumu la kudhibiti ujenzi na kusimamia usalama wa mabwawa nchini. Tathmini ya mabwawa yaliyopo nchini imefanyika kwa mabonde saba ya Pangani, Wami/Ruvu, Bonde la Kati, Ruvuma na Pwani ya Kusini, Rufiji, Ziwa Tanganyika na Ziwa Victoria na kubaini jumla ya mabwawa 639 yaliyo katika hali mbalimbali. Kanuni na miongozo inayobainisha viwango stahili vya usanifu na mambo muhimu ya kuzingatia katika ujenzi wa mabwawa zinatayarishwa. Hatua hii inalenga kuhakikisha ubora unaolingana na thamani ya fedha zinazolipwa kwa wakandarasi katika ujenzi wa mabwawa nchini ili yadumu na kuwa endelevu. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kukamilisha utayarishaji wa kanuni hizo na kuendelea kubaini mabwawa na hali yake katika Mabonde ya Ziwa Nyasa na Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imechukua hatua za awali za utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Farkwa katika Bonde la Kati ambalo likikamilika litakuwa chanzo kipya cha maji kwa mji wa Dodoma. Wizara pia itaanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa bwawa la Ndembera katika Bonde la Rufiji litakalotumika kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na kuzalisha umeme. Mabwawa haya ni kati ya miradi mikubwa ya kipaumbele inayokusudiwa kutekelezwa nchini. Kazi ya kuwapata wataalam washauri watakaofanya tathmini ya athari za kimazingira na kijamii inaendelea. Katika mwaka 2011/2012, Serikali itakamilisha tathmini za kimazingira na kijamii ili ujenzi wa miradi hiyo uanze mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uvunaji wa maji ya mvua. Wizara yangu imeendelea kuhamasisha wananchi na kutoa elimu juu ya uvunaji wa maji ya mvua kupitia matamasha mbalimbali ikiwa ni pamoja na maadhimisho ya Wiki ya Maji, maadhimisho ya Wiki ya Usafi wa Mazingira, maonesho ya Saba Saba, na Nanenane, na Wiki ya Utumishi wa Umma. Katika jitihada za kueneza teknolojia ya uvunaji wa maji ya mvua, Halmashauri zimetakiwa zitunge sheria ndogo zinazolazimisha michoro yote ya nyumba za kisasa mijini na vijijini ihusishe miundombinu ya kuvuna maji ya mvua kupitia mapaa ya nyumba kabla ya michoro hiyo kuidhinishwa kwa ajili ya ujenzi. Nachukua fursa hii kuzihimiza Halmashauri zote nchini kutunga sheria hizo ndogo na kuzisimamia.

Pia, katika kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, wataalam washauri watasaidia Halmashauri kujenga matanki matatu ya mfano kwa kila Halmashauri na kutoa mafunzo kwa mafundi 2 katika kila kijiji, na kutoa elimu ya uvunaji wa maji ya mvua kwa kutumia mapaa ya nyumba katika vijiji vyote 10 vya Programu katika kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utayarishaji wa mipango shirikishi ya kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kutayarisha mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji kwa lengo la kuweka taratibu endelevu za matumizi ya maji katika mabonde. Kazi zinazofanyika ni pamoja na kutathmini wingi na ubora wa rasilimali za maji, kuainisha mahitaji ya maji ya sekta mbalimbali ili kuepusha migogoro, na kusimamia na kuendeleza rasilimali za maji katika njia endelevu. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu mwaka jana, Wizara yangu itatayarisha mipango hiyo katika makundi matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la kwanza linahusu Bonde la Rufiji na Bonde la Kati. Katika Bonde la Rufiji, baada ya taarifa ya awali ya Mpango kukubaliwa na wadau, sasa utayarishaji wa mpango wenyewe unaendelea. Kwa upande wa Bonde la Kati, mtaalam mshauri anafanya tathmini ya hali ya maji katika mabonde madogo ya maji ya Namanga, Olduvai na Monduli. Kundi la pili linahusu Bonde la Ziwa Victoria na Bonde la Wami/Ruvu.

Wizara kwa kushirikiana na Kamisheni ya Ziwa Victoria inaendelea na taratibu za kumpata mtaalam mshauri atakayetayarisha Mpango kwa Bonde la Ziwa Victoria. Kwa upande wa Bonde la Wami/Ruvu, baada ya taarifa ya awali ya Mpango kukubaliwa na wadau, sasa utayarishaji wa Mpango wenyewe unaendelea kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (*JICA)*. Kundi la tatu linahusu Mabonde ya Pangani, Ruvuma, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa.

Kwa Bonde la Pangani, utekelezaji unafanyika kupitia Shirika la Kimataifa la Umoja wa Kuhifadhi Rasilimali Asilia (*International Union for the Conservation of Nature -IUCN)* ambapo tathmini ya awali ya rasilimali za maji chini ya ardhi imefanyika kama sehemu ya utayarishaji wa Mpango shirikishi wa Bonde hilo la maji; na kwa mabonde mengine ya maji utaratibu wa kuwapata wataalam washauri unaendelea. *(Makofi)*

Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itakamilisha Mipango shirikishi kwa Bonde la Rufiji na Bonde la Kati, mabonde ya maji yaliyo katika kundi la kwanza, na Bonde la Wami/Ruvu lililo katika kundi la pili. Wizara pia, itaanza utayarishaji wa Mipango hiyo katika Bonde la Ziwa Victoria lililo katika kundi la pili na Mabonde yote yaliyo katika kundi la tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu imeendelea kuimarisha Ofisi na Bodi za Mabonde ya Maji kwa kuzijengea uwezo ili ziweze kuchangia kukua kwa sekta ya maji. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi; kuajiri watumishi wapya katika fani za haidrolojia, haidrojiolojia na uhandisi mazingira; ujenzi wa ofisi na ununuzi wa vitendea kazi kama ifuatavyo:-

(a)Wataalam 206 walipatiwa mafunzo katika fani za uandaaji wa mipango shirikishi ya usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji, matumizi ya taarifa za kijiografia kwa kutumia mfumo wa kompyuta, usimamizi wa benki ya takwimu, usuluhishi wa migogoro katika matumizi ya maji na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, sheria za kazi, usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, sheria mpya ya usimamizi wa rasilimali za maji, na matumizi ya programu mbalimbali za kompyuta. Elimu hiyo ilitolewa kwa wataalam katika mabonde ya Pangani (63), Ziwa Nyasa (33), Ruvuma (34), Ziwa Rukwa (21), Rufiji (36), Ziwa Tanganyika (5), Wami/Ruvu (11), na Bonde la Kati (3).

(b)Kukamilika kwa usanifu wa majengo ya ofisi na maabara za maji katika Mabonde yote tisa ya maji na kuanza ujenzi wa Ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa. Ujenzi wa jengo la ofisi ya Bonde la Ziwa Nyasa umefikia asilimia 40. Ofisi hiyo itakapokamilika itatoa msukumo katika usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi hasa katika uratibu wa mradi wa pamoja wa uendelezaji wa Bonde la Mto Zambezi ambalo tunashirikiana na nchi za Zambia, Zimbabwe, Malawi, Msumbiji, Botswana, Namibia na Angola.

Kazi za ukarabati zimekamilika katika ofisi za bwawa la Nyumba ya Mungu katika Bonde la Pangani na vyumba viwili vya ofisi katika Bonde la Maji la Mto Ruvuma zilizopo Mtwara.

Kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuziimarisha Ofisi za Mabonde ya Maji kwa kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Mabonde na Maabara za maji, kuzipatia wataalam, vitendea kazi na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji unaolenga kupunguza migogoro baina ya watumiaji maji, na kuongeza ukusanyaji wa ada za matumizi ya maji. Hatua zilizochukuliwa ni kubaini makundi ya watumiaji maji katika vidakio maji ili kuanzisha kamati za mabonde madogo ya maji za kusimamia matumizi ya maji *(sub-catchment committees)* na vyama vya watumiaji maji *(water users associations)* kwenye Mabonde yote ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu iliendelea na zoezi la kutambua vyanzo vipya vya maji katika Mabonde ya maji vikiwemo mito, vijito, chemichemi na visima. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya vyanzo 26 vilitambuliwa katika Mabonde ya Pangani (5), Wami/Ruvu (2), Rufiji (3), Ruvuma (2), Ziwa Nyasa (2), Bonde la Kati (4), Ziwa Rukwa (3), Ziwa Tanganyika (2) na Ziwa Victoria (3). Mabonde madogo ya maji 86 yametambuliwa katika mabonde ya Pangani, Wami/Ruvu , Rufiji , Ruvuma , Ziwa Nyasa , Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika, na Ziwa Victoria ili yasimamie kikamilifu rasilimali za maji zilizopo katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya kupitia timu za uwezeshaji (*catchment and district facilitation teams*) iliendelea kutoa elimu ya uundaji wa vikundi vya watumia maji, pamoja na vyama vya watumia maji, katika Mabonde ya maji ya Rufiji, Wami/Ruvu na Ziwa Nyasa.

Jumla ya vyama vya watumiaji maji *(Water Users Associations)* 11 vimeundwa kwenye Mabonde ya Pangani (6), Ziwa Nyasa (1), Ziwa Rukwa (1), Ruvuma (2), na Bonde la Kati (1) ili kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji unaolenga kupunguza migogoro baina ya watumia maji na kurahisisha ukusanyaji wa ada za matumizi ya maji. Jumla ya vikundi vya watumia maji 20 vilianzishwa katika Bonde la Ruvuma (16) na Tanganyika (4). Vyama 11 vya watumiaji maji, viliimarishwa kwa kupewa mafunzo juu ya Sheria Na. 11 ya 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji katika Mabonde ya Rufiji (3), Wami Ruvu (2), na Pangani (6).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara itaanzisha timu 10 za kutoa elimu katika ngazi za Wilaya na Mabonde madogo ya maji na kuimarisha nyingine 23 zilizopo. Ofisi za Mabonde ya maji zitaanzisha na kuimarisha vikundi na vyama vya watumiaji maji katika Mabonde yote tisa ya maji ikiwa ni pamoja na kuvisajili kulingana na Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Wizara itaendelea kubaini maeneo yanayofaa kutengwa ili kuyakinga dhidi ya uchafuzi wa mazingira na kutoa elimu ya kusaidia uanzishwaji wa kamati za mabonde madogo ya maji, vikundi na jumuiya za watumiaji maji katika Mabonde yote ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makusanyo ya Maduhuli. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kuzihimiza Bodi za Mabonde ya maji kuweka mikakati ya kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli kutoka kwa watumia maji na kuyatumia mapato hayo kwa malengo yaliyokusudiwa kulingana na taratibu zinazotawala matumizi ya fedha za umma. Lengo ni kuziwezesha Ofisi za Mabonde ya Maji kujitegemea katika uendeshaji. Makusanyo ya maduhuli hadi kufikia tarehe 31 Mei 2011, yalikuwa jumla ya shilingi 863,818,511 sawa na asilimia 72 ya lengo la shilingi 1,198,390,517. Katika mwaka 2011/2012, Ofisi za Mabonde ya Maji zinakadiria kukusanya kiasi cha shilingi 1,181,000,000 kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 3. Kwa kuwa ofisi za mabonde ya maji sasa zimepata watumishi zaidi na vitendea kazi hasa usafiri, kasi ya kuwatambua watumiaji maji na kuanzisha vyama vya watumiaji maji itaongezeka na hivyo, kuongeza maduhuli ya Mabonde ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kudhibiti Migogoro baina ya Watumiaji Maji. Mwaka 2010/2011, Wizara yangu ilishughulikia migogoro 21 kutoka Ofisi za Mabonde ya Pangani (11), Wami/Ruvu (2) na Bonde la Kati (6), Ziwa Nyasa (1), Rufiji (1). Kati ya migogoro hiyo, 17 ilisuluhishwa. Ili kupunguza migogoro hiyo, Ofisi za Mabonde ya Maji zimeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kuunda kamati za pamoja za kusuluhisha migogoro katika maeneo yao, kuhamasisha uundaji wa vyama vya watumiaji maji na pale inapobidi, kutumia vyombo vya kisheria. Katika mwaka

2011/2012, Serikali kwa kushirikiana na Bodi za Mabonde ya Maji itaendelea kusuluhisha migogoro ya watumiaji maji kadri inavyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uhifadhi wa Mazingira na Vyanzo vya Maji. Kama ilivyo kwa miradi mingine, miradi ya maji inalazimika kufanyiwa tathmini ya athari za kimazingira katika hatua mbalimbali za utekelezaji wake kama inavyoelekezwa na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004. Katika mwaka 2010/2011, miradi mikubwa 26 imefanyiwa uchunguzi wa awali na kubaini kuwa miradi 9 itahitaji kufanyiwa tathmini ya kina ya athari ya mazingira, ili kuchukua tahadhari zinazopaswa katika ujenzi na uendelezaji wake. Miradi 17 ilibainika kuwa haihitaji tathmini ya kina, bali kuchukua tahadhari za msingi. Tathmini ya athari kwa mazingira ya miradi ya uchimbaji wa visima vya Kimbiji na Mpera na ujenzi wa bomba kuu la maji kutoka Ruvu Chini ambayo itatumika kuongeza maji katika Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo, imekamilika. Wizara yangu itazingatia mapendekezo yanayotokana na tathmini hizo wakati wa ujenzi na uendeshaji wake. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kufanya tathmini hizo kwa miradi inayostahili ili kukabiliana na athari za kimazingira na kijamii zitakazobainika. Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa mabwawa ya Kidunda, Farkwa na Ndembera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Udhibiti wa Uchafuzi wa Vyanzo vya Maji. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira (*NEMC*), inatekeleza mikakati ya kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji na kudhibiti uchafuzi unaotokana na matumizi ya maji katika kilimo, viwanda na majumbani. Jumla ya wataalam 21 walihudhuria mafunzo maalum ya ukaguzi wa mazingira ili kujifunza namna ya kukagua uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kudhibiti uchafuzi wa vyanzo vya maji, Wizara yangu kwa kupitia ofisi za mabonde ya maji imekagua jumla ya viwanda 16 na migodi sita na kutoa maelekezo ya kuboresha miundombinu ya majitaka. Wizara yangu ilifanya ukaguzi mara nne katika mgodi wa dhahabu wa *North Mara* uliopo katika Bonde la Ziwa Victoria na mara moja katika migodi ya dhahabu ya *Resolute Golden Pride* uliopo katika Bonde la Kati, *Tulawaka* uliopo katika Bonde la Tanganyika na *Epoch* uliopo katika Bonde la Ziwa Rukwa. Migodi mingine ya shaba na *bauxite* iliyopo katika Bonde la Pangani nayo ilikaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sampuli 20 za majitaka kutoka migodi ya dhahabu ya *North Mara* (9) na *Resolute Golden Pride* (11) zilifanyiwa uchunguzi wa viwango vya ubora wa maji. Uchunguzi huo umebaini kuwa viwango vya madini ya chuma na chumvichumvi aina ya *sulphate* vilivyo katika chemchemi zilizo pembezoni mwa bwawa la majitaka katika mgodi wa Resolute, ni vikubwa kuliko vinavyokubalika. Hii inaashiria kuwa kuna uvujaji kutoka katika bwawa. Kwa upande wa mgodi wa *North Mara*, uvujaji umedhibitiwa kabisa kwani vipimo vya kemikali kwenye sampuli za maji zinazokusanywa kila wiki vinaonesha kuwa hali imerudia kawaida. Migodi hiyo imepewa maelekezo ya kudhibiti uchafuzi huo kwa kuzuia uvujaji wa majitaka kutoka katika miundombinu ya migodi hiyo kwa mujibu wa Sheria Na. 11 ya Mwaka 2009 ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kupitia ofisi za Bonde la Ziwa Victoria na Bonde la Kati kwa kushirikiana na *NEMC* itaimarisha ukaguzi na kuhakikisha kwamba wahusika wanatekeleza maagizo yaliyotolewa na wataalam katika kuyalinda mazingira na vyanzo vya maji. Sampuli za maji zitakusanywa na kuchunguzwa ubora wake ili kubaini kama kuna viashiria vyovyote vya uchafuzi ili hatua za kudhibiti zichukuliwe mapema. Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika zoezi hilo muhimu la kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Serikali wa Hifadhi ya Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ubora na Usafi wa Maji. Wizara yangu ina jukumu la kuhakiki ubora na usafi wa maji katika vyanzo vikuu vya maji kwa lengo la kulinda afya za wananchi. Jukumu hilo hutekelezwa kwa kukusanya sampuli ambazo hupimwa ubora wake kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Wizara ilipanga kukagua vyanzo vya maji 1,750 ambapo sampuli 3,500 za maji zingekusanywa na kuhakikiwa ubora wake

kwa kutumia maabara za maji zilizopo nchini. Hadi kufikia mwezi Mei 2011, jumla ya sampuli 3,004 zilikusanywa katika maeneo ya mijini na vijijini na kuchunguzwa viwango vya kemikali na uwepo wa vijidudu. Kati ya sampuli hizo, 2,374 zilikuwa kwenye viwango vinavyokubalika kitaifa. Sampuli 630 hazikukidhi viwango ambapo sampuli 238 zilibainika kuwa na chumvi chumvi nyingi aina ya *chloride* na *sodium* hivyo, kutofaa kwa matumizi ya nyumbani; na sampuli 392 maji yake yalionekana kuwa na uchafuzi wa vijidudu, hivyo ushauri ulitolewa kuwa maji hayo yatibiwe kabla ya kutumika kwa matumizi yaliyokusudiwa. Maabara zote zimeimarishwa kwa kupatiwa magari kwa ajili ya kukagua na kuhakiki ubora wa maji katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yanayosambazwa kwa matumizi mbalimbali yanapaswa kuwa na viwango vinavyokubalika kitaifa. Hivyo madawa ya kusafisha na kutibu maji yanatakiwa kuhakikiwa ubora wake. Jumla ya sampuli 31 zilihakikiwa ubora wake, kati ya hizo, 14 ni aina ya shabu – *Aluminium Sulphate* inayotumika kusafisha maji, na 17 ni aina ya *Calcium Hypochlorite* ambayo hutumika kuua vijidudu katika maji, zilihakikiwa ubora wake. Matokeo yalionyesha kuwa dawa hizo zipo katika viwango vinavyokubalika na ushauri ulitolewa kuhusu matumizi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kila mwaka inashiriki katika zoezi la Kimataifa la kupima uwezo wa kiutendaji wa maabara (*Laboratories Performance Evaluation),* hasa katika kutoa takwimu sahihi ikiwa ni pamoja na kukidhi matakwa ya kutambulika kimataifa kwa kupata Ithibati (*Accreditation*). Mwaka 2010/2011 maabara tatu ambazo ni:- Maabara Kuu iliyopo Dar es Salaam, maabara za Mwanza na Arusha zilishiriki katika zoezi hili chini ya mpango wa *Southern African Development Community Measurement Traceability (SADCMET)* linaloratibiwa na Shirika la Maji la Namibia (*NAMWATER)*. Pia mwezi Desemba 2010, tulipokea ripoti ya matokeo ya zoezi lililofanyika chini ya mpango wa *Global Environmental Monitoring System* (*GEMS/WATER*). Matokeo ya mazoezi hayo yameonyesha kuwa Maabara zetu kwa wastani zinafanya vizuri kwa kiwango cha asilimia 65. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuhakiki ubora na usafi wa maji ili kulinda afya za wananchi na mazingira kwa ujumla. Vyanzo vikuu 4,000 vya maji vitatathminiwa ubora wake na imepanga kupima sampuli 8,000 kutoka katika vyanzo hivyo. Wizara yangu itaendelea kuziboresha Maabara za Maji kwa kuzipatia watalaam, madawa na vifaa vya kuchunguza ubora wa maji pamoja na kuziwezesha ili kukamilisha taratibu za kupata Ithibati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Rasilimali za Majishiriki. Asilimia 43 ya rasilimali za maji nchini tunachangia na nchi nyingine. Kutokana na sababu hiyo, tunashirikiana na nchi hizo kuhakikisha inakuwepo mifumo ya uwazi na usawa ya uendelezaji na utumiaji wa rasilimali za maji kwa njia endelevu na kwa manufaa ya nchi shiriki. Wizara yangu imeendelea kushirikiana na nchi tunazochangia rasilimali za majishiriki kwa kuendelea kuunda vyombo vya pamoja na kuimarisha vilivyopo ili kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali hizo. Utekelezaji katika eneo hilo unafafanuliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Nile. Nchi zinazoshirikiana katika Bonde la Mto Nile ni Burundi, Eritrea, Ethiopia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC)*, Kenya, Misri, Rwanda, Sudan, Tanzania na Uganda. Ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali hizo nchi hizo zimeunda vyombo mbalimbali vya ushirikiano. Nchi zote katika Bonde kwa kutambua umuhimu wa kushirikiana katika matumizi endelevu ya rasilimali za maji, zilichukua hatua ya kihistoria ya kuanzisha chombo cha mpito cha usimamizi wa rasilimali hizo kinachojulikana kama ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile *(Nile Basin Initiative - NBI).* Madhumuni makubwa ni kupata maendeleo ya kiuchumi na kijamii na faida zinazotokana na usimamizi wa pamoja wa matumizi ya usawa na endelevu wa rasilimali za maji za Bonde la Mto Nile

Mheshimiwa Mwenyekiti, Umoja wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile *(NBI)* umesimamia utekelezaji wa miradi ya maji, mazingira, nishati, kilimo, mafunzo na kujenga uwezo katika Bonde zima. Umoja huo pia, umesimamia utekelezaji wa miradi kama hiyo katika kila nchi chini ya Programu mbili tanzu za nchi za Maziwa Makuu *(Nile Equatorial Lakes Subsidiary Action Program)* na Nchi za Bonde la Mashariki la Nile *(Eastern Nile Subsidiary Action Program)*. *NBI* pia imeratibu majadiliano ya Mkataba wa Kudumu wa Ushirikiano wa Nchi za Bonde la Mto Nile

utakaoanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Katika Mkutano wa dharura uliofanyika Kinshasa tarehe 22 Mei 2009, Baraza la Mawaziri wa Maji wa Nchi za Bonde la Mto Nile liliamua kuhitimisha majadiliano na kuweka utaratibu wa kusaini Mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Ushirikiano umekuwa wazi kwa nchi wanachama wa Bonde la Mto Nile kuanza kusaini. Hadi kufikia tarehe 13 Mei 2011, nchi sita kati ya tisa za Umoja huo ambazo ni Burundi, Ethiopia, Tanzania, Uganda, Rwanda na Kenya zimesaini Mkataba huo utakaoanzisha chombo cha kudumu cha ushirikiano katika Bonde la Mto Nile - Kamisheni ya Bonde la Mto Nile. Nchi za Misri na Sudan bado hazijasaini kwa kutaka mkataba utambue matumizi ya maji ya Mto Nile na haki kama zilivyo katika mikataba ya kikoloni. Maana yake ni kuwataka wanachama wengine watambue mikataba ya mwaka 1929 na 1959. Mikataba hiyo inazipa nchi hizo mbili karibu mgao wote wa maji na haki zaidi kuliko nchi nyingine wanachama, jambo ambalo halikubaliki kwa nchi nyingine. Licha ya msimamo wa nchi hizo mbili, juhudi za mazungumzo zinaendelea kuzishawishi Misri na Sudan kuukubali na kusaini mkataba huo. Jitihada zimeendelea kuishawishi Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ili iweze kusaini mkataba huo. Katika mwaka 2011/2012, Tanzania na nchi nyingine zilizosaini mkataba wa ushirikiano zitaendelea na juhudi za kuridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi wa Mazingira ya Ziwa Victoria. Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria awamu ya pili ulianza rasmi tarehe 20 Agosti 2009. Mradi unalenga katika kuchangia mafanikio ya dira ya bonde la ziwa yenye dhamira ya kuona "Jamii inayozunguka Bonde la Ziwa Victoria inaishi maisha bora katika mazingira yaliyo endelevu kwa kuzingatia mgawanyo wa fursa sawa kwa jamii kati ya nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki".

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni makuu ya mradi huu ni kuimarisha usimamizi wa pamoja wa rasilimali za Bonde la Ziwa Victoria kwa manufaa ya jamii zote zinazolizunguka ziwa, na kupunguza uharibifu wa mazingira katika Ziwa Victoria ili kuboresha maisha ya jamii ambazo hutegemea rasilimali za ziwa hilo. Kwa upande wa Tanzania, mradi huu unachangia katika kuimarisha taasisi zinazohusika na hifadhi ya rasilimali za maji na samaki katika Ziwa Victoria, kukarabati mifumo ya kusafisha majitaka katika miji mikubwa iliyo kando kando ya Ziwa ikiwa ni pamoja na Mwanza, Musoma na Bukoba. Walengwa katika awamu ya pili ni Halmashauri za Wilaya ya Maswa, Bariadi, Magu, Meatu, Bunda na Kwimba. Mradi unafadhili miradi midogo ya kurekebisha mazingira katika bonde dogo la Mto Simiyu ambalo lilichaguliwa liwe la majaribio *(pilot area)* katika awamu hii ya Mradi kwa kuwa lina changamoto nyingi za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania, kuanzia mwezi Julai 2010 hadi mwezi Machi, 2011, Mradi umetumia kiasi cha shilingi 2,011,800,000 kutoka Benki ya Dunia, na shilingi 216,425,000 kama mchango wa Serikali katika kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuwaelimisha wadau na wananchi mbalimbali katika eneo la mradi kuhusu dira, dhima, malengo na shughuli zitakazofanyika kwa kupitia semina, mikutano, kongamano na maonesho;

(ii) Kutoa mafunzo ya mazingira na uendeshaji wa mradi kwa watendaji na timu za Uwezeshaji za Wilaya zilizo katika bonde dogo la Mto Simiyu, lengo likiwa ni kutekeleza sera na kusimamia sheria na kanuni zinazosimamia matumizi bora na endelevu ya rasilimali katika Ziwa Victoria;

(iii) Kukusanya takwimu mbalimbali zinazohusu mazingira, samaki, misitu, magugu maji pamoja na zile za ubora na wingi wa maji katika ziwa na kuzihifadhi katika benki ya takwimu;

(iv) Kuendelea na uandaaji wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na usimamizi wa taarifa kwa kutumia mfumo wa kompyuta wa kuandaa taarifa za kitafiti;

(v) Kuanza kazi ya usanifu wa mifumo ya miundombinu ya majitaka katika miji ya Musoma, Bukoba na Mwanza kufuatia uteuzi wa wataalam washauri; na

(vi) Kutayarisha mpango kabambe wa kukarabati mazingira ya bonde dogo la Mto Simiyu kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Bariadi, Kwimba, Magu, Meatu na Maswa, na kuibua na kuandaa miradi ya jamii ya kuhifadhi mazingira na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kushirikiana na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinazotekeleza mradi huu, na kwa kushirikisha Wizara na taasisi nyingine husika, mradi utatayarisha mifumo na mikakati ya usimamizi wa pamoja wa rasilimali za maji na samaki ikiwemo uanzishwaji wa mfuko wa mazingira *(Lake Victoria Environmental Trust Fund),* mfuko wa ushuru wa samaki *(Fish Levy Trust Fund*) na mkakati wa kudhibiti magugu maji. Masuala mengine yatakayotekelezwa ni uanzishwaji wa mfumo wa kutunza kumbukumbu za kitaalam na kuboresha mfumo wa upatikanaji wa taarifa, kuandaa sera ya pamoja ya utoaji na utiririshaji wa maji ya Ziwa Victoria kwa matumizi mbalimbali, na uainishaji wa sera, sheria na miongozo mbalimbali kwa faida ya nchi zetu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea na uratibu na utekelezaji wa awamu ya pili ya mradi huo kulingana na kazi zilizoainishwa katika Andiko la Mradi. Utekelezaji wa miradi ya miundombinu ya udhibiti wa majitaka katika miji ya Mwanza, Musoma na Bukoba utaanza. Pia, utekelezaji wa miradi ya jamii yenye lengo la kuhifadhi mazingira katika eneo la bonde dogo la Mto Simiyu, sambamba na miradi ya kuongeza kipato kwa vikundi na jamii mbalimbali katika eneo hilo utaanza. Mradi utaendelea kuelimisha umma kuhusu matumizi bora ya ardhi na hifadhi ya mazingira na kuimarisha timu ya uratibu wa mradi kwa kuongeza wataalam wa fani mbalimbali zikiwemo za maendeleo ya jamii, mawasiliano, na ununuzi ili kulinda vyanzo vya maji katika Bonde la Ziwa Victoria. Mradi huo utahusisha uboreshaji wa huduma ya maji katika miji ya Nansio, Geita na Sengerema ambao umeainishwa kwa kina katika Aya ya 116. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Zambezi. Tarehe 8 Februari 2010, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliridhia Mkataba wa kuanzisha Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi *(Zambezi Watercourse Commission (ZAMCOM*). Taarifa rasmi kutoka kwenye Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* ni kwamba, hadi kufikia mwezi Juni, 2011 nchi 6 tayari zimeridhia Mkataba huo, ambazo ni: Angola, Botswana, Msumbiji, Namibia, Tanzania, na Zimbabwe. Mkataba huo kwa sasa utaanza kufanya kazi. Kikao cha Baraza la Mawaziri wa Maji wa nchi za Bonde la Mto Zambezi kilichofanyika Maputo, Msumbiji mwezi Julai, 2009 kiliamua kwamba iundwe Sekretarieti ya muda itakayoendeleza shughuli za *ZAMCOM* wakati nchi wanachama zikiendelea kuridhia Mkataba. Nchi ya Botswana ilichaguliwa kuwa mwenyeji wa Sekretarieti hiyo. Sekretarieti ya muda imeanzishwa na ilianza kazi rasmi tangu tarehe 6 Mei, 2011. Kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea na uratibu wa shughuli za Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Mto Ruvuma. Katika kuhakikisha kuwa rasilimali za maji za Bonde la Mto Ruvuma zinasimamiwa vizuri na kutumiwa kwa manufaa ya nchi za Tanzania na Msumbiji, kandarasi ya kutayarisha takwimu za matumizi na ubora wa maji na kuandaa Mkakati wa Maendeleo wa Bonde hilo (*Development of River Basin Monographs and Strategies)* ulisainiwa tarehe 20 Machi 2010 kati ya *SADC* na mtaalam mshauri (*SWECO*). Utekelezaji wa Mradi huo unategemewa kukamilika mwezi Machi 2012. Hadi mwezi Machi 2011, awamu ya kwanza ya kazi ya utayarishaji wa takwimu za matumizi na ubora wa maji wa mto Ruvuma ilikamilika na taarifa ya awali (*inception report*) itajadiliwa na wadau katika mkutano utakayofanyika mwezi Juni, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upembuzi wa takwimu hizo utawezesha kufahamu kiasi cha maji yaliyopo katika Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini, ubora wake na aina ya matumizi yake. Hatimaye, mapendekezo yatatolewa ya miradi inayofaa kutekelezwa ili kuwa na matumizi endelevu ya rasilimali za maji katika bonde hilo la maji. Kwa kuanzia, kila nchi inatekeleza mradi mmoja wa matokeo ya haraka ili wananchi waanze kunufaika na rasilimali za bonde la mto Ruvuma. Tanzania inatekeleza mradi wa umwagiliaji wa hekta 600 katika kijiji cha Namatuhi, Wilaya ya Songea, Mkoa wa Ruvuma. Kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika itaendelea na utayarishaji wa mpango wa matumizi ya maji ya Mto Ruvuma na itaratibu utekelezaji wa mradi wa Namatuhi pamoja na shughuli za Kamisheni ya Pamoja ya Maji kati ya Tanzania na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe. Mto Songwe una tabia ya kuhamahama wakati wa mafuriko katika ukanda wa chini wa tambarare kuelekea Ziwa Nyasa. Hali hiyo huathiri takriban hekta 15,000 za mazao mbalimbali pamoja na maisha na mali za wananchi wanaoishi kwenye maeneo tambarare. Bonde la Mto Songwe lipo katika wilaya za Ileje, Kyela, Mbozi na Mbeya Vijijini kwa upande wa Tanzania na wilaya za Chitipa na Karonga kwa upande wa Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto ya kuhamahama kwa mto Songwe na athari zitokanazo na tatizo hilo, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Malawi ziliamua kufanya uchunguzi utakaowezesha kutekeleza mradi wa kudhibiti kingo za mto huo. Matokeo ya uchunguzi huo yameziwezesha Serikali hizo mbili kuwa na Programu ya Maendeleo ya Bonde la Maji la Mto Songwe yenye miradi mitano:-

(i) Uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji;

(ii) Ujenzi wa miundombinu;

(iii) Uendelezaji na usimamizi wa rasilimali ardhi;

(iv) Udhibiti wa mazingira; na

(v) Uendelezaji wa taasisi zitakazosimamia utekelezaji na uendeshaji wa programu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Programu hii ni juhudi za nchi za Bonde la mto Zambezi kuanza kunufaika na rasilimali za bonde hilo la maji hata kabla ya Mkataba wa Kamisheni ya Bonde la Mto Zambezi kuanza kufanya kazi. Manufaa kwa Tanzania ni ujenzi wa miundombinu ya rasilimali za maji itakayojengwa kwa ajili ya kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji na kuzuia mafuriko ambayo huharibu mali na mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania na Malawi zimekubaliana kuwa makao makuu ya Programu yatakuwa katika mji wa Kyela, Mkoa wa Mbeya. Pamoja na mchango wa fedha, Tanzania itatoa jengo la ofisi na samani. Ukarabati wa jengo la ofisi ya muda kwa ajili ya Programu umekamilika. Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB)* imepitia na kuridhia Hati ya makubaliano ya ushirikiano *(Memorandum of Understanding – MoU)* kati ya Tanzania na Malawi ambayo yatahusu utekelezaji wa awamu ya pili ya miradi itakayohusisha usanifu wa kina na maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya awamu ya tatu. Tanzania ilisaini hati hiyo tarehe 8 Machi, 2011. Hatua hii ilikuwa ni muhimu kwa Serikali hizi mbili kama sehemu ya mchakato wa Benki kuingia mkataba wa fedha (*Grant Agreement*). Mkataba wa fedha (*Grant Agreement*) umesainiwa mwezi Mei, 2011. Kazi ya usanifu wa miradi inatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zetu mbili zitapatiwa msaada wa jumla ya Euro 5.7 milioni kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya pili. Mchango wa Tanzania utakuwa kiasi cha Euro 300,000 kila mwaka kwa miaka miwili ya awamu hiyo. Baada ya usanifu, ujenzi wa miradi iliyoainishwa utafanyika kwenye awamu ya tatu iliyopangwa kuwa ya miaka kumi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaanza ujenzi wa ofisi ya kudumu ya Programu mjini Kyela, kushiriki katika uratibu wa miradi na ajira za Meneja wa Programu na Waratibu wa Programu kwa kila nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi wa Matumizi ya Maji ya Ziwa Tanganyika. Kina cha maji katika Ziwa Tanganyika kimeshuka kwa kiasi cha mita kati ya 2 na 2.5 katika kipindi cha takriban muongo mmoja. Kushuka huko kwa kina cha maji kumeathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za usafiri wa majini katika nchi zinazozunguka ziwa hilo ambazo ni Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC),* Tanzania na Zambia. Sababu za kushuka kwa kina hicho hazijaweza kubainishwa kikamilifu lakini kuna uwezekano kwamba kumesababishwa na shughuli za binadamu zinazofanyika katika eneo linalozunguka ziwa hilo, mabadiliko ya tabianchi na kuachiwa kwa maji mengi kupitia banio la matoleo ya maji la Mto Lukuga lililobomoka, mto pekee unaotoa maji kutoka ziwa hilo na kuyapeleka mto Congo. Hali hii ni changamoto kubwa ambayo inahitaji juhudi za pamoja za nchi shiriki ili kupata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Agosti, 2010 nilifanya ziara nchini DRC ambapo niliwasilisha ujumbe kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC),* Mheshimiwa Joseph Kabila. Pamoja na mambo mengine, ziara hiyo ilitumika kusisitiza juu ya tatizo la kushuka kwa kina cha maji cha Ziwa Tanganyika, athari zake na kukubaliana hatua za kuchukua. Pendekezo muhimu ni kuandaa mkakati mahsusi wa kushughulikia kushuka kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Water Level Initiative)*. Kazi hiyo itahusisha ukusanyaji wa takwimu na kuweka mfumo wa ufuatiliaji kwa kujenga vituo vya kupima wingi wa maji, upimaji wa hali ya mwinuko (*elevation*) ya vituo vya takwimu na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la jitihada hizi ni kupata takwimu sahihi za mwinuko juu ya usawa wa bahari *(land survey benchmarks);* utayarishaji wa mizania ya maji (*water balance study*); usanifu na ukarabati wa banio la matoleo ya maji ya Mto Lukuga. Kazi za kutathmini mchango wa mabadiliko ya tabianchi katika kupunguza kina cha maji ya ziwa; kutathmini athari za kiuchumi na kijamii zinazotokana na kushuka kwa kina cha maji zinafanyika kwa kushirikisha nchi zote za Bonde hilo la maji kupitia Mamlaka ya Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Authority (LTA*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu iliwasilisha pendekezo la kuandaa mkakati mahsusi wa kushughulikia tatizo la kushuka kwa kina cha maji ya Ziwa Tanganyika kwenye kikao cha wataalam cha Mamlaka ya Ziwa Tanganyika kilichofanyika Bujumbura, tarehe 5-7 Oktoba, 2010 na hatimaye kwenye kikao cha Baraza la Mawaziri wa nchi za Bonde la Ziwa Tanganyika mwezi Novemba, 2010. Kikao hicho cha Mawaziri kiliiagiza Mamlaka kuchukua hatua stahiki za kukabiliana na tatizo la kushuka kwa kina cha maji ya Ziwa kwa kushirikiana na nchi wanachama.

Pamoja na juhudi hizo, mapendekezo yaliyotolewa kukabiliana na tatizo la kushuka kwa kina cha maji bado hayajatekelezwa. Kazi nyingine zinazofanywa na Mamlaka ni hifadhi ya mazingira kuzunguka ziwa ili kukabiliana na mmomonyoko wa udongo unaoweza kusababisha kuingia kwa tope ziwani na hivyo kuweza kuathiri kina chake. Katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea kuwasiliana na DRC na kushirikiana na Mamlaka ya Ziwa Tanganyika, nchi nyingine na Washirika wa Maendeleo ili kuendeleza juhudi za hifadhi ya Bonde la Maji la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Usimamizi na Uendelezaji wa Ikolojia ya Ziwa Chala – Jipe na Mto Umba. Mkutano wa pamoja kati ya nchi za Kenya na Tanzania ulifanyika mjini Moshi mwezi Oktoba, 2010 kujadili namna ya kutunza na kuendeleza majishirikishi na ikolojia ya Ziwa Chala – Jipe na Mto Umba. Sekretarieti ya Kamisheni ya Nchi za Bonde la Ziwa Victoria ilialikwa na ilishiriki kwenye mkutano huo. Maazimio ya mkutano wa Moshi yalijadiliwa katika mkutano wa nane wa Baraza la Kisekta la Mawaziri wa Maji wa nchi za Bonde la Ziwa Victoria uliofanyika Kisumu, Kenya tarehe 21 Januari, 2011. Sekretarieti iliagizwa na Baraza hilo kutoa msaada wa kitaalam pamoja na ushauri wa namna ya kutunza na kuendeleza ikolojia ya Ziwa Chala-Jipe na Mto Umba ambapo kwa sasa tathmini ya kina ya rasilimali za maji chini ya ardhi katika maeneo ya maziwa hayo imeanza. Lengo la tathmini hiyo ni kubaini wingi na ubora wa rasilimali za maji zilizopo na kuweka utaratibu wa matumizi ya pamoja kwa nchi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa Kamisheni ya Nchi za Bonde la Ziwa Victoria katika kutoa msaada wa kitaalam wa usimamizi na uendelezaji wa ikolojia ya Ziwa Chala-Jipe na Mto Umba pia, utasaidia kupanua wigo wa kupata fedha za kutekeleza miradi itakayohusu utunzaji na uendelezaji wa ikolojia hiyo. Kwa sasa sehemu kubwa ya Ziwa Jipe kwa upande wa Tanzania imefunikwa na magugu maji aina ya *typha* ambayo kwa kiwango kikubwa yanatokana na virutubisho vinavyoingia ziwani kutokana na mmomonyoko wa ardhi. Katika kukabiliana na tatizo hilo la magugu maji, Serikali za Tanzania na Kenya zitaunda Kamati ya Pamoja ya Uongozi ya Makatibu Wakuu kutoka Wizara zinazosimamia maji, mazingira, uvuvi, kilimo, serikali za mitaa na zile zinazosimamia masuala ya ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuratibu uandaaji wa mpango shirikishi wa usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji katika Bonde la Mto Pangani ambao utabaini mahitaji katika utunzaji na uendelezaji wa ikolojia ya ziwa Chala-Jipe na mto Umba. Hati ya

makubaliano kati ya Tanzania na Kenya itakayoainisha majukumu ya kila nchi katika usimamizi na uendelezaji wa ikolojia hiyo, itakamilishwa na kusainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Huduma ya Maji Vijijini. Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM - TAMISEMI) imeendelea kutekeleza Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini tangu mwezi Julai 2007 kwa kutekeleza miradi inayoleta matokeo ya haraka kulingana na mipango na vipaumbele vya kila Halmashauri. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya vituo vya kuchotea maji 934 vilijengwa au kukarabatiwa ambapo watu 233,500 wananufaika na huduma ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, utekelezaji wa miradi katika vijiji 10 kwa kila Halmashauri uliendelea na kufikia katika hatua mbalimbali. Tarehe 14 Februari 2011 nilitoa taarifa hapa Bungeni kuhusu hatua iliyofikiwa na kila Halmashauri katika utekelezaji. Halmashauri 124 kati ya Halmashauri 132 zilipata ridhaa kutoka Benki ya Dunia kuhusu kusaini mikataba baina yake na wataalam washauri. Hivi sasa, Halmashauri 130 zimeajiri wataalam washauri na wameanza kazi. Orodha ya Halmashauri ambazo zimesaini mikataba baina yake na kampuni za wataalam washauri, hadi kufikia mwezi Juni 2011 imeonyeshwa katika Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Halmashauri ya Morogoro, gharama za kufanya kazi za kampuni zilizokuwa zimeshinda zilikuwa juu kuliko kiwango kinachokubalika. Halmashauri hiyo ilitakiwa kuandaa orodha nyingine fupi ya kampuni za wataalam washauri kwa ajili ya kupitishwa kwenye vikao vya Bodi ya zabuni ya Halmashauri ili ipelekwe Benki ya Dunia kupata ridhaa ya kuendelea na hatua inayofuata. Halmashauri inaendelea kufanya tathmini ya kifedha, kuandaa rasimu ya mkataba na kufanya majadiliano na mtaalam mshauri. Halmashauri ya Simanjiro ilirudia matangazo lakini hakuna wataalam washauri waliojitokeza kuomba kufanya kazi hiyo. Halmashauri hiyo iliandaa orodha fupi ya kampuni za wataalam washauri, kupata mapendekezo yao na kupata ridhaa ya Benki ya Dunia kufanya tathmini ya kifedha, kuandaa rasimu ya mkataba na kufanya majadiliano na mtaalam mshauri atakayeshinda. Halmashauri inakamilisha zoezi hilo kwa lengo la kuwasilisha taarifa Benki ya Dunia ili kupata ridhaa ya kusaini mkataba kati yake na mtaalam mshauri atakayeshinda. Upatikanaji wa wataalam washauri unazingatia kasi ya Halmashauri katika kutekeleza ushauri na maelekezo yanayotolewa na Wizara na Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ambazo zimesaini mikataba baina yake na wataalam washauri, wataalam hao wanaendelea na uchunguzi na tathmini ya vyanzo vya maji, usanifu wa miradi ya maji, uhamasishaji wa jamii kuhusu usafi wa mazingira, kuunda vyombo vya watumiaji maji, na kuandaa zabuni za ujenzi wa miradi. Hadi mwezi Mei 2011, Halmashauri tatu za Babati, Hai na Mji wa Mpanda zilikuwa zimetangaza zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu. Katika Halmashauri tisa za Kilolo, Iringa, Bukoba, Karagwe, Mbulu, Bukombe, Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga na Iramba wataalam washauri wamefanya usanifu wa miradi ya maji na kuandaa zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi wa kujenga miundombinu ya maji. Halmashauri hizo zimepata kibali cha kutangaza zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri sita za Ludewa, Makete, Mji wa Njombe, Njombe, Moshi na Mbinga, wataalam washauri wamefanya usanifu wa miradi ya maji ya mtiririko na kuandaa taarifa za usanifu pamoja na zabuni kwa ajili ya kutafuta wakandarasi wa kujenga miundombinu ya maji. Halmashauri 47 zimekamilisha uchimbaji wa visima. Halmashauri hizo na mikoa husika ni kama ifuatavyo: Arusha: Manispaa ya Arusha, Longido, Monduli, Meru; Dodoma: Bahi, Chamwino, Kongwa; Iringa: Iringa; Kagera: Bukoba, Chato; Kilimanjaro: Mwanga, Same; Lindi: Kilwa, Mji wa Lindi, Liwale, Nachingwea, Ruangwa; Manyara: Hanang', Mbulu; Mara: Serengeti; Mbeya: Ileje, Mbarali, Mbeya; Morogoro: Kilombero; Mtwara: Masasi, Mtwara, Nanyumbu, Newala; Mwanza: Magu; Pwani: Kibaha, Mji wa Kibaha; Rukwa: Mpanda; Ruvuma: Songea, Tunduru; Shinyanga: Bukombe, Kahama, Kishapu, Shinyanga, Manispaa ya Shinyanga; Singida: Iramba, Manyoni, Singida; Tabora: Manispaa ya Tabora, Sikonge; Tanga: Kilindi, Korogwe na Mkinga. Jedwali Na. 6 linaonesha visima vilivyochimbwa katika Halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ambazo uchimbaji wa visima vya maji bado unaendelea ziko 49. Idadi ya Halmashauri hizo kwa kila mkoa ni kama ifuatavyo: Arusha (2); Dar es

Salaam (1); Dodoma (2); Iringa (2); Kagera (4); Kilimanjaro (2); Kigoma (1); Lindi (1); Mara (1); Manyara (2); Mbeya (4); Morogoro (2); Mtwara (2); Mwanza (6); Pwani (4); Rukwa (2); Ruvuma (2); Shinyanga (2); Tabora (3) na Tanga (4). Halmashauri mbili za Arusha na Kondoa zimepata kibali cha kusaini mikataba baina yao na wakandarasi wa uchimbaji wa visima lakini bado wanafanya mawasiliano na wakandarasi kwa ajili ya kusaini mikataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri 3 za Ngara, Musoma, na Tarime zimetangaza zabuni za kupata wakandarasi watakaochimba visima na zimefanya tathmini ya kupata wakandarasi kwa ajili ya uchimbaji. Halmashauri 6 zimetangaza zabuni za kupata wakandarasi watakaochimba visima vya maji. Halmashauri hizo ni Sumbawanga, Manispaa ya Ilala, Manispaa ya Moshi, Kisarawe, Rorya na Tabora/Uyui. Katika Halmashauri 6 za Manispaa ya Temeke; Jiji la Mbeya; Manispaa ya Bukoba; Kasulu; Handeni na Jiji la Tanga, wataalam washauri wameandaa taarifa za awali na kuainisha kazi zitakazofanyika (*scoping study).* Halmashauri 5 za Kibondo, Manispaa ya Kigoma, Kilosa, Manispaa ya Singida, na Bariadi wataalam washauri wanaendelea na kazi ya kukusanya takwimu, kuainisha vyanzo vya maji na kuwasaidia wananchi kuchagua teknolojia wanayoiona inawafaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usanifu uliofanywa na wataalam washauri unaonesha kuwa wananchi kwenye vijiji vingi katika miradi ya vijiji wamechagua visima kama vyanzo vya kuwapatia maji. Hii inatokana na jiolojia na haidrolojia ya maeneo mbalimbali ya nchi yetu.. Jumla ya visima 843 vimechimbwa. Kati ya hivyo, visima 578 sawa na asilimia 69, vina maji. Kwa kuzingatia jiolojia na haidrolojia ya nchi yetu, kiwango hiki cha upatikanaji wa maji kinakubalika kitaifa. Vijiji ambavyo vimekosa maji chini ya ardhi vitaingizwa katika awamu ya pili ya Programu itakayoanza mwaka 2012/2013 kwa kuhusisha vyanzo vingine vya maji. Halmashauri 16 zilizoajiri wakandarasi wa kuchimba visima hazijaanza uchimbaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi ilipeleka jumla ya shilingi bilioni 6.831 kwenye Halmashauri zote kwa ajili kutekeleza miradi kwenye vijiji vilivyoainishwa kwenye Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Jedwali Na. 9 linaonesha fedha zilizotumwa kwenye Halmashauri kuanzia mwezi Juni 2007 hadi Mei 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwaka 2011/2012, Halmashauri zitaanza ujenzi wa miundombinu ya maji kwenye baadhi ya vijiji 10 vya kila Halmashauri. Kiasi cha shilingi bilioni 86.7 kimekasimiwa katika Halmashauri na Sekretarieti za Mkoa kwa ajili ya shughuli za ujenzi wa miundombinu ya maji, kujenga uwezo wa watekelezaji wa programu, uhamasishaji, kutoa elimu ya usafi binafsi na mazingira, usimamiaji, ufuatiliaji na kulipa wataalam washauri kwa ajili ya usimamizi wa wakandarasi wa ujenzi. Fedha zaidi zitatengwa katika mipango ya miaka inayofuata kwa ajili ya vijiji 10 kwa kuzingatia maendeleo ya kazi na mahitaji ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuziwezesha Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa kutekeleza majukumu yao, Wizara yangu imeendelea kutoa nyenzo za kufanyia kazi. Hadi kufikia mwezi Mei 2011, Halmashauri zimepata magari 120, pikipiki 252, *printer* 124, kompyuta 111 na *scanner* 116. Taratibu zinaendelea ili kupata magari 5 zaidi yaliyoagizwa kwa ajili ya Halmashauri. Sekretarieti za Mkoa zimepata magari 21, *printer* 20, kompyuta 21 na *scanner* 20. Katika awamu ya pili ya Programu itakayoanza mwaka 2012/2013, Serikali itaendelea kuzipatia Halmashauri vitendea kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea kuzisaidia baadhi ya Halmashauri kusanifu na kuandaa zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji vijijini. Katika mwaka wa 2011/2012 Wizara yangu itazisaidia Halmashauri husika katika kutekeleza miradi ya Lukululu, Masoko, Mwakaleli I, Mwakaleli II, Kakonko, Mandela University, Iwungilo, Mputwa, Milola, Matema, Michire, Ingri Juu, Kidete, Nyamongo, Oljoro-Muriet-Losinyai, Gabimori, Kongoto, Lifua Manda, Kabembe, Ilamba, Ngeleka, Chiwambo, Komuge, Masonga, Masuguru, Kawa, Sadani, Ujuni, Kilulu, Manyovu, Lutete, Haruzale, Bungu na Mbumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu kwa kushirikiana na Halmashauri, itaandaa miradi ya maji katika wilaya kame zenye mifugo mingi. Kwa kuanzia, miradi itaandaliwa katika Wilaya za Longido, Monduli, Simanjiro na Kiteto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa maji wa Wilaya za Moshi Vijijini na Hai. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (*KfW*) iliendelea na utekelezaji wa mradi wa maji katika wilaya za Moshi Vijijini na Hai. Mradi wa maji wa Moshi Vijijini ulihusisha ujenzi wa vyanzo vitatu vya maji vya Kisanja, Korashi na Kombishi, ujenzi/ukarabati wa matanki 28 yenye mita za ujazo kati ya 20 na 150, ujenzi/ukarabati wa matanki 14 ya kupunguza msukumo wa maji, uchimbaji wa visima 4 na kufunga pampu za kutumia nguvu ya jua, uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba urefu wa kilomita 85, ujenzi wa vituo 78 vya kuchotea maji na uunganishaji wa maji katika nyumba 814 za watu binafsi. Katika mwaka 2011/2012 ujenzi wa mradi utaendelea katika maeneo ya Kilototoni – Himo Njiapanda na mto Rau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Mradi wa Maji wa Hai ulihusisha ujenzi wa miradi ya maji ya Machame, Mkalama na West Kilimanjaro. Mradi wa Machame umekamilika na umekabidhiwa kwa wananchi ambapo zaidi ya kaya 800 zimeunganishwa kwenye mtandao wa maji. Ujenzi wa mradi wa Mkalama umefikia kiwango cha asilimia 65 na ule wa West Kilimanjaro umefikia kiwango cha asilimia 30.

Katika mwaka wa fedha 2011/2012, ujenzi wa miradi ya Mkalama na West Kilimanjaro utaendelea na ujenzi wa mradi wa North West Kilimanjaro utaanza. Mradi wa Mkalama unategemewa kukamilika mwezi Desemba 2011 na ule wa West Kilimanjaro unategemewa kukamilika mwezi Februari 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Mradi wa maji wa Same – Mwanga – Korogwe. Wizara yangu imeendelea na maandalizi ya mradi wa maji wa wilaya za Same, Mwanga na Korogwe. Wizara imefanya tathmini ya mapendekezo ya kiufundi ili kumpata mtaalam mshauri ambaye atafanya mapitio ya usanifu na atasimamia kazi za ujenzi wa mradi. Katika mwaka 2011/2012, taratibu za kumpata mkandarasi zitafanyika na ujenzi unatarajiwa kuanza. Mradi huu umegawanywa katika awamu mbili. Awamu ya kwanza itatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania, *BADEA* na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-OFID)*. Awamu hiyo ya mradi italenga katika kusambaza majisafi na salama katika vijiji saba (Kirya, Kiti cha Mungu, Njia Panda, Handeni, Kagongo, Bora, na Nyabinda) vya wilaya ya Mwanga na vijiji viwili (Ruvu Mferejini na Ruvu Jiungeni) vya wilaya ya Same. Kazi zitakazotekelezwa katika awamu ya kwanza ni ujenzi wa miundombinu, kama ifuatavyo:-

(a) Chanzo cha maji katika bwawa la Nyumba ya Mungu;

(b) Mtambo wa kusukuma maji toka chanzo cha maji;

(c) Mtambo wa kusafisha maji eneo la kijiji cha Njia Panda (Mwanga);

(d) Mtambo wa kusukuma maji safi eneo la kijiji cha Njia Panda;

(e) Tanki kuu la kuhifadhi na kusambaza maji katika kijiji cha Kisangara;

(f) Matanki ya kuhifadhi maji katika vijiji vya awamu ya kwanza;

(g) Bomba kuu na mabomba ya kusambaza maji katika vijiji vya awamu ya kwanza; na

(h) Njia ya umeme kwenda mitambo ya kusukuma maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili itahusu ujenzi wa miundombinu ya maji kwa ajili ya vijiji 11 vya wilaya ya Mwanga, vijiji 14 vya Wilaya ya Same, vijiji vitano vya wilaya ya Korogwe na miji ya Same na Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza itagharimu Dola za Marekani milioni 35.76. Serikali itachangia Dola za Marekani milioni 13.76, *OFID* itachangia Dola za Marekani milioni 12 na

*BADEA* itachangia Dola za Marekani milioni 10. Mradi katika awamu zote mbili unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 147. Awamu ya pili itagharimu Dola za Marekani milioni 111.24 na fedha hizo zitatoka Serikalini. Serikali itaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Mradi wa maji vijijini katika mikoa ya Mwanza na Mara. Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan iliendelea kutekeleza mradi wa maji vijijini katika mikoa ya Mwanza na Mara. Mradi huo unalenga kuwapatia huduma ya maji wananchi katika vijiji 44 vya mikoa ya Mwanza (26) na Mara (18) Jumla ya visima 177 vitachimbwa na kufungwa pampu za mkono. Hadi mwezi Machi 2011, chini ya awamu ya kwanza na ya pili, jumla ya visima 114 vilikuwa vimechimbwa na kufungwa pampu za mkono. Kwa Mkoa wa Mwanza jumla ya visima 72 vimechimbwa katika wilaya za Geita (30), Kwimba (9), Misungwi (10), Sengerema (23), na kwa Mkoa wa Mara jumla ya visima 42 vimechimbwa katika wilaya za Musoma (5), Rorya (21), Tarime (3) na Serengeti (13). Awamu ya tatu ya mradi huu iliyoanza kutekelezwa mwezi Aprili 2011 inahusisha uchimbaji wa visima 63 katika Mikoa ya Mwanza (36) na Mara (27). Kati ya hivyo, visima 20 tayari vimekwishachimbwa katika Mkoa wa Mara. Utekelezaji wa mradi umepangwa kukamilika mwezi Januari 2012. Uzinduzi wa Awamu ya kwanza ya mradi ulifanywa na Mheshimiwa Dr. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Machi, 2011 katika kijiji cha Ng'hungumalwa Wilayani Kwimba, Mkoa wa Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa maji Vijijini katika mkoa wa Tabora. Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Japan inatekeleza mradi wa maji vijijini katika mkoa wa Tabora. Mradi huo unalenga kuwapatia huduma ya maji wananchi wapatao 44,977 katika vijiji 20 vya mkoa wa Tabora. Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa mradi ulitekelezwa kuanzia Septemba 2009 hadi Mei 2011 ambapo mpango wa maji vijijini kwa Halmashauri zote 6 za mkoa wa Tabora umeandaliwa. Katika mwaka 2010/2011, jumla ya visima 16 vilichimbwa na visima 45 vyenye pampu za mikono vilikarabatiwa katika Halmashauri za mkoa wa Tabora. Usanifu wa awali umeonyesha kuwa, visima 5 kati ya visima 16 vilivyochimbwa ndivyo vitatosheleza miradi ya maji ya kusukuma kwa mashine katika vijiji 4 vya Isanga (Nzega), Kakola (Manispaa ya Tabora), Mpumbuli na Mabama (Uyui). Jumla ya visima 114 vitachimbwa katika wilaya za Igunga (12), Nzega (23), Sikonge (20), Uyui (12), Manispaa ya Tabora (15) na Urambo (32). Katika mwaka 2011/2012, utafiti na usanifu wa kina wa miradi katika maeneo ambayo yameonyesha kuwa na maji ya kutosha utafanyika na baada ya hapo, ujenzi wa miundombinu utafuata. Mradi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara iliendelea kusimamia ujenzi wa mabwawa mapya ya Habiya (Bariadi), Nyambori (Rorya), Salama Kati (Bunda), Seke Ididi (Kishapu), Wegero (Musoma Vijijini), Iguluba (Iringa), Kawa (Nkasi), Sasajila (Chamwino), Matwiga (Chunya) na Mwanjoro (Meatu). Ujenzi wa mabwawa hayo upo katika hatua mbalimbali za ujenzi kwa asilimia kama inavyoonyeshwa katika mabano: Habiya (42%), Nyambori (98%), Seke Ididi (35%), Wegero (77%), Iguluba (40%), Kawa (95%), Sasajila (72%), Matwiga (36%), na Mwanjoro (93%). Katika mwaka 2011/2012, ujenzi wa mabwawa ya Habiya, Nyambori, Seke Ididi, Wegero, Iguluba, Kawa, Sasajila, Matwiga na Mwanjoro utaendelea na mabwawa mawili ya Kanyisambo (Rorya) na Mugeta (Bunda) yataanza kujengwa. Shilingi bilioni 7.033 zimekasimiwa kwa mwaka 2011/2012 kwa ujenzi wa mabwawa na uchimbaji wa visima. Ujenzi wa mabwawa madogo utafanywa na Halmashauri kulingana na vipaumbele vyake; Wizara yangu itatoa ushauri wa kiufundi utakaohitajika. Uchimbaji wa visima utafanywa kwa Wizara kuzisaidia baadhi ya Halmashauri kutekeleza ahadi za viongozi wakuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendelevu wa miradi ya maji vijijini. Pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kuhakikisha kuwa idadi kubwa ya wananchi waishio vijijini wanapata majisafi na salama ifikapo mwaka 2025, ni muhimu kuweka taratibu zitakazohakikisha kuwa miradi iliyojengwa na inayoendelea kujengwa inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa uendeshaji na usimamiaji wa miradi ya maji unafanyika ipasavyo, wananchi wanawajibika kuunda vyombo vya watumiaji maji na kuvisajili kwa mujibu wa sheria. Aina ya vyombo vya watumiaji maji vilivyoundwa na kusajiliwa, na idadi yake hadi mwezi Mei 2011, ni kama ifuatavyo:- Jumuiya za Watumiaji Maji 700 kwa

mchanganuo ufuatao kimkoa: Arusha (52), Iringa (21), Mbeya (6), Dodoma (59), Ruvuma (12), Kilimanjaro (17), Kagera (25), Shinyanga (35), Lindi (8), Morogoro (39), Tabora (19), Manyara (57), Mara (85), Singida (52), Kigoma (13), Dar es Salaam (53), Pwani (14), Tanga (18), Mtwara (10), Mwanza (51) na Rukwa (54). Kampuni 18 za Morogoro (17) na Kilimanjaro (1); na Bodi za Udhamini 21 zilizo Kilimanjaro (11), Mtwara (Mbuo) (1), Dodoma (Kibaigwa) (1), Arusha (7) na Manyara (Namewadi) (1) na Shirika Dola *(Corporation Sole)* (1) la Mtwara (Lulindi) zilisajiliwa.

Juhudi zaidi za kuhamasisha uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji zinaendelea kufanywa na Halmashauri na Mikoa. Hii itachangia kwa kiasi kikubwa kwa miradi kufanya kazi katika njia endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusisitiza tena kwamba kamati za maji za vijiji zilizopo ni ngazi tu ya muda ya kuelekea kwenye uundaji wa vyombo huru vya kuendesha na kusimamia miradi. Halmashauri na wananchi wasiishie kwenye uundaji wa kamati za maji za vijiji. Kamati ya maji ya kijiji si chombo huru kwani ni sehemu ya Serikali ya kijiji. Halmashauri inabidi zisaidie kamati za maji zifanye kazi ya kuunda vyombo huru vitakavyosajiliwa kisheria kwenye Halmashauri. Kwa kuwa uundaji na usajili wa vyombo vya watumiaji maji sasa unafanyika katika ngazi ya Halmashauri, Halmashauri zote zihakikishe kwamba miradi iliyopo na mingine itakayojengwa, ikiwa ni pamoja na ile itakayojengwa kupitia programu ya maji vijijini, inaundiwa vyombo huru vya watumiaji maji. Kanuni inayohusu Usajili wa Vyombo vya Watumiaji Maji *[The Water Supply and Sanitation (Registration of Community Owned Water Supply Organisations) Regulations, 2009, GN. No. 21 of 22/01/2010]* imekamilika na imeanza kutumika. Mwongozo wa uundaji na usajili wa vyombo hivyo ulikamilika na kutumwa kwa Halmashauri zote nchini mwezi Agosti 2010. Halmashauri zinatakiwa ziandae mipango kazi ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu kuanzisha na kusajili vyombo vya watumiaji maji. Pia, Halmashauri zimeagizwa kutoa taarifa ya utekelezaji wa mipango hiyo kila robo mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto inayoikabili Wizara yangu ni kuwa na mfumo mzuri wa kupata takwimu sahihi zinazohusiana na huduma ya maji. Wizara yangu imeajiri mtaalam mshauri anayefanya kazi ya kuainisha vituo vyote vya kuchotea maji nchi nzima. Kuainishwa kwa vituo hivyo kutawezesha kufahamu vizuri zaidi, na kwa kutumia teknolojia ya kisasa, kuandaa ramani ya vituo vya maji (*water point mapping*), mahali vilipo, vinavyofanya kazi, visivyofanya kazi, na idadi ya watu wanaohudumiwa na vituo hivyo. Taarifa zitakazopatikana na ufahamu wa mtandao wa vituo vya kuchotea maji zitawezesha Halmashauri kufahamu upatikanaji wa maji katika vijiji na kata, pia kuwezesha kupanga vipaumbele. Taarifa hizo pia zitasaidia katika ufuatiliaji wa uendelevu wa miradi ya maji nchini. Mtaalam mshauri alianza kazi tarehe 15 Novemba 2010 na ameshakusanya taarifa katika Halmashauri 45. Katika mwaka 2011/2012, kazi hiyo itaendelea kufanyika na imepangwa kukamilika mwezi Desemba 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, iliendelea kutekeleza Programu ya Majisafi na Uondoaji wa Majitaka Mijini kwa kukarabati, kujenga na kupanua mifumo ya majisafi na majitaka pamoja na kuzijengea uwezo Mamlaka za maji mijini. Lengo la utekelezaji huo ni kuwapatia wananchi wengi zaidi huduma hizo katika miji mikuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo, na miradi ya maji ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa miji mikuu ya mikoa 19 imeongezeka hadi kufikia asilimia 86 mwaka 2011 kutoka asilimia 84 mwaka 2010. Kutokana na ongezeko hilo, wastani wa muda wa upatikanaji wa maji katika miji hiyo ulikuwa saa 19 kwa siku ikilinganishwa na saa 18 kwa siku mwaka 2010. Hali ya upatikanaji wa huduma ya majisafi kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo inayohudumiwa na DAWASA kwa sasa ni asilimia 55 kwa wastani wa saa 9 kwa siku. Huduma ya uondoaji majitaka imebakia kuwa asilimia 18 kwa Mamlaka za majisafi na majitaka za miji ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Morogoro, Moshi, Mwanza, Tabora, Tanga na Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha mamlaka za majisafi na majitaka. Katika mwaka 2010/2011, Mamlaka za maji za makao makuu ya mikoa, miji mikuu ya wilaya, miji midogo na

miradi ya kitaifa, ziliendelea kujengewa uwezo na Wizara yangu ili kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma katika miji hiyo. Kazi zilizotekelezwa ni pamoja na zifuatazo:

(i) Kujenga majengo ya ofisi za Mamlaka za Maji katika miji ya Babati na Sumbawanga ambapo ujenzi utakamilika mwezi Juni, 2012;

(ii) Kukamilisha upembuzi yakinifu, usanifu na kuandaa vitabu vya zabuni kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa miundombinu katika miradi ya kitaifa ya Makonde na *Handeni Trunk Main*. Kazi za dharura zitaanza kutekelezwa mwaka 2011/2012.

(iii) Mafunzo juu ya usimamizi wa Mamlaka kwa Bodi za Mamlaka 19 za miji mikuu ya mikoa yalitolewa. Mafunzo ya kujenga uwezo kwa Mamlaka 86 za maji za miji mikuu ya Wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa yalitolewa.

(iv) Mikataba kati ya Wizara na Mamlaka za Maji za miradi ya Kitaifa inayoainisha viwango vya kukidhi viashiria vya utendaji kazi iliandaliwa na kusainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kutekeleza miradi inayotoa matokeo ya haraka katika miji mikuu ya Wilaya, Miji midogo, na Miradi ya kitaifa katika kipindi hicho, usanifu, upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya maji ulifanyika katika miji midogo ifuatayo:-

(a)Mji wa Lamadi: kazi ya usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni za mradi imekamilika. Ujenzi utaanza mwaka 2011/2012;

(b)Mji wa Mlowo: kazi zilizofanyika ni pamoja na kufunga pampu, kulaza mabomba ya usambazaji maji ya umbali wa kilomita 3.75 na ujenzi wa magati 17 ya kuchotea maji. Mradi huu umekamilika kwa kiwango cha asilimia 90 na sasa wakazi wa mji wa Mlowo wanapata maji kwa njia ya vioski. Ulazaji wa mabomba ya usambazaji maji ya umbali wa kilomita 0.95 na ujenzi wa magati matatu utakamilika katika mwaka 2011/2012 ili kutimiza lengo lililowekwa; na

(c)Mji wa Same: Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imechimba visima virefu viwili katika eneo la *Stirling*, kimoja kinatoa maji mita za ujazo 26 na kingine 35 kwa saa, hivyo kuwapatia wakazi wa Same wastani wa mita za ujazo 1,400 kwa siku. Kazi ya kuchimba visima vingine vitatu itafanyika mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea kuchangia gharama za uendeshaji kwa kulipia ankara za umeme kwa Miradi ya Kitaifa ambapo hadi mwezi Mei 2011, jumla ya shilingi bilioni 1.542 zilitumika. Katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu, itaendelea kuchangia gharama za umeme katika miradi ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi wa Mamlaka za majisafi na majitaka mijini hususan, mamlaka za miji mikuu ya wilaya na miji midogo, Wizara yangu inaandaa utaratibu wa kuziwezesha mamlaka za miji ya mikoa kuzipatia utaalam wa kiufundi na kiutawala (*management contracts*) mamlaka za miji ya wilaya na miji midogo. Utaratibu huo utatekelezwa kwa kuzingatia kikamilifu Sera ya Serikali ya ugatuaji wa madaraka kwa Serikali za mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu ilianza ujenzi, ukarabati na upanuzi wa vyanzo vya maji ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima, upanuzi wa mitandao ya usambazaji maji na ujenzi wa matanki katika miji ya Mtwara, Babati, Lindi na Sumbawanga. Ujenzi wa miundombinu ya maji kukidhi mahitaji ya maji kwa muda mfupi kwa mji wa Mtwara umefikia asilimia 75, Babati asilimia 54, Lindi asilimia 90 na Sumbawanga ni asilimia 40. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itakamilisha ujenzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za upembuzi yakinifu, usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni za ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka ya kukidhi mahitaji ya maji ya miji hiyo

kwa kipindi cha muda mrefu hadi mwaka 2025 ziliendelea kutekelezwa na zitakamilika mwezi Septemba 2011. Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali na Umoja wa Ulaya chini ya mpango wa *ACP – EU Water Facility.* Miji iliyo katika mradi huo ni Lindi, Mtwara, Musoma, Sumbawanga, Kigoma, Babati na Bukoba. Katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) na Umoja wa Ulaya chini ya programu ya *MDG – EU Initiative* itaanza ujenzi wa miradi katika miji ya Babati, Mtwara, Lindi, Sumbawanga na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 kazi ya usanifu na utayarishaji wa zabuni kwa miradi ya majisafi katika mpango wa muda wa kati kwa miji ya Musoma na Bukoba, inayotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)* imekamilika. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, ujenzi wa miradi ya maji kwa miji ya Musoma na Bukoba utaanza na utagharimu Euro milioni 47. Katika mwaka 2010/2011 usanifu wa kina wa mradi wa majitaka Musoma na miradi ya maji katika miji midogo iliyo katika Mkoa wa Mara (Bunda, Mugumu, Tarime) na Mradi wa Kitaifa wa Mugango/Kiabakari ulianza na utakamilika mwezi Julai, 2011. Katika mwaka, 2011/2012 utekelezaji wa kazi za dharura katika mji wa Bunda utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu kupitia Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Bukoba ilianza taratibu za kumwajiri Mtaalam Mshauri wa kusanifu miradi ya majisafi katika miji ya Ngara, Muleba, Karagwe, Biharamulo na Bunazi. Mtaalam Mshauri wa kutekeleza kazi hiyo ataajiriwa mwanzoni mwa mwaka huu wa fedha 2011/2012. Kazi ya usanifu inakadiriwa kuchukua miezi 9 mpaka 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya *Lake Victoria Water and Sanitation* (LVWATSAN*)* ulisainiwa tarehe 15 Aprili, 2011 mjini Arusha. Mradi huu unatekelezwa na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Utekelezaji wa Programu hiyo kwa upande wa nchi yetu ni pamoja na kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira katika miji ya Geita, Sengerema na Nansio. Makubaliano ya kutekeleza Programu hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu kati ya Serikali, AfDB na nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki, jumla ya Dola za Marekani Milioni 30.4 ambapo mji wa Geita umetengewa Dola za Marekani Milioni 6.4, mji wa Sengerema Dola za Marekani Milioni 14.8, mji wa Nansio Dola za Marekani Milioni 8.6 na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mwanza wametengewa Dola za Marekani Milioni 0.7 kwa ajili ya usimamizi na uratibu wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hicho cha miaka mitatu kazi zitakazofanyika ni kuongeza mtandao wa majisafi, ununuzi wa vifaa na vitendea kazi, kununua na kufunga dira za maji, ujenzi wa matanki ya maji na ujenzi wa vyoo vya jumuiya katika shule na sehemu za mikusanyiko ya watu wengi. Katika mwaka 2011/2012, shilingi bilioni 3.5 zimekasimiwa kwa ajili ya kuanza kazi ya ujenzi wa miradi ya kukidhi mahitaji ya maji ya muda mfupi katika miji hiyo ambayo itakamilika mwaka 2013. Katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba 2011, Halmashauri ya Mji wa Geita kwa kushirikiana na mgodi wa madini wa Geita (*Geita Gold Mine – GGM*) itatekeleza kazi ya ujenzi wa chanzo, chujio la maji, bomba kuu na matanki mawili kwa gharama ya Dola za Marekani Milioni 4.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Serikali iliendelea kuboresha huduma ya maji mjini Kigoma/Ujiji kwa kununua na kufunga transfoma yenye ukubwa wa KVA 1500 ya gharama ya shilingi milioni 60 ikiwa ni hatua ya dharura katika kukabiliana na tatizo la upungufu wa maji katika mji wa Kigoma/Ujiji. Transfoma hiyo inafanya kazi.

Katika hatua za muda wa kati wa kuboresha huduma ya maji mjini Kigoma, zabuni ya ujenzi wa mradi wa maji zitatangazwa na ujenzi utaanza mwaka 2011/2012. Hatua hizi zitahusu kuboresha mfumo wa majisafi na zitagharamiwa na Serikali kupitia Mfuko wa pamoja wa Sekta ya maji na zitaongeza uzalishaji wa maji kwa wakazi wa Kigoma kutoka mita za ujazo 15,990 kwa siku kwa sasa hadi kufikia mita za ujazo 26,660 kwa siku uboreshaji utakapokamilika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Uswisi kupitia Shirika lake la Maendeleo (*SECO)*, inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupanua na kukarabati mifumo ya majisafi na majitaka ya miji ya Tabora na Dodoma. Kwa mji wa Tabora ufungaji wa

mita kubwa (*Bulk water meter*) katika kituo cha Igombe, mita za maji za Kanda na ujenzi wa chemba za kuhifadhi mita umekamilika.

Katika mwaka 2011/2012 kazi za upanuzi wa mtambo wa kusafisha maji kwenye bwawa la Igombe na mfumo wa usambazaji majisafi zitafanyika na kukamilika mwezi Juni 2013. Kukamilika kwa kazi hizo kutaongeza uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 15,000 hadi kufikia mita za ujazo 30,000 kwa siku. Kwa upande wa mji wa Dodoma kazi ya kufunga mita kwenye chanzo na kwenye kanda mbalimbali imekamilika. Katika mwaka 2011/2012 kazi za upanuzi wa mfumo wa usambazaji majisafi katika maeneo ya Kisasa na Kilimani zitatekelezwa. Mradi huu utagharimu Dola za Marekani milioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Serikali iliendelea kuboresha huduma ya majisafi na majitaka ili kukidhi mahitaji ya muda mfupi katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika kutatua tatizo la maji katika Chuo hicho, Serikali ilitoa shilingi bilioni 2.06 kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu tisa vya maji vya dharura katika eneo la chuo kikuu, maeneo ya Ng'ong'ona, na Iyumbi. Kazi zilizokamilika hadi sasa ni uchimbaji wa visima virefu saba ambapo visima vitano vina maji, kufunga transfoma na uvutaji wa umeme kwenye visima viwili, na ulazaji wa bomba za urefu wa kilomita 1.4. Kazi zinazoendelea ni ufungaji wa transfoma na uvutaji wa umeme kwenye visima vitatu, ununuzi wa pampu tano za uwezo wa mita za ujazo 22 kwa saa kila moja, uchimbaji wa visima viwili vilivyobaki na ujenzi wa mabwawa ya majitaka. Kazi hizo zinatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itatekeleza mradi wa mfumo wa majisafi na majitaka hasa kwa kulenga Chuo Kikuu cha Dodoma. Kazi zitakazotekelezwa ni ulazaji wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 15.5, ulazaji wa mabomba ya kusambaza majisafi umbali wa kilomita 7.5 na ujenzi wa matanki matatu; ulazaji wa bomba kuu la majitaka la umbali wa kilomita 12 na ujenzi wa mabwawa ya majitaka. Mradi huo hadi kukamilika mwaka 2013/2014, utagharimu Dola za Marekani Milioni 26. Taratibu za kumwajiri Mkandarasi zinaendelea na ataanza kazi mwezi Oktoba, 2011.

Katika mwaka 2011/2012, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Korea Kusini itaanza kutekeleza mradi wa maji katika mji wa Dodoma ili kukidhi mahitaji ya muda wa kati, ambapo zimetengwa shilingi bilioni 6. Mradi utahusisha uchimbaji wa visima ili kuongeza uzalishaji kutoka mita za ujazo 30,000 hadi mita za ujazo 61,000 kwa siku, kulaza mabomba mapya na kukarabati mfumo uliopo. Mtaalam Mshauri ataanza kazi mwezi Agosti, 2011 ya kupitia usanifu, kufanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi na uandaaji wa vitabu vya zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 ujenzi wa mradi wa uboreshaji wa miundombinu ya majisafi mjini Singida unaotekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na BADEA na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development-*OFID*)*. uliendelea. Hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 40 ambapo visima virefu sita vimechimbwa kati ya visima 10. Kati ya visima vilivyochimbwa, visima vyenye maji ni vitatu tu. Mabomba ya kusambaza maji yenye urefu wa kilomita 44 yamelazwa. Katika mwaka 2011/2012, ujenzi utaendelea na utakamilika mwezi Juni 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la *Millenium Challenge Corporation* (MCC), iliendelea na utekelezaji wa mradi wa majisafi katika Manispaa ya Morogoro. Hatua zilizofikiwa ni kuanza upanuzi wa mitambo ya kuchuja maji ya Mambogo na Mafiga na ujenzi wa bomba kuu linalochukua maji kutoka chujio la Mafiga kwenda tanki la maji lililo katika maeneo ya Tumbaku na ukarabati wa matanki ya kugawa maji. Mradi huo kwa mwaka 2011/2012 umetengewa jumla ya shilingi bilioni 8.6 na utakamilika mwezi Desemba, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na KfW na EU iliendelea kutekeleza awamu ya pili ya Programu ya majisafi na majitaka katika miji ya Mwanza, Iringa na Mbeya. Katika mji wa Mbeya, ujenzi wa majengo kwa ajili ya mitambo ya kutibu maji maeneo ya Sisimba, Sawaya na Imeta umekamilika, ufungaji wa mitambo ya kutibu maji umefikia asilimia 40; Ujenzi wa matanki 7 yenye ujazo wa mita 6,900 ya kuhifadhia maji

umekamilika eneo la Forest, Iwambi, Iganzo, *VETA,* Iganjo, Nsoho na Idunda; mabomba ya usambazaji maji ya urefu wa kilomita 252 kati ya kilomita 280.15 (asilimia 90) yamelazwa, ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa kilomita 56.8 umekamilika; ujenzi wa mfumo wa majitaka wa urefu wa kilomita 34 kati ya kilomita 38 umekamilika na ujenzi wa mabwawa ya majitaka katika eneo la Kalobe umekamilika kwa asilimia 90. Vyumba vya vyoo 18 vimejengewa katika shule 14 za msingi. Katika mwaka 2011/2012, ujenzi wa mradi utaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mji wa Mwanza, kazi za upanuzi na ukarabati wa miundombinu ya majitaka katika maeneo yasiyo rasmi, uunganishaji wa wateja kwenye mtandao wa majisafi na majitaka na ujenzi wa mitambo ya kusukuma majitaka unaendelea.

Magari matatu ya kuondoa majitaka yamenunuliwa. Mradi wa majitaka ulikamilika na kuzinduliwa tarehe 16.03.2011 wakati wa sherehe za wiki ya maji kitaifa. Wateja 700 kati ya 2,600 wameunganishwa katika mtandao wa majitaka na uunganishaji wa wateja unaendelea. Katika mwaka 2011/2012, kazi ya uunganishaji wateja kwenye mtandao huo itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mji wa Iringa, katika mwaka 2010/2011 kazi ya ujenzi wa miundombinu ya majisafi na majitaka katika mji huo ziliendelea. Hadi kufikia mwezi Mei, 2011 bomba zenye urefu wa kilomita 202 za mtandao wa majisafi kati ya kilomita 428 zimelazwa; ujenzi wa Kitekeo (*intake*), matanki nane na mtambo wa kusafisha maji umekamilika na ujenzi wa mfumo wa majitaka umekamilika kwa asilimia 40.

Katika mwaka 2011/2012, kazi za ukarabati wa mabwawa ya majitaka, ukarabati wa mtambo wa zamani wa kusafisha maji, kulaza bomba za usambazaji majisafi na kumalizia mfumo wa majitaka zitatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea na usanifu wa miradi ya maji kukidhi mahitaji ya maji mpaka mwaka 2025. Kwa upande wa miji mikuu ya mikoa ya Songea, Mbeya, Iringa na Mwanza, kazi ya usanifu na utayarishaji wa zabuni za ujenzi wa miundombinu kwa miji hiyo pamoja na miradi ya maji katika miji midogo na miradi ya kitaifa iliyo katika mikoa hiyo inaendelea.

Katika mwaka 2011/2012, usanifu utakamilika. Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Songea inasimamia usanifu wa miradi katika miji midogo ya Mbinga, Tunduru na Namtumbo, Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mbeya inasimamia miji midogo ya Rujewa, Vwawa, Chunya, Kyela, Kasumulu, Tunduma, Mbalizi, Itumba na Tukuyu; Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Iringa inasimamia miji midogo ya Njombe, Kilolo, Ilula, Mafinga, Ludewa, Makete, Makambako na mradi wa Kitaifa wa Wanging'ombe na Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Mwanza inasimamia miji midogo ya Magu, Nansio, Geita, Misungwi, Ngudu na Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu imekamilisha kazi ya usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni wa miradi ya majisafi na uondoaji wa majitaka katika miji mikuu ya mikoa ya Moshi, Tabora, Arusha, Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Tanga na Kigoma ili kuboresha huduma ya majisafi na majitaka katika miji hiyo. Hatua za utekelezaji wa miradi katika miji midogo iliyo kwenye mikoa mbalimbali imeainishwa kwenye Jedwali Na. 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Kahama na Shinyanga ulizinduliwa tarehe 30 Mei, 2009.

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika miji ya Shinyanga na Kahama na Vijiji 41 imeimarika. Kwa upande wa mji wa Shinyanga hali ya huduma imeongezeka ambapo kwa sasa wakazi wanaopata huduma hiyo wamefikia asilimia 77 ikilinganishwa na asilimia 60 kabla ya kukamilika kwa mradi, na kwa mji wa Kahama imeongezeka kutoka asilimia 40 hadi kufikia asilimia 70.

Hadi kufikia Machi, 2011 wateja 13,117 katika mji wa Shinyanga na 8,308 katika mji wa Kahama waliunganishwa kwenye mtandao na kuanza kupata huduma ya majisafi na salama. Mwaka 2011/2012 Mamlaka za Majisafi katika miji hii zitaendelea na kazi ya kuunganisha wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea kuimarisha uendeshaji wa mradi huu mkubwa wa maji wa Kahama-Shinyanga kwa kuchangia shilingi 578,720,000 ikiwa ni sehemu ya gharama za uendeshaji ikiwemo umeme na madawa ya kutibu maji.

Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Kahama-Shinyanga (*Kahama Shinyanga Water Supply and Sewarage Authority* – KASHWASA) inasimamia uendeshaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, KASHWASA itaendelea kufanya usanifu na kuanza ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji baadhi ya Vijiji ambavyo havijaanza kupata huduma ya maji pamoja na kufanya upanuzi wa mtandao ili kuongeza vituo vya kuchotea maji kwenye Vijiji 41 ambavyo hivi sasa vina matanki na kila kijiji kina kituo kimoja cha kuchotea maji.

Wataalam Washauri wa kufanya usanifu na kutayarisha vitabu vya zabuni za ujenzi wa mradi wa kufikisha maji kutoka Ziwa Victoria hadi miji ya Nzega, Igunga na Tabora pamoja na mradi wa kupeleka maji katika miji midogo ya Kagongwa, Isaka hadi Tinde watapatikana mwezi Oktoba, 2011. Kazi ya usanifu wa miradi hiyo itaanza mwezi Novemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na OWM – TAMISEMI na Halmashauri za Wilaya iliendelea na ukarabati, ujenzi na upanuzi wa miradi ya maji ya miji mikuu ya wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa. Utekelezaji wa kazi hizo ni kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa Chalinze (Awamu ya Pili), unajumuisha usambazaji wa majisafi katika vijiji 48 vilivyogawanywa katika makundi tisa ya utekelezaji. Utekelezaji kwa kundi la vijiji (*package)* F na H unatekelezwa na Serikali kwa kushirikiana na *BADEA*.

Kazi zinazotekelezwa ni ujenzi wa matanki na vituo vya kusukuma maji na kuunganisha maji katika vijiji nane vya wilaya ya Bagamoyo, mkoa wa Pwani ambavyo ni Mdaula, Msolwa, Ubenazomozi, Kaloleni, Mwidu, Visakazi, Matuli na Tukamisasa. Ujenzi ulianza mwezi Septemba 2009 na utaendelea kutekelezwa katika mwaka 2011/2012 na utakamilika mwezi Desemba, 2011.

Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya China inatekeleza kundi la J katika mkoa wa Morogoro kwenye vijiji sita vya Kinonko, Kizuka, Sinyaulime, Sangasanga, Kidugalo na Ngerengere. Ujenzi ulianza mwezi Desemba 2009 na umefikia asilimia 90. Katika mwaka 2011/2012 ujenzi utaendelea na utakamilika mwezi Desemba, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa mradi wa maji Chalinze awamu ya pili. Wakandarasi sita kwa ajili ya utekelezaji katika maeneo yaliyobaki walisaini mikataba ya ujenzi kati ya mwezi Agosti, 2010 na Februari, 2011 na ujenzi wa maeneo haya ambayo yamegawanywa katika makundi sita umeanza. Vijiji vitakavyohusika ni Mihuga, Kwekonje, Mkange, Masimbani, Mandamazingara, Kiwangwa/Mwavi, Fukayosi, Makurunge, Mkenge Kidomole, Masunguru/Mwetemo, Msinune, Pongwe, Msungura, Madesa, Kisanga, Malivundo, Mindukeni, Kinzagu, Makombe, Talawanda, Msigi, Vigwaza, Chamakweza, Buyuni, Visezi, Magindu, Lukenge, Chahua, Gwata, Gumba, Kwaruhombo, Kwang'andu, Pongwe, Kiona na Kifuleta. Katika mwaka 2011/2012, ujenzi utaendelea na utakamilika mwezi Oktoba 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji katika miji ya Ikwiriri, Kibaigwa, Kilosa, Turiani, Mvomero, Kibiti na Gairo. Katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea na ujenzi wa miradi ya maji katika miji saba ya Ikwiriri, Kibiti, Kibaigwa, Kilosa, Turiani, Mvomero na Gairo. Ujenzi wa miradi ya maji katika miji ya Kibiti na Ikwiriri umefikia asilimia 96 na asilimia 75 sawia. Ujenzi wa miradi ya

maji katika miji ya Kibaigwa, Gairo, Turiani, Kilosa na Mvomero umeanza na utakamilika mwezi Juni, 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maji ya Masasi/Nachingwea, Bunda, Igunga na Orkesumet, katika mwaka 2010/2011, miradi ya kuboresha huduma za maji katika miji ya Masasi, Nachingwea, Bunda, Igunga na Orkesumet iliendelea kutekelezwa. Utekelezaji upo katika hatua mbalimbali zifuatazo: -

(a) Mradi wa maji wa Masasi - Nachingwea; ujenzi wa mradi umeanza mwezi Februari, 2011 na mabomba yenye urefu wa kilomita 97 kati ya kilomita 110 Mjini Masasi na kilomita 72 kati ya kilomita 79 yamelazwa Mjini Nachingwea. Bomba kuu la kilomita 3.44 kuelekea Nachingwea limelazwa. Mradi utagharimu jumla ya shilingi bilioni 31. Katika mwaka 2011/2012 ujenzi wa mradi huo utaendelea na utakamilika mwezi Mei, 2012.

(b) Mradi wa maji wa Bunda; katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea na usanifu na uandaaji wa vitabu vya zabuni vya mradi wa maji chini ya Mamlaka ya Maji Mjini Musoma. Katika mwaka 2011/2012, ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi utakaojumuisha chanzo cha maji na bomba kuu kutoka kwenye chanzo utaanza kutekelezwa.

(c) Mradi wa maji wa Igunga; utekelezaji wa awamu ya kwanza ya kuboresha huduma ya maji katika mji wa Igunga ulikamilika mwezi Aprili, 2010 ulihusu ujenzi na ukarabati wa mtandao wa maji, matanki, mbauti za mifugo na vituo vya maji pamoja na ufungaji wa dira za maji. Utekelezaji wa awamu ya pili ambao ulihusisha ujenzi wa chujio ulioanza mwezi Mei, 2010 umekamilika mwezi Juni, 2011.

(d) Mradi wa maji wa Orkesumet; katika kutatua tatizo la maji kwa wakazi wa mji wa Orkesumet, tarehe 21 Aprili, 2011 Serikali ilisaini makubaliano ya awali *(Aide-Memoire)* na Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika *(BADEA)* na Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development - OFID)* kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa mradi wa kuboresha huduma za maji katika mji huo. Katika makubaliano hayo, jumla ya dola za Marekani milioni 18.42 zimepangwa kutumika ambapo dola za Marekani milioni 16 utakuwa ni mkopo wa riba nafuu kutoka *BADEA* na *OFID* na dola za Marekani milioni 2.42 zitatolewa na Serikali. Mkataba kati ya Serikali na *BADEA/OFID* utasainiwa mwezi Agosti, 2011. Katika mwaka 2011/2012 kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na kumwajiri Mhandisi Mshauri atakayepitia usanifu na zabuni zilizoandaliwa awali pamoja na kumteua mkandarasi wa kutekeleza mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa kuboresha huduma za majisafi na majitaka Jijini Dar es Salaam, Jiji la Dar es Salaam na miji ya Kibaha na Bagamoyo inayohudumiwa na *DAWASA* inakabiliwa na uhaba mkubwa wa huduma ya majisafi na huduma duni ya uondoaji wa majitaka. Miongoni mwa changamoto zinazosababisha uhaba huo ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Uchakavu mkubwa wa miundombinu iliyopo ya kuzalisha na kusambaza maji, na uondoaji wa majitaka;

(ii) Kupungua kwa maji ya Mto Ruvu kutokana na uharibifu wa mazingira na ongezeko la vipindi vya ukame;

(iii) Uwekezaji mdogo katika kuboresha na kupanua miundombinu ya kuzalisha na kusambaza maji na pia, uondoaji wa majitaka usiolingana na ongezeko la mahitaji ya huduma husika;

(iv) Ongezeko kubwa la idadi ya watu katika Jiji la Dar es Salaam la asilimia sita kwa mwaka ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4.5 mijini Kitaifa;

(v) Asilimia 70 ya maeneo ya makazi katika Jiji la Dar es Salaam hayajapimwa, hali inayosababisha gharama za usambazaji wa huduma za majisafi na uondoaji majitaka kuwa kubwa; na

(vi) Kuongezeka kwa haraka shughuli za kiuchumi na kijamii katika Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeandaa mpango wa kuboresha huduma ya majisafi na uondoaji wa majitaka Jijini Dar es Salaam unaolenga kuongeza uwezo wa uzalishaji wa maji kutoka mita za ujazo 300,000 kwa sasa hadi 710,000 kwa siku mwaka 2014 na kuongeza kiwango cha huduma ya upatikanaji wa majisafi kutoka asilimia 55 za sasa hadi asilimia 75 ifikapo mwaka 2014 na kufikia asilimia 90 mwaka 2015 na kuongeza uwezo wa uondoshaji wa majitaka kutoka asilimia 10 za sasa hadi asilimia 25 ifikapo mwaka 2014. Mpango huo umeanza kutekelezwa rasmi kuanzia mwezi Februari, 2011 na umepangwa kukamilika mwaka 2013/2014. Mpango huo umekadiriwa kugharimu jumla ya shilingi bilioni 653.85 ambapo kiwango hicho kitachangiwa na Serikali, Mfuko wa Pamoja wa Maji, Shirika la Marekani *(MCC),* Serikali ya Norway na Serikali ya India. Serikali itaendelea kuwasiliana na washirika wengine wa maendeleo katika kuhakikisha mradi huo unatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zinazoendelea kutekelezwa na zitakazotekelezwa kufanikisha mpango huo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Bwawa la Kidunda, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea na tathmini ya athari za jamii na mazingira *(ESIA).* Usanifu na uandaaji wa zabuni ya ujenzi wa bwawa utakamilika mwezi Desemba, 2011. Katika mwaka 2011/2012 ujenzi wa barabara ya kuingilia eneo la bwawa utaanza baada ya kulipa fidia mali za wananchi watakaoathiriwa na ujenzi wa bwawa hili. Kiasi cha shilingi bilioni sita zimetengwa.

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu visima virefu vya Kimbiji na Mpera, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu iliendelea na utekelezaji wa mradi wa uchimbaji wa visima virefu vya Kimbiji na Mpera. Hatua iliyofikiwa hadi Juni 2011 ni kama ifuatavyo:-

(a) Tathamini wa mali katika maeneo ya kuchimba visima 20 vya uzalishaji umefanyika na fidia yenye thamani ya shilingi milioni 617 imelipwa katika eneo la mita 60 kuzunguka eneo la kila kisima;

(b) Mhandisi Mshauri wa kusimamia uchimbaji visima virefu vya Kimbiji na Mpera amepatikana na ameanza kufanya mapitio ya usanifu wa awali. Kazi hiyo itakamilika mwezi Agosti, 2011. Mshauri atasimamia upatikanaji wa mkandarasi atakayechimba visima hivyo; na

(c) Tathmini ya kina ya kubaini mwenendo wa rasilimali za maji chini ya ardhi katika eneo la Kimbiji *(Comprehensive Aquifer Assessment)* imeanza mwezi Aprili, 2011 na itachukua miezi 14 kukamilika. Mtaalam Mwelekezi wa kusimamia kazi hiyo atapatikana hivi karibuni. Uchunguzi huu unafadhiliwa na Serikali ya Norway. *(Makofi)*

Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaanza uchimbaji wa visima virefu 20 vya uzalishaji na kukamilisha tathmini ya mwenendo wa maji ardhini. Makisio ya awali ni kuweza kupata mita za ujazo 260,000 kwa siku kutokana na visima hivyo.

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu, Wizara inaendelea na taratibu za kumwajiri Mhandisi Mshauri atakayefanya usanifu wa upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu na kusimamia ujenzi wa bomba kuu kutoka Kibaha hadi Kimara. Mhandisi Mshauri atapatikana mwezi Oktoba, 2011 na ataanza kazi mwezi Novemba, 2011. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Juu utaongeza uwezo wa mtambo kutoka mita za ujazo 83,000 mpaka mita za ujazo 143,000. *(Makofi)*

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Miradi ya *Millennium Challenge Corporation,* katika mwaka 2010/2011, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Marekani la *Millenium Challenge Corporation (MCC),* iliendelea na utekelezaji wa mradi wa majisafi katika Jiji la Dar es Salaam. Hatua zilizofikiwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, upanuzi wa chujio la maji la Ruvu Chini ulianza mwezi Machi, 2011 na utakamilika mwezi Februari, 2013. Hadi mradi huo ukikamilika utagharimu jumla ya shilingi bilioni 32. Katika mwaka wa fedha 2011/2012 kazi ya upanuzi wa mitambo hiyo itaendelea ambapo jumla ya shilingi bilioni 24.6 zimetengwa. Upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini utakapokamilika utaongeza uwezo wa kuzalisha maji kutoka mita za ujazo 180,000 mpaka mita za ujazo 280,000.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na upanuzi wa mtambo wa Ruvu Chini, Serikali kwa kutumia fedha za ndani na Mfuko wa Pamoja *(Water Basket Fund)* inatekeleza ujenzi wa bomba kuu la maji *(duplícate line)* kutoka mtambo huo hadi Jijini Dar es Salaam. Ujenzi wa bomba hilo utaanza mwezi Oktoba, 2011. Kiasi cha shilingi bilioni 8 zimetengwa kwa kazi hiyo katika mwaka 2011/2012.

(v) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Upunguzaji maji yanayopotea *(Non Revenue Water)* unahusisha utafiti wa matumizi na upotevu wa maji Jijini Dar es salaam. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2011 maeneo nane ya Masaki, Oysterbay, Kinondoni, Mwananyamala, Sinza, Kawe na Upanga yalifanyiwa utafiti kujua idadi halisi ya watumiaji maji, maeneo yanayoendelea kufanyiwa utafiti ni Mikocheni, *Mbezi Beach* na Tegeta.

Upimaji wa upotevu wa maji ulifanyika maeneo ya Mikocheni, *Mbezi Beach,* Tegeta, Oysterbay, Kinondoni, Sinza, Mwenge, Kawe na Upanga. Upimaji wa upotevu wa maji unaendelea kwa maeneo ya Masaki na Mwananyamala. Utafiti umeonesha kwamba upotevu wa maji unatofautiana kati ya eneo moja na lingine na maeneo yenye maji mengi ndiyo yenye upotevu mkubwa wa maji. *(Makofi)*

(vi) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu huduma ya majisafi Dar es Salaam, Kibaha na Bagamoyo, ili kuboresha upatikanaji wa huduma ya maji katika jiji la Dar es Salaam, katika mwaka 2010/2011 Mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam *(Dar es Salaam Water Supply and Sewarage Authority – DAWASA)* imefanya kazi zifuatazo:-

(i) Kuchimba visima virefu saba katika maeneo ya Mburahati (2) na Kimara (5); na

(ii) Kuunganisha wateja 5,000 katika maeneo ya Kimara, Tabata, pia uunganishaji wa wateja 8,800 umefanyika kwenye maeneo ya Kibaha Mjini, Kibaha kwa Matiasi, Kongowe, Visiga na Mlandizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa kuboresha huduma ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam, katika mwaka 2010/2011, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Ubelgiji *(BTC)* na Umoja wa Nchi za Ulaya imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kuboresha upatikanaji wa majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya pembezoni mwa Jiji la Dar es Salaam ambayo hayakuunganishwa na mfumo wa maji wa Jiji. Kazi ya kuchimba visima 18 vya uchunguzi pamoja na usanifu wa mradi imekamilika.

Katika mwaka 2011/2012, visima vitano kati ya 18 vya uchunguzi vitaendelezwa na uchimbaji visima 10 vipya utafanyika. Ujenzi wa mfumo wa majisafi na utoaji wa elimu ya afya na usafi wa mazingira na uhamasishaji wa wananchi kufungua akaunti na kuunda Kamati za maji utafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi na uendeshaji wa huduma za maji mijini, huduma ya majisafi na uzalishaji wa majisafi kwa Mamlaka zote 19 za miji mikuu ya mikoa uliongezeka kutoka wastani wa mita za ujazo 302,857 kwa siku kwa mwezi Machi, 2010 hadi mita za ujazo 306,875 kwa siku mwezi Machi 2011. Kwa upande wa Jiji la Dar es Salaam, mwaka 2010/2011, uzalishaji maji ulikuwa wastani wa mita za ujazo 245,196 kwa siku ikilinganishwa na mita za ujazo 256,055 kwa siku mwaka 2009/2010. Kiwango hicho cha uzalishaji maji kinajumuisha vyanzo vya Ruvu Juu, Ruvu Chini, Mtoni na Visima. Kiwango hiki cha uzalishaji kilipungua kutokana na tatizo la mgao wa umeme na kupungua kwa kina cha maji kwenye mto Kizinga (Mtoni) na mto Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli yatokanayo na mauzo ya maji katika Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa yameongezeka kutoka shilingi bilioni 41.04 mwaka 2009/2010 hadi kufikia shilingi bilioni 42.3 mwaka 2010/2011 sawa na ongezeko la asilimia tatu. Katika kipindi hicho Shirika la Majisafi na Majitaka Dar es Salaam *(Dar es Salaam Water Supply Corporation – DAWASCO)* imeweza kukusanya shilingi bilioni 26.8, ikilinganishwa na shilingi bilioni 26 mwaka 2009/2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufikia mwezi Machi, 2011 ufungaji wa dira za maji kwenye miji mikuu ya mikoa 19 umeongezeka hadi kufikia dira 245,306 ukilinganishwa na dira 226,005 zilizoripotiwa Juni 2010. Ongezeko hilo limefanya idadi ya wateja waliofungiwa dira katika miji hiyo kufika asilimia 92. Hadi kufikia mwezi Machi, 2011 *DAWASCO* ilikuwa na wateja 113,962. Kati ya hao, wateja 95,728 sawa na asilimia 84 wamefungiwa dira za maji. Lengo ni kuwafungia wateja wote wa maji mijini ifikapo Desemba, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wastani wa upotevu wa maji kwenye Mamlaka za Majisafi na Majitaka ngazi ya mikoa kwa mwaka 2009/2010 ulikuwa asilimia 36. Kufikia Machi, 2011 upotevu wa maji umepungua hadi kufikia asilimia 33.5 lengo ni kupunguza upotevu huo hadi asilimia 30 ifikapo mwaka 2015 na hatimaye kufikia asilimia 20 kiwango ambacho kinakubalika Kimataifa. Kwa Dar es Salaam upotevu wa maji umepungua kutoka asilimia 53 mwezi Juni, 2010 hadi kufikia asilimia 48 mwezi Machi, 2011. Lengo ni kufikia asilimia 30 ifikapo mwaka 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, hatua mbalimbali zilichukuliwa katika kuboresha huduma ya maji mijini na yafuatayo ni baadhi ya mafanikio yaliyopatikana:-

(i) Mamlaka za maji ngazi ya miji mikuu ya mikoa kwa sasa zinasambaza maji yenye ubora unaokubalika kutokana na kuwepo kwa uwezo wa kugharamia dawa za kusafisha na kuulia vijidudu kwenye maji. Katika mwaka 2010/2011 Mamlaka ya Majisafi na Majitaka mjini Arusha imefanikiwa kuwa Mamlaka ya pili baada ya Tanga kupata Cheti cha Ubora wa Huduma ya Maji cha Kimataifa cha *ISO* Na, 9001 2000 na Mamlaka zilizobaki za daraja ‘A’ zipo kwenye mchakato wa kupata cheti hicho; na

(ii) Mamlaka zote zinafanyiwa ukaguzi wa hesabu zake *(Audited Accounts)* kwa wakati na kupata cheti cha usahihi kulingana na mwongozo *(operational guidelines).* Mwaka 2009/2010 Mamlaka zote zilipata hati safi *(unqualified)* isipokuwa Mtwara, *DAWASA* na *DAWASCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma ya uondoaji wa majitaka, malengo ya MKUKUTA II ni kuboresha huduma hadi kufikia asilimia 22 ifikapo mwaka 2015 ambapo kwa sasa huduma hiyo inatolewa kwa kiwango cha asilimia 18. Hali hii imetokana na mwamko mdogo wa wananchi kuomba kuunganishwa kwenye mtandao, uchakavu wa miundombinu iliyopo, ongezeko kubwa la watu mijini pamoja na miji mingine kutokuwa na mitandao ya majitaka. Hata hivyo, jumla ya wateja wa majitaka wameongezeka kutoka 17,700 mwaka 2009/2010 hadi kufikia 18,240 mwezi Machi, 2011 sawa na ongezeko la wateja 540. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imeendelea kusimamia Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)* na katika mwaka 2010/2011, *EWURA* imeendelea kudhibiti utoaji wa huduma kwenye sekta za umeme, mafuta ya petroli, gesi asilia, majisafi na majitaka nchini ambapo ubora wa huduma husika umeimarika na bei za huduma hizo zimeendelea kuwa wazi zaidi na za kueleweka kwa wadau mbalimbali. Majukumu ya *EWURA* kwa uchumi wa Taifa ni makubwa. *EWURA* iliendelea kujenga uwezo wake kwa kuajiri watumishi wapya 13 wa fani mbalimbali, kutoa mafunzo kwa watumishi na kuandaa nyenzo mbalimbali za udhibiti zikiwemo sheria ndogo ili kuboresha utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya maji, *EWURA* inadhibiti jumla ya Mamlaka za Maji 129 ikiwa ni pamoja na Mamlaka 19 za Miji Mikuu ya Mikoa, 102 za Miji Mikuu ya Wilaya na Miji Midogo, Miradi ya Kitaifa saba na *DAWASA/DAWASCO.* Hadi mwezi Machi, 2011 Mamlaka za Maji za Miji Mikuu ya Mikoa ya Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza, Tabora, Tanga, Moshi na Morogoro zilitimiza masharti na kupewa leseni za kudumu. Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya mwaka 2009, Sehemu ya 29 (4), leseni

zitadumu kwa kipindi kisichopungua miaka 10. *DAWASA* na *DAWASCO* zinaendelea kutumia leseni waliyopewa mwaka 2005 ambayo nayo itadumu kwa miaka kumi. Mamlaka za mikoa zilizobakia zinaendelea kutoa huduma kwa kutumia leseni za muda. Leseni hizo za muda zinatolewa kwa lengo la kutoa fursa kwa Mamlaka kutimiza masharti ya leseni za kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi mwezi Machi, 2011 Mamlaka 81 kati ya 109 za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa zilikuwa zimeomba leseni za muda. Uchambuzi wa *EWURA* unaendelea ili kuzipatia Mamlaka hizo leseni. Katika mwaka 2011/2012, *EWURA* itaendelea kutoa mafunzo kwa Mamlaka Ndogo, kuchambua na kufanya taftishi kwa maombi ya leseni yatakayowasilishwa na hatimaye kutoa leseni za kudumu kwa watoa huduma za majisafi na majitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, *EWURA* ilipitia na kuchambua taarifa mbalimbali za mwaka 2009/2010 kutoka Mamlaka 19 za Mikoa, *DAWASCO* na Mamlaka 77 za Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Kwa Mamlaka za Makao Makuu ya Mikoa, uchambuzi ulizingatia malengo yaliyo kwenye Makubaliano ya Utendaji *(Performance Agreement)* yaliyosainiwa kati ya *EWURA* na Mamlaka husika. Kutokana na uchambuzi huo, *EWURA* iliandaa taarifa ya pili ya utendaji ya mwaka 2009/2010 inayolinganisha utendaji wa Mamlaka za Maji za Mijini. Taarifa hiyo pia itapatikana katika tovuti ya *EWURA (www.ewura.go.tz). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala muhimu yaliyojitokeza ni, mahitaji ya maji ni makubwa kuliko kiwango cha maji yanayozalishwa na kusambazwa; pamoja na juhudi za ufungaji wa dira za maji kwa wateja bado kiwango cha upotevu wa maji ni kikubwa na mifumo ya majitaka bado ni midogo kuweza kukidhi mahitaji yaliyopo kwenye maeneo ya usambazaji wa huduma. Katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea na utafiti wa vyanzo mbadala vya maji ili kuweza kukidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *EWURA* ina jukumu la kuhakikisha kuwa miundombinu ya majisafi na majitaka inafanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa. Katika mwaka 2010/2011, *EWURA* ilifanya ukaguzi wa miundombinu na kuelekeza namna ya kuboresha ufanisi katika Mamlaka 44 za majisafi na majitaka zilizo katika Miji Mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa. Mamlaka hizo ni za Kasulu, Kibondo, Sengerema, Ngudu, Misungwi, Magu, Mugumu, Kishapu, Mwanhuzi, Sikonge, Urambo, Kiomboi, Manyoni, Bariadi, Kyela, Tukuyu, Rujewa, Njombe, Ludewa, Kilwa-Masoko, Ruangwa, Nachingwea, Masasi, Mangaka, Tunduru, Namtumbo, Mbinga, Chamwino, Kondoa, Kongwa, Mpwapwa, Kilosa, Ifakara, Mahenge, Dakawa-Mvomero, Kilindoni, Mkuranga, Same, Mwanga, Katesh, Mbulu, Babati, Kibaya na Monduli zilizoko katika Miji Mikuu ya Wilaya; Makambako, Kasumulu, Turiani, Gairo na Orkesumet zilizo katika miji midogo, pia Maswa, Makonde na Chalinze zilizo katika ngazi ya Miradi ya Kitaifa. *EWURA* itaendelea kukagua miundombinu ya Mamlaka ili kuhakiki viwango vya huduma za majisafi na majitaka zitolewazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, *EWURA* ilipokea na kuchambua maombi 16 ya bei za maji. Maombi yote yalipata kibali cha kubadilisha bei. *EWURA* iliidhinisha bei mpya za maji kwa Mamlaka za Iringa, Mlowo, Kahama, Ushirombo, Shinyanga, *KASHWASA,* Songea, Nzega, Ilula, Tanga, Moshi, Morogoro, Sumbawanga, Mtwara, Mbeya na Singida. Mwaka 2011/2012, *EWURA* itaendelea kupokea, kuchambua na kuyafanyia maamuzi yanayostahili maombi ya bei mpya za maji yatakayowasilishwa. Kutokana na umuhimu wa maamuzi ya *EWURA* kwa sekta zote inazodhibiti, Mamlaka itaendelea kufafanua kwa wadau misingi ya maamuzi yake na faida zinazopatikana kwa wadau hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kupitia Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji, ina jukumu la kujenga uwezo wa kitaalamu wa fani za ufundi zinazohitajika katika utoaji wa huduma za maji na usimamizi wa rasilimali za maji. Katika mwaka 2010/2011, kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo, kupitia *EU* na *GIZ,* mpango mkakati wa kuanzia 2011 mpaka 2014 wa uendeshaji wa Chuo hicho uliandaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji kilidahili wanafunzi 213 na kukifanya kuwa na wanafunzi 423 wa Stashahada ambao kati ya

hao wanafunzi 98 walihitimu mafunzo yao mwezi Mei, 2011 katika fani za Uhandisi wa Mifumo ya Ugavi wa Majisafi na Uondoaji Taka *(Water Supply and Sanitation)* (52), Utafutaji wa Maji Ardhini na Uchimbaji Visima vya Maji *(Hydrogeology and Well Drilling)* (19), Haidrolojia (9) na Teknolojia ya Maabara za Uchunguzi wa Maji (18), Mafundi Stadi *(Artisans)* 98 watahitimu mafunzo mwezi Novemba, 2011 katika fani mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa katika kuboresha Chuo hicho ni kama ifuatavyo:-

(i) Kununua dawa kwa ajili ya maabara ya ubora wa maji;

(ii) Kukamilisha na kuwasilisha *NACTE* mitaala ya stashahada ya uhandisi wa umwagiliaji na shahada ya kwanza ya uhandisi wa rasilimali za maji na umwagiliaji. Mitaala hiyo imehakikiwa na kuonekana inakidhi mahitaji. Hatua inayofuata ni uhakiki utakaofanywa na *NACTE* wa uwezo wa Chuo kuhusiana na rasilimali watu, majengo, vifaa vya kufundishia na mifumo ya kimenejimenti ya uendeshaji wa Chuo, ili kuamua kama uwezo uliopo unakidhi mahitaji au la.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji kitaendelea kutoa mafunzo kwa ngazi za cheti, stashahada sambamba na kuanzisha mafunzo ya shahada. Ili kupunguza uhaba wa mafundi sanifu, Chuo kinalenga kuongeza idadi ya wanafunzi wanaosajiliwa kwa mwaka ngazi ya stashahada kutoka 213 ya sasa na kufikia 300 wakiwemo wanafunzi wa stashahada ya umwagiliaji ambayo inatarajiwa kuanza mwaka 2011/2012 na idadi ya wanafunzi 40. Chuo kinatarajia kuanza kutoa mafunzo ngazi ya shahada ya kwanza kwa kusajili wanafunzi wapatao 50, mafundi stadi 98 katika ngazi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Pia Chuo kinatarajia kutoa mafunzo ya muda mfupi kwenye fani mbalimbali zinazohusiana na sekta ya maji. Matarajio kwa mwaka 2011/2012 ni kudahili washiriki 500 wa mafunzo ikilinganishwa na washiriki 249 katika mwaka 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Chuo kitaanza kutekeleza mapendekezo yaliyoainishwa kwenye mpango mkakati wa uendeshaji wa Chuo wa kuanzia mwaka 2011 mpaka 2014, ikiwa ni pamoja na kuendelea kutoa mafunzo ngazi ya cheti na stashahada sambamba na kuanzisha mafunzo ngazi ya shahada ya kwanza; kuendelea kuboresha mitaala ya cheti na stashahada katika fani zote zinazotolewa kwenye Chuo hicho na kuboresha mifumo ya *TEKNOHAMA* na ukarabati wa majengo. *(Makofi)*

Katika mwaka 2010/2011, Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa *(DDCA)* umechimba visima virefu 236 nchini kote na unaendelea na ujenzi wa bwawa la Misozwe (Muheza). Wakala pia umefanya uchunguzi wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu katika maeneo 187. Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji imeendelea kuimarisha Wakala huu kwa kununua mitambo mipya sita na vifaa vyake *(rigs and drilling accessories)* kwa ajili ya uchimbaji wa visima, vifaa vya usanifu wa mabwawa na maabara ya udongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji itaendelea kuimarisha Wakala huu kwa kununua mitambo minne mipya ya uchimbaji wa visima. Wakala utakuwa na uwezo wa kuchimba visima virefu 450 katika maeneo mbalimbali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bohari Kuu ya Maji ina jukumu la kununua, kuhifadhi na kusambaza vifaa vya maji. Vifaa hivyo ni pamoja na mabomba na viungio vyake, pampu za kusukuma maji na vipuri vyake, dira za maji na dawa za kutibu na kusafisha maji. *(Makofi)*

Katika mwaka 2010/2011 Bohari Kuu ya Maji iliendelea na shughuli zake za kusambaza vifaa vya maji katika Halmashauri, Mamlaka za maji na miradi mbalimbali ya maji hapa nchini. Miradi iliyopata pampu, mabomba na viungio ni Mugumu, Mvomero, Monduli, Chamwino na Same. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kuibadili Bohari Kuu ya Maji kuwa Wakala wa Serikali zimeanza, lengo ni kuiboresha ili iweze kutoa mchango mkubwa zaidi katika upatikanaji na usambazaji wa vifaa vya miradi ya maji. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea na taratibu za kuibadili Bohari hiyo kuwa Wakala wa Serikali. Wizara itatekeleza mpango wa kuhamisha shughuli za Bohari Kuu ya Maji kwenda eneo la Boko, Dar es Salaam, eneo ambalo ni kubwa zaidi kwa kuhifadhi vifaa na dawa za kutibu na kusafisha maji. Mpango huu, utawezesha upanuzi wa shughuli za ugavi wa vifaa na nyenzo za ujenzi wa miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala mtambuka na sheria, baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, Sheria Na.11 ya mwaka 2009 na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 na Sheria hizo kuanza kutumika rasmi tarehe 1 Agosti, 2009 Wizara yangu imesambaza sheria hizo kwa Halmashauri, Ofisi za Mabonde ya Maji, Mamlaka za maji na wadau wengine wa sekta ya maji. Wizara inaendelea kutoa ushauri wa kisheria kuhusu utekelezaji wa sheria hizo, utayarishaji wa kanuni na mchakato wa kuzitafsiri sheria hizo kwa lugha ya Kiswahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011, Kanuni mbili zilitayarishwa na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali na zimeanza kutumika. Kanuni hizo ni:-

(i) Uteuzi wa wajumbe wa Bodi *(Water Resources Management (Procedure for Nomination of Board Members) Regulations, 2010, GN. No 187 of 21/05/2010). (Makofi)*

(ii) Kuchukua maji kwenye vyanzo na kutiririsha majitaka yanayokidhi viwango kwenye vyanzo. *(The Water Resources Management (Water Abstraction Use and Discharge) Regulations 2010, GN. No. 190 of 21/ 05/2010). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zinazohusu usalama wa mabwawa *(Dam Safety Regulations)* zimeandaliwa na maoni ya wadau yanaendelea kukusanywa ili kuzikamilisha. Maeneo mengine yaliyobaki yanaendelea kufanyiwa tafiti kwanza na taratibu za kuwapata wataalam waelekezi kwa ajili ya kufanya tafiti hizo zimekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea kukamilisha utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, kuzitafsiri sheria hizi kwa lugha ya Kiswahili na kutoa ushauri wa kisheria kwa wadau wote wa sekta ya maji pale unapohitajika.

Mhesimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu wa masuala ya mazingira, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira *(NEMC),* inatekeleza mikakati ya kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji, kudhibiti uchafuzi unaotokana na matumizi ya maji kwa shughuli mbalimbali na kuweka mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Wataalam 21 kutoka katika ofisi za mabonde ya maji walihudhuria mafunzo maalum ya ukaguzi wa mazingira. Katika kutoa elimu ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi jumla ya watendaji wa sekta 50 walipatiwa mafunzo, kati ya hao, viongozi 19 na wataalam 31. Kwa mwaka 2011/2012, Wizara yangu itashirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais katika utekelezaji wa Mkakati wa Hifadhi ya Ardhi na Vyanzo vya Maji na katika kutoa elimu ya mazingira kwa wadau wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la habari, elimu na mawasiliano, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea kuimarisha na kuboresha mawasiliano kati yake na wadau wa sekta ya maji. Elimu na taarifa mbalimbali zilitolewa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari na tovuti ya Wizara ya Maji. Jumla ya vipeperushi 10,000 viliandaliwa na kusambazwa kwa wananchi wakati wa Maonesho ya Nane Nane 2010 yaliyofanyika kwenye viwanja vya Maonesho vya Nzuguni (Dodoma); Maonesho ya Kimataifa ya Biashara yaliyofanyika kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Jijini Dar es Salaam na maadhimisho ya Wiki ya Maji ambayo kwa mwaka huu yalifanyika Kitaifa Mkoani Mwanza. Vipeperushi vingine vilitolewa kwenye maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja mwezi Juni 2011. Vipindi sita vilitolewa kupitia televisheni ambavyo vilifafanua na kuelimisha

masuala mbalimbali ya sekta ya maji. Makala 15 ziliandikwa na kutolewa magazetini na kwenye mitandao ya kijamii ya mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuelimisha wananchi na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu sekta ya maji kwa kuboresha na kutumia tovuti ya Wizara, kuandaa, kutangaza vipindi katika luninga na redio pamoja na kuchapisha jarida la Wizara (Maji Yetu), lengo kuu likiwa ni kuongeza uelewa na kuboresha mawasiliano kati ya wadau wa sekta ya maji na Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu itaendelea kutoa elimu juu ya sheria mpya zinazosimamia utekelezaji wa masuala ya sekta ya maji, mabadiliko ya tabianchi na jinsi yanavyoathiri vyanzo vya maji. Wadau wataelimishwa pamoja na mambo mengine mipango ya sekta ya maji kwa kipindi kijacho mafanikio na changamoto ambazo sekta ya maji imepata tangu tulipopata Uhuru mwaka 1961. Kazi hii itafanyika nchi nzima kama sehemu ya maadhimisho ya sherehe za miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara 1961 - 2011. Vyombo vya habari vitatumika kikamilifu katika azma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu teknolojia ya habari na mawasiliano, katika kipindi cha mwaka 2010/2011 Wizara yangu ilianza kutekeleza mfumo wa kielektroniki wa menejimenti ya takwimu na taarifa za sekta ya maji *(Water Sector Management Information System).* Mfumo huo umeanza kutekelezwa Wizarani, Ofisi za Mabonde ya Maji, Mamlaka za Majisafi na Majitaka ya Miji Mikuu ya Mikoa, Mamlaka za Majisafi ya Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa ya Maji. Watumishi waliopata mafunzo ya Mfumo ni kama ifuatavyo; Wizara (60), Ofisi za Mabonde ya Maji (25), Mamlaka za Majisafi na Majitaka za Miji Mikuu ya Mikoa (40), Mamlaka za Majisafi ya Miji Midogo (99) na Miradi ya Maji ya Kitaifa (10). *(Makofi)*

Awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mfumo huu utaiwezesha Wizara na wadau wote kupata taarifa zinazohusu mipango, mikataba na matumizi ya fedha za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kote nchini kupitia tovuti ya Wizara *www.mowimis.go.tz. (Makofi)*

Wizara yangu pia kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imeanza hatua za utekelezaji wa mfumo huu wa kielektroniki kwenye ngazi ya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Mafunzo ya jinsi ya kutumia mfumo kwa ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa *(LGAs)* yameanza kufanyika kote nchini ambapo jumla ya watumishi 157 watakuwa wamepewa mafunzo kufikia mwezi Agosti, 2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu itaendelea kuimarisha utekelezaji wa mfumo wa kielektroniki wa menejimenti ya taarifa za sekta ya maji *(Water Sector Management Information System)* kwa kutoa mafunzo zaidi na kupanua matumizi yake (utekelezaji wa awamu ya pili) ili uweze kupokea taarifa na takwimu zote zinazohusiana na utekelezaji wa mipango na utoaji wa huduma. Wizara itaendelea na uboreshaji wa mifumo ya mitandao ya mawasiliano katika sekta ya maji ambapo itahusisha pia ununuzi wa vifaa na vitendea kazi vya kisasa vya *TEKNOHAMA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia itaanza kutekeleza mifumo miwili ya kielektroniki inayohusu usimamizi na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali magari *(Fleet Management and Control System)* pamoja na ule wa utunzaji na ufuatiliaji wa kumbukumbu na nyaraka mbalimbali *(Records Management and Files Tracking System).* Lengo ni kuwezesha Wizara kupunguza gharama za uendeshaji na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu jinsia, katika kutekeleza Sera ya Taifa ya Maji ya mwaka 2002 na Sheria za Maji za mwaka 2009, Wizara yangu imehamasisha uundaji wa jumuiya za watumia maji ambazo kisheria zinawashirikisha wanaume na wanawake. Usajili wake hufanywa na Ofisi za Mabonde ya Maji na katika Halmashauri za Wilaya. Kupitia Sheria Na. 11 ya mwaka 2009 ya Rasilimali za Maji, jumla ya jumuiya za watumia maji 51 zikiwa na jumla ya vikundi 188 zimeandikishwa kote nchini. Kupitia Sheria Na. 12 ya mwaka 2009 ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, jumla ya jumuiya za watumia maji 700 zimeandikishwa kote nchini. Jumuiya hizo zina maamuzi makubwa katika masuala ya kutumia maji katika maeneo yao. Kimsingi zinaundwa kwa

kuelekeza kuwepo uwiano wa kijinsia. Watumishi watano wanawake walishiriki katika uzinduzi wa Muongo wa Wanawake wa Afrika 2010 – 2020 uliofanyika Nairobi, Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea kuhamasisha jamii kusajili jumuiya za watumia maji na kutoa mafunzo ya usimamizi wa utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini, mafunzo ambayo yanawashirikisha wanaume na wanawake katika jumuiya zao. Wizara itaendelea kutoa fursa sawa kwa jinsia zote katika ngazi za maamuzi na uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vita dhidi ya rushwa, katika mwaka 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa iliendelea kuwaelimisha watumishi umuhimu wa kuzingatia maadili katika kazi zao. Kupitia kitengo cha ukaguzi wa ndani na Kamati ya Huduma kwa Mteja katika Wizara yangu, Wakurugenzi na Wajumbe wote wa Kamati ya Menejimenti walipatiwa mafunzo ya tahadhari *(Risk Management).* Kitengo hiki na Kamati hii vimejiimarisha katika kutoa ripoti zake za ukaguzi wa masuala ya uongozi na utawala mara kwa mara taarifa ambazo zimesaidia kuwakumbusha watendaji na watumishi wote kwa ujumla kufanya kazi kwa bidii wakizingatia taratibu, kanuni na sheria za kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2011/2012 Wizara yangu itaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa katika sekta ya maji. Mapambano hayo yatahusisha uimarishaji wa Kamati ya Maadili ya Wizara, matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya kuharakisha ufuatiliaji na uwazi wa matumizi ya fedha za umma na utoaji wa taarifa zinazohusu matumizi ya magari. Mifumo hiyo mikubwa ya kielektroniki ni pamoja na *water sector management information system, document management system, and fleet management and control system.* Mifumo ya kielektroniki itaweka wazi mipango ya Wizara, matumizi ya rasilimali na pia kuondoa urasimu wa kupata taarifa na kutoa huduma. Wizara itaendelea kuimarisha Kamati ya Kusimamia Uadilifu ili iweze kutimiza majukumu yake ipasavyo. Wizara itahakikisha Sheria, Kanuni na Taratibu zinazohusu maadili katika utumishi wa umma zinazingatiwa ipasavyo katika kutoa huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara yangu iliendelea kuwahamasisha watumishi kuelewa athari zitokanazo na janga la UKIMWI, kutoa elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na kuwahamasisha upimaji wa hiari ili kufahamu hali za afya zao. Wizara iliwaelimisha watumishi kwa njia ya vitabu na vipeperushi vyenye ujumbe wa UKIMWI. Jumla ya vipeperushi 6,000 na vitabu 350 viligawiwa kwa watumishi. Wizara kupitia Waraka wa Utumishi kuhusu kutoa huduma ya posho kwa lishe bora ya walio na maambukizi itaendelea kutoa posho hiyo kwa watakaojitambulisha kuwa na maambukizi. Tayari watumishi saba wenye VVU wanapatiwa fedha kwa ajili ya kununua lishe ya mlo kamili na mahitaji mengine muhimu kwa afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu pia imekuwa ikitumia utaratibu wa kuzialika Taasisi zinazotoa huduma ya kuelimisha umma kuhusu UKIMWI ikiwa ni pamoja na *AMREF,* kuwepo katika mabanda ya Wiki ya Maji ili kutoa elimu kwa wadau kuhusu UKIMWI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara iliendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi na usimamizi wa mipango ya kisekta. Wizara ina jumla ya watumishi 1,766. Watumishi 180 wamepandishwa vyeo katika nafasi mbalimbali na watumishi 23 wameajiriwa. Katika mwaka 2011/2012, Wizara itaajiri watumishi 81 ili kukidhi Ikama ya watumishi 1,857. Jumla ya watumishi 243 watapandishwa vyeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2010/2011 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi za Utekelezaji *(Implementing Agencies)* wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)* imeanza kutekeleza mpango wa kuwajengea uwezo watumishi *(capacity development plans).* Katika utekelezaji wa mpango huo wa kuwajengea uwezo, watumishi wameweza kupata mafunzo mbalimbali yaliyoainishwa katika mpango. Watumishi na watendaji katika Halmashauri za Wilaya na Mikoa ya Mwanza, Arusha, Dodoma, Morogoro na Mbeya wameweza kupata mafunzo ya usimamizi wa utekelezaji wa programu ndogo ya maji vijijini. Watumishi 290 walipatiwa mafunzo katika usimamizi wa rasilimali maji. Watumishi 200 walipatiwa mafunzo kupitia Mkutano wao Mkuu wa mwaka kuhusu Uendeshaji wa Mamlaka za Maji Mijini. Watumishi 18 wanahudhuria mafunzo ya

muda mrefu katika ngazi ya Shahada na Shahada ya Uzamili na watumishi 284 wanachukua mafunzo ya muda mfupi ngazi ya Cheti na Stashahada. Kwa mwaka 2011/2012 utekelezaji wa mpango wa kuwajengea uwezo watumishi *(capacity development plans)* utaendelea kutekelezwa kwa kuwapatia mafunzo watumishi na wadau wetu wengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika kutimiza majukumu iliyokasimiwa inakabiliana na changamoto mbalimbali na imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuzikabili. Changamoto hizo na hatua zinazochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

(a) Kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi na kijamii nchini;

(b) Utoaji wa huduma ya maji unakabiliwa na changamoto ya kuongezeka kwa idadi ya watu kusikoendana na uwekezaji. Hali hiyo ni dhahiri katika maeneo ya mijini ambapo kiwango cha ongezeko la watu kwa mwaka ni asilimia 4.5 tofauti na maeneo ya vijijini ambapo wastani wa ongezeko la watu kwa mwaka kitaifa ni asilimia 2.3. Mathalan, Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kutokana pamoja na mambo mengine, ongezeko kubwa la watu la asilimia sita kwa mwaka tofauti na wastani kitaifa wa asilimia 4.5. Kukua kwa shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ongezeko kubwa la viwanda na kupanuka kwa ujenzi wa makazi kumeongeza mahitaji ya maji. Kutokana na ukuaji huo wa kasi, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kiwa ni pamoja na:-

(i) Kushirikisha wananchi hususan katika maeneo ya vijijini katika hatua zote za miradi ikiwa ni pamoja na kubuni, kujenga, kusimamia, kuendesha na kuchangia gharama za uendeshaji.

(ii) Kukarabati na kujenga miradi ya kipaumbele ambayo inatoa huduma kwa wananchi wengi zaidi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mradi wa maji wa vijiji 10 kwa kila Halmashauri; na

(iii) Mradi wa dharura wa kuboresha huduma za maji Jijini Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na kujenga bwawa la Kidunda na kuchimba visima virefu vya maji vya Mpera na Kimbiji, kujenga mradi wa maji wa Mwanga – Same - Korogwe, kujenga bwawa la Farkwa kwa ajili ya mji wa Dodoma na kutekeleza mradi wa maji wa Masasi - Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi yanasababisha kutokutabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu, mafuriko ya mara kwa mara hali inayoathiri ujenzi wa miundombinu ya maji na upatikanaji wa rasilimali za maji. Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na:-

(a) Kujenga mabwawa madogo na makubwa kwa ajili ya hifadhi ya maji kwa ajili ya matumizi mbalimbali;

(b) Kuimarisha ukusanyaji wa takwimu zinazohusu rasilimali za maji na mabadiliko ya tabianchi.

(c) Kutoa mafunzo kwa wataalam ili kuongeza weledi kuhusu mabadiliko ya tabianchi.

(d) Kutumia utaalam asilia *(Indigenous knowledge)* katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

(e) Kushirikisha wadau mbalimbali katika kutunza vyanzo vya maji.

(f) Kuhamasisha uvunaji wa maji ya mvua.

(g) Kuendeleza matumizi ya teknolojia sahihi za umwagiliaji zinazotumia maji kwa ufanisi; na

(h) Kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais na Taasisi za Kiserikali na Zisizo za Kiserikali zinazofanya utafiti kuhusu mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kufanya utafiti wa pamoja na kutathmini matokeo ya tafiti mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa rasilimali za maji, pamoja na nchi yetu kuwa na maji mengi yanayopatikana kwenye mito, maziwa, chini ya ardhi na maeneo oevu, baadhi ya maeneo hukumbwa na uhaba wa maji kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Maji yanayofaa kwa matumizi mbalimbali yanaendelea kupungua mwaka hadi mwaka kutokana na ongezeko la watu, ongezeko la uzalishaji mali katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme, kilimo cha umwagiliaji na matumizi ya viwandani na majumbani na uharibifu wa mazingira ya vyanzo vya maji. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Serikali inaendelea kusimamia na kuhakikisha vyanzo vya maji vinatunzwa dhidi ya uharibifu na uchafuzi na kuhakikisha maji yanatumika kwa njia endelevu kwa kutumia sheria za maji na kanuni zake na kuzihimiza Halmashauri kutunga sheria ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine inayoikabili sekta za maji ni uwezo mdogo katika ngazi za utekelezaji na usimamizi wa miradi ya maji. Pia uwezo wa sekta binafsi katika kushiriki kikamilifu kwenye utekelezaji wa miradi katika sekta ya maji. Ili kuimarisha uwezo wa kitaasisi na uwezo wa kiutendaji wa watumishi, Wizara inatekeleza Mpango wa Kuimarisha Uwezo wa Kiutendaji *(Capacity Development Plan)* ambao ulianza kutekelezwa mwaka huu wa fedha 2010/2011. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, limekuwepo tatizo la kupata takwimu sahihi za matumizi ya fedha ngazi za Halmashauri, Mamlaka za Maji Mijini na Ofisi za Mabonde ya Maji kutokana na kukosekana kwa mtandao wa kuratibu masuala ya fedha katika ngazi hizo.

Pia kumekuwepo mawasiliano hafifu na wadau wengine wanaotoa mchango mkubwa wa kuendeleza utoaji wa huduma ya maji ikiwa ni mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya dini na watu binafsi. Hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na mapungufu haya ni zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa taasisi za sekta kuhusu uboreshaji wa utoaji wa taarifa za utekelezaji.

(ii) Kuweka Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa na Takwimu za Sekta ya Maji *(Water Sector Management Information Sytem)* utakaoboresha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati.

(iii) Wizara yangu, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na Wizara ya Fedha tunaendelea na majadiliano kuweka utaratibu wa kupata taarifa za matumizi ya fedha za Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira kwa usahihi na kwa wakati; na

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, kubaini michango ya wadau wengine wa sekta ya maji, kumekuwepo mawasiliano hafifu na wadau wengine wanaotoa mchango wa kuendeleza utoaji wa huduma ya maji ikiwa ni pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Dini na watu binafsi. Mapungufu haya yanasababisha kutoelewa kiwango cha uchangiaji, muda wa utekelezaji, na idadi ya wananchi wanaofaidika na huduma hizo. Hatua zinazochukuliwa katika kukabiliana na changamoto hiyo ni pamoja na kuimarisha mawasiliano na wadau hao kwa kuwashirikisha katika vikao mbalimbali vinavyojadili masuala ya sekta ya maji ili kubadilishana uzoefu na kubainisha kiwango cha uchangiaji, muda wa utekelezaji na idadi ya wananchi wanaofaidika na huduma hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sasa kutumia fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyingine katika kuiwezesha Wizara yangu kufanikisha majukumu yake. Nakiri kwamba mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2010/2011 ni kutokana na jitihada za pamoja, ushirikiano na misaada ya kifedha na kitaalam kutoka kwa washirika wa maendeleo ikiwa ni pamoja na nchi wahisani, mashirika ya misaada, taasisi zisizo za Kiserikali, mashirika ya kidini na taasisi za kifedha. Napenda kuzishukuru Serikali za Ujerumani, Japan,

Ufaransa, Jamhuri ya Watu wa China, Uholanzi, Uswisi, Ubelgiji, Uingereza, Ireland, Korea ya Kusini, Sweden, Norway, India, Misri na Marekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa taasisi za fedha za Kimataifa ikiwa ni pamoja na Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika *(BADEA),* Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya *(EIB),* Mfuko wa Maendeleo wa Nchi Zinazozalisha Mafuta *(OPEC Fund for International Development - OFID),* Benki ya Maendeleo ya Ujerumani *(KfW),* Shirika la Kiufundi la Ujerumani *(GIZ),* Umoja wa Ulaya *(EU),* Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo *(UNDP),* Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Makazi Duniani *(UN Habitat),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto *(UNICEF),* Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA),* Shirika la Marekani la *Millennium Challenge Corporation (MCC)* na Shirika la Misaada la Marekani *(USAID)* kwa misaada ya fedha na michango yao ya utaalam katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayashukuru mashirika ya kidini ya *World Islamic League,* Shirika la *Ahmadiya Muslim Jamaat Tanzania, Islamic Foundation,* Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania, Kanisa la Kilutheri la Ujerumani, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Kanisa Katoliki Tanzania, Kanisa la Kianglikana Tanzania, *Catholic Agency for Overseas Aid and Development (CARITAS), Norwegian Church Aid* na *Livingwater International. (Makofi)*

Nashukuru pia taasisi zisizo za Kiserikali za *Tanzania Water and Sanitation Network (TAWASANET),* Wahamasishaji wa Maji, Maendeleo na Afya *(WAMMA), Southern Highlands Participatory Organizasition (SHIPO), WaterAid, World Vision, Plan International, Concern, Netherlands Volunteers Services (SNV),* Shirika la Kimataifa la Kuhifadhi Uasili *(IUCN), World Wide Fund for Nature (WWF), African Medical Research Foundation (AMREF), Clinton HIV Aids Initiative (CHAI)* na *Bill and Melinda Gates Foundation* na wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wameendelea kuisaidia sekta ya maji katika kutekeleza majukumu tuliyopewa. Naomba kwa dhati kabisa, kupitia kwako Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwashukuru wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mnyimi wa fadhila kama sitawashukuru watu binafsi wanaotoa mchango katika utoaji wa huduma ya maji nchini. Nitumie fursa hii kumshukuru kwa njia ya kipekee Mzee Mustafer Jaffer Sabodo kwa uamuzi wake wa kugharamia uchimbaji wa visima 700 katika mikoa yote nchini. *(Makofi)*

Nayashukuru pia makampuni binafsi ikiwa ni pamoja na Kiwanda cha Bia Tanzania *(TBL)* na vyama vya hisani vya *Lions Club* na *Rotary Club* na makampuni binafsi mengine ambayo siyo rahisi kuyataja yote, kwa misaada yao ambayo wanaendelea kuitoa katika kuboresha huduma za maji kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii haitakuwa imekamilika kama sitatoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamana kubwa aliyonipa kwa mara nyingine tena kuiongoza Wizara yenye dhamana juu ya uhai wa Watanzania. Naomba nitumie fursa hii kumthibitishia kwamba nitajitahidi kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia kutoa utumishi kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa utayari wake wa kushirikiana nami pamoja na wananchi katika kuboresha huduma ya maji nchini. Pia natoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake uliotukuka ambao umetusaidia katika kutekeleza majukumu yetu. Ni imani yangu kuwa kama ilivyokuwa katika kipindi cha kwanza cha uongozi wake, Wizara yangu itaendelea kunufaika na maelekezo yake katika kipindi chake hiki cha pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kutoa shukrani za pekee kwa wananchi wote na wadau wengine ambao sikuweza kuwataja mmoja mmoja ambao naamini walishirikiana vyema na Wizara yangu katika kutekeleza majukumu yake. Naomba kutoa shukrani za pekee kwako wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge ambao uongozi wenu mzuri wa Bunge lako Tukufu umechangia kwa kiwango kikubwa katika

kuboresha utoaji wa huduma za maji nchini. Nawashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao wanayotoa ndani na nje ya Bunge hili inayolenga kuboresha sekta ya maji. Wizara yangu itaendelea kushirikiana nao kwa lengo la kuinua hali ya maisha ya wananchi na uchumi wa Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu haitakuwa kamili kama sitatoa shukrani za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Rungwe Mashariki kwa imani yao kubwa waliyoionyesha kwangu kwa kunirejesha kwenye nafasi ya Ubunge kwa kunipitisha bila ya kupingwa kwa mara ya tatu mfululizo. Hii ni heshima kubwa sana kwangu waliyonipa wananchi wa Rungwe Mashariki. Nami nawaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa juhudi na maarifa na unyenyekevu mkubwa kwa kadri Mwenyezi Mungu atakavyonijalia. *(Makofi)*

Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo la Njombe Magharibi kwa niaba ya Mheshimiwa Mhandisi Gerson Hosea Lwenge, Naibu Waziri wa Maji kwa ushirikiano wanaompatia katika kutekeleza majukumu ya Jimbo lake na yale ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa njia ya pekee nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mhandisi Gerson Hosea Lwenge, Naibu Waziri wa Maji, kwa msaada na ushirikiano anaonipatia katika kipindi kifupi tulichofanya kazi pamoja katika kuiongoza Wizara ya Maji. Umahiri wake hasa katika kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge umeisaidia sana Wizara yangu. *(Makofi)*

Naomba pia nitoe shukrani zangu kwa Mhandisi Christopher Nestory Sayi, Katibu Mkuu, Mhandisi Bashiri Juma Mrindoko, Naibu Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Vitengo, viongozi wa Mashirika na Taasisi chini ya Wizara yangu, wataalam na watumishi wote kwa kujituma katika kusimamia utekelezaji wa majukumu tuliyopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mhandisi Ngusa Izengo, Katibu wa Waziri kwa sasa na aliyekuwa Katibu wangu hapo awali, Mwenyekheri Ndimbo. Nawashukuru Makatibu Mahsusi katika ofisi yangu Bibi Loice Mwakatundu na Bibi Janeth Petro, Msaidizi wa Ofisi Bibi Bevenia Myolla. Namshukuru Bwana Athumani Fernandes, dereva wangu wa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, naishukuru familia yangu, mke wangu Lucy, watoto Max, Sekela na Emmanuel, mkwe wangu Digna na wajukuu Tusekile na Lusekelo. Siku zote wamekuwa nguzo iliyo imara katika kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 446,094,636,000 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka 2011/2012. Kati ya fedha hizo, Matumizi ya Kawaida ni shilingi 17,455,673,000 ambapo shilingi 11,868,205,000 ni mishahara ya watumishi *(PE)* na shilingi 5,587,468,000 ni fedha za Matumizi Mengine *(OC).* Jumla ya Bajeti ya Maendeleo ni shilingi 428,638,963,000 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 41,565,045,000 ni fedha za ndani na shilingi 387,073,918,000 ni fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena nitoe shukrani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anwani *www.maji.go.tz .* Maji ni uhai, na usafi wa mazingira ni utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki! *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono na hivyo inakidhi vigezo vya kuendelea. *(Makofi)*

Sasa kabla sijamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, nilitaka kidogo nichukue muda mchache kuweka sawa sawa kwa maslahi tu ya taarifa za Bunge.

Wakati Mheshimiwa Spika akitambulisha wageni, aliwataja wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge na akauliza mama yuko wapi! Labda kwa taarifa tu ni kwamba Mheshimiwa Gerson Lwenge, Naibu Waziri wa Maji, mkewe alikwishatangulia mbele za haki mwezi Oktoba, 2008. Kwa hiyo, nilidhani tuweke vizuri ili isije ikaleta shida kidogo.

Lakini pia kuna wageni walikuwa wamesahaulika, wageni wa Mheshimiwa Vick Kamata, Grace Kamata, Joseph Kamata, Deo, Hassan na Ray, karibuni sana na wageni wa Mheshimiwa Suleiman Bungara, Waheshimiwa Madiwani hawa, Mheshimiwa Mahadh Nangoma na Mheshimiwa Abdallah Oga, karibuni sana. Basi tuendelee sasa. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA M. HAMID (K.N.Y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha taarifa hii. *(Makofi)*

Kwa niaba ya Kamati na kwa masikitiko makubwa napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Mussa Khamis Silima kwa kufiwa na mke wake katika ajali mbaya ya gari iliyotokea jana. *Innah lillah wainnah lillah rajuun.*

Pia napenda kumpa pole Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mwandosya na kumwombea kwa Mungu apate nafuu haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru mume wangu mpenzi Bwana Hamid Ahmed Hamid na mtoto wetu Aisha Hamid, mama yangu mpendwa Apia Sauga na wadogo zangu George Mgaya na Monica. Napenda pia niwashukuru wapiga kura wangu, vijana wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dar es salaam na Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani za pekee na kwa heshima kubwa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge akinamama wa Chama cha Mapinduzi kwa kuniamini na kunichagua kwa kura nyingi katika nafasi Baraza Kuu UWT Taifa kupitia Bunge, nami nawaahidi ushirikiano mzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji ilikutana na Wizara ya Maji tarehe 26 Mei, 2011 katika Ofisi Ndogo ya Bunge ya Dar es Salaam ili kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti, maoni ya Kamati, changamoto zilizojitokeza kwa mwaka 2010/2011 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2010/2011 wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa Serikali. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni ya Kamati. Napenda kutaja baadhi ya maeneo ambayo utekelezaji wake unaonekana ikiwa ni pamoja na Wizara imeshalipa jumla ya shilingi bilioni 90.8 ikiwa ni madeni iliyokuwa inadaiwa na wadai mbalimbali wakiwemo makandarasi ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi haukwami kutokana na malipo kutofanyika kwa wakati. *(Makofi)*

Pia maji kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam, tathmini ya athari ya mazingira na kijamii kwenye maeneo ya Kimbiji na Mpera imekamilika na Waziri wa Nchi mwenye dhamana ya Mazingira ametoa hati ya kukubali utekelezaji wa mradi. Aidha fidia ya shilingi bilioni 617 imelipwa kwa wanachi 130 wenye maeneo yaliyopo ndani ya mita 60 kuzunguka eneo la kila kisima kitakachochimbwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupungua kwa kiasi cha maji Dodoma, Serikali imetuma kwenye mamlaka ya Majisafi na Majitaka Dodoma jumla ya shilingi bilioni 2.06 kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu vinne na ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uchimbaji wa mabwawa ya majitaka katika Chuo Kikuu cha Dodoma. Aidha, ujenzi wa bwawa la Farkwa utaongeza vyanzo vya maji kwa mji wa Dodoma. *(Makofi)*

Mradi wa Maji wa Vijiji Kumi, jumla ya Halmashauri 129 zimeajiri wataalamu washauri na wanaendelea na kazi ya utafiti na upimaji wa vyanzo vya maji na usanifu wa miradi ya maji. Pia upotevu wa maji kutokana na uchakavu wa miundombinu, *DAWASA* imefunga mabomba mapya na kufanya ukarabati wa mabomba yenye urefu wa kilomita 1,550. Aidha, uhamasishaji wa wananchi kuhusu elimu ya uvunaji wa maji ya mvua kwa njia mbalimbali umefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Wizara katika kutekeleza majukumu yake, bado inakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa ni kikwazo katika kufikia malengo iliyojiwekea, baadhi ya changamoto hizo ni:-

(i) Kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa na ucheleweshaji wa utoaji fedha za maendeleo na hivyo kuathiri utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Wizara;

(ii) Kuongezeka kwa idadi ya watu na shughuli za kiuchumi na kijamii nchini hususan katika maeneo ya mijini wakati miundombinu ya maji bado ni ya zamani. Hii husababisha wananchi wengi kutofikiwa na huduma ya maji;

(iii) Athari za mabadiliko ya tabianchi zimesababisha kutotabirika kwa msimu na mtawanyiko wa mvua, ukame wa muda mrefu kwa baadhi ya maeneo kukauka kwa vyanzo vya maji na mafuriko kwa maeneo mengine ambayo yameleta uharibifu wa miundombinu ya maji na umwagiliaji;

(iv) Uchafuzi wa vyanzo vya maji kutokana na matumizi ya kemikali katika maeneo ya uchimbaji wa madini; na

(v) Uwezo mdogo wa utekelezaji wa miradi katika ngazi zote zinazotekeleza na kusimamia miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maombi ya fedha na malengo ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Maji na Umwagiliaji chini ya Fungu 49 ili kutekeleza majukumu yake inaomba jumla ya shilingi 446,194,636,000/=. Kati ya fedha hizo shilingi 17,455,673,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 428,638,963,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi 13,145,374,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 4,310,299,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, kati ya fedha za maendeleo, shilingi 41,565,045,000/= ni fedha za ndani na shilingi 387,073,918,000/= ni fedha za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zinazoombwa zitaiwezesha Wizara kutekeleza kazi mbalimbali ilizojipangia. Baadhi ya kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kuendeleza na kusimamia rasilimali za maji kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi;

(ii) Kuandaa mipango shirikishi kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za maji;

(iii) Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji;

(iv) Kuelimisha umma masuala yanayohusu sekta za maji;

(v) Kununua vifaa na nyenzo za kazi za Wizara;

(vi) Kuandaa na kusambaza sheria za maji na kanuni zake;

(vii) Kuandaa na kutekeleza *TEKNOHAMA* katika ngazi ya Mabonde ya Maji;

(viii) Kupanua na kukarabati miradi ya maji vijijini inayoendelea kutekelezwa;

(ix) Kufuatilia ubora wa maji na usimamizi wa mfumo wa ikolojia; na

(x) Kuratibu na kufuatilia utunzaji na udhibiti wa rasilimali za maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012, baada ya kuelezea utekelezaji wa maoni ya Kamati, mafanikio na changamoto zilizoikabili Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu Bajeti ya Wizara, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Maji toka shilingi bilioni 30.7 mwaka 2010/2011 hadi shilingi bilioni 41.5 mwaka 2011/2011. Pamoja na pongezi hizi, Kamati inashauri Serikali iendelee kuongeza Bajeti ya Maji ili kupunguza utegemezi wa fedha za wahisani na kufikia lengo la kuongeza maji na hatimaye kutokomeza kabisa tatizo la maji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maji yanahitajika kwa ubora na usalama wake katika jamii; na kwa kuwa dawa za kutibu maji hayo zinatozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT),* Kamati inaishauri Serikali kuondoa kodi hii ili kupunguza gharama za upatikanaji wa maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mtiririko wa utoaji wa fedha za maendeleo, miradi mingi ya maendeleo inashindwa kukamilika kwa wakati kutokana na utoaji wa fedha kutozingatia muda. Kamati inaishauri Serikali ifanye jitihada za kuhakikisha kuwa fedha za maendeleo zinatolewa kwa wakati ili iweze kufanya kazi iliyokusudiwa.

Aidha, utoaji wa fedha za maendeleo uzingatie tabianchi ili utekelezaji wa baadhi ya shughuli za maendeleo ufanyike kwa kuzingatia hali ya hewa, mfano kipindi cha masika na kipindi cha kiangazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni hitaji la msingi la maisha na uhai wa viumbe vyote katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa umeme, bidhaa za viwandani, matumizi ya majumbani na usafi wa mazingira. Katika nchi yetu huduma ya maji bado haijatosheleza mahitaji ndiyo maana maeneo mengi wananchi wanataja ukosefu wa huduma za maji kuwa ndiyo tatizo kubwa linalowasumbua. Kutokana na umuhimu huu, Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inazipongeza Mamlaka za Majisafi na Majitaka kwa kazi nzuri zinazozifanya za kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Pamoja na jitihada hizo, Kamati inashauri Mamlaka ziangalie upya taratibu zinazotumika katika kuandaa ankara za maji hususani maeneo ya mijini kwa kuwa kumekuwa na tabia ya kutoza wateja gharama kubwa kuliko kiasi cha maji wanachotumia na wakati mwingine wanatozwa bila hata kupata maji kabisa. Aidha, Serikali kupitia mamlaka zake iweke utaratibu wa kusajili visima vikubwa vinavyochimbwa kwa wingi mijini na kuviwekea utaratibu wa matumizi bora ya maji. Hatua hii itasaidia kudhibiti uchimbaji wa visima usio salama. *(Makofi)*

(ii) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa uhaba wa maji ni tatizo kubwa kwa nchi yetu, Kamati inashauri Serikali iendelee kuhimiza na kuhamasisha jamii kwa kutoa elimu ya utaratibu wa uvunaji wa maji ya mvua kwa ajili ya matumizi mbalimbali kuliko kutegemea maji ya visima au bomba ambayo hayatoshelezi. Aidha, kwa kuzingatia ukubwa wa tatizo hili kwa jiji la Dar es Salaam, Serikali itoe kipaumbele kwa upatikanaji wa maji katika jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

(iii) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kubuni mradi huu wa vijiji kumi ambao unalenga kupunguza tatizo la maji vijijini. Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kufanya yafuatayo:-

(a) Kutafuta namna ya kuuendeleza mradi huu ili uwafikie wananchi wengi zaidi;

(b) Kwa miaka ijayo, Bajeti ya mradi iongezwe na ipanue wigo wa mradi kwa vijiji vingi zaidi nchini;

(c) Serikali ihakikishe utafiti wa kina unafanyika kabla ya kuchimba visima ili kuepuka upotevu wa fedha nyingi zinazotumika kuchimba visima na maji yasipatikane;

(d) Serikali iweke mkakati wa kuvitazama upya visima vya asili ili viweze kupunguza tatizo la maji;

(e) Kuweka viwango vya ubora wa pampu za maji ya visima ili kuepusha hasara zinazotokana na kuharibika kwa pampu hizo mara kwa mara kutokana na ubora hafifu (sheria ya manunuzi itumike);

(f) Serikali itoe elimu kwa wananchi ya utunzaji mzuri wa pampu za maji ili kuepuka uharibifu unaotokana na matumizi yasiyosahihi ya pampu hizo. Aidha, usimamizi na ufuatiliaji wa visima vya maji uimarishwe sambamba na kuhakikisha kuwa vipuri vya pampu hizo na mafundi wa kuzihudumia pampu hizo wanakuwepo wakati wanapohitajika; na

(g) Kwa kuwa visima vingi hutoa maji kipindi cha masika ambapo mvilio *(water table)* huwa juu na kwa kuwa mvilio hushuka kipindi cha kiangazi na kusababisha ukosefu wa maji katika visima, Kamati inashauri visima vyote kuchimbwa kipindi cha kiangazi hii itahakikisha kwamba maji yanapatikana majira yote ya mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa maji yanayopatikana ni kidogo kulingana na mahitaji halisi, bado kuna kiasi kikubwa cha upotevu mkubwa wa maji unaotokea kutoka kwenye vyanzo vya maji kwenda kwa watumiaji. Kamati inashauri Serikali iendelee kukarabati miundombinu ya maji ili kutokomeza tatizo hili. Aidha, tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika vyanzo vya maji lipatiwe ufumbuzi wa kudumu kwani linapunguza kasi ya uzalishaji maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati. Pia napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, uvumilivu na michango yao mizuri wakati wa kupitia na kuchambua kwa kina Bajeti ya Wizara hii. *(Makofi)*

Naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo, Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Mwenyekiti na Wajumbe ambao ni Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, Mheshimiwa Abdulsalaam Amer, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Namelok Sokoine, Mheshimiwa Dkt. Christina Ishengoma, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mheshimiwa Moshi Kakoso, Mheshimiwa Sylvester Kasulumbayi, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Amina Makilagi, Mheshimiwa Mansoor Hiran, Mheshimiwa Maria Hewa, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa Rose Sukum, Mheshimiwa Juma Othman Ali, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Selemani Bungara, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani na mimi mwenyewe Neema Mgaya Hamid, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Maji Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Gerson Lwenge, Katibu Mkuu *Engineer* Christopher Sayi pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa ushirikiano na juhudi wanazofanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah na Katibu wa Kamati hii, Ndugu Elieka Saanya kwa kuihudumia vema Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha 2011/2012 jumla ya shilingi 446,194,636,000/=. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Maji, Mheshimiwa Highness Kiwia. *(Makofi)*

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba upokee shukrani zetu za dhati kwa kunipa nafasi hii kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kuhusu Mapitio na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 99(7), Toleo la mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mungu wetu ni *Alpha* na *Omega,* ndiye mwanzo na mwisho wa kila jambo. Ni wajibu wa kila chenye pumzi kumsifu na kumtukuza yeye. Nina kila sababu ya kumshukuru kwa kunipa fursa hii ya utumishi kwa nafasi ya Ubunge katika Jimbo la Ilemela. Ninaamini Mwenyezi Mungu anapokupa kazi, hakika anakupa na uwezo wa kuikamilisha. Hivyo, ni dhahiri kwamba ahadi zote nilizotoa kwa wananchi wa Ilemela, hakika zitatimia, na kama vile giza lisivyoweza kuishinda nuru, ni dhahiri kuwa kamwe udhalimu hautaishinda haki katika Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najivunia msimamo, ujasiri na ukakamavu wa wananchi wa Jimbo la Ilemela. Pamoja na vitisho vingi, mabomu ya machozi, virungu vya dola, nguvu ya pesa, kampeni chafu na mbinu zote za kujaribu kupindua chaguo halali la watu wa Ilemela, bado wenyewe hawakuwa tayari kurudi nyuma. Walipigania maendeleo yao ya miaka mitano kwa kuhakikisha nakuwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu kabisa nachukua fursa hii kuwashukuru wazee wa Ilemela, mama zangu wa Ilemela na vijana wenzangu wa Ilemele, kwa kuamini kuwa naweza kusimamia vema hatma ya maendeleo yao. Naahidi kuwa nguvu ile ile waliyoitumia kuhakikisha nakuwa Mbunge wao, ndiyo nitakayoendelea kuitumia katika kusukuma maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii pia kwa heshima na taadhima kubwa, kumshukuru Kiongozi wetu Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Naibu Kiongozi, Mheshimiwa Kabwe Zitto na Wabunge wenzangu wote, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge na yale ya Uwaziri kwa nafasi yangu kama Waziri Kivuli wa Maji na Umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa mke wangu Iyvone na watoto wetu Witness, Prudance, Highness Junior na Blessing, pamoja na mama yangu mzazi na ndugu na jamaa wote kwa kuendelea kuniunga mkono wakati wote ninapokuwa kwenye hekaheka za kuwapigania na kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchukua fursa hii kumpa pole Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mark Mwandosya na kwa niaba ya Kambi ya Upinzani tunamuombea ili aweze kurejea nchini aendelee kulitumikia Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji na Umwagiliaji Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliwahi kusema; “Ufisadi na rushwa ni adui mkubwa zaidi wa maslahi ya wananchi wakati wa amani kuliko vita.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nasaha hii, ni ukweli usiopingika kuwa jitihada zozote zinazofanyika katika Taifa hili, za kujaribu kuondoa kero na matatizo ya wananchi, ikiwemo shida kubwa ya maji, kamwe hazitafanikiwa bila kwanza kuupiga vita ufisadi. Wakati umefika sasa wa kuweka ushabiki wetu pembeni, itikadi zetu pembeni, vyama vyetu pembeni na kuunganisha nguvu zetu wote pamoja na kusema nchi kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai wa binadamu na viumbe vyote vilivyopo, na maji ndiyo injini ya msingi katika kusukuma maendeleo ya binadamu, hata wachunguzi wa masuala ya amani na usalama wa dunia wametahadharisha kuwa ikiwa kutatokea vita ya tatu ya dunia basi chanzo cha vita hiyo itakuwa ni kugombania maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa huduma ya maji, Serikali yoyote ile makini duniani haitarajiwi kwa namna yoyote ile kuipuuza sekta ya maji; haitarajiwi kutenga Bajeti ndogo kwa ajili ya maji, na wala viongozi na watendaji wake hawapaswi kufuja au kuiba fedha za miradi ya maji, maana kufanya hivyo ni kuuweka rehani uhai wa wananchi na kubomoa msingi mzima wa maendeleo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinyume chake pamoja na vyanzo vingi vya maji vilivyopo nchini, mito mikubwa, maziwa, chemichemi asilia na ardhi yenye maji, leo miaka 50 baada ya Uhuru katika kila Watanzania 100, ni Watanzania 50 tu ndio wanaopata maji, tena yasiyo na uhakika wa kutosha. Serikali imetumia miaka 50 kupeleka maji kwa nusu tu ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji na Umwagiliaji badala ya kuwa mstari wa mbele katika kulinda uhai wa wananchi na maendeleo yao, imekuwa ndiyo moja ya Wizara zilizo mstari wa mbele kabisa katika kufanya ubadhirifu wa fedha za umma zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maji. Kambi Rasmi ya Upinzani siku zote inahakikisha inatumia ushahidi wa kutosha kupinga ufisadi unaofanywa ndani ya Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili tuna ushahidi wa Ripoti ya Ukaguzi Maalum *(Special Audit)* uliofanywa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG),* uliofanywa kwenye Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita kwa mfululizo kuanzia mwaka 2007 hadi 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ripoti hiyo Wizara hii imegundulika kufanya ubadhirifu wa zaidi ya dola za Marekani milioni 39 (sawa na takribani shilingi bilioni 63 za Kitanzania) kwenye mazingira ya utata bila kuzingatia miradi na kiasi cha fedha zilizotengwa kwenye mpango kazi wa mwaka wa Wizara hiyo. Shilingi bilioni hizo 63 zilizofujwa, ni nyingi sana kuliko fedha zote zilizotengwa kugharamia miradi ya maji katika vijiji vyote nchini kwa mwaka wa fedha 2011/2012 (ambazo ni bilioni 50).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa fedha nyingi zinazoingia Serikalini kutokana na kodi za wananchi, mauzo ya rasilimali mbalimbali kama madini na misaada mingi iliyotolewa na nchi Wahisani kwa miaka yote 50 tangu Uhuru, zimekuwa zikifujwa ndani ya Wizara ya Maji na Idara zake mbalimbali, na matokeo yake Watanzania wa mijini na vijijini wanateseka kwa kukosa maji. Akinamama wengi vijijini wanatembea umbali mrefu wakiwa na watoto mgongoni kutafuta maji ambayo yangeweza kupatikana karibu na makazi yao kama fedha za miradi ya maji zisingekuwa zinafujwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ukaguzi huo imebainika kuwa fedha nyingi za umma zilifujwa katika ununuzi wa mashangingi *(Toyota Land Cruiser)* yapatayo 68 uliofanyika mwaka 2009 kwa Yen za Japan milioni 235.4 (sawa na takribani shilingi bilioni 5 za Kitanzania) kinyume

kabisa na Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004. Aidha, imegundulika kuwa ununuzi huo wa mashangingi umeisababishia nchi yetu hasara ya zaidi ya shilingi milioni 218, kutokana na tofauti ya viwango vya ubadilishaji wa pesa za kigeni kutozingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya maagizo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji, Mifugo katika mwaka wa fedha uliopita, yaliitaka Wizara ya Maji iendelee kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji kwenye Halmashauri. Sehemu ya agizo hilo la Kamati ilisema, nanuku; "Kamati bado inashauri, Serikali Kuu bado ni msimamizi wa miradi yote nchini, hivyo isiziachie Halmashauri pekee na badala yake isimamie kuratibu ili miradi ya maji iweze kuleta matokeo mazuri," mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ripoti hiyo imebainika kuwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, haikuwa inafuatilia kwa karibu matumizi ya pesa za miradi ya maji zinazopelekwa kwenye Halmashauri mbalimbali nchi nzima na hivyo kutojua kama pesa hizo zimetumiwa kwenye matumizi sahihi ama la. Matokeo yake, kumefanyika matumizi makubwa ya pesa kwenye miradi mbalimbali ya maji kuliko gharama halisi za awali zilizokubaliwa kwenye miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan mradi wa ujenzi wa Bwawa la Matwiga awali gharama halisi ilikuwa dola za Marekani 284,693, (sawa na takribani shilingi milioni 427), lakini Wizara hii iliongeza malipo ya ziada kwenye mradi huo ya dola 80,615 (sawa na takribani shilingi milioni 129 za Kitanzania). Kwenye mradi wa Mpwapwa na Utete, gharama halisi ya kutekeleza mradi huo ilikuwa shilingi milioni 69.6, lakini Wizara hii ilitumia fedha nyingine zaidi kiasi cha takribani shilingi milioni 56.7, sawa na ongezeko la asilimia 81 la bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maji Safi na Taka ya Moshi nayo ilitumia takribani shilingi bilioni 1.5 kuilipa kampuni ya *Seureca Consulting Engineers* ya Ufaransa kushirikiana na *NETWAS Tanzania Ltd.,* wakati mkataba na kampuni hiyo ulikuwa ni wa malipo ya shilingi milioni 485 tu. Malipo hayo ya ziada ni sawa na asilimia 212 ya gharama zilizokubaliwa awali za mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 7(2)(a) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma kinazitaka taasisi za umma zinazofanya manunuzi zitoe taarifa tu kwa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma *(PPRA)* juu ya mkataba na mabadiliko ya bei za mikataba zitakazotokea. Nanukuu, *"....to be advised of the award and, where applicable, the variation of any public contract by the procuring entity responsible for such contract,"* mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki hakisimamii vizuri manunuzi ya umma, kwani hakijaweka ukomo wa bei za mikataba, na kwa hiyo kimekuwa kikitoa mwanya kwa watendaji wasio waaminifu kufanya vitendo vya kifisadi kwa kushirikiana na wazabuni kama vile kuongeza gharama za miradi kutoka kwenye bei halisi za zabuni kulingana na makubaliano ya pande mbili husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani tunaitaka Serikali ikifanyie marekebisho kifungu hiki kwa kuhakikisha kuwa kinaweka ukomo katika ongezeko la bei za mikataba, ili kulazimisha mikataba kuingiwa kwa gharama sahihi na kuokoa fedha nyingi za umma zinazopotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukomesha tabia hii ya kifisadi uliokithiri, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka viongozi na watendaji wote wakuu waliokuwa na dhamana ya kuisimamia Wizara hii (kati ya mwaka 2007 - 2010), akiwemo Mheshimiwa Waziri wa Maji, wasimamishwe kazi mara moja kwa kuzembea au kushindwa kutimiza wajibu wao wa kuisimamia Wizara hii, hata kusababisha ubadhirifu mkubwa kufanyika na Taifa kuingia hasara kubwa ya zaidi ya shilingi bilioni 63. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunataka uchunguzi huru na wa haraka ufanyike kubaini uhusika wa kila mmoja wao katika ufisadi huo na hatimaye watakaobainika wachukuliwe hatua kali za kinidhamu na kushitakiwa kwa mujibu wa Sheria Namba 200 ya Uhujumu Uchumi ya mwaka

2002. Ni lazima Bunge la Kumi limalize utamaduni mbaya wa kulindana na kujenga utamaduni mpya wa kuwajibishana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa nchi yetu ipo hatarini kuingia kwenye mgogoro mkubwa na nchi jirani ya Malawi katika kugombania eneo la Ziwa Nyasa. Tuna taarifa kuwa Serikali ya Malawi inapanga kutoa leseni na kutafuta mafuta kwa Kampuni ya *Sure Stream Petroleum Ltd.* eneo ambalo lipo *block* hiyo imeenea inahusisha sehemu ya Tanzania. Uamuzi huu wa Serikali ya Malawi unaweza kuleta vurugu ya kimipaka na hata vita kati ya nchi hizi mbili. Wakati Serikali yetu inasema mipaka ya Ziwa Nyasa ni kati ya Ziwa hilo Serikali ya Malawi inasema mpaka ni ufukweni na kwa mantiki hiyo Ziwa lote wanalichukua kuwa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji ndiyo inahusika na usimamizi wa Bonde wa Ziwa Nyasa na kwa hiyo, inapaswa kuwa na taarifa hizi. Kambi Rasmi ya Upinzania tunahoji je, ni hatua gani Serikali yetu imechukua kulinda Ziwa Nyasa na maji yake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kipindi ambacho kampuni za mafuta duniani zinahaha kutafuta maeneo ya kuwekeza hata kuingilia maeneo ya maji, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba Serikali ifanye mazungumzo ya haraka na Serikali ya Malawi na kuunda *Joint Development Zone* na hivyo kutoa leseni hii kwa pamoja na utafutaji uendelee kwa kusimamiwa na nchi zote mbili wakati wa utatuzi wa mpaka huo unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali yetu iiambie Serikali ya Malawi kwamba kuendelea kutoa leseni kwa kampuni ya *Sure Stream* itakuwa ni sawa na kuvamia eneo la Tanzania na kwamba Tanzania itachukua hatua stahili kulinda mipaka yake. Mifano ya *Joint Development Zone (JDZ)* ipo katika nchi za Senegal, Guinea Bisau, Australia, Papua, Indonesia na Malyasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo wa Bajeti ya Maji 2011/2012, mbali na ubadhirifu mkubwa wa fedha za umma Wizara hii pia inakabiliwa na changamoto ya kutengewa fedha zisizolingana na ukubwa wa shida ya maji nchini. Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inayotengwa kutokana na fedha za ndani imeporomoka kwa asilimia 46, kutoka shilingi bilioni 78 za mwaka 2006/2007 hadi kufikia takribani shilingi bilioni 41.5 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, athari ya kuporomoka huko ni Serikali kuendelea kutenga fedha kidogo kwa miradi ya maji hususan kwenye maeneo ya vijijini, licha ya kuwa vijijini ndiko kwenye wananchi wengi wenye shida kubwa ya maji. Mathalan, wakati Jiji la Mwanza linahitaji jumla ya shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya kulaza mabomba ya kusambaza maji safi, Wizara imetenga jumla ya shilingi bilioni 2.2 tu kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji safi kwa Mwanza, Mbeya, Songea, Singida, Iringa na miji yote midogo iliyo ndani ya mikoa hiyo. Ni dhahiri kuwa Bajeti yote ya Wizara hii ni ndogo mno na haiwezi hata kidogo kupunguza shida ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, randama ya Wizara inaonyesha kuwa kwa mwaka 2011/2012, Wizara itatumia jumla ya shilingi bilioni 50.7 kwa ajili ya Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini sawa na asilimia 26.8 tu ya fedha zote na itatumia shilingi bilioni 313.5 kwa ajili ya Programu ya Maji Safi na Majitaka mijini ambazo ni sawa na asilimia 73.14 ya fedha zote za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina taarifa kuwa baadhi ya nchi wahisani zimetishia kukataa kutoa fedha kwa ajili ya Bajeti ya Maji kwa mwaka huu wa fedha kwa sababu fedha zao nyingi walizotoa huko nyuma zimefujwa. Wakati kukiwa na tishio hilo, Wizara hii katika mwaka wa fedha 2011/2012, inategemea kutekeleza Programu ya Maji Safi na Maji Taka Mijini kwa kutegemea fedha za Wahisani hao hao kwa asilimia 75. Kwa hiyo, Wahisani wasipotoa fedha zao, miradi ya maji mijini itakwama kwa asilimia 75. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza ukubwa wa Bajeti ya Miradi ya Maendeleo ya Maji hususan kwa maeneo ya vijijini ambayo yamepunjwa na kupunguza athari za Bajeti tegemezi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya marekebisho, yafuatayo:-

(i) Serikali itumie mapato ya ziada tuliyoainisha katika Bajeti yetu mbadala na kuhakikisha inaongeza ukubwa wa Bajeti ya miradi ya maendeleo hususan kwa vijijini.

(ii) Shilingi bilioni 213 zilizosalia kwenye fungu la *Special Roads Construction Projects, Sub vote 2005, item 4168* baada ya kutoa shilingi bilioni 95 kwenda Wizara ya Uchukuzi, kwenye Wizara ya Ujenzi, ziongezwe kwenye Bajeti ya Maji ili kutekeleza miradi ya maji, kwani fedha hizo bado hazina kazi mahsusi mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa maji wa vijiji kumi, kwa mujibu wa taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini iliyowasilishwa na Waziri wa Maji na Umwagiliaji Februari 14, 2011 hapa Bungeni hadi kufikia mwezi Desemba, 2010 kulikuwa na jumla ya miradi ya maji 4,134 tu iliyokuwa imejengwa au kufanyiwa ukarabati huku ikikadiriwa kuwanufaisha wananchi milioni 2.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizo inaweza ikajengeka dhana kuwa programu hii imewakomboa watu wengi sana wakati hali haiko hivyo. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali na Bunge lako Tukufu litilie maanani mambo yafuatayo:-

(i) Miradi ya maji 4,134 iliyopo vijijini mpaka sasa bado ni kidogo sana ikilinganishwa na mahitaji ya wananchi wote waliopo kwenye vijiji vyote 13,000 nchi nzima.

(ii) Kwa programu hii ya kupeleka maji kwenye vijiji kumi tu vya kila Halmashauri, hata Serikali ikifanikiwa kuanzisha miradi kwenye vijiji kumi vya Halmashauri zote 132 inazopanga kuzifikia, bado idadi ya vijiji vitakavyokuwa vimefikiwa itakuwa ni vijiji 1,320, sawa na asilimia kumi ya vijiji vyote 13,000 vilivyopo nchini.

(iii) Kwa hiyo, zaidi ya asilimia 90 ya vijiji italazimika kusubiri kwa miaka mingi zaidi hadi awamu yao ya kufikiwa na programu hii itakapofika.

(iv) Pia Mradi huu umekuwa na ushirikishwaji mdogo wa wananchi katika kuibua, kufuatilia na kusimamia miradi ya maendeleo, matokeo yake fedha za mifuko ya maendeleo zikimekuwa zikifujwa kutokana na kukosekana kwa usimamizi madhubuti kutoka kwa wanaotakiwa kusimamia ambao ni wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni Wilaya ya Hanang ambapo kwenye vijiji vya Katesh, Gehandu, Meng'enyi na Mirongori kwa mwaka 2007/2008, ruzuku ya maendeleo *(Capital Development Grants-CDG)* na fedha za programu ya maji kwenye vijiji kumi *(WSDP),* zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya miradi ya maji kwenye maeneo hayo takribani kila mwaka, lakini bado maji ni shida, takwimu zinaonyesha kuwa Mifuko ya *TASAF, SIROP, QUICKWIN* na wafadhili wa *ADRA* walishatekeleza miradi kwenye maeneo hayo. Jambo la kujiuliza ni je, fedha zilizotengwa na Serikali Kuu, Halmashauri pamoja na wafadhili hao zilikwenda wapi? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuchukua hatua za haraka sana katika kufuatilia suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza mapungufu ya mradi wa maji wa vijiji kumi; Kambi ya Upinzani tunaitaka Serikali kutekeleza yafuatayo:-

(i) Serikali izingatie mapendekezo yote tuliyotoa kuhusu kuongeza ukubwa wa Bajeti Kuu ya Serikali na Wizara hii ya Maji.

(ii) Wizara ya Maji na Umwagiliaji, ishirikiane kwa karibu na Halmashauri zote katika kusimamia miradi hiyo, huku ikizijengea uwezo wa kitaasisi na kitaalam Halmashauri hizo, ili baada ya muda mfupi ziendelee kuibua, kutekeleza na kusimamia miradi yake yenyewe.

(iii) Serikali ichunguze na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria viongozi na watendaji wote waliohusika kufanya ufisadi kwenye miradi ya maji vijijini, ili kuongeza nidhamu katika kusimamia miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tatizo la maji katika Jiji la Dar es salaam, kwa muda mrefu sasa Jiji la Dar es Salaam limekuwa likikabiliwa na shida kubwa ya maji. Taarifa ya Hali ya Uchumi inaeleza kuwa hadi kufikia mwezi Desemba, 2010 katika kila watu 100, ni watu 55 tu ndio wanaopata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukubwa wa shida hii unatokana na ukweli kuwa mahitaji ya maji katika Jiji la Dar es Salaam ni kiasi cha mita za ujazo 450,000 kwa siku, lakini mpaka sasa kiasi cha maji kinachopatikana ni mita za ujazo 300,000, ikiwa ni upungufu wa mita za ujazo 150,000; na asilimia 50 ya maji yanayozalishwa hupotea, kwa sababu ya uchakavu wa miundombinu na wizi wa makusudi wa maji unaofanywa na baadhi ya watu wanajiunganishia maji kinyume cha taratibu kwa maslahi yao binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakiwa wanakabiliwa na shida kubwa ya maji, Kambi ya Upinzani imebaini kuwa kasi ya Serikali katika kushughulikia shida hiyo bado ni ndogo sana, kwani taarifa iliyowasilishwa kwa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Maji na Mifugo, inaonyesha kuwa wakazi wa Dar es Salaam watalazimika kusubiri hadi mwaka 2013 ndipo miradi ya kupeleka maji zaidi kwenye jiji hilo ikamilike; wakati taarifa hiyo ikionyesha hivyo, Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano unaonyesha kuwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam watalazimika kusubiri hadi mwaka 2016, ndipo miradi ya kuwapatia maji ya uhakika ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ijieleze ni lini hasa maji ya kutosha na ya uhakika yatapatikana kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, maana taarifa ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Bunge na kile kilichopitishwa kwenye Mpango wa Maendeleo, vinapingana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, Kambi Rasmi ya Upinzani haiko tayari kuona wakazi wengi wa Jiji la Dar es Salaam hususan wale wa kipato cha chini wakiendelea kupata shida ya maji hadi mwaka 2016 au 2013 kama taarifa za Kiserikali zinavyoonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupunguza makali ya tatizo la maji katika Jiji la Dar es Salaam, Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali ichukue hatua za dharura zifuatazo:-

(i) Serikali itenge fedha za kutosha katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kuharakisha uchimbaji wa visima kwenye maeneo mengi yenye shida kubwa ya maji katika Jiji la Dar es Salaam, ili kupunguza makali ya tatizo hilo, huku tukisubiria miradi mikubwa kukamilika.

(ii) Serikali ichunguze na kudhibiti wizi na upotevu mkubwa wa maji katika Jiji la Dar es Salaam, kwa kuhakikisha inakarabati kwa haraka miundombinu chakavu na kuwachukulia hatua wale wote walioingilia mfumo wa bomba kwa kujiunganishia maji kibinafsi hata kusababisha wakazi wengi wakose maji.

(iii) Serikali kupitia *DAWASA* ivunjwe mara moja kwani imeshindwa kusimamia vizuri mkataba wake na *TAWASCO. EWURA* ikamilishe mara moja kanuni za kusimamia bei ya maji kwenye sekta binafsi na itangaze mapema bei elekezi za kuuzia maji kwani tafiti zinaonyesha kuwa mwananchi anayenunua kwenye vioski au madumu hulipia mara 15 zaidi kuliko yule anayepata huduma ya maji ya bomba. *(Makofi)*

(iv) Serikali ihakikishe Kampuni ya Usambazaji Maji Dar es Salaam *(DAWASCO),* inatekeleza kikamilifu mapendekezo yote yaliyotolewa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali toka mwaka wa fedha 2007/2008. *(Makofi)*

(v) Viongozi na watendaji wote walioisababishia *DAWASCO* hasara ya shilingi bilioni 12.6, wasimamishwe mara moja na kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu na kisheria. *(Makofi)*

(vi) Wizara ishirikiane na mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi Zisizo za Kiserikali na vyombo vya dola, kudhibiti biashara ya vyuma chakavu na kuelimisha wananchi kulinda miundombinu ya maji isihujumiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mapendekezo hayo ya dharura, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itumie mapema fursa za fedha za Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano, zilizotengwa kwa miaka ya 2013/2014, 2014/2015 na 2015/2016, kuharakisha ukarabati na upanuzi wa bomba kuu la maji kutoka Ruvu Juu, Ruvu Chini, ujenzi wa Bwawa la Kidunda na uchimbaji wa Visima Virefu vya Kimbiji na Mpera, ili miradi hiyo ikamilike angalau mwaka 2012, badala ya kusubiria hadi mwaka 2016. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani ina uhakika kuwa miradi hiyo ikikamilika, Jiji la Dar es Salaam litakuwa na maji ya kutosha, kwani tafiti zinaonyesha kuwa Mradi wa Kimbiji na Mpera pekee ukikamilishwa, visima vyake vitakuwa na maji mengi yanayokisiwa kufikia robo ya Maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo sugu la maji Tabora, Mji wa Tabora umekuwa katika tatizo kubwa la maji kwa muda mrefu sasa bila kupatiwa ufumbuzi. Ukosefu mkubwa wa maji Tabora unawaathiri zaidi akinamama na watoto kiasi cha kushindwa kufanya shughuli nyingine za maendeleo kwa kupoteza muda mwingi katika kutafuta maji. Ili kumaliza tatizo hili la maji, Serikali inapaswa kuunganisha Mji wa Tabora katika Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Kahama - Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati shida ya maji Tabora ikiwa ni kubwa sana, ya muda mrefu na inayohitaji kupatiwa ufumbuzi wa haraka, randama ya Wizara imeeleza kuwa Serikali itaanza kutekeleza mradi wa kupeleka maji Tabora mwezi Septemba, 2012 na mradi huo utakamilika mwaka 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshtushwa sana na mpango huo wa Serikali wa kupeleka maji Tabora mwaka 2014, kwa namna yoyote ile huo ni ukatili. Ni vema Serikali hii ikaelewa kuwa maji ni uhai na kadri yanavyocheleweshwa ndivyo maisha ya watu wa Tabora, Igunga, Kagongwa na maeneo mengine wanavyozidi kuteseka. Kambi Rasmi ya Upinzani haiko tayari kuona wananchi wa mkoa huo wakiendelea kuteseka kwa kukosa maji hadi mwaka 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 ni mbali sana, Serikali hii kama ilivyokubali hoja yetu ya kuwa na mpango wa umeme wa dharura, tunaitaka sasa ije na mkakati wa dharura wa kuhakikisha wananchi wa Tabora Mjini, Kagongwa, Igunga, Nzega, Tinde, Isaka na wa vijiji vingi vya mkoa huo, wanapata maji safi na salama haraka iwezekanavyo, huku mradi huo mkubwa wa kutoa maji Shinyanga ukiendelea kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na huduma bora za maji katika Majiji, Miji Mikuu ya Mikoa na Wilaya zote nchini, ni lazima kuwe na mamlaka imara za maji. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani imebaini kuwa Mamlaka nyingi za maji hapa nchini bado zinafanya kazi kwa kutumia mitandao ya kizamani sana katika kusambaza maji kwa wananchi. Mitandao hiyo imechoka hivyo kusababisha kiasi kikubwa cha upotevu wa maji yanayosambazwa kwa gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mamlaka za Maji katika Majiji na Miji mingine katika mwaka wa fedha wa 2010/2011, Mamlaka za Maji za Miji mbalimbali ziliendelea kuonyesha udhaifu wa kiutendaji kwa kusababisha upotevu mkubwa wa maji. Mfano wa mamlaka hizo ni Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Dodoma ilipoteza jumla ya mita za ujazo 4, 273,467; Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Shinyanga *(SHUWASA)* iliyopoteza mita za ujazo 856,687; Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Singida *(SUWASA)* iliyopoteza mita za ujazo 549,731 na mamlaka nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizi zinaonyesha kuwa wakati wananchi wa mijini wakihangaika kupata maji, maji mengi yanapotea bure kwa sababu tu ya udhaifu wa kiutendaji wa mamlaka hizi. Mathalan maji ya mita za ujazo 4,273,467 yaliyobainika kupotea katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Dodoma, ni sawa na mara tisa ya maji yanayohitajika kuwatosheleza wakazi wote wa Jiji la Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upotevu huu mkubwa wa maji umekuwa ukisababisha kupungua kwa mapato na uwezo wa mamlaka hizi katika kuongeza huduma za maji ambazo

mahitaji yake yanazidi kuongezeka kila siku. Hali hii pia inasababisha mamlaka hizi kuwa tegemezi kwenye mikopo na misaada kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Ukaguzi uliofanywa na *CAG* katika Mamlaka za Maji kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011, imebaini kuwa udhaifu huo umesababisha jumla ya shilingi bilioni 12.8 kutumika vibaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inahoji, je, ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watumishi ambao wamezembea wajibu wao hata kusababisha upotevu mkubwa wa maji katika miji hiyo? Na ni hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watumishi wa mamlaka za maji ambao wamekuwa wakizembea au kufanya ufisadi wa mabilioni ya fedha za maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa mteja anapohitaji huduma ya maji nyumbani kwake inamlazimu kujinunulia vifaa vyote muhimu kwa ajili ya kuunganishiwa maji, je, huu ndio utaratibu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iziwezeshe mamlaka hizi kupata mikopo ya benki, ili zifanye uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya maji ambayo kwa asilimia kubwa ni chakavu. Ili kuleta ufanisi wa kutosha kwa Mamlaka za Maji nchini ni vema Serikali ikahakikisha inalipa ankara za maji kwa taasisi zake kupitia Wizara mama za taasisi husika ili kuondoa udhaifu unaoonekana dhahiri kwa Taasisi za Serikali kuzembea kulipa ankara hizo. Mathalan ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha taasisi zake zinalipa deni la jumla ya shilingi milioni 360 linalodaiwa na Mamlaka ya Maji ya Jiji la Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na kutaka Serikali kupitia mamlaka hizi ichukue hatua za kudhibiti upotevu wa maji ya bomba na mapato, Kambi ya Upinzani tunashauri mamlaka hizi zianze kufanya uwekezaji wa kuchimba maji ardhini na kuyasambaza kwa bomba hususan kwenye maeneo ambayo ardhi ina maji ya kutosha ili kuongeza kiwango cha maji yanayounganishwa kwa wateja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumebaini kuwa mamlaka nyingi za maji zimekuwa zikiingia gharama kubwa katika kupata ardhi ya kupitishia miundombinu ya maji. Mathalan Mamlaka ya Maji Mwanza mpaka sasa inadaiwa jumla ya shilingi bilioni 200 kama fidia ya ardhi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Maji ishirikiane kwa karibu na Wizara ya Ardhi hasa kitengo cha Mipango Miji, ili kuhakikisha miundombinu ya maji inakuwepo kwenye ramani kwa ajili ya maendeleo ya maeneo husika, jambo hli litamaliza kabisa tatizo hili la fidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani haiungi mkono hoja ya Serikali kuendelea kuzungumzia uchimbaji kwenye miji inayozungukwa na Maziwa Makuu, mfano Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, badala yake tunaitaka Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini ifanye uwekezaji wa pampu kubwa zenye uwezo wa kusukuma kutoka kwenye vyanzo hivyo na kuhakikisha wananchi wa maeneo hayo wanapata maji ya bomba yaliyo salama na uhakika kwa mfano haiingii akilini kuzungumzia visima kwenye Jiji la Mwanza ambalo kimsingi limezungukwa na maji ya Ziwa Victoria ambayo kwa sasa yamekwishafika katika Wilaya ya Kahama Mkoani Shinyanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mamlaka karibu zote nchini, kwenye Majiji, Miji Mikuu ya Mikoa na Halmashauri, zinakabiliwa na tatizo kubwa la madeni, kushindwa kujiendesha kwa faida na kutoa huduma ya maji kwa ufanisi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Maji kwa kushirikiana na taasisi za utafiti, ifanye utafiti wa kina kubaini changamoto zote zinazoikabili mamlaka hizi za maji *(feasibility study),* ili kupata mkakati wa kuziboresha na kuhakikisha zinajiendesha kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya kuboresha sekta ya maji kwa ujumla, Kambi ya Upinzani imebaini kuwa huduma haba za maji safi na salama na kusuasua kwa mipango ya kilimo cha umwagiliaji, kunatokana na sekta nzima ya maji kukabiliwa na matatizo makubwa yafuatayo:-

(i) Serikali kutoipa kipaumbele cha kutosha sekta ya maji, hivyo kujikuta ikitenga fedha ndogo za ndani kwa ajili ya miradi ya maji. Kwa mfano, fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya maji zimepungua kutoka bilioni 50 mwaka 2009/2010, hadi kufikia bilioni 37.5 mwaka 2010/2011 na bilioni 45.5 kwa mwaka 2011/2012.

(ii) Serikali kutokuwa na mikakati madhubuti ya kuvuna maji mengi ya mvua ambayo kila mwaka yamekuwa yakipotea bure. Tanzania inapata mvua nyingi *(annual mean inflow)* ya mita za ujazo milioni 921,032; lakini asilimia 89.8 ya mvua hizo hupotea kutokana na jua, asilimia 9.7 hupotea kwa kuingia moja kwa moja kwenye maziwa na kuingia baharini. Ni asilimia 0.6 ya maji ya mvua ndiyo yanayotumika kwa matumizi ya kilimo, mifugo na matumizi ya majumbani.

(iii) Serikali kutochukua hatua madhubuti kudhibiti upotevu mkubwa wa maji ya bomba. Inakadiriwa kuwa kiasi cha maji ya bomba asilimia 36 kimekuwa kikipotea kila mwaka wakati kiwango kinachokubalika ni asilimia 20.

(iv) Mamlaka za Maji kujikita zaidi katika shughuli za usambazaji maji kuliko kuwekeza katika uzalishaji wa maji.

(v) Serikali kujikita zaidi katika kutekeleza miradi mingi midogo midogo ya maji hususan visima vidogo kwenye maeneo ya vijijini, badala ya kuwekeza kwenye miradi mikubwa itakayoweza kuwanufaisha wengi.

(vi) Kutumika vibaya kwa fedha zinazoelekezwa kwenye miradi ya maji na usimamizi mbaya wa miradi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa mapungufu yote haya yanayoikabili sekta ya maji, na kuifanya sekta ya maji kuwa bora na yenye manufaa kwa matumizi ya kawaida ya wananchi na shughuli za uzalishaji ikiwemo kilimo, Kambi ya Upinzani mbali na kuitaka Serikali itekeleze mapendekezo mahsusi ya Kibajeti tuliyotoa, pia tunaitaka ianze kutekeleza mapendekezo yafuatayo hatua kwa hatua kwa kadri itakavyoonekana inafaa:-

(i) Tunaitaka Serikali iimarishe na kuongeza vyanzo vyake vya mapato ili kutunisha Bajeti Kuu na kutenga fedha za kutosha kila mwaka kutoka kwenye fedha za ndani kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya maji.

(ii) Tunaitaka Serikali itekeleze lengo na mikakati mbalimbali, kuhakikisha asilimia 99.5 ya maji ya mvua yanayopotea bure kila mwaka, yawe yanavunwa katika ngazi za kaya, kitongoji, kijiji, kata, Wilaya, Halmashauri na Mikoa, kwa kila ngazi kuwa na mfumo wake wa kuvuna maji hayo, kwa matumizi ya nyumbani na shughuli za uzalishaji, hususan kilimo.

(iii) Tunaitaka Serikali ichunguze na kudhibiti wizi na upotevu mkubwa wa maji ya bomba unaofanyika chini ya usimamizi wa mamlaka nyingi za maji, kwa kuhakikisha inakarabati kwa haraka miundombinu chakavu na kuwachukulia hatua wote walioingilia mfumo wa bomba kwa kujiunganishia maji kinyume cha taratibu. *(Makofi)*

(iv) Tunaitaka Serikali na wadau wote wa maendeleo kuziwezesha Mamlaka za Maji kuwekeza kwenye uzalishaji wa maji yaliyopo ardhini kwa kuchimba visima virefu na kuvuna maji ya mvua, ili kuongeza mita za ujazo kwenye maeneo yenye upungufu. *(Makofi)*

(v) Tunaitaka Serikali itumie vyanzo vikubwa vya maji kama maziwa kuanzisha miradi mikubwa ya maji itakayohudumia sehemu kubwa ya nchi, kama maji ya Ziwa Victoria yanavyotumika hadi Shinyanga. *(Makofi)*

(vi) Miradi mingine mikubwa ianzishwe kwa kuchimba visima virefu kwenye mikoa au wilaya zenye maji mengi ardhini, kama ilivyo kwa miradi ya visima virefu vya Kimbiji na Mpera. *(Makofi)*

(vii) Tunaitaka Serikali mapema iwezekanavyo, ichukue hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya viongozi na watumishi wote wanaofanya uzembe na ufisadi katika sekta ya maji, ili kunusuru miradi mingi inayokwama au kusuasua kwa sababu hizo. *(Makofi)*

(viii) Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho tunaisisitiza Serikali ije na mipango ya dharura kumaliza tatizo la maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo yote haya naomba ninukuu maneno kutoka katika kitabu kitakatifu, Mithali 28:3 "Maskini anayemuonea maskini mwenzake ni sawa na mvua inayonyesha na kuharibu kila kitu *(A poor man who oppress the poor is a beating rain that leaves no food). (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati umefika tuunganishe nguvu zetu pamoja, bila kuangalia itikadi zetu, dini zetu wala makabila yetu na kwa pamoja turejeshe misingi ya Utanzania wetu, ambayo ni uzalendo na uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, huyu alikuwa ni Msemaji wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Highness Kiwia. Sijisikii vizuri kumkataza Mbunge, lakini muda unapokuwa umekwisha basi sina namna ya kufanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kumejitokeza wananchi wanakuwa wanalalamika kwamba tunatumia muda wetu vibaya kwa kushukuru sana familia zetu na kuwataja watu mbalimbali. Tunawashukuru na niliona kipindi kimoja cha Komedi cha Futuhi wanapigiana simu wanamwambia bwana hebu ngoja kwanza siwezi kusikiliza hii kwanza bado nashukuru kwanza halafu mimi nitakuja kusikiliza baadaye. *(Kicheko)*

Lakini nilitaka kusema tu lazima wananchi waelewe kwamba katika hotuba za Kimataifa ni kiwango cha kawaida kabisa mtu kumshukuru Mwenyezi Mungu na kushukuru familia au mwenzi wake. Ila tu inakera tu pale ambapo atamshukuru na bibi yake na majirani pale kidogo inaleta shida. *(Makofi)*

Lakini kwa maana ya kushukuru familia kama alivyofanya leo Mheshimiwa Kiwia nimeona ameshukuru mke wake na akashukuru na watoto ni jambo zuri na wengine wamefanya hivyo hapa Msemaji wa Kamati Mheshimiwa Neema Mgaya Hamid naye amefanya hivyo ni *style* ya kawaida. Kwa hiyo, tukubaliane tu kwamba katika viwango vya Kimataifa lazima tufanye hivyo, hatuwezi tukaacha, ila tusizidi sana kutumia muda mwingi sana. *(Makofi)*

Sasa hapa ninao wachangiaji lakini karatasi nilizozipata mpaka sasa hivi zimefika karibu 50 zikiomba *favour* ya Mwenyekiti, naomba niseme kabisa hiyo *favour* nitafuata utaratibu wa kawaida ambao hawajachangia kabisa wapo wane, waliochangia mara moja wapo 11, waliochangia mara mbili wapo 43, waliochangia mara tatu wapo 37. *(Makofi)*

Katika hali hii ni dhahiri watu wengi hawatapata nafasi, hata tukifanya namna gani hadi kesho atakapofika mchangiaji wa mwisho watachangia kati ya 30 au 31 kwa hesabu nilizopiga. Kwa hiyo, tujitahidi sana kuchangia kwa maandishi lakini tutatumia fursa ya mafungu lakini pia niwaombe sana kwa niaba ya ambao hawatapata nafasi wananchi wawasamehe tu kwamba matatizo ya maji yanafahamika. Hata kule Kibakwe matatizo ya maji yapo lakini na mimi sitapata nafasi ya kusema. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Maji. Nianze moja kwa moja kwa kuzungumzia suala zima la utamaduni wa ukarabati *(culture of maintenance).* Nadhani huu ni utamaduni ambao inabidi tuusisitize sana hasa katika Wizara hii ya Maji pamoja na Wizara nyingine ambazo kazi yake ni kutekeleza miradi kadhaa. Kwa nini tunazungumzia utamaduni wa

ukarabati, kwa sababu utamaduni wa ukarabati ukifanyika kwanza miradi iliyokamilishwa inakuwa endelevu. *(Makofi)*

Pili, tunatunza rasilimali na fedha za Serikali zilizokwisha tumika. Lakini tatu wananchi wataendelea kufaidika na matunda na miradi ambayo tayari imeshatekelezwa na Serikali. Lakini inaonekana bado utamaduni huu hatujaupa umuhimu mkubwa, kwa nini nasema hivi, nasema hivi kwa sababu kwa hoja tunayoizungumzia leo hii hata katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, imesisitiza suala la ukarabati, na kwa njia nyingine suala la utamaduni ambao nimeuzungumzia, kwa maana ya *culture* ya *maintenance.* Tukiangalia sura ya 6 ya Ilani ya Uchaguzi ukurasa wa 120 Ilani ya Uchaguzi imeagiza kabisa kwamba Wizara iangalie miradi mikubwa ya maji ya ya Kitaifa. Miradi hii ni kama Wanging'ombe, kuna mradi wa Makonde, kuna miradi ya Kyabakari kule, lakini hususani upo mradi wa *Handeni Trunk Main* ambao ndiyo nataka kuuzungimzia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa kweli miradi hii na hususani mradi wa Handeni kwa kweli haukupewa umuhimu mkubwa. Miradi hii imeshatumia fedha nyingi, imejenga miundombinu mizuri, wananchi wanatumia. Lakini inaonekana kama inaachwa iendelee kuchakaa na kuharibika. Sasa maana yake nini? Ikiachwa kuchakaa na kuharibika maana yake tunarudi pale pale tulipotoka, *we are going back to square one.* Miundombinu ipo, kazi kubwa ni kuendeleza masuala ya ukarabati na ku-*maintain* hii. Lakini hili kwa bahati mbaya bado halifanyika kwa umakini katika mradi wa *Handeni Trunk Main.* Sijui miradi mingine hiyo ya Kitaifa, lakini nadhani hali ni sawa sawa kama inavyojitokeza Handeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ule mradi wa Handeni ni *Trunk Main* ulianza mwaka 1974. Mradi ule ulipojengwa uliwekewa umri wa miaka 20. Sasa utaona wazi kwamba kuanzia mwaka 1974 mpaka sasa ni zaidi ya miaka 40. Mradi ule ulikuwa unahudumia vijiji 60 na watu takriban 180,000, hivi sasa mradi ule unahudumia miji midogo sita kwa maana Mji Mkuu wa Wilaya ya Handeni, Mkata, Kwamkonga, Kabuku na Segera, Michungwani na Kwamkono, takribani watu 250,000; mradi ndiyo ule ule. Sasa katika hali hii, mradi kama huu pamoja na kwamba umeshatumia fedha nyingi za Serikali hautaweza tena kuhudumia wananchi kwa kiwango kinachopaswa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tena linatupa wasiwasi mara nyingine tukizungumza takwimu za watu wapatao maji safi vijijini au mijini takwimu za Kitaifa tunazotoa zinatushawishi tuzifanyie *review* kuona kwamba je, ni kweli asilimia 80 au 90 ya watu wanapata maji safi na salama? Maana yake tunaweza kutoa takwimu tu lakini miundombinu tuliyoiweka kama hatutaifanyia ukarabati na *maintenance* kwa kweli tutakuwa hatupigi hatua yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuamini mradi wa *HTM* – Handeni, chujio pale Tabora halifanyi kazi. Kituo cha kuganga maji labda kinaitwa *treatment plant,* sijui wanaitaje kwa Kiswahili, hakifanyi kazi. Kwa maana hiyo tunaweza kusema wazi kabisa maji yanayokwenda Handeni na kwa bahati mbaya, kule hatuna mto, tunatoa maji, kutoka Mto Ruvu uliopo Korogwe hayachujwi wala hayawi *treated.* Sasa hali hiyo huwezi kusema kwamba kwa kweli wananchi wa Handeni tunapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Sasa sijui Serikali inasema nini kuhusu suala kama hili. Mimi nadhani suala hili linahitaji umakini mkubwa sana. Haiwezekani watu karibu katika vijiji 60 wanakunywa maji moja kwa moja yanatoka mtoni hata wakiambiwa wachemshe lakini kwa kweli kwa *volume* ya maji kama ile kwa kweli itakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, nilikuwa nasema hebu Serikali iliangalie hili. Tungekuwa na mito ingekuwa ni vizuri lakini moja ya athari kubwa katika Wilaya ya Handeni ni kwamba hatuna mto hata mmoja na mradi tunaotegemea ni *Handeni Trunk Main.* *(Makofi)*

Kwa nini mradi huu haujapata umuhimu wowote? Hata ukiangalia *series* ya Bajeti inayotolewa katika miaka mitatu, minne iliyopita mradi mkubwa kama ule unapata Bajeti ya shilingi milioni 100, 180. Inawezekana kabisa ikaonekana kwamba ni njia moja ya fedha hizi kuziweka katika matumizi yasiyo na tija. Mimi nadhani ni vizuri Serikali ikaliangalia kwa ukaribu na kwa umakini na kutenga fedha ambazo *at least* zitasaidia kufanya mradi huu uanze kufanya kazi yake kama ilivyokuwa unafanya kazi pale zamani.

Kuna ununuzi wa pampu katika maeneo mbalimbali, sasa hivi watu hawapati maji. Kuna ukarabati unatakiwa ufanyike katika mabomba kadhaa na mimi sijui kama safari hii kama katika Bajeti mradi huu umetengewa fedha lakini niliulizia kwamba tulikuwa tunahitaji kiasi cha chini kama shilingi bilioni 1.5 ili kuweka hali sawa. Sasa kama tunaomba bilioni 1.5 pamoja na matatizo ya rasilimali Serikali tunatenga kama shilingi milioni 60, milioni 100 mimi nadhani hatuwezi kumaliza tatizo la maji katika Wilaya yetu ya Handeni. *(Makofi)*

Mimi namwomba sana Mheshimiwa Waziri najua jitihada zake za kusaidia Wilaya ya Handeni, lakini fedha zinazotolewa katika ukarabati wa mradi kama huu tunataka fedha ambazo zitakuwa na *impact,* fedha ambazo zitashughulikia mradi mkubwa wa jinsi hiyo. Hali hii pia nadhani inakwenda na miradi mingine kama Makonde, Wanging'ombe na kule Tabora. Kwa sababu hii *infrastructure* tayari ipo, kinachohitajika ni kuiweka vizuri. Sasa sijui tatizo linakuwa ni nini? Mnapata taabu sana kukimbilia miradi mipya wakati hii ya zamani, kama ya Kyabakari kule tunaiacha yaani inakuwa *wasted.* Hii ndiyo changamoto ambayo naiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Mustapha Sabodo, ametuletea visima kule Handeni na vinachimbwa vizuri sana. Natoa pongezi kupitia kwa msaidizi wake Dkt. Msuya, visima vile vinachimbwa. Napenda vilevile kuwashukuru *NGO* wa *Serving Friends International* ambao nao wamechimba visima katika maeneo ya Mazingara kule. Lakini vilevile ningependa Serikali iifanyie sana tathmini huu utaratibu wa mradi wa vijiji kumi wa visima hivi. Tukiuangalia huu mradi kwa kweli unaweza kuwa ni *disaster.* Ule utaratibu wa *quickwins* na masharti yanatolewa na Benki ya Dunia pamoja na masharti wanayotakiwa wananchi wachangie fedha nyingi zinazokwenda katika maeneo haya mwisho wake zinabakia kuwa ni fedha ambazo hazitumiki na matumizi yake hayajulikani. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mimi nilikuwa napenda sana Serikali iuangalie huu mradi kwamba kweli tunawapa matarajio wananchi kwamba kuna miradi ya Benki ya Dunia wakati haipo?

Pale Handeni - Mkata tumejenga tenki kubwa la maji, pana vifaa vingi vya maji vimekaa tu, wala havitumiki, ukigusa unaambiwa ni vya *World Bank* wakati maeneo mengine yanahitaji zana kama hizo. Kwa hiyo, hili eneo la miradi ya *World Bank* ningeomba Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla iangalie vizuri ili fedha za Serikali zitumike vizuri na kupunguza kero hasa kero kubwa za maji ambazo zinawakabili wananchi wengi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sote tunamwombea kheri Profesa Mark Mwandyosa, Mwenyezi Mungu ampe nafuu, arudi aje afanye kazi zake za kujenga Taifa *Inshallah* Mwenyezi Mungu atampa nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Kigoda kwa matumizi mazuri ya muda na hiyo ndiyo hotuba ya Dokta, fupi lakini pia ametuachia muda. Sasa niwasome labda watakaofuata, atafuatia Mheshimiwa Abdulaziz Abood, na baada yake ataongea Mheshimiwa Rachel Mashishanga na baada ya hapo ataongea hapo Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Sasa namwita Mheshimiwa Abdul-Aziz Abood. *(Makofi)*

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, pili nawashukuru wananchi wa jimbo langu la Morogoro kwa kuendelea kunipa ushirikikano wa kutatua kero mbalimbali za Jimbo hili la Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wangu kwa maana ya wapiga kura wangu wamenipa salamu. Wameniambia sasa siasa za majukwaani basi, muda wanaotaka kuuona sasa ni vitendo, na mimi ninawaahidi kuwa nimeshaanza kuwatumikia kwa vitendo na hususan kwenye kero ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepewa shilingi milioni 90 za shangingi, nimechanganya na zingine nimeweza kununua gari la kuchimbia visima lenye thamani ya shilingi milioni 245. Kwa hiyo, gari sikununua badala yake nimeingiza kwenye mradi wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro tuna kero kubwa sana ya maji, katika maeneo mengi ya miji mipya ambayo ni Kihonda, Kilimanjaro, Mkundi, Kingolwira na maeneo mengine tuna kero kubwa sana ya maji. Kuna mradi wa *MCC* ambao upo Morogoro, lakini mradi huu hautasaidia kumaliza kero hizi za maji katika mji wa Morogoro. Kwa hiyo, mimi ningeishauri Serikali itusaidie kuweza kumaliza kero hii na hususan katika maeneo haya niliyoyataja ambayo ni kero kubwa. Wananchi wanapata taabu sana kwenda kilomita 15 mpaka 20 na ukizingatia maeneo haya ni wananchi wamejenga ni maeneo mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bwawa la Mindu limezungukwa na wananchi pia katika maeneo hayo ya Kasanga A na Kasanga B lakini cha kushangaza bwawa lile linahudumia maeneo mengine ya Morogoro lakini kwa wananchi walio karibu na bwawa lile hawahudumiwi na hawapati maji. Ningeishauri Serikali pia kwamba tupatiwe miundombinu ya kuweza kuwapatia maji maeneo hayo na wao ni waangalizi wakubwa na ni walinzi wakubwa wa bwawa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero nyingine kubwa ni bei ya maji katika Mji wa Morogoro imepanda bei kutoka 465 kwa *cubic meter* mpaka 762 karibu asilimia 55. Wananchi wa Morogoro wanashindwa kumudu bei hii ya maji kwa asilimia 55. Kuna sehemu zingine za Morogoro kuna miundombinu ya maji lakini hayatoi maji mpaka hivi leo lakini mwisho wa mwezi wanapata ankara ya kudaiwa maji. Ningeomba nalo Serikali ingeliangalia hili. Ili kuondoa kero kwa wananchi. *(Makofi)*

Lingine ni *treatment plant* ya Morogoro haifanyi kazi, maji yanatoka mpaka rangi ya kijani. Wananchi wanakuwa hatarini kutumia maji yale. Hata wakati huu wa kiangazi maji yanakuwa ni machafu mno, ningeiomba Serikali na hasa katika miji yetu mipya ya Morogoro, Kihonda, Kilimanjaro, Kingolwira, Mkundi na Bigwa tupatiwe maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namwombea kheri Waziri wetu wa Maji, Mungu ampe afya njema aweze kurudi salama na tujiunge naye tena ili aweze kufuatilia kero zetu kwa karibu mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaunga mkono hoja hii mpaka nipate tamko la Serikali kuhusu kuondoa kero katika Mji wa Morogoro. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abdulaziz Abood. Sasa nitamwita Rachel Mashishanga na baadaye atafuatiwa na Mheshimiwa Rosemary Kirigini na kama muda utaruhusu Mheshimiwa Zabein Mhita naye ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukrani kwa kupata nafasi hii kuweza kuchangia hoja hii iliyopo mbele yetu ndani ya Bunge lako Tukufu. Shukrani za pili nafikiri nizipeleke kwa wanachama wote wa CHADEMA na Watanzania wote waliotupigia kura na kuniwezesha na mimi kuwepo ndani ya hili jengo. Shukrani za tatu, naomba univumilie ni kwa familia yangu mume wangu Robert pamoja na watoto wangu Susan, Andrew pamoja Paul. Nawashukuru sana na nawapenda sana. Bila kumsahau mzee wa ukweli, Mzee Mashishanga, pamoja na mama yangu Susan najua sasa hivi wapo mbele ya luninga wananiangalia, nawapenda sana. *(Makofi)*

Mwisho naomba nitoe pole kwa Mheshimiwa Mussa Silima kwa kupata msiba wa kufiwa na mke wake mpendwa na yeye kupata majeraha kadhaa. Mungu amsaidie katika kipindi hiki kigumu. Amin.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniangalie jinsi nilivyosimama, mimi nafikiri na hii wewe itakusaidia. Naomba unipelekee salaam kwa Mheshimiwa Spika, atutafutie basi *microphone* ndefu, miaka mitano humu tutatoka na vibiongo. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashishanga hilo litazingatiwa, utatafutiwa wewe peke yako. Maana kwa *size* ya wanawake wa kawaida humu ndani wewe unawazidi wote urefu. Endelea! *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kama nikisimama sitasikika sana. *(Makofi/Kicheko)*

Naomba nijikite katika hoja hii iliyopo mbele yetu kwenye suala la maji hasa Mkoa wa Shinyanga. Kwanza niishukuru Serikali kwa sababu wamefanya kitu cha maana sana kupeleka maji kutoka Ziwa Victoria. Kwa kweli Shinyanga kwa wanaoifahamu Shinyanga sasa hivi imebadilika sana. *(Makofi)*

Kwa hilo, namshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Kikwete pamoja na Rais wa Awamu ya Tatu Mheshimiwa Benjamin Mkapa, kwa kutekeleza huo mradi. Kwa kweli kwenye mazuri nitawasifia. *(Makofi)*

Naenda sasa kwenye hoja zenyewe, tuna Mamlaka mbili Shinyanga, *KASHWASA* ambayo ni Mamlaka ya Maji Safi na Taka Kahama na Shinyanga pamoja na *SHUWASA* hii ni Mamlaka ya Maji na Taka ya Manispaa. Kumekuwa kuna matatizo mpaka sasa hivi mimi sielewi pamoja na wananchi wa Shinyanga kwa nini tunakuwa na mamlaka mbili za maji. Matokeo yake mwisho wa siku wananchi ndiyo wanaumia kwa sababu bili zinazidi kupanda na maji hawayapati inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *KASHWASA* inauza maji kwa jumla, yaani *bulk* wanawauzia *SHUWASA.* Lakini kwa mapendekezo yangu nilikuwa naomba iwezekane basi moja ivunjwe kama ibaki *KASHWASA,* nafikiri *SHUWASA* ingetoka. Nasema hivyo kwa sababu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SHUWASA* wamekuwa wazembe, kuna bonde la Mwawaza kule kulichimbwa visima 12 vya maji vikawekwa na pampu na visima vinane vina maji mengi sana lakini pampu hakuna. Inavyosemekana *TANESCO* wameshakwenda kutoa *transforma* iliyokuwa pale. Na hivi visima viligharamu shilingi milioni 600 na aliyeenda kufungua wakati huo alikuwa Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Sasa nataka kuuliza ina maana hizi shilingi milioni 600 na wananchi wa kule wanapata shida na visima wanaviona havitoi maji na vina maji ya kutosha, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho anieleze sasa hatma ya hawa watu wanaozunguka hayo maeneo watapata vipi maji kwa sababu kwenye mradi huu wa *KASHWASA* hawapo. *(Makofi)*

Pia nilitaka kuzungumzia sasa *SHUWASA. SHUWASA* wameweka tanki kule *Old Shinyanga.* Kibaya zaidi na cha kusikitisha, ni kwamba lile tenki wamefunga maji yanapoingia kwenye tenki hiyo mita inasoma *KASHWASA.* Sasa tatizo linakuja maji hayo yanapoingia kutoka *Lake Victoria* yanaingia moja kwa moja kupitia ile mita kwa hiyo unaingia mchanga na uchafu wote unaingia. Sasa hii inaleta hasara sana kwenye *KASHWASA* kwa sababu karibu kila wiki wanatoa mchanga. Sasa ule mchanga unakuwa tayari umehesabiwa. *(Makofi)*

Mimi nilikuwa nawashauri nafikiri viongozi wa *SHUWASA* wapo hapa, ile mita waihamishe waiweke mbele yaani wawe wanapima maji yanayotoka kwenda kwa *customer,* siyo yale yanayoingia ambayo yanaingia na mchanga na kila kitu. Kwa hiyo wanajikuta wanapata hasara kubwa sana. *(Makofi)*

Kuna Kata za Ibadakuli na Kolandoto, hazijapata maji kutoka kwenye huu mradi. Kulikuwa kuna bomba linatoa maji kutoka Mwadui linapeleka Shinyanga. Mimi nilikuwa naomba Mamlaka itumie huu mtandao wa hili bomba iiunganishe na *KASHWASA* ili Kolandoto na Ibadakuli waweze kufaidika na huo mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nasema kabisa yaani kama ikiwezekana kwamba *SHUWASA* ivunjwe, kuna *valve* imeharibika pale kwenye lile tenki ambalo linachukua maji kutoka Ziwa Victoria, yaani hilo tenki linalotoa maji *KASHWASA, valve* imekufa. Wanachokifanya

wanaenda kufungulia sehemu moja ipo mbali sana inaitwa Solwa. Kule ndiyo kuna ile *valve* wanafunga na kufungua. Kwa hiyo, hapa wanafungua kule Solwa yaani wanachoma mafuta kwenda Solwa badala ya kwenda *Old Shinyanga* kwenda kufungua maji, yakikaribia kujaa kwenye tenki wanachoma tena mafuta kuwahi kwenda kufunga hiyo *valve.* Sasa nafikiri haya ni matumizi mabaya ya fedha, hili nalo nafikiri liangaliwe. *(Makofi/Kicheko)*

Halafu kitu kingine *SHUWASA* wamekuwa wakidaiwa sana na *KASHWASA.* Wamekuwa na madeni makubwa na wamekuwa wakilimbikiza sana madeni matokeo yake *KASHWASA* inashindwa kufanya kazi zake vizuri, sasa hili na lenyewe nilikuwa naomba liangaliwe. Kwa sababu *KASHWASA* wanalalamika kwamba wanarudishwa nyuma na *SHUWASA.* Sasa kama kuna uwezekano wa kubakisha hiyo mamlaka moja kwa nini Serikali isiachie *KASHWASA* sasa ikatumia hiyo ruzuku wanayoitumia kutoka kwenye Serikali wakawa wanasambaza maji wao badala ya kuuza maji kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine kabla ya kupata maji kutoka *Lake Victoria* tulikuwa tunapata maji kutoka Bwawa la Ning'wa. Waliofika Shinyanga miaka ile ya zamani walikuwa wanaona maji yale yalikuwa ni meupe, yaani kama vile maziwa unakunywa. Sasa hili bwawa lilikuwa na pampu saba, sasa hivi zimebakia pampu tatu tu. Sasa nataka niwalaumu tena *KASHWASA,* kwa sababu wamewakatalia *SHUWASA* kuchanganya yale maji na Mkemia Mkuu inasemekana kwamba hayana shida kuchanganya kwenye lile bwawa na yataingia kwenye *system,* kwa sababu wenyewe *KASHWASA* wanataka wauze tu maji yao yanayotoka Ziwa Victoria sasa yale maji ya Ning'wa yatatumika vipi kama wanakataa kuyachanganya kuyaingiza kwenye *system? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni hili la ongezeko la bei, hili limetolewa na *EWURA* mwaka huu mwezi wa tano na limeanza kutumika. Inaonekana *KASHWASA* wanawauzia maji *SHUWASA* bei ya chini sana, yaani hiyo ni *flat rate* anauziwa bei ya chini sana, yaani hiyo ni *flat rate* anauziwa *SHUWASA* shilingi 462.

Lakini sasa bei alizopewa *SHUWASA* kwa anazotoa kwa wateja wa *domestic,* wa *commercial,* pamoja na *institution* ni kubwa sana, anapata zaidi ya nusu ya faida. Hapo hapo *service charge* ipo pale pale. Sasa mimi nilikuwa naiomba Wizara iangalie kwa sababu Watanzania waliopo Shinyanga wanapata shida sana, wamejitahidi pamoja na kuandamana lakini hakuna kilichofanyika. *(Makofi)*

Sasa tulikuwa tunaiomba Serikali hebu ijaribu kuliangalia hili kuona kwamba hii bei kwa sababu mmewapa maji lakini msiwatese. Mmesaidia sana kuwapa maji lakini nawaombeni sana muangalie upya hizi *rate* ambazo zimetolewa sasa hivi ambazo zimeanza kutumika kuanzia toka mwezi Mei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda naomba nimalizie. Hizi gharama ambazo nimezizungumzia sasa hivi kuna taarifa moja ya *KASHWASA* nimeiona wanasema mradi ni wa hasara. Ni hasara kubwa sana. Sasa kama ni mradi mkubwa sana na unaitia *KASHWASA* hasara kwa nini sasa Serikali isiongeze ruzuku kwenye hii Mamlaka ili isambaze maji *at least* watumie maji ya Ziwa Victoria ili mradi wautumie vizuri Watanzaia ili ufanane sasa na mradi wenyewe. Kwa sababu wanatumia watu wachache na ni mradi mkubwa. Nilikuwa naomba hilo Waziri anapojumuisha afanye majumuisho aliangalie hili kwa sababu wananchi wa Shinyanga kweli wanasilikiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri haya kwa leo yanatosha kabisa. *(Makofi)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii muhimu ya Maji. *(Makofi)*

Nianze kwa kumshukuru sana Waziri aliyesoma hotuba hii, ameisoma kwa umakini mkubwa. Lakini nawashukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa salamu za kipekee kabisa na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mara nawaomba kabisa kwa dhati ya moyo wetu tumshukuru mama yetu mpendwa mama Rweyemamu. Sijui kama amekuja siku ya leo naona yuko pale ananitazama. Kwa kweli mama huyu naomba

nimfikishie salamu nyingi sana kutoka kwa wanawake wa Mkoa wa Mara na hasa Wilaya ya Serengeti kwa usimamizi mzuri sana wa Bwawa la Manchila na hivi sasa wanawake wa Wilaya ya Musoma Vijijini kwa usimamizi mzuri sana wa Bwawa la Kwegelo vilevile mabwawa yaliyoisha katika Wilaya ya Bunda. Tunakushukuru sana Mama Rweyemamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeanza kwa kusema kwamba maelekezo ya Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi katika sekta ya maji kwa ujumla yanajieleza vizuri sana na kwa ruksa yako ningependa kunukuu yanasema kwamba; "Katika kipengele cha kwanza kuwawezesha wananchi wa mijini kupata maji safi na salama na ya kutosha kwa matumizi yao ya kawaida na karibu na sehemu wanazoishi. Lengo ni kufikisha huduma hiyo kwa asilimia 90 mijini na asilimia 65 kwa maeneo ya vijijini ifikapo mwaka 2010." Lakini sehemu ya pili inasema; "Kuhimiza utekelezaji wa ujenzi wa malambo au mabwawa mapya, ukarabati na kufufua malambo yote ya zamani ili maji mengi zaidi yaweze kupatikana kwa ajili ya matumizi ya wananchi na mifugo yao." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza na hii sehemu ya kwanza kuwapatia wananchi waishio mijini maji safi na salama na vijijini. Hapa imesemwa asilimia 90 lakini katika hotuba tumeambiwa katika mikoa 19 mpaka sasa wameshafikisha asilimia 86. Mimi niliposikia hivi nilitamani kulia, kwa sababu nikiangalia mji wangu mimi wa Musoma Mjini ni aibu. Na ninasimama hapa kwa masikitiko ninatamani hata kulia, Musoma Mjini inazungukwa kila kona na Ziwa Victoria, lakini katika Kata zake 13 ni Kata nne zilizopo pale mjini ndiyo zinapata maji safi na tena maji yenyewe siyo safi na salama kama Ilani yetu inavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji hayo ukiyafungua ni ya kijani na kila siku yanatoa minyoo, ni jambo la kusikitisha sana. Tunayo matemki matatu pale Musoma Mjini yanayotakiwa kukusanya maji kutoka Ziwa Victoria, lakini matenki haya hayana machujio, wala maji yale hayawekewi dawa. Kwa watu wetu wa Musoma Mjini hawapati maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikiangalia hata ugawaji wa visima pale mjini hatuwezi kupewa ile miradi ya visima, hatuna miradi yoyote ya visima. Visima vyote vinapelekwa katika Wilaya nyingine na Musoma Vijijini kuna visima vitano tu. Lakini Wilaya nyingine tumepeleka visima. Sasa sijui hawa watu wa Musoma Mjini tunawasaidiaje? Wapo pale karibu na chanzo kikubwa sana cha maji na Ziwa Victoria lipo pale. Lakini mpaka hivi ninavyozungumza Kata zote tisa za Nyamakale hazina maji, Mwisenge, haina maji, Buhalo ukienda haina maji, Buhale haina maji na kwangu ninakotoka mimi Kamnyonge maji yanapatikana mara moja kwa wiki. Nyacho pia hakuna maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha Kata hizo ni Kata ya Ilingo tu Migobelo, Kata ya Nkenge ndiyo wanaopata maji tena zipo mjini na maji yenyewe yanapatikana mara mbili au mara tatu kwa wiki nasikia. Kwa hiyo, ninaomba Wizara kupitia Bunge lako Tukufu iangalie mji wa Musoma Mjini waweze kupata maji safi na salama na waweze kuendana na hii asilimia 90 inayotakikana kupatikana kwa watu wa mjini. Lakini nikienda kwa asilimia 65 ya watu wa vijijini, tunashukuru tumepewa mradi wa kutoa maji kutoka Mgango kwenda Butiama mpaka Kyabakari. Lakini mradi huu ni kama unasua sua. Amezungumza pale Mbunge wa Handeni mimi nimefurahi sana, huo ni uzalendo. Mradi huu wa Kitaifa unasua sua hatuelewi ni kwa nini mradi unasua sua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepeleke maombi maalum pale ambapo yanatolewa maji kwenye mji ule wa Mgango, hakuna maji kabisa. Sasa maji yanatoka Mgango, yanaenda Butiama hadi Kyabakari. Wakati Mgango kwenyewe na vijiji vyote vinavyoizunguka Mgango hakuna maji. Naomba Wizara ifikirie itakapokuwa inashughulikia huu mradi wa Kitaifa ihakikishe kwamba maji yanapotoka pale kwenyewe Mgango wapate maji, wananchi wake wote wapate maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye utekelezaji wa ujenzi wa malambo na mabwawa. Napenda kuishukuru sana Serikali, kwa kweli sisi Mkoa wa Mara si haba, tumepewa mabwawa mengi sana. Katika ujenzi wa mwaka jana na mwaka huu katika Wilaya peke yake ya Bunda tunaishukuru sana Serikali, mabwawa karibu yote yaliyotarajiwa kujengwa ya Salama Kati, Kinyambwiga, Nyambwele na Kipangwa yote yamekamilika. Kwa hiyo, tuna imani hata hilo bwawa lililotajwa kwa mwaka huu, kujengwa hapo Wilayani Bunda la Mgeta tuna imani

litakamilika kama ilivyopangwa. Lakini pia tumepata bwawa la Nyamboli na bwawa la Umonshi na bwawa la Nyamasanda kwa Wilaya ya Rorya. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali na tunaipongeza. Tunaomba hili bwawa jipya la Kanyisambo ambalo limetajwa katika hotuba hii nalo liweze kukamilika. Lakini kwa suala la Musoma Vijijini hapa tunalo tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Musoma Vijijini tuna shida kubwa sana ya maji licha ya kwamba Musoma Vijijini linazungukwa Kata zote za nyingi za Tarafa za Wanyanche, inazungukwa na Ziwa Victoria, lakini tuna shida ya maji hatujapata kuona. Watu wale wanatumia maji ambao siyo safi na salama, wanachota moja kwa moja kutoka Ziwani na kuyatumia. Maji yale ni machafu, watu wanafua ziwani kama unavyojua, watu wanajisaidia wakati wanaoga, lakini maji yale yale pia yanatumika na wananchi hawa kwa mifugo yao na pia kwa kunywa kwa hiyo siyo maji safi na salama. *(Makofi)*

Napenda kuomba kwamba tumeambiwa hapa Bwawa la Oljoro lililoko katika Kata ya Buswahili, Tarafa ya Kiagata ujenzi wake umekamilika kwa asilimia 77. Nimwombe Mama Rweyemamu ukamilishaji huu uliotajwa kwenye hotuba si kweli, si sahihi. Kazi ndiyo kwanza inaanza. Bwawa lile sio kwamba ni jipya wala halihitaji ukarabati mkubwa, bwawa lile lilikuwepo. Linalohitajika pale ni kufukuliwa tu lile tope. Kwa hiyo, huu ukamilishaji hapa wa asilimia 77 mimi sikubaliani nao. Na ningemwomba Mama Rweyemamu tufuatane mimi na yeye na Mheshimiwa Naibu Waziri, twende Rwegelo tuhakikishe kwamba je, hii asilimia iliyotajwa hapa ni kweli? Maana yake kazi haijaanza. Bwawa hili ni muhimu, Bwawa la Wegelo ni muhimu. Wanawake wanatoka Tarafa ya Kiagata wanakwenda kuchota maji kilomita 21 mpakani mwa Serengeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kwa unyenyekevu kabisa Mama Rweyemamu ninakupigia magoti bwawa hili la Rwegelo liweze kwisha. Vilevile Bwawa la Chilolwe ambalo lilitajwa mwaka jana, mwaka huu hamjalizungumzia. Bwawa la Mwakinono, Kata ya Kugwema hamjalizungumzia. Bwawa la Bwalanga, mlitaja mwaka jana katika kitabu chenu cha hotuba ninacho hapa, mwaka huu hamjalizungumzia, mnataja tu mabwawa mapya. Kwa hiyo, ningeomba muunganishe hapa mabwawa ambayo mliyataja katika hotuba ya mwaka jana Bwawa la Balanga, Chilolwe, Masinono. Yote hayo yaingie katika mkakati, yaambatane na hilo bwawa la Bwelelo na yaishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni tuliambiwa kwamba hata yale maeneo ambapo bwawa lipo vijiji vile vyote vitapata maji, sasa vijiji vya Rwamchanga, Miseke, Bwitondi, vyote ambavyo vipo Manchila, havina maji. Inakuwa ngumu sana wale wananchi kuwa wazalendo kulinda kile chanzo kama wao wenyewe hawapati maji. Maji yanatoka pale Manchila yanaenda sehemu nyingine, inakuwa sio rahisi! Kwanza wale watu wenyewe wanaohusika na kile chanzo wapate maji ndio yasambazwe kwenda maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaiomba sana Wizara, Waziri na wahusika wote, mjaribu kuliangalia hili. Ujenzi wa bwawa umekamilika lakini bado usambazaji wa maji bado. Vioski vimejengwa, lakini machujio hakuna, maji yale ukiyaangalia ni mekundu yaani tunavyoongelea maji safi na salama sijui kama yale ni safi na salama! Ni mekundu, meusi, hayawekewi dawa! Kwa hiyo, tunaomba hili lizingatiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia ujenzi wa mradi wetu mkubwa sana wa maji unaofadhiliwa na Benki ya Ufaransa kwa kushirikiana na Serikali yetu ya Tanzania, mradi wa *AFD* kwa Miji ya Musoma na Miji ya Bukoba, lakini mimi ninaomba nizungumzie kwa upande wangu mji wa Musoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu nao umeonekana unasuasua sana, hatuelewi ni kwa nini! Sisi watu wa mjini, hatupati visima! Tunategemea tu hii miradi ya Kitaifa, sasa mradi huu usanifu umeshakamilika, lakini hatuelewi ni nini kinaendelea! Hebu ningemuomba Mheshimiwa Naibu Waziri au Waziri atakapokuwa ana-*wind up* hoja yake, atuambie mradi ule wa *AFD,* nini kinaendelea pale? Sisi watu wa Musoma Mjini ndio mradi pekee tunaoutegemea na sasa kama nilivyokwambia, Kata zangu zote kumi hazina maji! Tulikuwa tunausubiri mradi huu, tumeusikia muda mrefu tumeusubiri sana na tunaomba kwa kweli ukamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nirudi kwenye miradi ya visima, miradi ya visima inayofadhiliwa na Serikali ya Japan, tunawashukuru sana wenzetu wa Japan kwa kutufadhili, lakini niseme kwa Wilaya ya Musoma tumepewa visima vitano tu! Sasa Wilaya ya Musoma ina maeneo mawili, ina Musoma Mjini, lakini vilevile ina Musoma Vijijini. Musoma Vijijini peke yake inazo Kata 34, unaipa visima vitano, hebu fikirieni Waheshimiwa Wabunge! *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba hili lizingatiwe angalau hii Wilaya ambayo ni kubwa na ina shida kweli kweli ya maji, watu wake wanategemea maji kutoka Ziwani ambayo sio safi na salama, angalau sasa zile Kata zote 34, kila Kata ipate walau kisima kimoja, visima vitano kwa kweli havitoshi kabisa kwenye hii Wilaya. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kushiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na kengele naona inanigongea naomba niseme naunga mkono hoja na ninampongeza sana mama Rweyemamu, kwa kazi nzuri aliyoifanya kule kwetu Musoma. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rosemary Kirigini. Sasa ilikuwa afuate Mheshimiwa Zabein Mhita, lakini dakika zilizobakia hazitakuwa zimemtendea haki; lakini yupo mmoja ambaye yupo kwenye nafasi nzuri lakini kwa kuwa ana dharura ameomba tumfikirie. Sasa nitamuita Mheshimiwa Juma Njwayo, kwa dakika hizo zilizobakia kama 8, 9 hivi. Mheshimiwa Njwayo. *(Makofi)*

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niungane na wenzangu kuchangia hotuba ya Bajeti iliyoko mbele yetu. Kwa haraka haraka, naomba kwanza ni mpe pole Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Mussa Silima, kwa kufiwa na mkewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namuomba Mwenyezi Mungu, ampe nafuu haraka kwa majereha aliyoyapata, lakini pia kwa Waziri wetu wa Maji, Profesa Mark Mwandosya, Mungu ampe nafuu haraka arudi hapa ili tuweze kushirikiana naye kwenye mambo ya kuliendeleza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba pia Kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dokta Jakaya Mrisho Kikwete kwamba baada ya kumbukumbu ya Mashujaa wetu, tarehe 25 Julai, aliamua kufanya ziara ya makusudi na akatembelea kwenye vyanzo vya maji vilivyoko Mkoa wa Mtwara kujionea hali ilivyo. Hii kwangu ni dalili kwamba ana nia ya dhati ya kutaka kumaliza tatizo hili. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuishukuru Wizara, kwa kipindi kilichopita wametuletea pampu mpya kwenye mradi wetu mkubwa wa Makonde kule, wameleta pampu moja Mahuta, pampu nne Mitema, mbili Mkunya na sasa umeme umefika kwenye maeneo yale, maana hili lilikuwa moja la matatizo makubwa tuliyokuwanayo. Lakini pia naomba kuipongeza Wizara, kwenye Bajeti hii kwa kuonesha kwamba wameanzisha utafiti wa vyanzo vya maji kwenye mabonde yetu ikiwa ni pamoja na Bonde la Ruvuma na Pwani ya Kusini, ni matarajio yangu kuwa sasa tutaongeza kiasi kikubwa cha upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba kuishauri Serikali yafuatayo, la kwanza Serikali iamke kwenye hili tatizo la maji, kuna mambo mengine wala huwezi kujua yanatokana na nini. Kwa mfano, pale Makonde kwa hali iliyopo sasa wananchi hawana sababu ya kukosa maji! Maana mambo haya mawili niliyoyasema ya mitambo na umeme kwamba upo pale, kilichobaki ni kufanya ukarabati tu mkubwa tukamaliza, na Ilani yetu Ibara ya 87 na hata kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa ukurasa wa 7, amesema suala la kufanya ukarabati mkubwa kwenye miradi ile ya Kitaifa sita, ukiwemo wa Makonde. Sasa tunangoja nini kuanza tumalize hii? Maana vinginevyo tunawaletea matatizo, shida ya maji wananchi bila sababu! Tungeanza sasa ili tumalize! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo madogo madogo ambayo kwa kweli tunashindwa kuelewa tatizo ni nini! Maji yanapotea bure, maana sasa maji uki-*pump* yanapotea bure kwa sababu mabomba yetu yamechakaa na ni mabovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iamke hapa, turekebishe yale, tufanye ukarabati kwenye mabomba, watu wapate maji! Hakuna sababu ya kulegalega kama hivi ilivyo. Ukarabati wa mabomba ule unahitaji bilioni tano kumaliza ukarabati wa mabomba kwenye maeneo ya Makonde, kwa maana ya Tandahimba, Newala na Mtwara Vijijini. Hivi Serikali inashindwa kupata bilioni tano tukamaliza jambo hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lipo jambo lingine, kuna chujio pale lilitengenezwa na Wafinland pale Mitema Kitangali, wakati ule wananchi walikuwa wachache, chujio lile lilikuwa linaweza kuchuja maji kwa saa moja uwezo wa lita milioni tatu za maji. Sasa hili linatakiwa lifanyiwe tu utaratibu kidogo ili liweze kutoa maji lita milioni tisa, hatufanyi hivyo, kwa nini? Matokeo yake ni wananchi kulalamika, wakati jambo hili lipo ndani ya uwezo wetu! Tubadilike Wizara ya Maji, tuwaokoe Watanzania, wapate maji kwa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yapo mambo mengine madogo madogo pia, kuna urasimu mkubwa wa watendaji na wataalamu wetu katika kuwasaidia wananchi. Mimi ninao mfano, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifanya ziara mwaka juzi Mkoani Mtwara, akafika Kijiji cha Malamba pale, akakuta wananchi wamechimba bwawa lao la maji. Aliahidi kwamba angewasaidia na aliwaagiza watu wa Wizara ya Maji, wawasaidie wale watu walirekebishe lile bwawa liendane na hali ya sasa na pia wawawekee mabomba ili yaweze kufika kijijini kwao walipo, maana lile bwawa lipo mbali kidogo na kijiji. Lakini tangu mwaka juzi mpaka leo hii hakuna mtaalamu yeyote aliyekwenda kule wala Wizara haijaamka kujali maagizo ya Waziri Mkuu! Nini hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati wananchi wangu wa Kata ya Kitama, wao wenyewe wana mradi pale ulifadhiliwa na wa *JICA* pia na baadaye *TASAF* na unaendelea vizuri. Lakini ulikwama wamekosa maji kwa miezi mitatu kwa sababu ya kumpata tu Mhandisi kwenda pale kurekebisha tatizo hilo, hivi wanakaa miezi mitatu wanakosa maji kwa tatizo dogo tu! Baadaye Mhandisi Goyagoya akapatikana, tena baada ya kurudi toka safari, kana kwamba Goyagoya yuko peke yake Wizarani pale! Hivi hakuna Wahandisi wengine ambao wangeweza wakamaliza tatizo hili? Ndio maana nasema kuna urasimu usio wa lazima. Ni lazima tubadilike Serikalini na kama kweli tunataka kuwasaidia wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siridhishwi na namna mradi wa vijiji kumi kila Wilaya unavyokwenda. Umeanza muda mrefu, hakuna kinachoendelea! Kila siku hapa tunapewa *story* tu! Hadithi tu! Ooh, tupo hapa, tupo hapa, kwa nini hatumalizi? Kwenye visima vile vilivyo sasa vimetobolewa viko tayari, kwa nini sasa havi-*supply* maji? Kuna tatizo gani? Kwa nini tusiweke utaratibu wa kusambaza maji? Na zile pesa zilizokuwa *budgeted* kwenye maeneo ambayo hatukupata maji, zinakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi tuzipeleke kwenye maeneo ambayo maji yamepatikana ili tuweze kuboresha upatikanaji wa maji mengi ili tuwasaidie Watanzania. Mimi naomba jambo hili katika mwaka huu wa fedha, tuonekane kazi imeanza kufanyika! Mara hapa kuna mkandarasi, hapa sijui kuna mkataba, hapa sijui kuna jambo gani! Ni kwa nini jamani hatumalizi? Ndio yale yale tunayoambiwa Watanzania ni watu wa maneno mengi kuliko utendaji! Tubadilike sasa tuendane na wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine ningependa kuishauri Serikali. Kuna hawa Wakala wa Uchimbaji wa Visima na Ujenzi wa Mabwawa (*DDCA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nimeona kwenye Bajeti ya Mheshimiwa Waziri hapa, anasema katika kipindi cha Bajeti kilichopita walipewa mashine ya kuchimba, waliweza kuchimba visima sita na mwaka huu mashine nne za kuweza kuchimba visima, lakini pamoja na kuwasaidia vifaa, hawa jamaa wanapewa Bajeti ndogo mno kiasi hawawezi kujiendesha na kufanya shughuli

za uchimbaji wa hivi visima na mabwawa kwenye maeneo yenye shida. Matokeo yake wanakuwa na vifaa, hawana namna ya kwenda kufanya! Maana Bajeti yao ya kujiendesha haitoshi! Na visima hivi vitatusaidia sana kupunguza matatizo ya maji kwenye maeneo tunayoishi kama tukiwapa Bajeti ya kutosha. Malalmiko mengine yanaweza yakawa yamepungua sana pasipo na ulazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa mambo mawili madogo madogo. La kwanza, kwenye ule Mradi wa Makonde. Tunajenga pale *Mkunya Boosting Station* ambayo itasaidia kusukuma maji ili yaweze kufika maeneo yanayozunguka Mji wa Newala tangu tuanze kujenga, sasa ni miaka mitatu, mradi gani! Boosting Station tu! Kwa nini inachukua muda wote huo hatumalizi, inatakiwa tufanyeje? Tumalize, tumalize miradi tunayoipanga kwa wakati! Na wakandarasi wetu tuwape kila aina ya ushirikiano kutoka Wizarani, tusiwababaishe babaishe maana wakati mwingine kuchelewa kwao, sisi wenyewe ndio *causative agent* kwa kiasi fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho Wafinland walipojenga mradi wa Makonde ule, walipoondoka tukazubaa, kama Serikali na kama nchi, hakuna chochote tulichofanya kuendeleza. Matokeo yake sasa tunapata matatizo makubwa! Hivi Serikali ilikuwa wapi? Kwa nini, tusingechukua hatua sasa ya kuendeleza kile walichotufanyia?

Sasa nalisema hili kwa sababu tunaanzisha miradi mingine, yasirudiwe yale yaliyotokea wakati Wafinland wameamua kusaidia Newala, Tandahimba na Mtwara Vijijini. Nia hapa ni kusonga mbele. Sasa watu wanatusaidia, wakitoka tunakaa wenyewe tunatazamana tu! Haileti tija kwa Watanzania! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya dakika kumi hizi. Mungu akubariki sana, atubariki Wabunge wote na Watanzania wote. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Njwayo, nilikuwa naona unavyo-*enjoy* na hiyo *microphone* nikasema hiyo ndio *size* ya Wabunge wanaotakiwa. Kwa sababu wewe unaifikia vizuri kabisa, lakini Mheshimiwa Mashishanga, kwake ilikuwa shida kidogo. *(Makofi/Kicheko)*

Sasa labda niwasome tu wale watatu watakaonza jioni, ataanza Mheshimiwa Zabein Mhita, atafuatiwa na Mheshimiwa Dokta Festus Limbu na baadaye Mheshimiwa Omary Badwel. Kwa hiyo, hawa wajiandae ndio watakaoanza jioni saa 10.00 jioni wawe tayari. *(Makofi)*

Basi kwa kuwa muda wetu umekwisha wa asubuhi hii, nichukue nafasi hii kusitisha shughuli za Bunge hadi saa 10.00 jioni. *(Makofi)*

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na wachangiaji na jioni hii tutaanza kama nilivyosema wakati tukisitisha shughuli asubuhi, kwamba ataanza Mheshimiwa Zabein Mhita, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu na baadaye Omar Badwe,l na wengine nitaendelea kuwataja. Namwita sasa Mheshimiwa Zabein Mhita.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza mchana huu wa leo, Alhamdulilah Rabil Allamin. Namshukuru Allah Subhana Wataalah, Mola wa viumbe wote kwa kunijaalia kuwa hapa leo, nikiwa mwenye afya njema. Awali ya yote, naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara hii ya Maji kwa kuandaa bajeti nzuri na ya kisayansi kabisa. *(Makofi)*

Vilevile naomba nimpongeze Mheshimiwa Wassira, Waziri aliyesoma bajeti kwa ustadi mkubwa sana. Hongera sana Mheshimiwa Waziri. Aidha, nampa pole sana Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya - Waziri wa Maji na ninamwombea kwa Allah Subhana Wataalah ampe tahfifu, inshaallah, ili naye aweze kuja aweze kuungana na sisi kwa siku za hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie hoja iliyo mbele yetu. Katika jimbo la Kondoa Kaskazini, upatikanaji wa maji umekuwa ni tatizo sugu sana kwa miaka mingi sasa, kwani wanaopata maji ni chini ya asilimia 30. Naomba nirudie, katika Jimbo la Kondoa Kaskazini, wanaopata maji ni chini ya asilimia 30. Kwa idhini yako, naomba nitoe mifano michache ya vijiji ambavyo havina maji kabisa. Kata ya Thawi, vijiji vya Thawi Madukani, Thawi Juu, Sakami, vyote hivi havina maji. Kata ya Kwadelo, vijiji vya Kirere cha Ng'ombe, Kwadelo, Makrinya, hawana maji. Kata ya Kalamba ni karibu vijiji vyote havina maji, kijiji cha Hebi Juu, Hebi Chini, Baura, Loo, Kijiji cha Kalamba Juu, kijiji cha Kalamba Chini, vyote havina maji. Kata ya Haubi, kijiji cha Ntomoko, kijiji hiki ndiyo chanzo cha mtaro huu wa Ntomoko, lakini bado kijiji hiki hakina maji. Vilevile wananchi hawa wamekitunza chanzo hiki vizuri sana, lakini hawafaidiki kabisa na maji. Vijiji ambavyo havipati maji kabisa Ntomoko, Mafai, Haubi yenyewe na Mwisanga. Kata ya Kikore, Kikore, Nkurumuzi, Hurui na Madege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Bumbuta nayo pia ina tatizo. Vijiji vifuatavyo havina kabisa maji. Kijiji cha Mahongo na Kijiji cha Mauno havina maji kabisa. Hapa nimetoa mifano michache sana ya vijiji ambavyo havina maji. Kama laiti ningetaja vyote vingekuwa vingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaoathirika sana kwenye tatizo hili la ukosefu mkubwa wa maji ni wanawake na wasichana ambao hutumia masaa mengi zaidi ya masaa sita kutafuta maji kwenye makorongo, ama kuchimba kwenye mito, maji ambayo siyo safi wala salama na wakati mwingine hawayapati hayo maji kabisa. Wanawake hawa na wasichana wako ambao wamepata ulemavu baada ya kujeruhiwa na kupoteza baadhi ya viungo vyao na wanyamapori wakali na waharibifu.

Wako wengine ambao pia wamepoteza maisha yao katika harakati ya kutafuta maji, kwa sababu huwa wanakwenda kutafuta maji alfajiri sana kuanzia saa tisa za usiku, saa kumi za usiku, lakini maeneo ambayo wanakwenda kutafuta maji ndiyo maeneo hayo hayo wanyamapori nao wanakwenda kunywa maji. Kwa hiyo, athari hizi zinaweza zikawapata. Lakini tatizo hili linakuwa kubwa zaidi kwa wasichana kwa sababu athari hii inawafanya wasifanye vizuri kabisa katika masomo yao kwa sababu wanapoteza muda mwingi kwenda kutafuta maji na wakati mwingine hawaendi kabisa shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasichana hawa ambao wengi wao wana uwezo mkubwa wa kiakili ambao wangeweza kuwa wataalam wetu, wangeweza kuwa wahandisi wa maji kama ambavyo walivyo hapa leo, wangeweza kuwa madaktari, wangeweza kuwa warusha ndege, lakini matokeo yao yanakuwa siyo mazuri kwa sababu ya tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachosikitisha zaidi ni katika kuhangaikia hili tatizo la kupunguza makali ya ukosefu wa maji, kumezuka tena tatizo lingine kubwa zaidi. Tatizo hili ni katika ugawaji wa miradi hii ya maji katika majimbo mawili ya Wilaya ya Kondoa. Naomba nitoe mfano, Jimbo la Kondoa Kaskazini, lina Kata 28, lakini katika hii miradi ya maji ya Benki ya Dunia, katika miradi kumi wao wamepata miradi mitatu. Jimbo la Kondoa Kusini lina Kata 20, wao wamepata miradi saba. Kata 28 miradi ya maji mitatu; Kata 20 miradi ya maji saba. Tunashindwa kuelewa na katika miradi ya *BSSF,* Kondoa Kaskazini yenye Kata 28 wamepata miradi minne wakati Jimbo la Kondoa Kusini lenye Kata 20 wamepata miradi 10. Hii inavunja moyo kabisa. Inakuwaje Majimbo katika Wilaya moja na Majimbo yote yana tatizo kubwa la maji, Jimbo lingine linapata miradi mingi zaidi na lingine linapata miradi michache sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba lieleweke, hili niliseme wazi kabisa kwamba tatizo hili halimhusu kabisa Mbunge wa Jimbo la Kondoa Kusini, kwa sababu mchakato huu ulianza wakati yeye hajaanza kuwa Mbunge. Nimeona niliseme hili isije kukawa na dhana pengine Mbunge huyu amefanya *lobbing*. Kwa kusema kweli, hata yeye mwenyewe amesikitika. Ameniambia dada yangu, inakuwaje? Amesikitika.

Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri na namfahamu Mheshimiwa Waziri wa Maji, namfahamu Naibu wake ni watu waungwana, tena waungwana sana na ni wasikivu sana. Namwomba basi, katika majumuisho yake Mheshimiwa Waziri atoe kauli ya Serikali jinsi ambavyo itashughulikia hili tatizo lililotokea katika haya Majimbo mawili, ili wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini waendelee kuwa na imani na Serikali yao. Lakini kwa kuwa maji ni uhai, wote tunajua maji ni uhai, naamini hata wao wangependa watu wa Jimbo la Kondoa Kaskazini wawe nao na uhai, maana bila maji, hakuna uhai. Basi nao wapate uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuokoa muda. Katika kumi hili la mwisho la mwezi Mtukufu wa Ramadhani, namwomba Allah Subhanah Wataalah atujalie tuwe miongoni mwa watakaopata usiku wa Laila Tulkadir, Inshaalaah. Naomba nichukue nafasi hii niwatakie wananchi wote wa Tanzania na hususan wananchi wa Wilaya ya Kondoa na Jimbo la Kondoa Kaskazini Idd El Fitri Karim, Idd El Fitri yenye Amani na Upendo, Idd El Fitri yenye mshikamano. Inshaalah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na yote niliyoyasema kwa imani kubwa, ninaunga mkono hoja ambayo iko mbele yetu asilimia mia kwa mia, nikiwa na mategemeo makubwa sana kwamba Waheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu watatoa kauli ambayo italeta faraja kwa watu wa Jimbo la Kondoa Kaskazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru tena Kulumbu wangu kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia mchana huu wa leo. *(Makofi)*

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kulihutubia Taifa kupitia Bunge lako Tukufu. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa hotuba nzuri na ninamwombea Mheshimiwa Prof. Mwandosya aweze kupona haraka ili aweze kuendelea na kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniuliza tatizo namba moja kubwa kabisa kuliko yote katika Jimbo la Magu, ni maji. Tatizo la pili kubwa katika Jimbo la Magu ni Maji, na tatizo la tatu kubwa kabisa ni maji. Tarafa zote nne zina upungufu wa maji, Kata zote 18 zina hali ngumu ya maji kuanzia Mahaha huko, Tarafa ya Ndagalu, uje Tarafa ya Itumbili, uje Kahangala, uende mpaka Tarafa ya Sanjo, kila mahali ni shida kwenye Sekondari zote za Kata, isipokuwa moja ya Lugeye yenyewe afadhali. Nyingine zote hazina maji. Shule za Msingi karibu zote labda tano hivi zina matenki ya kuvuna maji, pale Shishani na baadhi ya Shule chache. Ukianza Mahaha mpaka Magu uende mpaka Lubugu, uende mpaka Nyakongoro Bujashi, uje mpaka Kisese Misambo hakuna bwawa lolote ambalo utasema kwamba hili ni bwabwa, wafugaji wananyeshea mifugo yao na wanalima bustani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali ilivyo, mimi naomba niseme siungi mkono hoja kwa sababu nitakazoendelea kuzieleza. Wakati wa kiangazi, wananchi wa Jimbo la Magu huwa hawalali, wanakesha kwenye visima. Nimesema ni Jimbo nzima, akina mama wanaamka usiku wanakwenda kuchota maji kwenye visima ambavyo vimechimbwa, wanahamahama. Tatizo kubwa katika Jimbo la Magu, lilichimbiwa visima chini ya mradi wa Esawa, ambavyo vingi vilikuwa visima vifupi ambavyo wakati wa kiangazi hukauka. Kwa hiyo, Jimbo zima la Magu na Wilaya ya Magu kwa ujumla huwa ni hali mbaya. Wafugaji wanahama, wanafuata maji, wanafuata malisho, afadhali hata kama hawana malisho, kama wana maji angalau wataweza ku-*survive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa malisho hakuna, maji hakuna, mifugo yao ndiyo benki yao. Wanatafuta malisho, wanabanana katika maeneo machache ambayo tunayo katika Jimbo la Magu, wanabanana kando kando ya mto Simi na wanabanana katika baadhi ya maeneo. Lakini kwa sababu mifugo ni mingi, wananchi wanahama, wanakwenda kwenye maeneo mengine. Wakienda kule nako wanafukuzwa, wanakuwa wahamiaji. Watanzania wanataka kula nyama, lakini hawataki mifugo. *(Makofi)*

Kama watu ambao wanataka ajira lakini kazi hawataki kufanya, kwa hiyo, Wasukuma mkitufukuza kwenye maeneo ambayo tumefuata maji, mtutengenezee mabwawa. Ndiyo maana nasema siungi mkono hoja kwa sababu wananchi wa Magu wanafuata maji mpaka Mkoa mwingine, wanafukuzwa wanafanywa wao kama wakimbizi katika nchi yao kwa sababu Serikali haiwatengenezei miundombinu ya maji. Siungi mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kueleza kwanini siungi mkono hoja. Kuna maeneo machache, kuna wafadhili wametusaidia kwa mfano Mfuko wa Chakula Duniani, *World Food Program* mwaka jana walikuwa na miradi kumi katika Wilaya ya Magu, mwaka huu wametupa miradi matatu, wanatusaidia chakula, na wamekubali kufadhili kutoa katika mradi wa Kabila. Nimeongea na *Director* wa *World Food Program* ameniambia katikati ya mwezi ujao wanaanza kuchimba lile bwawa la Kabila na wananchi mlioko wa Kabila, naomba mnisikilize vizuri. Huu mradi unakuja, kutakuja chakula, mahindi, maharage yatakuja na mafuta. Kwa hiyo, tujipange vizuri ili tutumie fursa hii vizuri. Tutaongeza fedha ambazo zimepitishwa hapa za TAMISEMI kwa ajili ya Lambo hili la Kabila ambalo lilijengwa mwaka 1981 na likafunguliwa na Mwalimu Nyerere toka wakati ule halijakarabatiwa. Siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi kumi ya *World Bank*, *is a shame.* Hii ni aibu ya Taifa. Hatuwezi kuendelea kushikilia *World Bank,* tunanyanyaswa kama hatuna mizizi kama nchi. Wilaya ya Magu ilikuwa na miradi kumi, Vijiji kumi. Katika Jimbo langu kulikuwemo Nyanguge Moda, Kigangama Lugeye, Msalabu Binza, Lubugu, Nichobera, Kisesa B, Misambo, ndiyo maeneo yenye matatizo makubwa ya maji. Lakini toka mwaka 2005 tunaambiwa sijui changeni hela, watu wakachanga; ooh, sijui sasa hii kitu ni biashara gani mimi sielewi. Halafu naomba miradi hii ibadilishwe, Serikali i-*take over,* ibadilishe miradi hii kuanzia sasa tutakapopitisha bajeti, japokuwa mimi nitaunga mkono baada ya Mheshimiwa Waziri kunieleza haya nitakayokuwa nimechangia, miradi hii ibadilishwe kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unachimba kisima kwenye eneo ambalo kuna maji karibu na Ziwa. Unapima kisima cha nini? Unachimba visima vya majaribio ili iweje? Kuna maji *next door* kwenye Ziwa, watu wanasema watu wa Magu maji yako karibu, kwa hiyo, mkachote maji kwenye Ziwa. Watu wangapi wameliwa na mamba? Maji yale yana kichocho, tunaambiwa sisi eti kwa sababu tuko karibu, tuachie maji yaende Kahama. Mbona sisi hatujalalamika? Watu wa kwenye migodi wanapata mrabaha, watu waliokaribu na mbuga za wanyama wanapata mrahaba, sisi tulio na samaki jirani, samaki wanavuliwa wanachukuliwa kila siku tunawatazama hivi, wanaondoka. Tukiomba mrahaba wa samaki, hawataki kutupa. *(Makofi)*

Mheshimiwea Mwenyekiti, bado najiuliza, kama nianzishe kampeni za kugomea baadhi ya mambo mpaka Serikali itakapotutendea haki wananchi tunaokaa karibu na Ziwa Victoria! Haiwezekani tukose maji, yatoke Mwanza yaende mpaka Kahama na wanapanga kupeleka mpaka Nzega, mpaka Singida. Sisi watu wa Magu hatuna maji, watu Bunda hakuna maji, hatukubali. Ndiyo! Kuna wanaume ambao wanapigwa na wake zao wameanzisha mtandao, nafikiri na sisi watu tunaokaa karibu na Ziwa Victoria tuanzishe mtandao wa kudai haki zetu. Mrahaba wa maji lazima Ziwa Victoria, samaki zilizovuliwa kutoka kule ni sawa sawa na madini, lazima mhesabu samaki wa Ziwa Victoria sawa sawa na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nasema siungi mkono. Nasema tuwe na mradi kama ule wa Kalemela, Kalemela kwenda Mariri, ulibuniwa vizuri, ulikuwa na Kata nne, Kalemela, Igalupilo, Mkulo, Mariri, Vijiji vingi karibu *one third* ya Jimbo la Busega ilikuwa inapata maji kutoka na mradi mmoja sasa hivi umetelekezwa. Miradi hii ya *World Bank*, sioni sababu ya kuendelea kuwa *implemented* katika utaratibu huu. Unachimba kisima Lugeyi, wakati Ziwa liko karibu, Kigangama! Kwa hiyo, napendekeza mradi wa Msola, Bubinza, Lubugu uende mpaka Kisamba, ifungwe pampu, Ziwa Victoria Msola Bubinza, Lubugu Kigangama, Lugeye bomba la maji. Bahati nzuri kwenye Halmashauri tumekubaliana. Nyanguge, Munda iende mpaka Kisesa B na Misambo halafu maji yatoke Ilungu yaende Ichobele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye maji kwa Jimbo la Magu Mjini. Muda wangu unakwenda haraka, kwa hiyo, nami nitakwenda haraka kidogo. Mradi wa maji Magu Mjini ulianzishwa miaka 17 iliyopita, yaani mwaka 1984, lakini ulijengwa kwa miaka kumi na ulilengwa ku-*expire* baada ya miaka kumi. Kwa hiyo, uli-*expire* mwaka 1994. Ulilengwa kuhudumia Vijiji sita kwa watu 6000 ambapo sasa hivi watu ni mara sita zaidi. Sasa mradi kama ume-*expire* na haujatengenezwa wala haujakarabatiwa, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja Magu tukamweleza matatizo yetu na ameniambia kwamba ametupa hela kidogo, humu mimi sijaziona. Tunaomba mtusaidie na mimi Magu Mjini nilikosa kura kwa sababu ya maji na sasa sikubali kuendelea kukosa

kura hizi, ndiyo maana siungi mkono hoja na wana Magu wanaonisikiliza wajue kwamba sasa niko pamoja nao, nitakuja na nitakapokuja kuanzisha kampeni yangu mniunge mkono, tutakuwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mradi huu wa Magu alikuja mtaalamu akafanya upembuzi yakinifu, akalipwa shilingi milioni 900. Alifanya upembuzi kwamba mabomba yatapita hapa, itakuwaje na kadhalika. Lakini hizo shilingi milioni 900 angalau mngetupa hata sisi, si tupo! Tungeweka mabomba yetu tuka-*survive*. Lakini mtaalamu amepima, amechukua shilingi milioni 900 amesema zinahitajika shilingi bilioni 25. Shilingi bilioni 25 tunazipata wapi Mheshimiwa Waziri? Sisi hizo Shilingi bilioni 25 kwa sasa hatutaki, tunataka utupe shilingi bilioni mbili tu. Katika hizi shilingi bilioni 25 mtaalamu alizoainisha tunaomba utupe shilingi bilioni mbili ili tuinusuru Magu, kwani hali ni mbaya sana. Nikifika magu sijui mahali pa kujificha kwa sababu maji yanatosheleza asilimia 17.

Kwa hiyo, katika watu kumi ni watu wawili tu ndiyo wanapata maji. Nitajificha wapi Mheshimiwa waziri ? Ndiyo maana siungi mkono hoja. Ndiyo !

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapa, lakini nawaombe Wanamagu, Mji wa Magu na Jimbo la Magu wawe wavumilivu, kwani matatizo haya ninayashughulikia na ninaamini Serikali ya CCM ni sikivu, kwa sababu siungi mkono mpaka nitakapopata maelezo, kesho nafikiri nitasema kwamba naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kuwa sikivu kwa kuwasikia wananchi wa Magu ambao sijaelewa toka uhuru wamekosa nini. Jimbo la Magu ni mojawapo kati ya Majimbo yenye matatizo mengi chungu nzima Huwa nazungumza hapa nikiwa nataka kulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kulia.

**MBUNGE FULANI :** Lia!

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Lakini siungi mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana kwa mchango wako ingawa naendelea kupata shida kama kila mtu atataka mrabaha wa eneo analotoka, wale wa Tanga na Dar es Salaam nao wakataka mrabaha wa bahari ya Hindi, sijui hali hii itakuwaje kama Taifa. Nadhani jambo hili linahitaji mjadala wa kitaifa. Pengine mirabaha siyo jibu la matatizo yetu.

Sasa namwita Mheshimiwa Omary Badwel na Mheshimiwa Bernadetha Mushashu ajiandae na baadaye Mheshimiwa Rita Kabati.

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwasilisha vizuri bajeti yao ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampe pole Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa hali ya afya aliyonayo na inshaallah basi Mwenyezi Mungu atamjaalia, atapona haraka na baadaye tutaungana naye ndani ya Bunge hili, ama nje kwa maendeleo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu za maji zinaonyesha kwa ujumla Watanzania wanapata zaidi ya asilimia 50 ya maji. Lakini ukienda kwenye hali halisi katika Majimbo yetu mbalimbali hususan Jimbo la Bahi utakuta wananchi wa Bahi wanapata maji chini ya asilimia 30 na kwa kweli wananchi wa Bahi wana matatizo ya maji na pengine hizi takwimu tusiendelee kuzitoa kwa ujumla kama ambavyo tumekuwa tukizitoa. Tunabweteka, hatufanyi kazi kwa bidii, hatuwajibiki vya kutosha kuhakikisha kwamba wananchi wanatatuliwa matatizo ya maji kwa sababu tunaona zaidi ya asilimia 50 tukisoma hizi takwimu wananchi wanapata maji. Lakini ni vizuri wakati tunatoa takwimu kwa kweli tuainishe kwamba maeneo fulani yanapata maji asilimia fulani

na fulani na yale ambayo kwa kweli yataonekana yanapata asilimia ndogo yapewe kipaumbele badala kubeba takwimu hizi kwa ujumla.

Tumekuwa tukiendelea kuwaumiza wananchi na wao wanashangaa wanaposikia sisi Wabunge tunapokea taarifa kwamba wao wanakunywa maji zaidi ya asilimia 50. Ukiangalia katika Mikoa yenye ukame kama Dodoma mvua hazipatikani vya kutosha. Sasa unaposema watu watahifadhi maji, maji hayapatikani vya kutosha ikifika wakati huu wa kiangazi ndiyo akina mama na watoto wanahangaika sana. Akina mama hawafanyi shughuli nyingine za kiuchumi, watoto wetu hawaendi shule vizuri kwa sababu ya tatizo la maji. Leo hii sisi Wabunge unakwenda katika Mikutano ya kushukuru wananchi na kwa eneo hilo ndiyo umeingia kwa mara ya kwanza, cha kwanza wanakuonyesha vumbi la mwili walilonalo kwa sababu ya ukosefu wa maji katika eneo lile. Wanakwambia Mbunge, sisi tuna wiki mbili au mwezi hatujaoga wala hatujapata maji ya matumizi.

Kwa kweli tatizo ni kubwa na kama mnavyosema ni kweli Serikali sasa iangalie kwa makini na ione na kuainisha matatizo na kuwe mpango kabambe wa kupambana na tatizo la ukosefu wa maji kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu. Kama ambavyo tunaweza kupambana na UKIMWI na matatizo mengine na sasa tunapambana na umeme, lakini tuweke mikakati ya kupambana na maji. Mimi nilidhani kwa kuwa tulikataa hapa hotuba ya Wizara ya Nishati na Madini ingelipaswa kwa kweli tukatae na hotuba ya maji ili na wao tuwape changamoto ya kwenda kuweka miradi kabambe kuhakikisha kwamba wanatatua tatizo la uhaba wa maji katika maeneo ambayo sisi tunawaongoza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie habari ya Makao Makuu ya Wilaya ya Bahi na hapa nimeona katika vitabu kwamba Mji wa Bahi umewekwa katika miradi itakayopata upembuzi yakinifu katika miaka minne ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kweli hatuwatendei haki wananchi wa Bahi kwa sababu wakati wote ilikuwa ni Kijiji na miaka saba iliyopita Bahi imepandishwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya na leo uhamiaji wa wananchi ni mkubwa na chanzo cha maji ni kile kile. Watumishi wa Halmashauri wamehamia Bahi, wafanyabiashara wamehamia na wawekezaji wengine wamehamia pia, lakini Mji wa Bahi bado una matatizo makubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda katika Ofisi za Halmashauri ambazo ni nzuri na mpya zimejengwa kisasa, lakini vyoo vyote vimefungwa kwa sababu hakuna maji. Lakini kwenye bajeti Mheshimiwa Waziri anaposema kwamba Mji wa Bahi umetengewa fedha katika miaka minne ijayo ndiyo uweze kupata maji, mimi sielewi! Hata sijui Wizara wanafanya utafiti gani na tathmini gani ili kujua kwamba kuna Miji mipya na kuna Miji inayokua kwa haraka waiwekee mipango na mikakati ya kuhakikisha kwamba Miji hii inayokua kwa haraka kama Mji wa Bahi unawekewa mpango kabambe wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa kweli siwezi kuunga mkono hoja na nitaeleza kwa kwa nini. Pia siungi mkono hoja kwa sababu yapo mengi ambayo yatanifanya mimi nisiunge mkono hoja na wananchi wa Bahi hawawezi kunielewa kwa hizi takwimu nitakazozitoa za mtiririko wa fedha uliokwenda Bahi katika miaka minne mfululizo kwa ajili ya kutatua tatizo la maji. Kama nitasimama hapa kusema naunga mkono hoja ya Wizara hii nitakuwa nawasaliti wananchi, kitu ambacho siwezi kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge inyanyue *microphone* yako vizuri kidogo.

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2007/2008 Wilaya ya Bahi ilitengewa Sh. 497,903,576/= lakini fedha zilizokwenda ni shilingi milioni mbili. Leo naunga mkono kwa ajili ya nini? Ili waendelee kuniumiza na kuwaumiza wananchi wa Bahi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2008/2009 zilitengwa Sh. 915,163,597/= lakini zimekwenda Shilingi milioni 382, zaidi ya asilimia 50 kidogo. Mwaka 2009/2010 zilitengwa Sh. 473,496,000/= lakini

zilikwenda Shilingi milioni 291. Mwaka 2010/2011 ndiyo ilikuwa kichekesho, kwani Bahi tulitengewa Sh. 1,614,,724,795/= lakini zimekwenda Shilingi milioni 87. Hivi unatarajia watu wa Bahi watatatua lini mzigo wa matatizo ya maji? Mwaka huu nimeona kwenye kitabu tumetengewa Sh. 650,840,000/= sina hata hamu nazo kwa sababu najua na hizi hazitakuja. Tumebaki sisi tunadanganywa kama watoto wa mama kuku wanavyodangannya kwamba mtanyonya kesho; kesho wanaamka hawanyonyi, wanaambiwa tena mtanyonya kesho, na kesho yake wanaamka hawanyonyi. Hii maana yake nini? Kwa nini jambo hili liwe Bahi tu? Kama Waheshimiwa Wabunge wengine kwao kuna matatizo kama haya, watasema, lakini mimi nasemea habari ya Bahi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwa miaka minne mfululizo ya kunyimwa Bahi pesa? Kwa nini?

**MBUNGE FULANI:** Bajeti!

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL:** Bajeti tunaipitisha hapa, tunapitisha vizuri, Halmashauri yangu inajipanga vizuri na Wataalamu wanahangaika wakati wa kuandaa bajeti hawalali usiku wala mchana, bajeti zinakuja, lakini pesa hawapati. Leo mpaka imefika Shilingi bilioni 1,600 lakini unawapelekea Shilingi milioni 87 kati ya Shilingi milioni 497 unawapelekea shilingi milioni mbili, hata kwa mafuta tu ya kwenda kuhudumia visima tu ambavyo vinatoa maji sasa hivi hawawezi. Hii maana yake nini? Huu ni uonevu kwa kweli. nataka maelezo kwa Waziri, ni kwa nini Wilaya yangu ya Bahi imeshindwa kupata fedha vya kutosha katika miaka minne mfululiko na anihakikishie mwaka huu Shilingi milioni 654 zinakwenda asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa anazunguma habari ya maji katika Mji wa Bahi. Halmashauri ina mpango kabambe wa kutoa maji katika Kijiji cha Mbwasa Wilaya ya Manyoni kwenda katika Mji wa Bahi. Naiomba Serikali itoe tamko juu ya namna ambavyo itaweza kusaidia mpango huu wa Halmashauri ambapo kwa kweli tumeomba fedha miaka minne sasa mfululizo hatujapewa pesa hata senti tano katika mpango huu. Ninaomba Serikali itoe tamko hapa ili wananchi wa Bahi wajue na wao hatma yao ya ukosefu wa maji inakaribia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumzie habari ya miradi ya *World Bank.* Miradi ya *World Bank* imekuwa ni kichekesho!

**MBUNGE FULANI:** Sana!

**MHE. OMARY AHMAD BADWEL:** Sisi tumepata wakati mgumu sana, na kama nilivyosema kwamba sasa tunapita kushukuru kwenye Majimbo, maswali makubwa katika vijiji vile kumi unaulizwa habari ya *World Bank.* Tumechoka kwa kweli kutaja misamiati mbalimbali inayotumiwa na Wizara kwa mfano upembuzi yakinifu, sijui wawekezaji waelekezaji, sijui tenda zimetangazwa na kadhalika. Kila siku ukiulizwa unapewa misamiati katika eneo hili la miradi ya *World Bank.* Hii misamiati itakoma lini ili watu wanywe maji?

Leo wakichimba visima katika vijiji sita, basi vinne havina maji na viwili vina maji, lakini ukiangalia mamilioni ya fedha yamepotea. Mimi nashangaa sana kwa kweli, utaratibu wa sasa wa namna ya kutoa hizi tenda, huo ushauri elekezi ni ghali mno, kuchimba ni ghali mno lakini maji hayapatikani. Sasa katika hili pia tuambiwe, vile vijiji ambavyo havikupata maji Serikali ina mpango gani? Maana tunaona vimerushwa miaka miwili hadi mitatu mbele na wananchi wana matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli sisi tulifurahi sana tuliposikia habari ya vijiji kumi, kwa mfano karibu miaka sita sasa imepita toka mwaka 2005 tukawa tunajua vijiji kumi kumi angalau kila baada ya miaka miwili, lakini leo kwa mimi mwenye vijiji 56 na ningekuwa nazungumzia habari nyingine hapa, leo ningesimama kupongeza Serikali hapa, juu ya hali halisi ya utatuzi wa matatizo ya maji. Lakini leo miaka sita imepita, hata kijiji kimoja hakijapata maji, wakati kwa maana ya vijiji kumi kumi, mimi leo ningekuwa namalizia katika Wilaya ya Bahi kwa maana nina vijiji 56, Jimbo na ndiyo Wilaya. Lakini habari hiyo imekuwa ni hadithi na imekuwa ni kutudanganya. Nasema safari hii hapa kwa kupitia Wizara hii na bajeti yake itoe tamko ambalo tutalibeba ambalo litakwenda kufanyiwa kazi na kwa kweli maji yapatikane sasa katika hivyo vijiji kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme katika habari ya vijiji kumi, Jimboni kwangu ninaomba Mheshimiwa Waziri hili aliruhusu. Kuna kijiji kinaitwa Kijiji cha Mundemu. Kijiji cha Mundemu kimefanyiwa utafiti na uchimbaji, lakini maji hayakupatikana. Lakini Kijiji cha Mundemu kipo karibu sana na Mzakwe ambapo ndipo *station* kubwa ya maji yanayokuja hapa Dodoma na bahati nzuri Mzakwe kulikuwa na kijiji wakati fulani kikaja kikaondolewa kwa ajili ya kuhifadhi vyanzo vya maji. Lakini pale kuna kisima cha maji chenye uwezo wa kutoa lita zaidi ya 40,000 kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukihangaika tukasema, basi kwa sababu hapa ni karibu, huu mradi wa *World Bank* uko hapa badala ya kuchimba kisimba ambacho ni ghali sana, maji yakachukuliwe Mzakwe. Lakini kulikuwa na kizungumkuti sijui, lakini kwa sababu mimi nafikiri wenzetu wanataka lazima wachimbe ili hizo fedha wazitumie, lakini sisi tunasema pale mahali ambapo inawezekana kuchukua maji turuhusiwe Kijiji cha Mundemu kuchukua maji Mzakwe na maji yakichukuliwa Mzakwe yanaweza kwenda Mundemu, Nguji mpaka katika Kijiji cha Chilungulu, yakasaidia kwa uhakika wananchi wakaondokana na tatizo hilo la maji. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, tumeandika barua, bado iko *DUWASA* hatujapata majibu. Tunaomba tusaidiwe tupate majibu ili tuweze kutumia kisima hicho kwa ajili ya watu wa Mundemu, Nguji na Chilungulu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mingine ambayo ni kizungumkuti nayo ni miradi ya *BSF* zamani ilikuwa ni *BFS*, nayo leo ni miaka saba wananchi wameombwa kuchanga, wananchi wamechanga tena kwa asilimia ya thamani ya miradi ambayo itatengenezwa pale kwao, lakini mpaka leo pale wananchi hawajanywa maji.

Ukifika wewe Mbunge wanakwambia mchango tumechanga na sasa hatutaki kuchangia tena kwa sababu hatuoni maji, tunaona Wataalamu kila siku wanapishana, ni misamiati tu. Tunataka tuambiwe na hii miradi ya *BFFS* ina utaratibu gani? Mbona miradi inayofanywa na Halmashauri haina mzunguko mkubwa kama miradi inayokuja kufanywa na wafadhili? Unaambiwa mpaka wakubaliwe, mnakuja mnaandika *document* inakwenda sijui Ulaya, inarudishwa, inaandikwa nyingine na kila siku ni matatizo mpaka tupeleke huko kwao. Hivi Watanzania hawa hawana uwezo wa kununua hivyo vitu? Kama wametuamini kutupa fedha nyingi nyingine katika miradi mingine, kwa nini katika miradi ya maji lazima hizi fedha wazing'ang'anie wao na wananchi wanachelewa kupata hii huduma ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Wataalamu ni wachache mno. Wizara hii iangalie leo vijijini kule mashine zikiharibika ili wampate mtaalamu kutoka Halmashauri kwenda kutengeneza, ni wiki moja, mbili au tatu na mwezi mpaka Mbunge upigiwe simu, upige kelele watu wajipange waende kule. Naomba tuangalie na hili suala la Wataalamu wanaosaidia mashine na pampu zetu mbalimbali nao waongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia usimamizi wa miradi sehemu nyingi ni mbovu. Miradi mingi inakufa haraka, Kamati hazina uwezo, watu wa Halmashauri uwezo wa kusimamia umekuwa mdogo, hawajitumi. Naomba tupate utaratibu mzuri ambao Wizara itaandaa juu ya usimamizi wa miradi mbalimbali ya maji katika maeneo yetu. Miradi inakufa haraka, miradi mipya unashangaa mara siku mbili au tatu tunahitajika kutengeneza. Lakini pia hakuna vifaa mbalimbali, leo *load* moja ikianguka tu chini Wilaya hiyo kupata hiyo *load* mpaka wakaazime gari mahali fulani ili kubeba ule mtambo. Tunadhani hata vitu hivi vingekuwa kwa wingi hata kwa Mkoa kiwe kimoja au viwili kwa kuandaliwa na Wizara ili tatizo la maji linapotokea wananchi wasikae tena kwa muda mrefu kukosa maji katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko miradi mingine inachakaa haraka mno. Kwa mfano, *hand pump* zinafungwa sijui zinathibitishwa na nani uimara na ubora wake. Zinaletwa katika vijiji vyetu, zinafungwa siku mbili au tatu hakuna *pump. Pump* zimeshaharibika na hazitumiki tena. Tunadhani kwa kweli vitolewe viwango stahili ili wananchi wanapopata hizo *pump* waweze kweli kuondokana na tatizo la maji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho pia kuna mahali maji yanaendelea kutolewa bure. Sera inasemaje? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko, hivi kuendelea kutoa maji baadaye unakwenda Mbunge ndiyo unaambiwa mashine hapa imeharibika, gharama ya

kutengeneza ni shilingi laki mbili, unawauliza hivi ninyi hamna? Unaambiwa laki mbili hatuna, kwa sababu maji tunakunywa bure. Hebu yatolewe maelekezo ili wananchi wachangie hii miradi ya maji kwa manufaa yao na kwa maslahi yao. Hatuwezi kuwa tunachukua ndoo kumi au ishirini za maji bure, unatumia kwa siku, halafu siku *pump* zinaharibika hakuna mifuko ya maji na wala hakuna hata senti tano mahali husika, kazi inakuwa ya Mbunge na Diwani. Kwa hiyo, nadhani kwa kweli yatolewe maelekezo makini juu ya watu kuchangia hata kama kwa bei ndogo, lakini watu wachangie miradi ya maji ili miradi ile iwe endelevu na iweze kudumu na hata waweze kusambaza mahali pengine wao wenyewe kwa kujitegemea kupitia ile mifuko yao ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mahali pengine nimekuta mifuko ya maji ina fedha nyingi kama shilingi milioni tatu, nne au tano. Lakini ukifika Mbunge wanakwambia tunaomba utusaidie kusambaza maji. Ukimwuliza mtaalamu gharama ya kusambaza maji ni shilingi ngapi, anakwambia ni shilingi milioni mbili na wana shilingi milioni nne Benki. Pia hawana maelekezo ya kutumia fedha, wengine wanadhani fedha zile ziendelee kujilundika, waendelee kuzitazama Benki wakati wenzao wanazikopa na kuzitumia, wao wanaendelea kulia shida ya maji. Kwa hiyo, ni vizuri maelekezo yakatolewa na pengine hata watalaamu wa Wilaya wanakuwa wanaogopa namna ya kutumia fedha zile ambazo tayari zipo kwenye akaunti za maji za vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, na mimi nasema siungi mkono hoja mpaka nisikie Bahi ni lini wanakunywa maji na nijue bajeti sasa zitakwenda Bahi kwa mtiririko na nijue ni kwa sababu gani Wilaya yangu ya Bahi kwa miaka minne kwa mfululizo haipati fedha zake kama ambavyo tumepanga na tumepitisha hapa katika Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Omary Badwel - Mbunge wa Bahi na ninajua Bahi wamekusikia. Sasa nitamwita Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu.

**MHE. BENARDETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyo mbele yetu.

Kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kuandaa hotuba nzuri. Lakini vilevile namwombea Waziri apone haraka ili arudi tuweze kushirikiana naye katika mambo ya maendeleo. Pia nampongeza rafiki yangu na mtani wangu Mheshimiwa Wassira, amewasilisha vizuri hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Ofisi za Maji zote za Bonde, pamoja na Bodi za Maji za mabonde yote tisa Tanzania, kwa kazi nzuri ya usimamizi wa vyanzo vya maji na usimamizi wa raslimali maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapa pole Ofisi ya Bonde ya Maji ya Ziwa Victoria pamoja na Bodi ya Maji ya Ziwa Victoria kwa kufiwa na Mwenyekiti wa Bodi - Ndugu John Mayunga. Alikuwa ni mchapakazi, tulimpenda sana, lakini Mwenyezi Mungu kampenda zaidi. Tunaomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema Peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali kwa hatua walizochukua, miradi mbalimbali iliyotekelezwa ambayo imeweza kuongeza upatikanaji wa maji safi na salama vijijini kutoka asilimia 53.7 hadi asilimia 57.8. Lakini tunasema bado kwa sababu wote tunatambua kwamba maji ni raslimali muhimu, na bila maji, hakuna kilimo, bila maji maendeleo yatadumaa, bila maji kutakuwa na ukame na bila maji kutakuwa na uhaba wa chakula. Kwa hiyo, wote tunatambua kwamba maji ni uhai.

Nchi yetu imejaaliwa na Mwenyezi Mungu, tunayo mito mikubwa, mirefu na mingi, tunayo Bahari ya Hindi, lakini vilevile tunayo maji mengi yanayopita ardhini kama ilivyo hapa Dodoma. Lakini inabidi hayo maji tuyatunze, tutunze vyanzo vya maji, tuache kukata miti hovyo, watu wahamasishwe waache kuchoma mioto hovyo na kila mtu ikiwezekana apande miti mingi tuweze kulinda maji yetu. Kwa sababu watu tunaongezeka na shughuli za binadamu zinaongezeka, matumizi ya maji yanaongezeka, maji yaliyopo yanazidi kupungua hivyo inabidi tuyatunze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitika kusema kwamba kuna uchafuzi mkubwa wa maji hadi leo. Ukienda kwenye migahawa, mabaa, majumbani usiku wanatiririsha maji ya choo kwenye mitaro ambayo inabeba maji ya mvua na yale maji machafu yanatiririshwa moja kwa moja kwenye mito, maziwa hata kwenye bahari. Lakini ukienda kwenye viwanda vya nguo, viwanda vya samaki kwenye migodi na machimbo mbalimbali unakuta kwamba wanatumia maji viwandani. Hawa watu wanatumia kemikali kali, wanatumia sumu mbalimbali, lakini wanavyoyarudisha yale maji, wanayarudisha na uchafu ule ule. Unakuta baadhi ya viwanda hawana miundombinu ya kutosha, hawana *oxidation ponds* za kutosha kuweza kusafisha yale maji na kurudisha kule yakiwa na hali inayotakiwa. Haya maji machafu yakishaingia kwenye maziwa, mito, au kwenye bahari unakuta yanaathiri samaki, viumbe hai na hata watu wanaotumia yale maji wanaweza kupata hata kansa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza basi kwa Serikali, kwanza kabisa, waajiri wataalam wa kutosha wa kuweza mara kwa mara wakawa wanapima ubora wa maji kusudi kama kuna uchafuzi wowote uweze kugundulika mara moja. Lakini la pili, naomba Wizara ya Maji niwashauri mfanye kama Wizara ya Afya. Nendeni mkafanye *suprise check* kwenye migodi, kwenye viwanda mbalimbali mkikuta watu hawana *oxidation ponds* za kuweza kusafisha yale maji, funga hivyo viwanda, funga hiyo migodi kwa sababu inaathiri watu. Mpaka pale watakapokuwa wameweka miundombinu inayotosha inayoweza kusafisha maji, basi muweze kuwafungulia, hivyo viwanda vyao au sivyo watu wataendelea kuathirika wakati sheria zipo, lakini sheria hazifuatwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kagera una upungufu mkubwa sana wa maji kwa wastani hapo vijijini, upatikanaji wake ni asilimia 53. Lakini ukienda kwenye Wilaya moja moja unakuta kwamba upatikanaji wa maji safi na salama ni mdogo kuliko huo wastani. Watu wanataabika, wanahangaika kutafuta maji safi na salama. Lakini wote tutambue kwamba bila ya maji hakuna maendeleo. Bila maji hatuwezi kutengeneza viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao yetu. Bila maji, kutakuwa na milipuko ya magonjwa ya hapa na pale watu hawataisha kuhara mpaka kuhara damu. Mkoa wa Kagera kuna Wilaya zenye maeneo ambayo hayana maji ya kutosha nikianza na Bukoba Mjini. Bukoba Mjini imepakana kabisa na Ziwa Victoria, utashangaa watu wa kule juu *Green Belt,* wengine bado wanaendelea mpaka leo kuchota maji kwenye mito, wakati ziwa wanaliona pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Karagwe, kuna maeneo mengi makavu, wana mifugo mingi, unakuta Karagwe kuna milima mingi, wana matatizo makubwa ya maji. Upatikanaji wa maji Karagwe ni asilimia 46 tu. Muleba kuna maeneo makubwa makavu, kuna mifugo mingi, upatikanaji ni asilimia 55 tu na ya Muleba ina visiwa vingi na visiwa mnajua vinakuwa vimezungukwa na maji ndiyo maana asilimia inaonekana ni 55. *Actually,* ni chini ya hapo. Misenye na yenyewe ina maeneo makavu mengi. Ukienda kule Minziro, ukaenda Kilimilile, Bubale, Byejwe unakuta maeneo ni makavu, kuna watu wanaishi kule, kuna mifugo, lakini hakuna maji. Naomba Serikali itoe fedha kusudi waweze kujengewa mabwawa makubwa na visima virefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuamini, lakini hadi leo Biharamulo upatikanaji wa maji uko kati ya asilimia 40 na 45. Mji wenyewe wa Biharamulo unahitaji karibu *cubic metres* 38,000 kwa siku, lakini wanapata 12,000 tu. Kwa hiyo, unaweza kujua tatizo ni kubwa kiasi gani. Lakini pale pale kuna chanzo cha Ruziba, Serikali itoe fedha wakitengeneze kusudi wakazi wa Biharamulo Mjini waweze kupata maji. Ukiangalia huko Biharamulo kuna Kata za kina Nyamigogo, Nyakahura, haya ni maeneo makavu. Kulikuwa na miradi ya *Concern,* wanachimba visima vifupi vifupi, havitoshi. Ukienda pale Nyakahura *Secondary School* utaumia. Tunaomba Serikali itoe fedha kwa Biharamulo kusudi kwenye Kata nilizozitaja waweze kuwachimbia visima virefu. Ndugu zangu nilipotembelea pale nilikutana na akinamama wa pale Nyakahura wakaniambia mwanamke anapoondoka asubuhi anatumia zaidi ya masaa matano mpaka saba kwenda kuchota maji muda ambao angeutumia kufanya kazi nyingine za maendeleo. Ninaomba kwa kupitia kwangu mkisikie kilio cha Wana-Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 1971 mpaka 1991 kulikuwa na mradi mkubwa wa maendeleo ya maji vijijini. Wakati sisi tunasoma Shule ya Msingi watu ambao tunalingana tulikuwa tunachota maji kwenye mito. Lakini wakati tumefikia sekondari tulikuwa tunachota maji ya bomba, maji yalikuwepo mpaka vijijini. Huu mradi uliweza kuenea katika vijiji vingi. Nashangaa

sasa hivi watu wamerudi kule kule tulikotoka wanachota maji mitoni. Bukoka Vijijini kuna miradi ya namna hiyo ambayo ilianzishwa tangu mwaka 1971.

Kwa mfano, ule mradi wa *pumping scheme* wa Maruku ambao ulikuwa unapashwa kusambaza maji Kata ya Maruku na Kanyangeleko. Kuna mradi wa Katoma ambao ulikuwa unapashwa kusambaza maji katika vijiji vya Ilegelo, Kashenge na Lukindo, yote imeharibika, hakuna ukarabati, inabidi sasa tuanze upya. Hii ni aibu. Haiwezekani tunazidi kurudi nyuma. Vile vile kuna Tarafa ya Rubale kule Kibirizi, Luhunga, Mikoni, Butainamwa, Rukoma wote wana matatizo ya maji, inabidi wajengewe mabwawa makubwa. Vile vile kuna mahali ambapo kuna vyanzo vya maji, wawekewe mabomba, wachimbiwe visima ili waweze kupata maji tuondokane na haya matatizo tunayoyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifikiri kwamba mkombozi atakuwa mradi wa maji ya vijiji kumi kwa kila Halmashauri. Mwaka 2008/2009 hakuna, mwaka 2010/2011, sasa hivi tunaingia 2012 hakuna. Maji ya vijiji kumi yako wapi? Kwa *speed* hii ina maana Halmashauri nyingine zina vijiji mpaka 100, ina maana watachukua miaka 20 kabla maji hayajafika kwenye kila kijiji? Hii ni aibu. Tumechoka! Kila siku mnasema wanaajiri wataalam washauri, wanatengeneza makabrasha ya zabuni, wanafanya usanifu, vyanzo vinatafutwa na wamepata ridhaa ya Benki Kuu, watu wamechoka na hizi *statements,* wanachotaka ni maji. Walianza na vijiji kumi, mara wakasema vijiji viano, sasa ni vijiji kumi au vitano? Ningependa kujua kati ya vile visima 83 vilivyokwishajengwa vyote vinatoa maji au viko pale tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *trans-boundary waters.* Nchi yetu inapakana na nchi jirani, tuna-*share* maji. Kwa mfano, Ziwa Victoria tuna-*share* Uganda, Kenya na Tanzania na Ziwa Tanganyika tuna-*share*, Ziwa Nyasa tuna-*share,* mito ya Kagera tuna-*share,* Mto wa *Nile* na wenyewe tuna-*share*. Yote haya maji tunayotumia tunachangia na nchi jirani, ni maji shirikishi au *trans-boundary water*. Kwa Tanzania, maji yote tunayotumia asilimia 43.4 yote ni maji ambayo tunashirikiana na nchi nyingine. Kila nchi ina matumizi yake bila kujali nchi nyingine inafanyaje. Juzi juzi hapa Uganda walitumia maji mengi waka-*over draw* kwa sababu walikuwa na miradi mikubwa wamefungua ya umeme. Ziwa Victoria kina kiliporomoka, ikawa ni hatari kweli. Je, Tanzania tunayo mikataba ya kulinda maji yetu haya ambayo tunashirikiana na nchi nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya wakati huu, wakati maji safi yamepungua duniani tunayo mikakati gani ya kulinda haya maji ambayo tunashirikiana na nchi nyingine. Tusije tukakuta tumefikia mahali pabaya. Wataalam wamesema vita kuu ya tatu itatokana na uhaba wa maji, tutafika pale Ziwa Victoria, Uganda wanasema Tanzania msitumie, sisi tunasema Kenya msitumie, tutagombana. Je, mikataba inatosha? Tunazo sheria zinazotosha au irudishwe hapa Bungeni tujiandae kwa sababu hali huko tunakokwenda siyo nzuri, tunaweza tukakuta tunaanzisha vita hapa kwa sababu ya kutokuwa na mikakati ambayo inalinda maji vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na wengine, mimi nasema wanawake wamechoka kuchota maji mpaka wameota sugu kichwani. Watoto wamechoka kuchota maji! Napendekeza kwamba Serikali iongeze bajeti kwa Wizara hii ili tuweze kupata maji ya kutosha. Lakini vile vile kusudi hizi shilingi karibu bilioni 874 walizopewa nisipounga hoja mkono ina maana kwamba hata vile visima haviwezi kujengwa. Kwa hiyo, naunga mkono hoja kusudi wale wakazi wa Mkoa wa Kagera waweze kujengewa visima vingi zaidi, waweze kupata maji ya mabomba na waweze kutengenezewa mabwawa mengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kunisaidia muda. Namwita Mheshimiwa Lekule Laizer atafuatiwa na Mheshimiwa Suleimani Zedi na Mheshimiwa Mipata ajiandae.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ningependa kusema, ubarikiwe sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kuhusu kero iliyopo katika Jimbo langu la Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu nizaliwe nimekuta kero hii ya maji katika Jimbo la Longido mpaka hivi leo na sioni dalili ya kuondoka. Tatizo la maji katika Wilaya ya Longido ndiyo limeiletea umaskini katika jambo hilo. Wananchi hawana maji, acha maji salama yanayosemekana maji

salama, hatuna. Mifugo haina maji na ndiyo maana wanakufa kila wakati, hata maisha bora yanayosemekana kwamba maisha bora kwa kila Mtanzania, bado ni kitendawili kama maji hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Longido, wananunua maji debe ni Sh. 1,500/=. Unanunua maji ya kufulia, kunywa na ya kuoga, hata wanafunzi katika shule hawana tena nafasi ya kusoma wakienda kutafuta maji. Jana nilikwenda Shule ya Sekondari ya Longido, nilikuwa na Wabunge wawili, Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Nyambari Nyangwine. Wanafunzi wanatuambia tatizo la shule yetu ni maji, siku hizi hatusomi, tunahangaika kutafuta maji. Hakuna tena kufuata ratiba, hata taaluma inashuka katika shule hiyo pamoja na kwamba ilikuwa ni shule mojawapo nzuri katika Mkoa wa Arusha, lakini kwa ajili ya tatizo hili la maji taaluma inaanza kushuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nashangazwa na Halmashauri zetu kwa sababu ukiangalia ni kama Serikali imeitupa Halmashauri. Fedha zinazopelekwa kule zinakwisha kwa Watendaji. Fedha za maji tunayosomewa hapa, kuna fedha za uwezeshaji, ambapo sijawahi kuona uwezeshaji unaofanyika, lakini kwenye bajeti ya Waziri iko *column* kabisa fedha za uwezeshaji zinakwenda wapi? Zinaishia katika mikono ya watu, matumbo ya watu, lakini TAMISEMI iko kimya. Sasa naishangaa TAMISEMI, fedha za maji zinakwenda TAMISEMI, barabara TAMISEMI, mifugo TAMISEMI na mabwawa pia, lakini hakuna kinachofanyika. Hakuna ukaguzi wowote unaofanyika katika Halmashauri zetu. Hii TAMISEMI inashindwa kazi. Imeshindwa kusimamia miradi iliyopo katika Halmashauri. Kwa hiyo, kero nyingine katika Serikali yetu, ni usimamizi wa miradi. Ufisadi uko hapo TAKUKURU, uko kila Wilaya, lakini nao wamekaa kimya. Sijui kwa nini fedha za Halmashauri Serikali haina huruma nazo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la vijiji kumi kwa kila Halmashauri. Nadhani hakuna Mbunge atakayesimama kuzungumzia maji ambaye hataacha kuzungumzia vijiji kumi kwa kila Halmashauri. Kama walivyozungumza wenzangu, hii imekuwa kero. Tumetumia kwenye kampeni, kwa kila kampeni tumetumia vijiji kumi. Katika bajeti hii Serikali itoe msimamo, ifute kuanzia leo kwamba hakuna tena hivyo vijiji na sisi twende kuwaambia wananchi jambo la kweli. Kuna watu wengine ambao hawawezi kusema uongo. Mkipitisha bajeti hapa mkatueleza na sisi tutakwenda kuizungumzia ilivyo, sisi Wabunge wa Majimbo ndio tutaulizwa kwamba iko wapi miradi ya *World Bank?* Mpaka leo Serikali haitaki kusema ina kigugumizi kutuambia ukweli. Tunajua kwamba kama ni fedha za mkopo, mkopo unaweza ukakosekana siku yoyote. Kama imekosekana mtuambie hizi fedha haziko tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la mabadiliko ya tabia nchi. Ni kweli hali imebadilika, wote tunaona kwamba miaka iliyopita ni tofauti na miaka ya sasa na inawezekana ikabadilika ikawa ni mbaya zaidi katika miaka ijayo. Inafaa Serikali sasa ikae na kutumia wataalam tulionao waangalie hali hii kwamba badala ya ongezeko kuongezeka itakuwa nafuu wananchi wakapata maji kumbe baadaye ikawa mbaya zaidi. Sasa Serikali itumie wataalam wake tuone kwamba hali inakwendaje ili Serikali iweze kujiandaa kikamilifu wananchi wasije wakakosa maji kabisa katika baadhi ya maeneo badala ya kusema kwamba maji yataongezeka na miradi inayofanyika itaendelea, kumbe maji hayatakuwepo katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila bajeti inaandikwa Wilaya kame. Kila mwaka unakuta Longido, Monduli, Simanjiro, Kiteto, ukiangalia katika bajeti zote za kila mwaka ipo, lakini Serikali haijawahi kuangalia tatizo lililoko, haijawahi kujenga mabwawa katika maeneo hayo. Lakini kwenye bajeti wanasema kwamba tutajenga mabwawa katika Halmashauri kame mpaka lini? Kila bajeti, hata bajeti hii Waziri leo amesoma ametaja Longido, Monduli, Simanjiro, Kiteto. Mwaka ujao atataja hivyo hivyo na mwaka mwingine tena hivyo hivyo, mpaka lini? Mnajua hakuna mabwawa yanayojengwa. Mwaka juzi Serikali imetujengea bwawa wakatoa shilingi milioni 640, lakini ukiangalia hilo bwawa siyo la shilingi milioni hata mia moja. Hakuna usimamizi na nimemwita Waziri aende kuzindua hilo bwawa. Amekwenda mwenyewe akashangaa, akasema lazima Serikali ijenge hili bwawa tena. Lakini sikusikia yule mkandarasi amefanywa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli Waziri amehakikisha kwamba fedha zimeliwa, wakanyamaza kimya kana kwamba hakuna kilichofanyika mpaka leo. Hata kwenye bajeti

sikuona pamoja na ahadi ya Waziri, sikuona lakini nategemea kwamba litafanyika kwa sababu nina imani sana na Waziri na Katibu Mkuu Christopher Sayi. Nina imani kwamba watatekeleza. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, siyo kwamba fedha hazipelekwi katika Halmashauri zetu, fedha zinaliwa. Kuna mtu hapa katika Halmashauri zetu na tusipolisimamia hilo hata bajeti ikiwa kubwa namna gani hakuna litakalofanyika.

Mheshimimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kwa kuiomba Serikali kwamba katika mwaka huu wa fedha muiangalie Longido. Mji wa Longido umekuwa ni mji mkubwa kwa sasa lakini kuna tatizo kubwa la maji. Kwa hiyo, naomba Serikali iokoe maisha ya watu wa Longido ili nao waweze kupata maendeleo. Huwezi ukajenga kwa kutumia maji ya kununua kwa Sh. 1,500/= kwa ndoo. Huwezi kufanya jambo lolote la usafi wa mazingira bila maji. Naomba jambo la Longido liwe ni jambo la dharura na haraka kuokoa Mji ule ambao una matatizo makubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niseme wananchi wa Longido wanisikie, wasije wakasema kwa nini Mbunge amenyamaza na tuna tatizo la maji. Wamesikia na nadhani Serikali nao wamesikia, kwa hiyo, tutasubiri majibu na kesho nao watakaa karibu na televisheni kusikiliza majibu ya Waziri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Laizer mliosema mmepata bahati, lakini pia hata ambao hatujasema pia wananchi wanajua kwamba tunawawakilisha na naamini Serikali itachukua matatizo yetu kwa pamoja. Sasa namwita Mheshimiwa Selemani Zedi atafuatiwa na Mheshimiwa Desderius Mipata.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa niaba ya wananchi Jimbo la Bukene niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji. Kwanza nachukua fursa hii kumpa pole Mheshimiwa Silima ambaye amepoteza mke wake katika ajali ya gari na yeye mwenyewe nimwombee apate nafuu mapema. Vilevile nachukua fursa hii kumtakia Waziri wa Maji - Mheshimiwa Mwandosya apate ahueni mapema ili arudi katika kutekeleza majukumu yake ambayo yanaikabili Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tunasheherekea Miaka 50 ya Uhuru wa Nchi yetu. Lakini nasikitika baada ya miaka 50 ya uhuru wa nchi yetu tatizo la maji bado ni kubwa sana. Upatikanaji wa maji safi na salama hasa maeneo ya vijijini bado ni tatizo kubwa sana. Naungana na Mheshimiwa Badwel ambaye katika mchango wake alisema sasa hivi umefika wakati tuachane na takwimu za ujumla. Kiukweli takwimu za ujumla zinatuambia kwamba katika maeneo ya vijijini upatikanaji wa maji safi na salama umefikia asilimia 57 au 58 lakini hali halisi ya upatikanaji wa maji safi na salama maeneo ya vijijini bado ni shida kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka 50 baada ya uhuru kuna maeneo ya vijijini, kama Jimbo langu la Bukene kuna Kata ambazo mpaka leo Kata nzima haina hata kisima kimoja cha kisasa. Mimi nina Kata ya Semembela, Kata nzima na wananchi wote wa Kata nzima wanategemea maji ambayo yanapatikana katika visima vya kienyeji katika makorongo na ambayo wakati wa kiangazi maji hakuna kabisa. Wananchi wanateseka kwa kiwango cha juu. Maeneo ya Kata za Semembela, Kata ya Kasela, maeneo ya Kata ya Sigili, shida ya maji ni kubwa sana. Sasa athari ya kutopatikana kwa maji salama na safi na ya uhakika katika maeneo ya vijijini inaathiri mpaka sekta nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu kwamba wazalishaji wakubwa maeneo ya vijijini ni akina mama. Sasa kunapokuwa na upatikanaji mbovu wa maji, akina mama wanatumia muda mrefu, wanaamka alfajili saa tisa na saa kumi kwenda kutafuta maji na huko katika maji akina mama wanatumia muda mrefu, anarudi nyumbani saa nne na ndoo moja au mbili za maji. Kwa hiyo, huyu ambaye ni mzalishaji anatumia masaa matano au sita kuhangaika kutafuta maji. Kwa hiyo, kwa ujumla wake unakuta sekta nyingine za uzalishaji kama kilimo zinaathirika kutokana na tatizo kubwa la upatikanaji wa maji hasa maeneo ya vijijini. Kwa hiyo, rai yangu kwa Wizara ni kwamba ni lazima tuwe na mikakati ya makusudi tutoke hapa tulipo. Ni lazima tutoke hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nitumie fursa hii nizungumzie mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria kutoka Kahama kupelekwa katika Wilaya ya Nzega, Igunga na hatimaye Tabora Mjini. Mkoa wa Tabora ni moja kati ya Mikoa ambayo kwa Uchaguzi Mkuu uliopita walitoa kura nyingi sana kwa Chama cha Mapinduzi na Serikali yake hii. Niseme tu kwamba kama kuna jambo kubwa lililowavutia, lililowapa imani wananchi wa Mkoa wa Tabora, wananchi wa Jimbo la Bukene, Nzega, Uyui na Tabora kwa ujumla kukipatia kura Chama cha Mapinduzi. Ni ahadi kubwa ya kutekeleza mradi mkubwa wa kutoa maji Kahama kupita Nzega, Igunga na hatimaye kufika Tabora Mjini. Hii ilikuwa ni ahadi kubwa sana ambayo wananchi wa Tabora waliitilia maanani na kukiamini Chama cha Mapinduzi na kuamua kukipa kura nyingi za kishindo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa rai yangu kwa Wizara, inatakiwa ijue kwamba imebeba jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na imani na Serikali yao. Katika utekelezaji wa mradi huu mkubwa wa maji kutoka Kahama kupitia Bukene ambako utapita Igusule, Mwamala, Itobo, Shigamba na hatimaye itaingia Wilaya ya Nzega Mjini itapita vijiji kadhaa vya Nzega mpaka Uyui na hatimaye kufika Tabora Mjini Wizara ihakikishe kwamba mradi huu unatekelezwa kwa *seriousness* ya hali ya juu. Huu ndiyo mradi mkubwa ambao umefanya maeneo haya yote ambayo mrati utapita, wakiamini Chama cha Mapinduzi. Mradi huu umezungumzwa sana katika Ilani ya CCM, Mheshimiwa Rais katika kampeni alikuja Bukene, akaenda Nzega na kwenda Tabora ameusisitiza sana akasema kwamba hiki ndiyo kitu ambacho anataka aache kama historia. Kwa hiyo, Wizara ya Maji tusimwangushe Rais, tusiiangushe Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tuhakikishe mradi mkubwa wa maji kutoka Kahama kwenda Tabora, kupita Nzega na Igunga ni lazima utekelezwe, kusiwe na ucheleweshwaji, kusiwe na visingizio kwa sababu safari hii wananchi wa Tabora na sehemu zote mradi huu utapita kuanzia Bukene, vijiji nilivyovitaja, Igusule, Mwamala, Itobo, Shigamba wananchi wa Nzega maeneo ya Uyui ambao mradi huu utapita na Tabora Mjini hatutakuwa tayari kusikiliza visingizio. Tumechoka kusikiliza visingizio, watu wanataka maji wayatumie. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nashauri rai yangu kwa Wizara, nakumbuka mwezi uliopita, Naibu Waziri wakati akijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mbunge wa Nzega aliahidi kwamba mwezi wa Kumi hatua ya usanifu ya bomba hili itaanza kufanywa. Kwa hiyo, naomba na ni rai yangu kwa Wizara kwamba hiki kitekelezwe kwa sababu mradi huu wananchi wa Tabora hatutakuwa tayari na *excuse* yoyote. Tunataka utekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie miradi kumi ambayo inatekelezwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Wananchi katika maeneo mengi, Halmashauri nyingi ambako kote miradi hii inatekelezwa wamechoka kusikiliza *story*. Wananchi wamechoka kusikiliza hadithi ya hatua hii, hatua hii na inaonekana kutoka hatua moja kwenda hatua nyingine inachukua muda mrefu sana. Sasa mradi huu katika Jimbo langu unatekelezwa katika vijiji sita. Vijiji vya Igusule, Nawa, Mahene, Buhondo, Ikindwa, Itobo na Sigili na bahati nzuri kati ya vijiji sita hivi vijiji vitano maji yamepatikana. Kwa hiyo, rai yangu kwa Wizara ni kwamba hatua ya pili sasa ya kuanza kutengeneza miundombinu ya kuhakikisha maji yanasambazwa na mantaki ya maji sasa ifanyike na isiwe *story* tena. Ile *speed* ya kutekeleza miradi inaleta maswali mengi sana. Inafanya Wizara ionekane sio *efficient*, Serikali ionekane. Watu wana maswali mengi na hakuna kitu kibaya kama kuahidi kitu halafu ukashindwa kutekeleza. Kwa sababu kama huwezi ni afadhali mapema ijulikane kitu hakiwezekani. Lakini kuahidi halafu baadaye kufuatiwa na visingizio ni jambo ambalo sasa hivi halina nafasi tena. Kwa hiyo, miradi kumi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia katika Halmashauri ya Nzega ifike mwisho, watu waanze kuyatumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ambalo napenda nichangie ni upungufu mkubwa wa mafundi sanifu wa maji katika maeneo mengi hapa nchini. Naishauri Wizara iwe na hatua ya makusudi za kukisaidia Chuo cha Maendeleo na Usimamizi wa Maji kwa kuhakikisha kwamba kinaongezewa uwezo ili kiweze kutoa ma-*graduate* wengi, Wahandisi wa Maji wa kutosha. Kwa sasa hivi naambiwa kwa mwaka chuo hiki kinatoa Wasanifu wa Maji mia moja, lakini mahitaji ni makubwa sana. Kwa mfano, upungufu huu kwa Wilaya ya Nzega nzima haina Msanifu wa Maji hata mmoja. Wilaya nzima ya Nzega kuna Mhandisi mmoja wa maji Bi Mariam Majala ambaye anakimbia huku na huko kuangalia miradi ya maji Wilaya nzima. Huyu mama anajitahidi lakini anazidiwa na miradi mingi.

Kwa hiyo, tuhakikishe wasanifu wa maji wanapatikana wa kutosha. Kwa kuanzia naiomba Wizara ifanye kila inaloweza angalau hawa wasanifu wa maji 100 wanaohitimu mwaka huu angalau watatu au wanne wapelekwe Halmashauri ya Wilaya ya Nzega wamsaidie huyu Mhandisi wa Maji wa Wilaya ili kuweza kutekeleza miradi hii.

Kwa mfano, sasa hivi hii miradi kumi ikitekelezwa, tutakuwa na miradi mingi ambayo sasa tusipokuwa na Msanifu wa maji kama ilivyosasa tuwe tu na Mhandisi aliyepo mmoja, miradi itamzidi, kwa hiyo, atashindwa kui-*manage* na tutakuwa sasa hatuna miradi endelevu. Kwa hiyo, naomba tatizo hili la Wasanifu wa maji liweze kupatiwa ufumbuzi na hasa Wilaya ya Nzega angalau tupate watatu au wanne ili waweze kwenda kuongeza nguvu kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kama nilivyosema mwanzo, namwombea Mheshimiwa Mwandosya aweze kupata nafuu ya haraka, lakini vilevile niikumbushe Wizara kwamba tarehe 12 Januari, 2011, Mheshimiwa Mwandosya alitembelea Jimbo langu na alifika katika Kata ya Igusule na baada ya kujionea tatizo la maji lililoko pale aliahidi kama Waziri kwamba atatupatia kisima kimoja cha maji. Kwa hiyo, hii ni ahadi ya Wizara, napenda iifuatilie kwa sababu wananchi wa Igusule wamenituma nifuatilie utekelezaji wa ahadi ya Waziri ya kutupatia kisima kimoja cha maji katika Kata ya Igusule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingependa kengele ya pili inililie, lakini napenda tu kusisitiza kwamba Wizara ya Maji ijue imebeba jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa na imani na Serikali yao kwa kutekeleza miradi ya maji. Miradi ya maji ni *very sensitive,* miradi ya maji ni kero kubwa kwa wananchi, miradi ya maji watu wanaitumia kupima *efficiency* ya Serikali yao. Kwa hiyo, Wizara ya Maji ijue kwamba imebeba jukumu hilo na miradi ya maji isitekelezwe kwa kimzahamzaha, itekelezwe kwa *serious* ya hali ya juu, kama hakuna fedha ziombwe lakini itekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja, lakini Wizara ifanye kazi yake kutatua shida ya maji.

**MHE. DEUSDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nichukue nafasi hii pia kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Nkasi Kusini kwa kunichagua kuwa Mbunge wao bado nawahakikishia kwamba mimi nitakuwa mwaminifu kwao. Vilevile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulindia uzima na nimtakie kheri Mheshimiwa Mwandosya anayeumwa apone haraka. Vilevile namtamkia Mheshimiwa Silima apone haraka na Mungu airehemu roho ya Marehemu mke wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ilianza rasmi mwaka 1979 na historia ya huduma ya maji, pale kulikuwa na kituo kimoja kinaitwa kituo cha Mfili kilichokuwa kina-*support* kijiji. Leo hii ni miaka 32, bado chanzo hicho ndicho kinachofanya kazi na kwa maana hiyo tuna historia mbaya ya mji wa Namanyere kukosa maji. Jitihada mbalimbali zimefanyika na Halmashauri yetu lakini bado hazijafua dafu. Wameanzisha vioski pale kwa kutumia visima, lakini bado *output* ya maji yanayopatikana Namanyere ni asilimia 16 tu ya mahitaji yanayotakiwa. Tulipata bahati ya kutembelewa na Mheshimiwa Rais tarehe 18 Juni, 2010. Mheshimiwa Rais alisikia kilio cha wananchi wetu wa Nkasi juu ya suala la maji. Akamwagiza Mhandisi aje na apate maelezo. Namshukuru sana Mhandisi yule ni shupavu, alimweleza kinagaubaga Mheshimiwa Rais kwamba sasa hivi jitihada zote tunazozifanya hazijafua dafu na hatujazidisha asilimia 16 ya mahitaji ya wananchi wa Namanyere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa hapa mimi nimezungumza kwenye maswali ya nyongeza juu ya shida tunayoipata na nikiwa naeleza kwamba tunawasindikiza wake zetu saa tisa usiku kwenda kuchota maji. Hali siyo shwari, hali ni taabu, hali haielezeki Namanyere. Mheshimiwa Rais aliagiza akasema wewe Mhandisi kaa na wenzako uongeze *output* ya maji hapa ifike angalau mara mbili ya kiasi kinachopatikana sasa. Jambo ambalo amelifanya, kazi hiyo imefanyika na kwa kupanua chanzo cha Mpili na gharama ya fedha inayotakiwa ni zaidi ya Shilingi bilioni 1.3.

Leo Waziri amekuja mikono mitupu bila kutaja kitu chochote katika Wilaya ya Nkasi na Mji wa Namanyere. Hii ni aibu kubwa na sijui tutarudi namna gani. Lakini inastaajabisha zaidi jinsi

Wizara inavyotaka Watanzania waamini kwamba kuna hela nyingi sana zimetengwa kwa ajili ya maji Wilayani Nkasi kwa kutaja bwawa la Kawa. Bwawa moja la Kawa lipo ukurasa wa 158, lilitengewa na limetumia zaidi ya shilingi bilioni 1,062, liko Jimboni kwangu. Kijiji cha jirani cha Nkundi hakina habari, kijiji cha jirani cha Kalundi hakina habari. Hivi ndivyo wanapata habari kutoka kwa Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Fyekengelezya nacho ni Kijiji ambacho kiko Sumbawanga, nao nadhani hawana habari. Lakini, yote hii ni ujanja wa watu wa Wizara. Tuna watumishi wa namna gani hawa? Nasikia yupo mama mmoja hapa anaitwa Mama Rweyemamu - Mkurugenzi wa Maji Vijijini, amefunga safari mara tatu kwenda Sumbawanga, kushawishi Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi na wadau wengine, wakubali kwamba mradi huu haukwenda kwa *maneuver*, ulikwenda kwa utaratibu wa Kiserikali. Siyo kweli! Mwenyekiti wa Halmashauri katika kikao kilichowakutanisha wadau alibaki peke yake. Watu wote ni watumishi wa Serikali wakamgeuka. Sasa, huu siyo utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa, kama Wizara inataka tuelewane, mimi nilikuja kwa nguvu za umma, nguvu za wananchi, wahakikishe kwamba Vijiji vinavyotajwa kwenye mradi huu sasa vinapata maji Nkundi wapate maji, Kalundi wapate maji, Fyekengelezya wapate maji, na wasitake Wilaya ya Nkasi ndiyo itafute hela za kupeleka maji hapo, hatutaelewana. Tutafikisha kilio hiki mpaka kwa Mheshimiwa Jakaya Kikwete, namfahamu ni shupavu, lazima atachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini mambo yaende kienyejienyeji katika hali ngumu kama ile? Ni udhulumati wa hali ya juu. Mheshimiwa Nyami alikuwa Mbunge na ameadhibiwa kwa kukosa kura kwa sababu ya mambo kama haya. Alishauri kwamba mradi huu uelekezwe kwenye Vijiji vinavyohusika, lakini bado ushauri wake haukufuatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nakubali *PPP*, wala sina tatizo nayo, lakini mpaka mradi unatekelezwa asilimia 95, Kijiji hakijui. Maana yake nini? Alipokuja Mheshimiwa Keissy akaingia kwenye *PAC* ndiyo mambo yakaanza kujulikana julikana na watu kufunga safari mbili mbili kwenda Sumbawanga kushawishi watu. Siyo utaratibu hata Kidogo! Naomba Wizara walichukulie hili jambo *serious*, wahakikishe kwamba hela zinapatikana, Vijiji vinavyohusika vipate maji. Hiyo ndiyo rai yangu mimi. Vinginevyo, ni mapambano tu! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshmiwa Rais alipotembelea Wilaya yetu, pamoja na kutoa maagizo yale, Waziri wake ametuacha mikono mitupu. Kwenye bajeti hii inayofuata tu baada ya Mheshimiwa Rais, ametuacha mikono mitupu, hakuna kitu. Wananchi pale Namanyere kuna sekondari tatu, kuna Chuo cha Manesi, kuna Hospitali ya Wilaya moja, kuna Shule za Msingi saba, kuna watu waliotengeneza *population* pale zaidi ya 12,000. Lakini, hawana maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 16 ndiyo *output* ya maji ya Namanyere. Hebu angalieni hali hiyo. Tugawane jamani raslimali za nchi kwa usawa. Hii hali haivumiliki, tuleteeni maji tena mwaka huu huu. Tutarudia wapi? Au tupeni mbinu tukajifiche wapi sisi? Tuko Wabunge wawili sasa, tutakwenda kujificha wapi Namanyere? Haielezeki! Lazima mwezi wa Tisa huu, watu sasa hivi ni kusindikizana, mtu na mke wake na mkuki, wanakwenda kutafuta maji kwenye mbuga huko! Utaratibu gani? Magonjwa hayaishi sasa, watumishi wanatukimbia. Watakaaje katika hali hii? Halafu tuko pembezoni. Kumbe ukiwa pembezoni hufikiriwi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali kabisa itusikilize. Naamini wadau wanasikiliza kwa masikio mawili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhangaika, Wilaya ya Nkasi na Halmashauri ilifanya jitihada kubwa ya kubaini vyanzo mbalimbali vya maji. Wakajaribu kutafuta chanzo cha Zuma, chanzo hiki kiko katika Milima ya Kate kwenye Jimbo langu. Ni kwamba, katika chanzo kile kama tungepata maji, yangeweza kupatikana kwa *gravity* mpaka Namanyere na kuhudumia Vijiji zaidi ya kumi njiani, Kijiji cha Kate, Kijiji cha Ntalamila, Kijiji cha Chonga, Chenje, Kitosi, Ifundwa, Ntuechi, Isale, Msilihofu, Ntemba na Nkata, bila kuacha Ntalamila. Lakini sasa mradi ule wa Halmashauri, tena wakati ule nakumbuka nilikuwa Mwenyekiti wa Halmashauri mwaka 2002, mradi ule

ungeweza kugharimu Shilingi bilioni 2.2. Tukatoa Shilingi milioni tano kwa ajili ya kutafuta Wahandisi waweze kufanya usanifu. Lakini mpaka hivi tunavyosema, andiko liko Wizarani, hakuna anayelifanyia kazi. Tunakumbushia mara kwa mara lakini hakuna chochote.

Mheshimiwa mwenyekiti, Mheshimiwa Mwandosya aliweza kuja kwenye Wilaya yetu, akatuambia juu ya umuhimu wa kupeleka maandiko. Tukamwambia andiko liko huko huko, lakini mpaka sasa hatujaona kitu chochote. Naomba mtusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi hii ya Benki ya Dunia, nayo ni vichekesho kama wenzangu wanavyosema. Kwetu sisi ndiyo tumetengewa Shilingi milioni 600. Hebu fikiria, Shilingi milioni 699 wakati mradi ule uliopita wa kwanza ulikuwa Sh. 1,092,000,000/=, hauna matunda yoyote na wala hauna tija. Lakini Wilaya nzima sasa ni Shilingi milioni 600. Bado hautaweza kuleta maji katika Vijiji vyote. Nilikuwa nafanya mawasiliano na Mhandisi wangu leo akasema kwamba pesa hizo zinatosha kuchimba visima bila kusogeza maji kwa mtu yeyote. Lakini, ni Kijiji kimoja tu cha Mkinga ambacho kiko kwa mwenzangu ndicho kinaweza kupata maji. Kwa maana hiyo, Kijiji cha Mpasa, Kijiji cha Kisula, Kijiji cha King'ombe, Isale, Chala, watabaki bila maji, watabaki wanayaona tu bila kusambazwa. Sasa hali ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule mwambao mwa Ziwa Tanganyika kote hakuna maji. Wambembe pale palikuwa na *gravity* nzuri, lakini pesa hakuna, hata ukienda kwenye bajeti hakuna! Nikienda, nitaulizwa, sina la kujibu. Bora hata wanasikia kwamba nalisemea. Hali ni ngumu na kipindupindu ni lazima kwetu. Tunapata kipindupindu kila wakati. Tunafikiria bora hata yale maporomoko ya Kalambo yangekuwa imara yale mkayawekea umeme, halafu tukapata maji kama vile wenzetu wa hapa katikati walivyopata maji kutoka Ziwa Victoria. Kule mwambao kote tungeweza kupata maji pengine mpaka Mpanda kama ingewezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hali ni mbaya. Naiomba Wizara, kwa masikitiko makubwa, waje na jibu zuri kuhusu maji Namanyere, waje na jibu zuri kuhusu maji Chala. Nimeona katika mpango wa baadaye sana ndiyo wanataja Chala, Namanyere, Laela na Mpanda. Kuna mpango wa kufikisha maji, uko katika hatua ya kutafuta watalaam wahandisi. Sasa ni lini? Chala ni mji unaokua kwa haraka sana, sasa bila maji ni taabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Wizara na ninamwomba Waziri anayehusika ahakikishe kwamba kuna tamko linalohusu suala la maji Namanyere na kwenye mradi wa Zuma, Kate. Kama haiwezekani, basi wekeni katika mipango ya hivi karibuni ituletee tija. Hatuna chochote! Nimeona kwenye randama kuna watu wengi tu wana mabwawa mengi, wengine bilioni 10. Nimeona! Sisi ndiyo hatuna watu kule? Sisi ndiyo waaminifu kwa Chama cha Mapinduzi kilichounda Serikali hii hapa. Waaminifu kweli kweli, wanatuacha, wanatukacha, hawa watu hawa! Hapana! Fikirieni vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jakaya Kikwete, tusikilizeni! Wanawaangusheni! Wanakuangushia nchi yako Mheshimiwa Rais. Waaminifu tumebaki ni sisi wa Vijijini! Sasa mtupatie huduma. Kama hatuwezi kupata huduma, watu watageuka, tabia itajenga watu hovyo. Tunalilia huduma, mnatudanganya danganya kila siku, mwisho watu watasema kweli na sisi tuwe kama watu wa Kaskazini. Kaskazini, wala hawaungi Chama cha Mapinduzi mkono na wanapata huduma, lami mpaka mlangoni. Huu utaratibu gani? Tugawane! Kwa usawa, nchi moja, lakini tugawane *resources* za Taifa kwa usawa na suala la maji liwe ni muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naamini ujumbe umefika. Suala la maji Namanyere ni kizungumkuti, hakuna amani. Watu tunakwenda kusindikiza wake zetu, tukirudi, hatutalala usingizi, hakuna amani, watu wanapigana na shule hazisomeki. Baada ya kusema hayo, nashukuru. Kama zipo dakika mbili zimebaki, zibaki kwa ajili ya wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kunisaidia muda. Sasa nitamwita Mheshimiwa Selemani Bungara na baadaye Mheshimiwa Tambwe ajiandae.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye amewapa akili watu wa CCM na watu wa CUF na watu wa CHADEMA, kwa sababu ni Mwenyezi Mungu ambaye anatoa haki sawa kwa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Na hawa wa vyama vingine, Mwenyezi Mungu hawapi chochote?

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Unasema! Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza wanachama wote wa CCM, wa *CUF*, wa CHADEMA, wa *TLP* ambao walinipigia kura siku ya uchaguzi. Nawapongeza sana. Pia nawapongza sana wapigakura wote wa Jimbo la Kilwa Kusini kwa kutambua kwamba mimi naweza kuwatetea watu wa Jimbo la Kilwa Kusini. Pia nampongeza sana na namshukuru sana Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, nampongeza sana kwa sababu wakati nikichangia Wizara ya Kilimo, nilikuwa naongea sana habari za ufuta na yeye akasema mimi nina maslahi binafsi katika zao la ufuta. Nampongeza kwa kuwa mimi sina maslahi binafsi katika zao la ufuta, isipokuwa nilikuwa nawatetea wapigakura wangu, na *inshallah* kwa kuwatetea kwangu wamepata bei nzuri ya ufuta. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Stella Manyanya. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana wagombea wote wa Jimbo la Kilwa Kusini, wagombea wa CHADEMA, *NRA* na Mgombea wa CCM - Mheshimiwa Ramadhan Madabiba, nampongeza sana na namshukuru. Pamoja na ana elimu kubwa, ni tajiri, lakini aliangushwa na mtu wa Darasa la Saba ambaye siyo tajiri. Namshukuru sana. Lakini, ninachomwomba Mheshimiwa Madabida akubali kushindwa. Asiyekubali kushindwa si mshindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudi katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa nne. Maelezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kifungu cha 8(i) kinasema: “Upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya Vijijini umeongezeka kutoka asilimia 53.7 mpaka asilimia 57.8”. Nawashukuru sana CCM kwa kusema maneno ya ukweli katika Bunge hili. Angalau Wabunge wa CCM wanasema kwamba *data* hizi ni za uongo. Mimi nasema siyo za uongo, ni za ukweli kabisa. Nawashukuru sana! Lakini, wanaosikiliza wanajua kwamba haya maneno yaliyotolewa katika hotuba hii ni kweli au uwongo! Wanaosikiliza wanajua! Lakini mimi naamini kwamba CCM kweli wametimiza asilimia 57.8 katika Vijiji. Lakini, siyo Kilwa! Lakini siyo Kilwa! Pengine katika Majimbo ya CCM mmepata asilimia hiyo, lakini Majimbo ya Kilwa ahahaaa, Kilwa hawajapata asilimia 57.8.

**MBUNGE FULANI:** Maji!

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji *yes.* Maji! Sisi Kilwa tuna matatizo ya maji, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa. Pengine hata asilimia 10 hatujapata. Lakini, tunashangaa leo Mheshimiwa Waziri kutuambia kwamba Vijijini watu wamepata asilimia 57.8. Inasikitisha sana! Namwomba Mheshimiwa Waziri aje Kilwa kututhibitishia kwamba kweli tumepata asilimia 57.8 katika mpango wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha miaka 50 ya uhuru wa Tanzania, tunaomba kura kwa wapigakura wetu kwa kuomba, “tuchagueni ili tukupeni maji.” Miaka 50 ya uhuru wa CCM! Lakini, mimi najua...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara, miaka 50 ya uhuru wa Tanganyika!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Wa Tanganyika, *inshallah*!

**MWENYEKITI:** Siyo wa CCM!

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Haya, miaka 50 ya uhuru wa Tanganyika, tunakwenda katika Majimbo kuwadanganya Watanzania kwamba tuchagueni ili tukuleteeni maji. Uzuri zaidi,

mnaandika katika vitabu kabisa kwamba asilimia 57 watu wa Vijiji wamepata maji. Ni vizuri zaidi ili waonekane kwamba CCM siyo wakweli. Serikali ya CCM siyo wakweli, inawaongopea Watanzania. Lakini, ninachojua mimi, sisi Wabunge na viongozi wakubwa hamna matatizo, maji ya kunywa safi, tena maji safi na salama mnakunywa, mnaweza kunywa, mnaweza mkaoga, mnaweza mkafulia, wala hamna matatizo. Lakini, Waheshimiwa Watanzania tunapata taabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa Masoko kuna Vitongoji saba. Vitongoji vyote vina matatizo ya maji. Lakini, kuna mradi katika Kijiji cha Mpala ambao ulikuwa unasimamiwa na *FINWATER*. Wamechimba visima vitatu mwaka 1979, mpaka leo maji yale hayajafika Kilwa Masoko, kilomita 12. Visima vitatu virefu na kila kisima kinatoa lita 4,500 kwa saa. Tenki limejengwa na *FINWATER* mwaka 1979 lenye uwezo wa kuingiza maji lita 450,000.

Tatizo, kutoa mabomba kutoka Mpala kufika Kilwa Masoko Wilayani. Tatizo, miaka sasa hivi inafika, 1979 mpaka leo 2011, miaka 30! Inashindwa Serikali ya CCM! Msaada wa *FINWATER*, watu wa *Finland* wamesaidia, wamechimba, wameweka matenki, kila kitu kipo, lakini Serikali ya CCM inashindwa kupeleka mabomba kilomita 12. Lakini, wametoa maji Mwanza mpaka Shinyanga. Sisi watu wa Kusini tumekosa nini? Sisi watu wa Kusini tumekosa nini Waheshimiwa? Tukienda katika mrabaha wa Songo Songo, gesi ya Songo Songo, tunaambiwa ngojeni kwanza, kesho kutwa. Sisi tumekosa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali ya CCM itukumbuke watu wa Kusini na sisi watu wa Kusini ni chanzo cha uhuru katika nchi hii. Tumemwaga damu mwaka 1905 katika Vita vya Maji Maji kwa sababu ya kuikomboa nchi hii. Tunaomba Serikali ya CCM watuheshimu watu wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilwa Kivinje kuna Hospitali ya Wilaya, tumepewa msaada na Serikali ya Uingereza. Maji hakuna Hospitali ya Wilaya! Miaka 50 ya Serikali ya CCM inashindwa kuleta maji katika Hospitali ya Wilaya! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamwomba Waziri aje Kilwa, aje kuona Hospitali ya Wilaya. Tena Wazungu, Waingereza wametengeneza ile hospitali mwaka 1963, safi kabisa, vyoo vya kuvuta. Vyoo vya kuvuta, maji hakuna. Mnasemaje? Vyoo vya kuvuta, maji hakuna! Ndiyo Hospitali ya Wilaya hiyo! Ndiyo kuna Mganga Mkuu wa Wilaya, kuna Afisa Afya wa Wilaya, maji hakuna! Vyoo vya kuvuta! Tunamwomba Waziri, aje Kilwa. Kama hakuja Kilwa kuongea na watu wa Kilwa, mimi siungi mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

Kilwa Kivinje Mji Mkongwe mpaka sasa hivi ukitaka kupata maji dumu moja linauzwa Sh. 500/=, *hehee*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, dumu moja Sh. 500/=, siku moja inabidi upate madumu kumi Sh. 5,000/=. Sh. 5,000/= mara 30 ni Sh. 150,000/= kwa mwezi. Masikini Mtanzania atapata wapi laki moja na nusu ili anywe maji safi na salama? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Pande maji hakuna. Hoteli tatu maji hakuna. Nanjilinji kwa Mwenyekiti wa Mkoa wa CCM, maji hakuna. Tunakuja hapa tunadanganyana kwamba asilimia 57.8 vijiji maji safi! Hii ni dalili ya unafiki. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni dalili ya unafiki. Dalili ya mtu mnafiki zipo tatu. Mtu akisema anasema uwongo; akiahidi, hatimizi; na akipewa amana, hafikishi. Sifa zote tatu hizi Serikali iliyopo madarakani inazo! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, CCM wakisema, hawatimizi; wakipewa amana, hawafikishi, wanakula chakula njiani. Tunawaomba Watanzania, tunaiomba CCM kama hamkujirekebisha mwaka 2015 nchi tunaichukua*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uwongo umekwisha! Mtawala yeyote ambaye anategemea kuishi au kutawala kwa kutumia uwongo ajue wakati wake naye umekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Vyama vyote vya Upinzani tuungane. Bila kuungana hatuitoi CCM. Tunataka mwaka 2015 upande huu wote wawatakuwa wapinzani watupu! Wananchi wasioelewa CCM, ni longo longo! Waarabu wanasema, 'mandhala banafsi yarabuk,' yaani anayejipiga halii. CCM msilie mnajipiga wenyewe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, namwomba Waziri aje Kilwa aonane na mimi Mbunge, jina langu ni Suleiman Said Bungara maarufu kwa jina la Bwege. Kama hujanithibitishia kuja Kilwa na ukatatua kero za maji Kilwa, sitaunga mkono hoja hii. Najua mtashinda kwa kura nyingi, lakini mimi nitapinga. *(Kicheko)*

*(Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bungara, muda wako umekwisha.

**MHE. SULEIMAN SAID BUNGARA:** *Inshallah!*

**MWENYEKITI:** Jina lingine umesema unaitwa nani?
**MHE. SULEIMAN SAID BUNGARA:** Bwege. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya ahsante! *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hiyo ndiyo raha ya ndani ya Jumba hili. Unapata michango ya aina tofauti na ndiyo raha ya demokrasia iliyojengwa na CCM. Tunaendelea. Namwita Mheshimiwa Tambwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Ruhwanya.

Mheshimiwa Tambwe kwanza.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza hotuba iliyotolewa na Wizara hii pamoja na watalaam wote, lakini vile vile namwombea Waziri Mwandosya Mwenyezi Mungu amsaidie aweze kupona haraka aweze kuungana na sisi katika kuendeleza nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwenye pointi. Kwanza kabisa naomba nitoe shukrani zangu kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kutupa ahadi za kupata maji ndani ya Mkoa wa Tabora huku akijua kabisa kwamba Mkoa wa Tabora tunalo tatizo la maji. Mheshimiwa Rais alikuja Tabora mwaka Februari, 2009 kwenye Sikukuu ya Wanawake Duniani. Alituahidi kupata maji ya muda mrefu na maji ya muda mfupi. Kutatua tatizo kwa muda mrefu ambalo litatatua tatizo la maji kabisa ndani ya Mkoa wa Tabora, lakini kutatua kwa muda mfupi ili kuhakikisha wananchi hawa angalau waanze kupata maji, nampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nirudi kwa Waziri Mwandosya mara tu baada ya kuteuliwa, alifanya ziara ndani ya Mkoa wa Tabora, alitembea Wilaya zote akaona matatizo makubwa tuliyonayo ya maji. Aliahidi kutusaidia, lakini pia aliahidi kutekeleza ahadi za Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeze pia Injinia wa Maji Mkoani Tabora, Ndugu Bwire, ni Injinia Kijana mchapakazi anafanya kazi vizuri. Mkoa wa Tabora tuna tatizo kubwa sana la maji, tuliahidiwa kupata maji ya Ziwa Victoria lakini mpaka sasa hatujui hizi ahadi za Rais zimefikia wapi kwa sababu hatuoni chochote kinachoendelea. Wananchi wa Tabora wanataka waelewe sasa kwamba Serikali imefikia wapi. Jambo la kushangaza, leo wakati nafuatilia hotuba ya Waziri wa Maji iliyosomwa na Waziri Wassira amesema kwamba mwaka 2011/2013 wataanza upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napinga kabisa kufanya upembuzi yakinifu miaka mitatu, kwa sababu hali yetu ni mbaya sana kuhusu suala la maji. Haiwezekani! Ahadi hii alianza kuitoa Waziri Mkuu Mstaafu, mwaka 2008 Mheshimiwa Edward Lowassa, leo tupo mwaka 2011, unatuambia mpaka mwaka 2013 ndiyo utakamilika upembuzi yakinifu, kwa kweli kitu hiki hakikubaliki. Wananchi wa Tabora hawakubaliani kabisa na kitu hiki!

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai. Wanawake wa Tabora wanasumbuka sana na maji. Hatulali, tunaamka saa kumi usiku kwenda kutafuta maji, lakini leo Serikali yetu bila huruma inatuambia mwaka 2013 ndiyo itamaliza upembuzi yakinifu. Kwa kweli tunapinga, suala hili tunaomba watufikirie, shida ya maji ni kubwa sana ndani ya Mkoa wa Tabora. Wananchi wa Tabora wamechoka kuahidiwa, wamechoka kuambiwa upembuzi yakinifu, wanachotaka kujua ni kwamba ujenzi unaanza lini ili maji yafike Mkoani Tabora na siyo mwaka 2013/2014. Hilo suala hatulikubali kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba kabisa Waziri atakapokuja ku-*wind up* atupunguzie hiyo miaka, toka mwaka 2008 mmeanza kutuahidi, tumesubiri mwaka 2008, mwaka 2009, mwaka 2010, mwaka 2011 tuendelee kusubiri mpaka mwaka 2014! Kwa kweli huu siyo ubinadamu wala siyo uungwana, wala siyo utendaji!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni ahadi za kumuahidi mtoto mdogo, huwezi kumuahidi mtu kwa miaka saba. Naiomba sana Serikali ibadilishe hii ahadi yake ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilimwuliza Waziri wa Maji kwamba ana mpango gani au mkakati gani wa kutuletea maji ya Ziwa Victoria katika Mkoa wa Tabora kupitia Nzega, Igunga na Tabora Manispaa, alinijibu kwamba mpango upo tayari, watatimiza wanafuatilia siyo muda mrefu. Siyo muda mrefu, 2014! kwa kweli hiki kitu mimi binafsi sikikubali kabisa! Abadilishe uamuzi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie kwenye mradi wa kuendeleza Sekta ya Maji. Kuna mradi unaitwa *(WSDP) Water Sector Development Programme*, Serikali imetuletea mtalaam wa kufanya upembuzi yakinifu, mtalaam amefanya akapita kila sehemu kwenye vyanzo vyetu vya maji. Amefanya Tabora Manispaa, amefanya Urambo, amefanya Sikonge. Mtalaam huyu akasema Tabora Manispaa tunahitaji Shilingi bilioni 45, Sikonge wanahitaji Shilingi bilioni 14 lakini Urambo pia wanahitaji Shilingi bilioni 18.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza, nimepitia vitabu hivi kwenye randama, Tabora Manispaa inaonekana tumetengewa Shilingi bilioni 4.2 kwenye vitu vyote vya Shilingi bilioni 45. Kwa kweli hiki kitu sijui nikiitaje! Sijui nikisema usanii nitafanya vibaya, lakini kwa kweli Shilingi bilioni nne ndani ya Shilingi bilioni 45, hatuwezi kufanya chochote kile kikazaa matunda mazuri kwa wananchi wa Tabora wakaondokana na adha hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuwa ni adha kubwa ninapofanya ziara kama mimi ni mama, akina mama wote wanakuuliza habari za maji, ukienda Wilaya zote unaulizwa habari za maji, unasema Serikali inashughulikia, lakini leo tunaambiwa mpaka mwaka 2013/2014, kwa kweli hiki kitu hakiwezekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia randama, utakuta tumetengewa Shilingi bilioni saba lakini wamechanganya Tabora na Morogoro Shilingi bilioni saba. Nitaomba ufafanuzi wakati Waziri ana *wind-up,* nini maana ya kutuwekea Shilingi bilioni saba Tabora na Morogoro? Lakini vile vile atupe ufafanuzi, kwanini Urambo kwa Mzee wangu Sitta na Sikonge hakututengea fedha za maji ambazo zimefanywa na mtalaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtalaam huyu amelipwa fedha za walipa kodi wa Tanzania, amefanya kazi, amepeleka vitabu Wizarani halafu matokeo yake vitabu vinatupwa, pesa ameshalipwa, hakuna chochote kinachoendelea. Hii inakuwa ni mipango au ni kitu gani? Unapomleta yule mtalaam afanye kazi, wakati unajua huna kazi, una maana gani? Nitaomba kupata majibu ya Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee sasa mpango wa maji wa muda mfupi wa Tabora Manispaa. Tabora Manispaa tuna bwawa la Igombe ambalo lilichimbwa na Mkoloni, tuna Bwawa la Kazima lilichimbwa na Mkoloni, bwawa la Kazima, limekauka maji tunatumia bwawa la Igombe ambalo limemaliza muda wake sasa. Mabwawa wataalamu wanasema yanakuwa na umri labda wa miaka 40 isizidi. Sisi umri wa bwawa letu la Igombe unakaribia miaka sitini. Mtalaam mshauri amekuja amefanya upembuzi wake akasema, Tabora Mjini pana maji, sasa tunapata ujazo wa maji mita 15,000, tunatakiwa tupate ujazo wa maji mita 30,000, akasema tutenge Shilingi bilioni kumi kwa ajili ya bomba kubwa litatoa maji kwenye bwawa la Igombe kuleta Mjini. Tutenge Shilingi bilioni kumi kwa ajili ya kurekebisha mitambo, umeme, chujio kubwa na kadhalika. Lakini Serikali hii imetutengea Shilingi bilioni 4.2 kwa maana kwamba hakuna mradi hata wa muda mfupi utakaowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi wananchi wa Tabora tutaendelea kupata shida ya maji daima, na tumekuwa *royal* kweli sisi wananchi wa Tabora kwa Chama cha Mapinduzi. Hata Igunga tunawahakikishia itarudi ndani ya Chama cha Mapinduzi lakini Serikali hii ituangalie. Serikali hii itambue hilo jambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kinauma sana. Hali ya maji Tabora ni mbaya sana. Hivyo, tunaomba fedha tuweze kufanya hata mradi wa muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Magereza yetu ya Uyui tulikuwa tunapata maji kwenye bwawa la Kazima, nadhani Waziri anatambua. Maji ya Kazima yamekauka, kwa hiyo, maji hayaendi tena kule rada, Kata ya Mtendeni ambako kuna gereza kuu, maji hayaendi Ipuli, na hayaendi Isevya. Yanaenda kwa shida sana kwa sababu bwawa limekauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo masikitiko makubwa kusema kwamba gereza kubwa la Uyui maji yanapelekwa kwa *water bozer* (kwa gari). Ofisi zetu unazifahamu, siku nyingine utaambiwa gari halina mafuta, siku nyingine utaambiwa dereva anaumwa, siku nyingine utaambiwa gari bovu, Wafungwa wanakaa zaidi ya siku mbili hawajapata maji. Huu ni ukiukwaji wa haki za binadamu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii iangalie vizuri, mle ndani kuna Wafungwa lakini pia kuna mahabusu ambao hawajahukumiwa na wengine hawana makosa na wengine wamesingiziwa. Kuna watu walifungwa na wakatoka jela bila kuwa na makosa: Je, huyu ambaye yupo rumande anakosa maji ya kutumia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali za Magereza zinajulikana, maji yanapokosekana mle ndani hali yake inakuwaje? Hebu tu-*imagine*! Bwawa limekauka tufanyeje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri kwa kweli atueleze utatuzi wa maji kwenye Wilaya, Tabora Manispaa na Mkoa mzima wa Tabora. Tulikuwa na mradi pia wa kubadilisha mabomba ya maji katikati ya Mji wa Tabora kwenye Kata za Chemchem, Gongoni, Tambuka Reli, Mbugani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabomba yetu yaliwekwa wakati wa mkoloni mpaka leo mabomba haya hayajabadilishwa, upitishaji wa maji umekuwa ni shida kweli! Lakini kwa bahati nzuri, naishukuru sana Serikali ya Uswis, imesema itatupatia fedha Shilingi bilioni nane kwa ajili ya kubadilisha mabomba ya katikati ya Mji. Naishukuru sana. Serikali hii pia imesema itatupatia mita za kisasa 5,000, naishukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna suala la kuongeza mtandao wa maji. Tabora inakua, Manispaa ya Tabora inakua, tunaendelea kujenga, kuna sehemu hakuna mtandao wa maji. Kwa hiyo, tunaomba fedha kwa ajili pia ya kuongeza mtandao wa maji. Katika hizo fedha, Shilingi bilioni 45 tumepewa Shilingi bilioni nne tu na laki mbili. Ninaiomba Serikali iangalie vizuri sana suala hili.

*(Hapa kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge kengele ya pili hiyo.

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Haa! Ni ya kwanza Mheshimiwa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Ni ya pili hiyo!

**MHE. MUNDE A. TAMBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini nataka Waziri aki-*wind-up* aniambie habari hizi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tambwe. Nitamwita Mheshimiwa Ruhwanya na baadaye muda ukiniruhusu nitamtaja mwingine.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia. Napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili na mimi niweze kutoa mchango wangu ukizingatia mimi ni mdau mkubwa wa Wizara hii. Mwaka 2008 mpaka 2010 nilikuwa Waziri Kivuli wa Maji, nilipata ushirikiano mkubwa sana kutoka kwa Mheshimiwa Mark Mwandosya. Namwombea kwa Mwenyezi Mungu amrejeshe salama lakini vile vile naomba asiache kumpa ushirikiano wa kutosha ambaye amechukua nafasi hii ya Uwaziri Kivuli Mheshimiwa Kiwia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa nianze kuchangia moja kwa moja. Maji ni uhai, asilimia 79 ya miili yetu sisi wanadamu tunategemea maji, lakini vile vile sayari yetu ya dunia, asilimia 75 imezungukwa na maji. Tanzania tumepata bahati kubwa sana kwamba tumezungukwa na maji ambayo ni safi na ambayo ni salama yanayoweza kutumika kwa ajili ya kilimo, kwa ajili ya binadamu na kwa ajili ya wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kaskazini, tunalo Ziwa Viktoria, upande wa Magharibi tunalo Ziwa Tanganyika, upande wa Kusini tunalo Ziwa Nyasa, lakini Mashariki pia tunayo Bahari ya Hindi, tusisahau vile vile maziwa yetu madogo madogo ambayo ni Ziwa Rukwa, Ziwa Eyasi, Ziwa Natron na Ziwa Manyara. Tunayo mabwawa ya asili na mabwawa ya kutengeneza lakini pia tunayo mito mingi. Nitasema kwa nini ninataja vitu vyote hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mto Malagarasi, Mto Kagera, Mto Mara, Mto Ruvuma, Mto Ruaha, Mto Ruhuhu, Mto Wami, Mto Ruvu, mto Mara, mto Pangani, vyanzo vyote hivi vya maji vinafaa kabisa kutumiwa na binadamu lakini kwa Tanzania maji bado ni tatizo sugu, sijui ni kwa nini.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya maji bado ni ghali na ni ngumu kupatikana kwa Mtanzania. Naiomba Serikali ihakikishe kwamba wananchi tunapata maji yaliyo safi na salama ili *water born diseases* isiendelee kutuumiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya dunia inaonyesha kwamba watoto chini ya miaka 16 kila baada ya sekunde nane mtoto mmoja anafariki dunia kutokana na matatizo yanayotokana na kukosa maji safi na salama na hii ni kwa dunia nzima. Lakini Barani Afrika tunaongoza na Tanzania tukiwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida, mtu mmoja anatumia takribani *cubic meter* 2,700 za maji kwa mwaka, lakini kulingana na ongezeko la watu, *cubic meter* hizo zinaendelea kupungua kwa sababu tunazidi kuongezeka. Pamoja na hilo, tatizo lingine lililopo ni la mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha upungu mkubwa wa maji. Ni wajibu wa Serikali kuwaelimisha Watanzania kuhusiana na hali hiyo ili waweze kutunza mazingira na wasiwe wanachafua maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba kuna juhudi mbalimbali za Serikali kuhakikisha kwamba mazingira yetu yanakua vizuri, kunakuwa na kampeni mbalimbali za

upandaji miti, lakini tafiti huwa hazifanyiki vizuri, miti mingine inayopandwa inaharibu vyanzo vya maji, kwa mfano mikaratusi inanyonya maji, kwa hiyo, siyo kwamba kila mti unaopandwa unafaa kwa ajili ya kutunza mazingira, unafaa. Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa kina uwe unafanyika kabla miti haijapandwa na wananchi waelimishwe kuacha kulima karibu na vyanzo vya maji na waache kunywesha wanyama karibu na vyanzo vya maji na wenye viwanda waache kuchafua maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta zote zinategemea maji. Huwezi kuendesha viwanda bila kuwa na maji, huwezi kufanya kilimo bila kuwa na maji, huwezi kuwa na ujenzi bila maji, huwezi kujenga mahoteli bila maji, huwezi kuwa na nyumba usitumie maji, maji vile yanatumika katika ufugaji. Maji ni kichocheo kikubwa sana cha uchumi wa wananchi. Kwa hiyo, tunaomba maji kwa kuwa maji ni uhai na maji ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie kidogo kuhusu maji vijijini. Kwenye malengo ya MKUKUTA ilionyeshwa kwamba ikifika mwaka 2009/2010 wananchi wanaoishi vijijini asilimia 65 watakuwa wamepata maji safi na salama. Lakini ilisemekana pia kwamba wananchi wa vijijini watapata maji ndani ya dakika 30 tu. Kwa hiyo, watapata muda vile vile wa kufanya kazi nyingine za uzalishaji. Lakini bado hali ni duni, maji yanayopatikana vijijini ni machafu, mengine yanaonekana kabisa kama tope, hata kunawa hunawi, lakini wananchi wanakunywa, wananchi wanatumia maji hayo kila siku pamoja na wanyama wao. Hili suala kwa kweli liangaliwe.

Akina mama wanatumia muda mwingi sana kutafuta maji, mama anatumia zaidi ya masaa sita kutafuta maji, hawezi kufanya kazi nyingine za uzalishaji mali. Kwa hiyo, tuangalie hilo bado ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika kitabu cha hali ya umaskini cha mwaka 2010, mwaka 2009 ilisemekana kwamba, naomba kunukuu: „wanavijiji ambao walipata huduma ya maji mwaka 2009 walikuwa 19,685,659 sawa na asilimia 57.8. Lakini mwaka 2010 walifika 20,545,945 sawa asilimia 58.7." Hili ni ongezeko la asilimia 0.9 tu. Ni ongezeko dogo mno maana yake ni kwamba hata yale malengo yaliyowekwa na MKUKUTA hayakufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ambao unaonyesha kabisa malengo ya MKUKUTA hayakufikiwa ni kwa upande wa Mkoa wa Shinyanga. Vijijini asilimia 39 tu ndio wanapata maji safi na salama. Mjini angalau wamefikia asilimia 60. Kwetu Kigoma vijijini angalau tumefikia asilimia 53, lakini bado hali ni duni, Serikali inatakiwa i-*pool up socks.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, Serikali imekuwa ina tabia ya kutegemea sana Wahisani katika miradi mbalimbali ya maji. Vile vile yapo malalamiko kutoka kwa Wakurugenzi/Watendaji mbalimbali wa Halmashauri, wanasema kwamba miradi hii ya *World Bank* imekuwa na *bureaucracy* sana. Yaani kupata *no objection* ili mradi uweze kuendelea inachukua muda mrefu. Kwa hiyo, unakuta miradi mingi inahadithiwa tu miradi ya vijiji 10, lakini haikamiliki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mwingine ni Mkoa wa Rukwa, hawakupata Shilingi milioni 195 ambazo zilikuwa zimetengwa kwa ajili ya mradi wa maji katika vijiji vyao na hii ni kwa sababu wahisani hawakutoa fedha. Tuache kutegemea wahisani. Nimesikitika sana kwamba katika mwaka huu, bajeti ya maendeleo Sh. 41,565,045,000/= ndiyo fedha za ndani. Halafu fedha tunazotegemea kutoka nje, ni Sh. 387,073,918,000/= tu. Hii ni fedha nyingi sana ambazo tunategemea kutoka nje, maana yake ni kwamba tutaendelea kushuhudia miradi mingi haitekelezeki kwa sababu wahisani inawezakana wasitoe fedha kama ilivyo (au kama tulivyozoea) kwa miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji Mjini ni tatizo kubwa sana. Nitatoa mfano wa Mkoa wa Kigoma. Tumezungukwa na Ziwa Tanganyika, Ziwa zuri sana, maji yetu yale yangeweza kutumika kabisa kwa shughuli mbalimbali kwa sababu kwanza hayana chumvi. Tanki lililoko ni la zamani

sana na umeme unapoendelea kukatika hata ile pampu haiwezi kusukuma maji na tumekuwa na shida ya maji muda mrefu vile vile kutokana na matatizo ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile miundombinu pia imechakaa. Wananchi wanaoishi maeneo ya Ujiji, Majengo, eneo la Kisangani, Mwanga wanapata taabu sana, maji wananunua kwa *gallon* Sh. 200/= mpaka Sh. 500/=. Sasa kwa mwananchi mwenye kipato cha chini ambaye anapata mshahara Sh. 75,000/= au mpaka Sh. 150,000/= maana yake ni kwamba fedha yake yote inaishia kwenye maji na bado haitoshi. Hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna wakati ambapo umeme ulikuwa haupatikani kabisa, ukienda kumwona mgonjwa hospitali inabidi uende na *gallon* la maji kwa sababu hakuna maji ya kutumia. Hospitali walikuwa wanatumia magari ya *bull dozer*. Sasa wanunue maji wasafishie hospitali, wapikie, wafulie mashuka; unakuta ukienda hospitali katika wodi kitanda kimefunikwa tu na *cover* la karatasi kwa sababu hawawezi kuweka mashuka, kwa sababu hawana uwezo wa kufua kwa sababu hakuna maji. Hili ni tatizo kubwa, halafu vile vile ni aibu, tunalo Ziwa Tanganyika halafu hatuna maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Jiji la Dar es Salaam, yaani hapa ndio tatizo limezidi. Kumekuwa na matabaka ya walionacho na wasionacho. Walionacho angalau wana uwezo wa kufunga pampu na kuweka *tanks* za maji. Wasionacho wameendelea kununua maji ambayo hawana uhakika kama ni safi na salama. Miundombinu imechakaa mno, na maji hayafiki kutokea Mto Ruvu, mengi yanaishia njiani na kama mkiangalia mkaona kwamba mto Ruvu basi umeelemewa upo Mto Rufiji, ule mto una maji mengi sana. Unaweza ukatumika kuhudumia maji kwa Mkoa wa Dar es Salaam na vile vile Mkoa wa Pwani. Serikali itafakari na ione umuhimu wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee kidogo mradi wa Ziwa Victoria. Mradi huu ni mradi mkubwa sana, umetumia zaidi ya Shilingi bilioni 250. Mashine zilizofungwa pale ni tatu, lakini zinazofanya kazi ni mbili. Tanki limejengwa la *Cubic Metre* milioni 35. Uwezo wa ile mashine kusuma maji kuwafikia wananchi kwa siku ni *cubic metre* 80,000. Lakini wakakadiria kwamba angalau kwa siku wasukume *cubic metre 31,000* ila kinachosikitisha ni kwamba kinachosikitisha, kinachotumika ni *cubic metre* 17,557 maana yake ni kwamba huu mradi ni *under utilized.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia gharama za uendeshaji za huu mradi ni kubwa mno. Kwa miezi tisa imetumika Sh. 1,857,000,000 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji ambapo kwa mwezi ni takribani Sh. 206,340,000/=. Gharama za umeme na dawa peke yake za kusafishia maji zimechukua Sh.1,206,000,000/=, yaani wastani wa asilimia 65 za gharama yote za kuendesha mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia gharama hii iliyotumika katika kipindi cha miezi tisa, gharama za usafirishaji maji bado hazijaunganishwa. Ina maana tukianza matengenezo ya mara kwa mara ukipiga mahesabu kamili kwa mwezi, mradi huu utagharimu shilingi milioni 330. Mradi huu unapita katika vijiji 54 na katika Wilaya za Miji ya Shinyanga, Kahama, Misungwi na Wilaya ya Kwimba ila inasikitisha kwamba vijiji hivyo siyo vyote vinavyopata maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, mradi huu ni *under utilized* na ni hasara. Naomba nitoe gharama kidogo ya miezi hii tisa kama nilivyosema mara ya kwanza kwamba wao katika uendeshaji na katika mauzo yao wamepata katika miezi tisa Sh. 932,809,000/= ni wastani wa Shilingi milioni 103.

Sasa angalia kwa hii miezi tisa, gharama ilikuwa Sh. 1,857,000,000/= halafu kwa wastani kwa mwezi ilikuwa gharama Shilingi milioni 206. Sasa ukiangalia hapa kuna tofauti sana. Inabidi watumiaji waongezeke ili mradi huu uwe na tija. Maana yake ni kwamba watapata fedha pia za kujiendesha. Fedha inayopatikana ni sawa sawa na asilimia 32 tu ya gharama zote za uendeshaji. Kwa hiyo, maana yake ni kwamba katika hii miezi tisa mpaka mwezi Mei Serikali ilikuwa imetoa ruzuku ya Sh. 578,720,000/=. Sasa mradi mkubwa kama huu ambao unaweza ukajizalisha wenyewe Serikali bado inatoa ruzuku, kwa kweli hii haiingii akilini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hiyo, Serikali imekuwa na tabia ya kuchelewesha ruzuku. Kwa hiyo, unakuta kwa kipindi mpaka cha Mei mradi huu ulikuwa unadaiwa shilingi milioni 344 na mzabuni anayewazuia dawa ya kusafisha maji, hii ni aibu. Serikali inatakiwa iangalie na izingatie changamoto hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijamaliza, naomba ninukuu maneno ya Mheshimiwa Rais. Tarehe 18 Novemba, 2010 hapa wakati Mheshimiwa Rais akifungua Bunge letu, alisema maneno yafuatayo. Naomba kusoma:

"Pamoja na Juhudi kubwa tulizozifanya katika kuboresha huduma ya upatikanaji maji nchini, uhaba wa maji bado ni tatizo kubwa katika maeneo mengi nchini. Sasa tumedhamiria kulivalia njuga tatizo hili. Tunawashukuru wenzetu wa Benki ya Dunia kwa msaada wao mkubwa kwenye sekta hii. Lakini sasa na sisi tutatia nguvu yetu kubwa zaidi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia bajeti yenyewe ya maendeleo kiasi cha bilioni 387 tunategemea kutoka nje, halafu Shilingi bilioni 41 ndiyo zitatoka ndani. Mimi naona bado dhamira haitoshi. Tuongeze fedha katika Wizara hii ili tuweze kufanikisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema kwamba: „Ukiondoa wawekezaji kwenye sekta lipo tatizo la kupotea kwa vyanzo vya maji tutaielekeza Mikoa na Halmashauri zote kuendelea kuchukua hatua madhubuti za kupunguza vyanzo vya maji. Mabonde ya mito na usafi wa mazingira ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua zitakazowezesha mito hiyo kuanza kutiririsha maji tena".

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge weka vizuri *microphone* yako.

**MHE. MHONGA SAID RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo bado ni kubwa Rais mwenyewe ameliona, sasa inabidi ahakikishe kwamba bajeti hii ikiwezekana irudishwe, iongezewe fedha ili tuweze kufikia malengo ya milenia na malengo ya MKUKUTA ambayo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nilikuwa nimekata tamaa, nilidhani sitapata nafasi. Lakini nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa, sisi wote tunamwombea Mheshimiwa Waziri Profesa Mark Mwandosya apone haraka ili aje aendeleze kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila wakati kila mmoja anasema anataka hiki, matatizo, ndugu yangu yule amesema miaka 50, sasa mimi najiuliza, ni nini ambacho kinahitaji kufanyika ili tatizo hili badala ya kuchukua miaka 50 mpaka leo tuko hapa tulipo angalau kwa miaka inayokuja, ichukue muda mfupi zaidi. Mimi nilikuwa nafikiri labda tumeweka mno mzigo huu wa maji kwa Serikali. Kila kitu Serikali, mimi nafikiri wakati sasa umefika tuangalie labda na mbinu nyingine, labda tuangalie na mbinu za kushirikisha watu binafsi katika kutoa huduma hii.

Hii huduma kama tunavyofahamu wote, wengi zaidi kama Mjini hatuipati bure, tunanunua. Kweli ina soko, kwa hiyo, maji ni mali kwa hiyo, maji unaweza kufanya biashara. Labda wakati sasa umefika tufikirie kwa mfano tuna maji mengi sana pale Mkuranga na pia Kisarawe na mambo kama hayo, Temeke haina maji, Masaki haina maji, kila mahali hakuna maji. Kwa nini tusifike mahali tunakubaliana na watu fulani fulani katika utaratibu huu wa kushirikiana na watu binafsi ambapo unamwambia wewe utashughulika na Temeke tu, wewe utashughulika na Masaki tu au utashughulika na viwanda tu? Maji yale yanauzwa na yule ataangalia hata kama ni upotevu wa maji, ataangalia na vitu kama hivyo.

Najua watu wengi tumejaribu pale tulipotengeneza Kampuni ya Maji Dar es Salaam, hatukupata faida sana kwa kushirikiana na yule mwekezaji. Lakini tatizo siyo kwamba utaratibu

huu ni mbovu, tatizo ni kwamba Tanzania hatujajifunza kutengeneza mikataba ambayo itatusaidia. Kila mkataba ambao tunautengeneza unaibana zaidi Serikali kuliko yule ambaye tunashirikiana naye. Sasa kama tatizo ndiyo hilo, basi tuwekeze humo katika kuhakikisha kwamba tumepata Watanzania ambao ni wazalendo, ambao wanapenda nchi yao na wahakikishe tunawatengenezea mikataba ambayo itahakikisha kwamba kuna njia ya kutoka kama mambo hayaendi sawa sawa *(Exit position).* Mimi nafikiri hii inaweza ikasaidia. Waziri wa Fedha anaweza akahamasisha watu kama hao tuwekeze kwa maji na kama kuna kodi ziondolewe, kama kuna kikwazo chochote, kiondolewe ili watu wengi zaidi waweze wakashiriki katika kutoa maji.

Tumefanya vizuri katika elimu kwa kushirikiana na watu binafsi. Hapa kuna *University* kama mbili tu za Serikali, kuna *University* lukuki za watu mbalimbali binafsi. Tumefanya vizuri katika upande wa afya ambapo kuna hospitali kubwa kama *KCMC*, Bugando kwa kushirikiana na Mashirika binafsi. Kwa hiyo, labda tugeuze *mindset* yetu kwamba maji siyo kitu ambacho ni huduma tu ya Serikali, bali maji ni kitu kinachouzika, maji ni kitu ambacho kinaweza kufanyiwa biashara kubwa. Mimi najua sasa hivi kama Japan watu wanauza maji kwa lita 20 dola 18 na maji hayo yamechafuka kwa sababu ya *Uranium* ambayo imewapata. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri badala ya kunung'unika tu, kila mmoja ananung'unika, Waziri ananung'unika, kila mmoja anasema maneno ya kila aina, lakini hatutoi njia. Waziri hebu fikiria jambo labda unaweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimeshukuru sana Mjumbe wangu wa *Public Accounts Committee* amezungumza juu ya mradi wetu mkubwa wa Kahama, Shinyanga, mradi safi sana. Hayo ndiyo matokeo ya kuwa na Kamati ambayo haikai ofisini tu inatembea pia. Maneno aliyosema Mheshimiwa Mhonga ni hakika kabisa na ni kweli. Mimi nataka kujazia kwa kusema kwamba mradi huu usiposaidiwa utakufa na mabilioni 265 yatapotea. Njia yake ya kuisaidia ni kitu kimoja tu, kusambaza maji mengi *periodically*. Maji yale ambayo Mungu ametusaidia unaweza ukayatiririsha bure mpaka Singida kwa sababu ya *gravity* tuliyonayo. Lakini upembezi yakinifu, hii hadithi na kutegemea *World Bank* haitufai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulithubutu kuweka ule mradi sasa tuthubutu kuutumia. Mimi nafikiri siyo lazima twende njia moja ambayo mmesema mpaka Tabora, maji haya yanaweza pia yakaenda Ngudu, yakaenda Maswa, yakafika mpaka Bariadi na sehemu kama hiyo. Sisi tunasema kile ni kiwanda, mtu yeyote ambaye anaweza kwenda kuangalia pale siyo tu ni *source,* ni kiwanda cha maji na naambiwa kwamba maji yale ni masafi hata zaidi ya maji ambayo tunakunywa katika chupa mbalimbali.

Mimi namshauri Waziri, hebu hamasisha watu wakaweke hata kiwanda cha kuweka maji katika chupa, wauze kwa watu. Hilo moja. Lakini la pili, ni kusaidia ule mradi. Wewe unafikisha yale maji kwa Sh. 4/= kwa kila lita 20 kwa kila kituo, kwa kila *kiosk* yule anayegawanya ambaye sijui *SHUWASA* sijui nani, anauza kwa Sh. 20/=. Kwa nini tumewekeza pale? Serikali hujawekeza, wewe mtu binafsi kwa nini una-*charge* mara tano ya gharama ya yale maji! Rafiki yangu *EWURA* pale najua ametoa kibali na vitu kama hivyo, lakini mimi nafikiri anahitaji kuangalia vizuri zaidi. Hakuna mtu ambaye atatumia Sh. 20/= kila siku kijijini apate maji ya kuoga, kila unapooga unaoga Sh. 20/=, ni mtu gani huyo kijijini ataweza kufanya kazi hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekit, lakini kama ikiwa Sh. 5/= au Sh. 6/= watu wengi zaidi watatumia yale maji na ule mradi utaweza kuendelea. Huu utaratibu uko hivyo hivyo pia Manchila. Kamati ya *Public Account Committee* ilikwenda Musoma, Igunga, Serengeti, huko tumekuta lile bwawa limejengwa kwa zaidi ya miaka 32. Baadhi ya watu wetu, Wabunge walikuwa ni vijana zaidi ya ule mradi, leo tuna maji mengi kweli, tuna bahati. Lakini wamepandisha yale, wala hawana gharama kubwa sana, yamefika kwenye *kiosk* Sh. 20/= kwa lita; ya nini? Kufikisha pale hai-*cost that much*. Kwa hiyo, na lenyewe liko pale, tunaangalia haitufai. Kwa hiyo, mimi nasema lazima tujaribu kutafuta njia ya kuweza kusaidia huu mradi, la sivyo, tunapoteza fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nataka kuzungumzia juu ya dhana ya kutafuta vyanzo vya maji kwa mabwawa kama vile bwawa la Nkoma, bwawa la Habia na mabwawa mengi ambayo yametajwa hapa tusiishie kwa kujenga mabwawa, lazima mradi uwe *complete*. Unajenga bwawa na unaweka pia fedha ya kusambaza yale maji. Hiyo ndiyo *complete*. Pale Bariadi tumeangalia

maji yale mpaka yametukaukia. Juzi hapo tumekuja kuweka chujio, hakuna maji ya kuchuja, maji yote lile bwawa limeshakuwa-*sealed.*

Mimi ningeshauri hiyo ndiyo iwe dhana ya namna ya kuweza kuhakikisha kwamba watu wanapata maji ya kutumia na kutumia pia isiwe tu kufikiria kunywa. Mimi hapa nimesikitika sana, nilikuwa naangalia Mheshimiwa Waziri, maji ya ng'ombe yako wapi? Maji ya kumwagilia, yako wapi? Mtu asije akaniambia kwamba hiyo ni Wizara ya Kilimo, Wizara ya Kilimo haina maji. Wizara iliyo na maji ndiyo hii. Mimi ningefikiria kwamba pia wangetuwekea utaratibu sisi, kwa mfano, sisi ambao tunalima pamba tunataka kulima hata kilimo cha kiangazi ili tuwe mamilionea. Kwa sababu angalau tumefikisha bei Sh. 1,100/=, kila kilo 1,000 ni Sh. 1,000,000/=. Kwa hiyo, njia ya kuondoa umaskini, njia ya kutengeneza mamilionea ni kuhakikisha kwamba kuna kilimo cha kumwagilia. Yako wapi hayo maji? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naona lazima tuangalie ni bili. Kuna Waheshimiwa Wabunge wamelitaja hilo. Teknolojia ipo, kwa nini tusiweke luku? Mimi hapa Dodoma nikiondoka miezi mitatu, nikirudi, bado nadaiwa maji kwa fedha nyingi tu. Lakini tukiweka luku, tutahakikisha kwamba angalau ile kampuni inalipwa na inalipwa hela taslimu. Sasa hii Ihelele inadai *SHUWASA* Shilingi milioni 657, lakini kama wangekuwa na luku wale wa *SHUWASA* wangekuwa wameshalipa ule mradi na ungeweza kuendelea. Kwa hiyo, hebu tuangalie hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini karibu na mwisho, nataka kusema, sasa hivi tuna Wilaya mpya ya Itilima na Lagangabilili pale tutaanza kupimiwa mji. Maji je, yako wapi? Tuna Mkoa mpya, Bariadi itapanuka, Mkoa wetu wa Simiu, maji je, yako wapi? Ningependa Wizara iangalie ili baadaye tusijaze watu, lakini hakuna maji ambayo yako salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ningeomba Waheshimiwa Wabunge kwamba nimefurahi sana kuona watu wanaotumia *CAG report,* safi sana na wana-*quote*. Lakini tuangalie, siyo kila kitu ambacho kimeandikwa kwa mfano masurufu hayajarudishwa.

Kwa mfano, *documents* hazipo, maana yake ni wizi. Halafu tunapozungumzia Wizara kama hii ambayo yenyewe inategemea wafadhili kuwapa fedha, unasimama hapa unasema hawa ni wabadhirifu, hawa ni wezi. Hawa kama ni wezi, kwa nini leo au kesho tunapitisha bajeti? Kwa nini unasema Wizara hii iongezewe bajeti? Kama ni wezi huwaongezei bajeti. Mimi ni Mwenyekiti wa Hesabu za Serikali, nimeangalia mwaka huu Wizara hii imepata hati safi yenye msisitizo. Kwa hiyo, tusiwalaumu sana wafanya kazi mpaka kila mmoja anarudi nyumbani anafikiria kwamba ni mwizi. Mimi nafikiri ndugu yangu Saya anafanya kazi vizuri sana pamoja na watu wake. Najua kuna watu ambao wana matatizo, lakini siyo matatizo ambayo hayawezekani kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuzungumza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru Mheshimiwa Cheyo kwa mchango mzuri. Hii ndiyo michango ya watu wazee. Sasa kwa kuwa dakika zenyewe ni chache, takribani tano Mheshimiwa Jenista Mhagama hebu kule Peramiho wakusikie. Najua hizo zitakutosha. *(Makofi)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi dakika tano zinanitosha sana. Ninachotaka kusema tu nizungumzie hoja moja, basi na wananchi wangu wa Jimbo la Peramiho watasikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasimama hapa nikiwawakilisha wananchi wangu wa Kijiji cha Mawezo, Kijiji cha Lilondo, Kijiji cha Mkongotema na ule mradi wa maji wa Benki ya Dunia unaotoka Lugagala mpaka kufika Peramiho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo hapa na ni lazima tukubaliane mradi wa Baji wa Benki ya Dunia ni tatizo. Ni tatizo, lazima tukubaliane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nikwambie kitu, wananchi wangu wamekimbizwa mchakamchaka usiku na mchana kwa ahadi ya kupata maji ambayo ndiyo tatizo kubwa. Kijiji cha Mawezo, Lilondo na Mkongotema, hebu fikiria, wale maskini wamejikusanya na kujikusanya wamechanga jumla ya Shilingi milioni 56 kama asilimia 2.5 na kijiji kingine wamechanga asilimia tano kukidhi mahitaji ambayo yanatakiwa kukamilisha ili wapate maji kwenye mradi wa Benki ya Dunia. Huu ni mwaka wa nne hakuna hayo maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kusema yuko Afisa wetu mtalaam wetu wa maji anaitwa bwana Kabonde, bwana Kabonde ndio alipewa jukumu la kwenda kuhamasisha huu mradi wa benki ya dunia akawa anawaahidi kila siku wale wananchi kesho maji yanakuja, kesho maji yanakuja.

Mpaka leo yule Bwana Kabonde akipita kule anaweza kupigwa mawe. Hebu niambie, hizi Shilingi milioni 56 leo nasoma hapa kwenye vitabu naambiwa kwamba ziwekwe zifanye mradi mwingine. Mradi wa maji kwenye vijiji hivi siyo chini ya Shilingi bilioni 1.5, zilizoletwa ni Shilingi milioni 217. Ninasema nini kwa wananchi wa Jimbo la Peramiho kwenye maeneo haya? Ama wale akina Kabonde wanawaambia nini wananchi hawa?

Leo tuki-*transform* hiyo Shilingi bilioni moja na kitu kwenye Shilingi milioni 56 eti ndio zianze kushughulika na maji, zinafika hatua ngapi? Mimi nafikiri hapo tukubaliane, tukae vizuri, Serikali tujiulize kwenye miradi hii ya Benki ya Dunia ambayo wananchi walishahangaika. Jamani, naomba Waziri ajue, wamehangaika sana. Tunasema nini kwenye huu mradi wa Benki ya Dunia, leo wananisikiliza hawa Mkongotema, mimi nilikwenda pale, wametolea macho, hawataki kunielewa, wananiambia hizi Shilingi milioni 56 nyingine walikopa *SACCOS* mpaka leo wanadaiwa kwenye Vyama vya Akiba na Mikopo ili wajikomboe wapate maji kwenye maeneo yao. Kitabu hiki kinaniambia kwamba sasa tumeshapata *point of no objection,* wakandarasi wataanza kazi. Ssasa wametutaja kwamba wakandarasi wataanza kazi kwenye vijiji hivi vyote, lakini fedha iliyotengwa ni Shilingi milioni 217, nyingine tutatoa wapi? Tutatoa wapi hizo zinazobaki?

Mimi nafikiri liko tatizo kwenye mradi huu wa Benki ya Dunia. Jamani tukubaliane, cha msingi hapa tujiulize tunafanya nini sasa baada ya mradi huu wa Benki ya Dunia kutuangusha, umeangusha Ilani ya Utekelezaji wa Chama cha Mapinduzi kwenye tatizo la kutatua kero ya maji kwa wananchi wetu na wale walioko vijijini. Mimi nadhani ifike wakati tuseme tatizo hili limetupata kubwa, tunafanya nini tuweke maamuzi ya kimsingi, hawa wananchi wakapate maji? Ni afadhali wangekuwa hawajachanga haya mamilioni yao ya fedha. Hapa kila anayesimama, huyu Shilingi bilioni 10, huyu Shilingi bilioni ngapi, milioni hizi ukikusanya, sasa fedha zilizochangwa na wananchi katika mchakamchaka huo wa kutafuta wananchi wamejitoa sadaka kuliko kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya sadaka hiyo yote, hakuna kinachoendelea. Kitabu hiki mimi nikakisoma, nikafikiri sadaka ya wananchi wangu hawa, kitabu hiki cha Wizara ya Maji leo wangeniambia baada ya sadaka ya Shilingi milioni 56 ya kujikwamua kuchangia nguvu kuisaidia Serikali sasa mkakati kama Benki ya Dunia imeshindwa kutupa hiyo fedha, tunayo *alternative* nyingine, wakandarasi, ma-*consultancy* wote wako *centred* Dar es Salaam na wala siyo kule kwenye Halmashauri zetu. Nadhani tukubaliane tupate majibu mazuri kwenye mradi huu wa Maji wa Benki ya Dunia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana kwamba hapa tukiruhusu mjadala huu uendelee kidogo tu, watu wanaweza wakalia na hiki ndicho kilichopo kwa wananchi wetu ambapo tatizo hili ni kubwa la maji. Kwa hiyo, Serikali ina kazi kubwa.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na matatizo haya tunayosema ya maji bado, tuna wajibu mkubwa wa kutunza mazingira yetu ili vyanzo visipotee. Kama hatutatunza mazingira, basi matatizo yatakuwa makubwa sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, basi mimi sina tangazo lingine lolote hapa, naomba nichukue nafasi hii kuahirisha Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12.28 jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumanne,
Tarehe 23 Agosti, 2011 saa tatu asubuhi)*